**8 FEBRUARI, 2024**

# BUNGE LA TANZANIA

______

## MAJADILIANO YA BUNGE

______

## MKUTANO WA KUMI NA NNE

### Kikao cha Nane – Tarehe 8 Februari, 2024

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

**NDG. NENELWA J. MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na: -

**MHE. FESTO R. SANGA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu Shughuli za Kamati kwa mwaka 2023.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

Katibu.

**NDG. NENELWA J. MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

## MASWALI KWA WAZIRI MKUU

**NAIBU SPIKA:** Maswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Sasa tutaanza na Mheshimiwa *Engineer* Stella Martin Manyanya. Mheshimiwa Waziri Mkuu karibu. *(Makofi)*

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jitihada kubwa ambayo Serikali inafanya ya kuhakikisha kwamba Nchi yetu inakuwa na sukari ya kutosha wakati wote, lakini katika siku za hivi karibuni kumekuwa na taharuki na upungufu wa sukari kiasi cha wananchi kuwa na malalamiko. Vilevile, ikizingatiwa kwamba katika kipindi hiki cha karibuni tunategemea kuwa na mfungo wa Ramadhan na Kwaresma, kwa hiyo wananchi wanakuwa na hofu juu ya suala hilo.

Je, ni lini kauli ya Serikali ili wananchi waweze kuondokana na hofu hiyo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya, Mbunge wa Mbamba Bay, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba tuna upungufu wa sukari nchini na upungufu huu umetokana na kuwepo kwa mvua nyingi ambazo maeneo yetu ya mashamba ya miwa inayozalisha sukari maji yamejaa kiasi cha kwamba, wale wa miliki wa mashamba haya hawawezi kutoa miwa kutoka mashambani kupeleka viwandani na kule viwanda vimebaki havina sukari.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa upungufu huu umeishafanyiwa kazi na Wizara ya Kilimo na Waheshimiwa

Wabunge na Watanzania mmepata kumsikia Mheshimiwa Waziri wa Kilimo akitoa maelezo hapa ya nini Serikali inafanya ili kukabiliana na upungufu huu ili Watanzania na wananchi kwa ujumla waweze kutumia bidhaa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja Wizara imetoa vibali kwa Wafanyabiashara mbalimbali wakiwemo wazalishaji wa sukari wenyewe. Kuingiza sukari nchini zaidi ya tani laki moja na zoezi hilo linaendelea na taarifa ambazo ninazo kutoka Wizara ya Kilimo tayari tumeanza kupata sukari kutoka nje. Hii itaendelea kupunguza makali ya kukosekana kwa sukari nchini ili Watanzania waweze kutumia bidhaa hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tumeendelea kukaa na viwanda kuona namna bora ya kupata bidhaa hii pale ambako mvua zinapungua ili waendelee kuzalisha, upungufu huu siyo wa muda mrefu na kipindi hiki tunaamini tutafika mpaka kipindi cha Ramadhan. Kwa hiyo ndugu zetu Waislam watafunga Ramadhan na Serikali itawahakikishia kwamba sukari itakuwepo nchini, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu ahsante. Mheshimiwa Salim Mussa Omar.

**MHE. SALIM MUSSA OMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuweza kumuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu swali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taifa letu linapitia katika changamoto kubwa ya migogoro ya ardhi sasa hivi, jambo ambalo linakuwa linazorotesha sana shughuli za kimaendeleo katika nchi yetu. Wananchi walio wengi wamekosa imani na Watendaji wa Wizara ya Ardhi. Je, hatuoni sasa kama ni muda muafaka wa kuweza kupitia mifumo ya utendaji katika Wizara hii ili kuweza kuepukana na changamoto hii? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Salim Omar, Mbunge wa Gando Zanzibar, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninakiri kwamba tuna migogoro mingi ya ardhi nchini na migogoro hii inatokana na mahitaji makubwa sasa ya matumizi ya ardhi hiyo, iko migogoro ya wakulima na maeneo yaliyohifadhiwa, iko migogoro ya wafugaji na maeneo yaliyohifadhiwa, lakini tuna migogoro hiyo iliyosababisha na utoaji wa hati mbili mbili kwa kiwanja kimoja na mipaka. Sasa nini Serikali inafanya? Kwa sasa hivi tunaendelea na maboresho ya Sera yetu ya ardhi nchini. Tunaamini Sera hii ikikamilika kuandaliwa ikipitishwa hapa kwetu Bungeni itasaidia sana kupunguza matatizo ya ardhi, kwa sababu kwenye Sera tutaainisha maeneo yale ambayo tumepata uzoefu wa migogoro yake kwa wakati huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kukabiliana na changamoto hii wakati huu tunaendelea kuiandaa sera, Serikali imeendelea kufanya maboresho ya utoaji vibali vya ardhi kwa wakulima na wale wanaotaka kujenga miundombinu mbalimbali. Mifumo hii tunaendelea kuihimarisha mifumo ya ki-*electronic* ili ipunguze kitendo cha kutumia makaratasi pekee katika utoaji wa vibali vya matumizi ya ardhi. Tunajua pia kwamba kuna Watumishi wachache kwenye Halmashauri zetu na Wizara ya Ardhi wanaokiuka taratibu na sheria tulizonazo kwenye ardhi na utoaji vibali kwa watumiaji wa ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati mwingine hulazimika kutoa Hati Mbili kwenye kiwanja kimoja hapo lazima mgogoro utakuwepo, ikiwemo na kuimarisha sheria tulizonazo maeneo yale yenye migogoro. Kwa hiyo Serikali kazi kubwa tunayoifanya sasa ni kutoa elimu na elimu hii tunashirikisha wananchi waweze kujua Sheria zetu za Ardhi na matumizi yake lakini pale ambako tunaona tunahitaji kufanya maboresho, Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya wanaendelea kwenye maeneo yao kusikiliza kero mbalimbali kwa wananchi ili kutatua migogoro ya ardhi pale ambako kero hiyo inawasilishwa kwa Mkuu wa Wilaya au Mkuu wa Mkoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaendelea kutoa wito kwa Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya kote nchini kuendesha vikao vinavyokusanya wananchi wenye changamoto na kusikiliza changamoto zao ikiwemo na ardhi, ili kutatua changamoto hizi na wananchi waweze kufanya shughuli zao kikamilifu. Tunaahidi kwamba migogoro hii tutaipunguza kwa kiasi kikubwa, kwa sababu sera ambayo inaandaliwa na utekelezaji wa kufuata sheria na usikilizaji wa kero kwa wananchi utasaidia na hasa matumizi ya ki-*electronic* ambayo tunaendelea sasa kuyaboresha ndiyo ambayo yataendelea kupunguza kero za ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho ni kwamba sasa hivi tumesogeza huduma za ardhi mpaka kwenye ngazi ya Mikoa. Mikoa yote tumepeleka Makamishna wa Ardhi ambao watasaidiana, watashirikiana na Mkuu Mkoa kutatua matatizo na Halmashauri zilizoko ndani ya Mkoa, lakini mpango wa baadaye pia ni kushusha Mamlaka za Ardhi ambazo zitakwenda kutatua matatizo hayo hasa kwenye maeneo ya Majiji na Manispaa ambayo kuna idadi kubwa ya watu na mahitaji makubwa ya viwanja ili huduma hii iweze kupatikana huko huko kwa ukaribu zaidi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, ahsante sana. Sasa namwita Mheshimiwa Nusrat Shaaban Hanje.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kumuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu swali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na maendeleo makubwa ya kiteknolojia duniani, watoto wetu wamekuwa wakiingia kwenye mitandao na wakitumia vifaa vya ki-*electronic* kwa ajili ya kujifunza masuala ya TEHAMA na masuala mengine ya kujipa maarifa katika masomo yao. Tunafahamu wanapoingia katika mitandao wanakutana na mambo mengi ambayo yanaweza kupelekea mmomonyoko wa maadili na udhalilishaji wa watoto mitandaoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu mwaka 2014 Umoja wa Mataifa ulielekeza dunia kuweka mikakati madhubuti ya

kuwalinda watoto dhidi ya ukatilii wa mitandao. Nchi nyingi zime-*adopt,* zimeweka sera madhubuti na sheria madhubuti za ulinzi wa watoto mitandaoni. Sasa nchi yetu imekuwa ikiendesha kampeni zisizo rasmi za ulinzi wa watoto mitandaoni, naomba kufahamu Serikali imejipangaje kuhakikisha inatengeneza mazingira bora ya kisera na ya kisheria kuhakikisha kwamba *online child protection* inapewa nguvu. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Nusrat Hanje, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, dunia sasa hivi inaendea kwenye maendeleo makubwa ya matumizi ya mifumo yetu mbalimbali ki-*electronic*. Pia dunia imeanza kuelimisha umma wake kutumia mifumo hii ya ki-*electronic* kwa urahisi zaidi, sasa mifumo hii imekuja ikiwa na faida lakini pia kuna changamoto zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto zilizopo ni miongoni mwa hayo uliyoyaeleza kwamba jamii baadhi yetu tunatumia vibaya matumizi ya TEHAMA, matumizi ya Mifumo hii ya ki-*electronic* vibaya kwa kukashfu, kutumia mitandao kudhalilisha watu wakiwemo watoto na wanawake, lakini pia hata juzi tulipokuwa tunapitisha Muswada wetu hapa wa Vyama vya Siasa tulilizungumza hili na tumeliwekea mbano kidogo wale ambao watatumia vibaya mitandao kwa ajili ya kudhalilisha kwenye eneo la siasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa huu ni mkakati ambao Serikali pia tumekubaliana na tumesaini mikataba ya kimataifa kukabiliana na unyanyasaji, vitendo vya kikatili kwa watoto na wanawake. Sisi kama Serikali tumeweka utaratibu wetu kupitia Wizara yetu ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto ili kukabiliana na wale wote wanaotumia vibaya mifumo hii kwa kudhalilisha watoto, wanawake na makundi mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu ambao tumeufanya huku tukiwa tunapeleka pia kwenye Mtaala wetu wa elimu kufundisha kutoka Shule za Msingi, Sekondari, Vyuo mbalimbali

mpaka elimu ya juu, elimu hii ya matumizi ya ki-*electronic* tumeweka pia na Sheria zinazowabana hawa wote wanaotumia vibaya mitandao hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo Serikali inaendelea kuwahakikishia Watanzania kwamba, tutaendelea kuimarisha kudhibiti wale wote ambao wanatumia vibaya mitandao hii na tutachukua hatua kali dhidi ya wale wote ambao watatumia vibaya matumizi haya ya TEHEMA kwa kudhalilisha na kukatili wengine wa aina yeyote ile kwao ili itoe mafundisho kwa wengine ambao wanaweza kuungana nao kwenye matumizi mabaya haya. Kwa hiyo, nitaendelea kuwahakikishia ya kwamba matumizi ya TEHAMA tutaendelea kuhamasisha yake lakini hamasa hii ni kwa matumizi sahihi na siyo vingine. ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu ahsante sana. Sasa namwita Mheshimiwa Ng'wasi Kamani.

**MHE. NG'WASI D. KAMANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru na mimi kwa kupata nafasi kuuliza swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Natambua kwamba mwaka 2006 Bunge hili lilipitisha Sheria ya Benki ya Tanzania, ambayo chini ya kifungu cha 27(1)(b) inaipa Mamlaka Benki hii ku-*design* fedha kwa kuweka nembo na *material* mbalimbali. Pia natambua mwaka 2021 nchi hii imepata Rais wake wa kwanza Mwanamke anaefanya kazi nzuri na anatambulika katika Bara la Afrika na Duniani kama Rais madhubuti na wa mfano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri Mkuu, natambua pia kwamba Bunge la Marekani sasa lipo katika utaratibu kupitisha sheria ambayo itawezesha Harriet Tabman, mwanamama, mwanaharakati aliyefanya kazi kubwa kwenye vita dhidi ya utumwa, kuwekwa kwenye dola ishirini kama kumbukumbu. Natambua kwamba katika Bara letu la Afrika nchi kama Nigeria, Malawi na Tunisia zimekwishafanya hatua hizi na zimetambuliwa na Benki ya Dunia na *IMF* kama hii hatua katika uelekeo unaofaa. Je, Serikali haioni sasa kwamba kuna haja ya kuweka kumbukumbu ya kudumu kwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuweka picha yake katika fedha za nchi hii? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ng'wasi, Mbunge Vijana, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge ameonesha kutambua kazi nzuri, mchango unaotolewa na Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na kuona kama je, Serikali inaweza kuona umuhimu wa kutumia picha yake kwenye fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, uwekekaji wa picha za viongozi mbalimbali ni maamuzi ambayo huko nyuma tulitoa kwa lengo la kukumbuka mchango wa Viongozi hawa kwenye Taifa hili, hasa picha ambazo zinatumika sasa za Baba wa Taifa hili, Mwalimu Julius Nyerere lakini pia na Mheshimiwa Sheikh Abeid Aman Karume Rais wa kwanza wa Zanzibar ili kutambua tu mchango wao walioutoa katika Taifa hili na kwa hiyo picha zao zilitumika kama sehemu ya kumbukumbu zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tunazo aina ya fedha noti na hizi sarafu ambazo pia tunatumia kuweka alama za wanyama wetu. Hii ilikuwa ni kuenzi tunu ya Taifa lakini pia kuuboresha hamasa kwenye Utalii. Sasa maamuzi ya kuweka picha kwenye noti mara nyingi yanafanywa na maamuzi ya kiongozi mwenyewe kwa kushauriana na Benki Kuu. Sasa kwa kuwa umelileta hili na sisi tunatambua kuwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ametoa mchango mkubwa kwenye Taifa hili, niseme tu tunapokea ushauri wako na litaingia Serikali litajadiliwa, pale ambako watafanya maamuzi kwa kushauriana na Benki Kuu taarifa zitatolewa rasmi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, ahsante sana. Sasa namuita Mheshimiwa Martha Nehemia Gwau.

**MHE. MARTHA N. GWAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa nafasi uliyonipa na mimi kumuuliza swali Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na ongezeko kubwa la watu kuhamahama kutoka eneo moja kwenda lingine kwa sababu mbalimbali. Moja ikiwa kutafuta malisho na maji kwa wafugaji lakini pia wakulima kutafuta maeneo ya kilimo na pia kutafuta maisha kwa ujumla. Wanakohamia kunakuwa hakuna huduma muhimu za kijamii. Je, Serikali haioni haja sasa ya kuongeza maeneo ya utawala kama kusajili Vijiji na Kata mpya ili kupeleka huduma za msingi katika maeneo hayo ambayo watu wamehamia? Nashukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Gwau, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhamahama kwa wananchi, kutafuta maeneo ya kuendesha shughuli za kijamii kwenye maeneo mengi, ndiyo hasa wananchi sasa hivi tumeona wakisambaa maeneo mbalimbali, lakini Mheshimiwa Mbunge anahitaji kujua kama je, Serikali haioni umuhimu kuanzisha maeneo mapya ya utawala?

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo mapya ya utawala yanaanzishwa kwa vigezo. Moja, idadi ya watu; pili, uwezo wa mapato wa maeneo hayo ili kuweza kuendesha mamlaka husika; tatu, uwepo wa huduma za jamii; vile vile, uwezo wa Serikali wa kujenga makao makuu ya mamlaka hiyo mpya iliyoko eneo hilo. Mara kadhaa tumepata maswali haya maeneo mengi. Binafsi nilipofanya ziara kwa wananchi, yapo maeneo wameomba kugawanywa ili wapate mamlaka mpya ya halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nini msimamo wa Serikali? Ni kwamba tukiwa tunaendelea kupata takwimu mbalimbali za maeneo haya na kuona umuhimu wa kugawa maeneo haya kuwa na utawala mpya, kwa miaka mitano iliyopita Serikali ilitoa mamlaka mpya kwa maeneo mapya ya vijiji, kata, wilaya, halmashauri na hata majimbo kwa upande wetu Wabunge na mikoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo haya bado tunaendelea kuratibu kwa kupeleka miundombinu wezeshi ya utoaji huduma ya wananchi wa eneo hilo kama makao makuu yake. Sasa hivi, tunaendelea na ujenzi wa ofisi, nyumba za kuishi watumishi wa viongozi kwenye maeneo haya na Serikali imeshaweka msimamo wake kwamba tunaendelea na kuimarisha meneo haya. Hatuwezi kuanzisha maeneo mapya huku tukiwa hatujakamilisha kuandaa mazingira mazuri ya maeneo ambayo tayari yametolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pindi itakapokamilika, ujenzi wa miundombinu wezeshi kwenye maeneo haya ili viongozi wa maeneo haya waweze kutoa huduma na wananchi wapate huduma kwenye maeneo hayo, sasa tangazo la Serikali litatoka. Halmashauri, mikoa, wilaya na maeneo mengine yanahitaji kuwa na mamlaka mpya zitaanza mchakato wa kuomba mamlaka hizo kwa kufuata taratibu zilizowekwa hasa zile ambazo zinajumuisha vikao vya wadau wenyewe kuanzia huko huko walipo, wakubaliane kugawana na pia kama kuna jambo lolote ambalo litahusisha mgawanyo huo, basi maamuzi ya vikao hivyo utakuja na baadaye muhtasari utakuja Serikalini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais atakapoona sasa tumekamilisha ujenzi wa miundombinu, anaweza kutoa kibali kupitia Ofisi ya Rais – TAMISEMI ili kutoa mamlaka nyingine mpya. Huo ndiyo utaratibu wa Serikali tulionao kwa sasa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, sasa namwita Mheshimiwa Cecil Mwambe.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru pia kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Serikali imefanya juhudi kubwa sana kwa kipindi kirefu kuondoa tozo mbalimbali hasa zaidi kwenye mazao ya biashara kama vile pamba, kahawa, korosho pamoja na mazao mengine. Nia ya kuondoa tozo hizi ilikuwa ni kumletea nafuu mnunuzi ambaye naye anakwenda kumpelekea

nafuu mkulima ili aweze kupata faida nzuri kwenye mazao yake ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo siku za karibuni kumeonekana kama tozo zilikuwa zinajirudia na kusababisha kuanguka kwa bei ya mazao ya kilimo, ikiwemo ya Korosho. Ni nini, kauli ya Serikali kuhusu kufanya marejeo ya tozo mbalimbali ambazo zinaathiri bei ya Korosho? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Cecil Mwambe, Mbunge wa Ndanda, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba haya mazao yetu yote na hasa yale mazao yanayolimwa kwa ushirika kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge ameyataja, ni mazao ambayo miaka mingi huko nyuma kumekuwa na ongezeko la tozo mbalimbali na ikasababisha hata kuanguka kwa bei na pia kero kwa wakulima kwa kupata kipato kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulifanya mapitio kwenye mazao yote yenye bodi na yanayouzwa kwa mifumo ya ushirika na kugundua kwamba tuna makato mengi. Mazao mengine yana makato mpaka 30 au 20. Tulifanya hizo jitihada kupunguza makato hayo na kufikia kiwango cha mwisho makato sita na kuleta unafuu mkubwa kwa wanunuzi na pia kuwapa kipato cha kutosha wakulima. Hiyo inaendelea hata sasa, mazao aliyoyataja pamoja na kakao kule Kyela, sasa hivi bei imepanda juu sana baada ya kuwa tumesimamia kuondoa tozo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali bado inaendelea na imeshatoa maagizo kwa bodi zote za mazao kufanya mapitio ya mara kwa mara ya tozo na pia mwenendo wa soko la mazao yenyewe. Lengo hapa, tunataka Serikali tuone kuwa mkulima anayelima zao hili, ambaye anatumia muda wake mwingi kulima zao hili, ananufaika kwa kupata bei nzuri. Sasa, bei nzuri ni pale ambapo tunapunguza gharama kwa wanunuzi ili gharama hiyo iweze kuhamia kwa wakulima wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchakato huu unaendelea na hasa usimamizi wa Vyama hivi vya Ushirika vya Msingi ambako ndiyo kunaanza kuwekwa kwa tozo, pia vyama vyake vikuu ambako nao ndio wanatoa vibali vya tozo kuhakikisha kwamba tozo hizi haziendelei. Tumeweka ukomo wa tozo muhimu kwenye zao husika kulingana na mazingira waliyonayo ili kuweza kuleta unafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nikuhakikishie kuwa Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wote ambao mnatoka kwenye maeneo yanayolima mazao yenye bodi na kuuzwa kwa ushirika kwamba, Serikali itaendelea kusimamia kwa ukaribu, kuhakikisha kwamba wakulima wananufaika na mazao haya kwa kuwatafutia masoko, lakini baada ya kuwa tumeuza tozo mbalimbali zisiingie bila kuwa na utaratibu. Bodi nazo tumesisitiza kufanya ufuatiliaji wa kuhakikisha kwamba hakuna tozo nyingi kwenye eneo hili ili makundi haya mawili; wanunuzi na wakulima waweze kunufaika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. Namwita Mheshimiwa Boniphace Butondo.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuuliza swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Sote tunatambua jitihada kubwa inayofanywa na Serikali yetu ya Awamu ya Sita, chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, hasa katika eneo la kuhakikisha kwamba miundombinu hasa ya barabara inaimarishwa mijini na vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipindi hiki tumekuwa na wakati mgumu wa mvua hasa katika baadhi ya mikoa, mfano Mikoa ya Kanda ya Ziwa, Nyanda za Juu Kusini, Mikoa ya Pwani Kaskazini, hali ambayo imekuwa ikisababisha kwa hali ya juu sana uharibifu wa miundombinu hii ambayo tumeijenga na kutumia fedha nyingi sana kwa ajili ya kuimarisha mawasiliano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali. Je, Serikali ina mpango gani wa haraka na wa dharura wa kibajeti ilimradi kuhakikisha kwamba tunanusuru hali ya mawasiliano kwa maana ya

barabara ambayo sasa imekuwa ni mbaya sana; katika maeneo ya vijijini na mjini, ili wananchi waendelee kutoa huduma na kusafirisha na kusafiri kama ilivyokuwa kawaida na kama ilivyo azma ya Serikali ya CCM? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Butondo, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa maelezo yake, anataka kujua mpango wa Serikali wa kibajeti wa kuwezesha kurudisha miundombinu iliyoharibiwa kutokana na mvua nyingi. Kwanza nikiri kwamba mvua ni nyingi na mvua inaendelea kunyesha kote nchini. Tumeendelea kushuhudia maafa mbalimbali ikiwemo na miundombinu zetu barabara, madaraja na makalavati yanabomoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo tu kwa barabara pia hata maisha ya watu. Kuna maeneo imesababisha mafuriko; nyumba, mali mbalimbali zimepotea, hata maisha ya Watanzania wengine hawapo, wametutangulia mbele ya haki kutokana na kusombwa na maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niungane na Waheshimiwa Wabunge kuwapa pole wale wote waliofikwa na maafa hayo. Wale ambao wametutangulia mbele za haki, Mwenyezi Mungu aweke roho zao mahali pema Peponi, Amina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa Serikali umeelezwa vizuri sana hapa. Kulikuwa na maswali kadhaa kwa Waziri wa Ujenzi ambaye aliulizwa swali la namna Serikali inavyoweza kukabiliana na jambo hili. Mtakumbuka pia Waheshimiwa Wabunge kwamba hata Mheshimiwa Spika alitoa nafasi nyingi kwa Wabunge kuuliza kwenye eneo hili na kuitaka Serikali itoe maelezo ya nini Serikali tumekifanya mpaka sasa?

Mheshimiwa Naibu Spika, maafa hayo na kuharibika kwa miundombinu ya barabara na makalavati, tumezipa jukumu zile

taasisi zetu mbili; *TANROADS* pamoja na *TARURA* inayosimamia barabara zilizoko wilayani na vijijini, kuhakikisha wakati wote wanafuatilia mwenendo wa mvua zinazoendelea kunyesha nchini na kama kuna eneo limeharibiwa, kulirudisha kwa haraka sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kila taasisi kupitia Wizara zake; TAMISEMI na Wizara ya Ujenzi, kibajeti zimejiweka vizuri na hata Mheshimiwa Waziri alipokuja hapa Waheshimiwa Wabunge waliouliza swali hili, kila mmoja aliambiwa fedha iliyopelekwa kwenye eneo lake. Kwingine tumeleta shilingi milioni 500, shilingi milioni 300. Kwa hiyo, Serikali imejipanga vizuri kuhakikisha kuwa, tunarudisha miundombuinu ili huduma za wananchi kwenye maeneo hayo ziendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, najua hatutarudisha kwa viwango vya awali, lakini muhimu ni kuwafanya watu waendelee kupita na kutumia miundombinu hiyo vizuri. Pia, tukiwa tunaendelea kuona mvua zinanyesha, nitoe tahadhari kwa Watanzania hasa walio kwenye maeneo hatarishi, kuondoka kwenye maeneo hayo hatarishi na kukaa kwenye maeneo ambayo yapo kwenye miinuko ili tuweze kupunguza maafa haya hasa pale ambapo maji yanazidi kiasi na kufika kwenye nyumba zilizo kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kuwahakikishia Watanzania kwamba Serikali tupo macho kupitia Taasisi zetu za *TARURA* na *TANROADS* pale ambako kuna uharibifu tunaanza na halmashauri yenyewe ambako *TARURA* ipo. Pia, kwenye *TANROADS,* Ofisi zipo kwenye mikoa, jukumu lao sasa ni kupita maeneo yote na kufanya ukaguzi wa mara kwa mara, kila mvua zinaponyesha kuona kama je, miundombinu yote imebaki salama au kuna tatizo limejitokeza, na kuhakikisha kwamba tunarudisha huduma hiyo kwa haraka zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huo ndiyo mpango wetu ndani ya Serikali, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha. Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa majibu yako sahihi. Hongera sana. *(Makofi)*

Ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge na ahsante tena Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa majibu sahihi ambayo yamekidhi mahitaji ya Bunge hili.

Waheshimiwa Wabunge, kwa maneno hayo sasa tunaendelea. Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, ndc – KATIBU WA BUNGE:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**NAIBU SPIKA:** Kabla hatujaanza na maswali ya kawaida, nachukua nafasi hii kumwita Mwenyekiti wa Bunge, Mheshimiwa Najma aendelee na ratiba zilizowekwa Mezani. *(Makofi)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Maswali ya Kawaida. Sasa ni Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji, Mbunge wa Mwera, aulize swali lake.

Na.127

**Athari za mvua nchini**

**MHE. ZAHOR MOHAMMED HAJI** aliuliza: -

Je, zipi athari za mvua zilizonyesha Novemba, 2023 na Serikali imejipangaje kuzuia athari hizo kujirudia?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU (MHE. UMMY H. NDERIANANGA)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zahor Mohamed Haji, Mbunge wa Jimbo la Mwera, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha kuanzia Mwezi Oktoba, 2023 hadi sasa, tumeshuhudia mvua kubwa ambazo zimenyesha katika maeneo mbalimbali nchini. Mvua hizo, zimeleta athari mbalimbali ikiwemo mafuriko, maporomoko ya ardhi, magonjwa ya milipuko kwa binadamu ikiwemo kipindupindu, matukio ya radi na matukio ya upepo mkali ambayo yamesababisha uharibifu wa miundombinu, madhara ya kiafya, kiuchumi, kijamii na upotevu wa mali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukabiliana na athari hizi, Serikali imechukua hatua mbalimbali za kuzuia, kujiandaa na kukabiliana na hali ikiwemo kuandaa Mpango wa Taifa wa Dharura wa Kukabiliana na Madhara ya *El-Nino* kwa kipindi cha Septemba, 2023 mpaka Juni, 2024. Vilevile, kuzijengea uwezo Kamati za Usimamizi wa Maafa katika mikoa 18 nchini, kufuatilia mwenendo wa majanga, kutoa tahadhari kwa umma kupitia Kituo chetu cha Oparesheni na Mawasiliano ya Dharura na kuimarisha ushirikiano wa kikanda na kimataifa kupitia utekelezaji wa mikakati na mikataba ya Kikanda na Kimataifa, ikiwemo Mkakati wa Kimataifa wa Sendai wa Upunguzaji wa Athari za Maafa wa Mwaka 2015/2030; na Mkataba wa Makubaliano wa kuanzisha Kituo cha Huduma za Kibinadamu na Oparesheni za Dharura cha Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika 2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, yapo madhara ambayo kwa msingi wake wa kuwa majanga ya asili pale yanapotekea hata athari zake hujirudia. Hivyo, Serikali imeendelea kujumuisha athari za majanga hayo katika mpango wa uzuiaji na urejeshaji wa hali pale inapobidi, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji.

**MHE. ZAHOR MOHAMMED HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi. Nina mambo mawili. La kwanza, naipongeza sana Ofisi ya Waziri Mkuu kwa sababu ya kujipanga

kupambana na maafa ambayo kwa kweli sote kama Taifa tumeyaona. Tunawashukuru na tunawaomba waendelee kujipanga zaidi kwa sababu mambo haya ni ya kujirudia na hasa ukizingatia mabadiliko ya tabianchi ambayo yanaendelea na sote tunashuhudia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili kwangu ni ushauri. Naomba sana Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa sababu mambo ya majanga ni mambo ambayo yasiyotabirika, na yanahitaji mafunzo na uwezo kwenye taasisi zake zote, na kwa sababu ni kazi zinazofanywa kwa ushirikiano kati ya Bara na Zanzibar, naomba Ofisi ya Waziri Mkuu, basi ione namna nzuri inavyoweza kuwasaidia wenzetu kwa upande wa pili ili nao waweze kujipanga vizuri kwa kuweza kukabiliana na maafa haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU (MHE. UMMY H. NDERIANANGA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapokea pongezi za Mheshimiwa Zahor, nasi tunaendelea kumpongeza lakini pia tunampa pole kwa maafa yaliyotokea kule Jimboni kwake Mwera. Tunamhakikishia kwamba Ofisi ya Waziri Mkuu tuko imara na tutaendelea kujipanga zaidi katika eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia jambo la pili kuhusu ushauri, tumepokea ushauri wake. Kwa kuwa masuala haya pia yanaratibiwa na Ofisi ya Makamu wa Kwanza, nasi Ofisi ya Waziri Mkuu tuna vikao vyetu vya mashauriano tunapitia Ofisi ya Makamu wa Pili, tutaendelea kuboresha ushirikiano huo ili kuendelea kuwafikia wananchi katika maeneo yote katika nchi yetu, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Mwantatu Mbarak Khamis, Mbunge kutoka Baraza la Wawakilishi.

Na.128

**Mafunzo na mikopo kwa vijana wenye ulemavu**

**MHE. MWANTATU MBARAK KHAMIS** aliuliza: -

Je, vijana wenye ulemavu wamenufaika vipi na mafunzo na mikopo inayotolewa na Serikali?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU (MHE. UMMY H. NDERIANANGA)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwantatu Mbarak Khamis, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa kutambua umuhimu wa mafunzo na mikopo kwa Vijana wenye Ulemavu inatekeleza mikakati na programu jumuishi mbalimbali inayolenga kuwapatia mikopo yenye masharti nafuu, mafunzo na ujuzi kwa lengo la kuboresha hali zao za maisha na kukuza ushiriki wao katika shughuli za kijamii, kisiasa na kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kitabu cha Hali ya Uchumi cha Mwaka 2022, kiasi cha mikopo ya shilingi bilioni 81.3 zilitolewa kwa watu 640,723 wenye ulemavu wakiwemo vijana wenye ulemavu. Mikopo hiyo imewezesha vijana wenye ulemavu kuanzisha au kuendeleza biashara zao na hivyo kupunguza utegemezi na kuwa na uwezo wa kuchangia kwa kiwango kikubwa katika mahitaji yao wenyewe na familia zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2022/2023, zaidi ya vijana wapatao 2000 wamenufaika na mafunzo yanayotolewa hapa nchini. Vijana hao wamepata mafunzo ya ufundi stadi na ujasiriamali kupitia vyuo vya ufundi na marekebisho, vyuo vya *VETA* na kupitia programu ya ukuzaji ujuzi iliyopo nchini, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwantatu Mbarak Khamis.

**MHE. MWANTATU MBARAK KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza kabisa, naipongeza Serikali kwa majibu mazuri. Pia naipongeza Serikali kwa kutambua umuhimu wa kujumuisha vijana wenye ulemavu katika programu mbalimbali. Vilevile, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, napenda kumuuliza swali dogo tu la nyongeza. Je, Serikali ina mkakati gani wa kufuatilia na kuwaendeleza vijana hao ili lile lengo la Serikali liweze kutimia? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU (MHE. UMMY H. NDERIANANGA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapokea pongezi za Serikali ya Awamu ya Sita ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kutoka kwa Mheshimiwa Mwantatu lakini na mimi nimpongeze sana Mheshimiwa Mwantatu kwa kazi nzuri anayofanya tangu nimemfahamu katika eneo letu hili la watu wenye ulemavu, anafanya kazi nzuri, lakini nimwambie kwamba, Serikali ya Chama Cha Mapinduzi ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia tunaendelea kuweka mikakati ya kuwafikia vijana hawa. Moja, Mheshimiwa Naibu Waziri anayehusika na eneo hili amekuwa akifanya programu za kuwatembelea na kuwaona vijana hawa na hata Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Mheshimiwa Profesa Ndalichako, anapita katika maeneo mbalimbali kuwatembelea kuona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Waziri Mkuu, kupitia kitengo cha watu wenye ulemavu imeendelea kufanya programu za kuwapitia na kuendelea kuwahamasisha vijana hawa kwa kushirikiana na wenzetu upande wa TAMISEMI, Maafisa Maendeleo ya Jamii, kuona namna wanaendelea vizuri. Lakini mwisho tunafanya mapitia ya Sera ya Taifa ya Watu Wenye Ulemavu ili kuweka mikakati ambayo ni endelevu itakayowezesha kundi hili kuendelea kushiriki lakini niwape moyo na kuendelea kuwaambia wenzangu, watu wenye ulemavu hasa vijana, waendelee kuchangamkia fursa ambazo zinatolewa na Serikali na sisi tuko pamoja na wao. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ng’wasi Kamani.

**MHE. NG'WASI D. KAMANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, imekuwa takribani miezi kumi tangu Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, atoe maelekezo ya kusitisha mikopo iliyokuwa inatolewa kwa vijana, wanawake na watu wenye ulemavu kwa kupisha utaratibu mpya ambao utakuwa na manufaa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujua ni lini hasa Serikali itarejesha utaratibu huu, ili vijana waendelee kunufaika na mikopo hii?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU (MHE. UMMY H. NDERIANANGA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge wa Vijana, Mheshimiwa Ng'wasi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili kwa kuwa lilifuata utaratbu na wenzetu wa TAMISEMI, wameendelea kulizungumzia, tuendelee kuwaachia wenzetu wa upande wa TAMISEMI watatupa taarifa rasmi ya wapi wamefikia na lini wataanza kutoa mikopo hiyo, lakini niwahakikishie kwamba, mikopo ile ipo, fedha ipo. Utaratibu utakapoanza makundi haya yajiandae kwa ajili ya kunufaika na programu hiyo.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu hayo. Tunaendelea sasa na Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Mheshimiwa Josephine Tabitha Chagula, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 129

**Hitaji la walimu Nyang'hwale**

**MHE. JOSEPHINE T. CHAGULA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itapeleka walimu katika shule za sekondari na msingi Wilayani Nyang'hwale?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Josephine Tabitha Chagula, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka 2023 Serikali iliajiri Walimu 13,130 ambapo Walimu 20 wa shule za msingi na 55 wa shule za Sekondari walipelekwa Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'hwale. Serikali inatambua mahitaji ya Walimu katika Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'hwale na maeneo mengine. Hata hivyo, kila mwaka Serikali inaendelea kupunguza mahitaji ya walimu katika sekta ya elimu na hivi karibuni Serikali itatangaza ajira za walimu baada ya taratibu za kibali kutoka Ofisi ya Rais – Utumishi kukamilika na kadri ya upatikanaji wa fedha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Josephine Tabitha.

**MHE. JOSEPHINE T. CHAGULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina swali la nyongeza:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, shule za sekondari za kata zimeonesha mafanikio makubwa sana katika ufaulu, lakini tatizo lililopo ni kufeli kwa somo la hesabu na mwanafunzi anapopata *F* ya hesabu inakuwa imemuharibia kabisa kombi yake.

Je, Serikali ina mpango gani sasa wa haraka wa kupeleka walimu wa somo la hesabu katika shule zetu hizi za kata, ili tuweze kupunguza au kutoa F hizo zinazojitokeza kwa watoto wetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini swali la pili, kumekuwa na changamoto kubwa kwa walimu wetu wa shule za msingi na sekondari kupata uhamisho kuwafuata wenza wao na hasa hawa ajira mpya. Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kuwapangia moja kwa moja walimu hawa kuwafuata wenza wao kwa vile

wana vyeti vya ndoa, ili tuweze kutoa usumbufu huo wanaoupata walimu wetu hawa? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya maswali hayo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Chagula; la kwanza hili juu ya kuajiri walimu wa hesabu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema kwenye majibu yangu ya msingi, Serikali hivi karibuni itatangaza ajira za walimu. Na katika ajira hizo kipaumbele kitakuwa kwa walimu wa sayansi na hisabati ambao wataajiriwa. Kwa hiyo, nimuombe Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wengine humu ndani, kuwa na subira pale ajira hizi zitakapotangazwa basi walimu hawa wa hesabu na sayansi wataajriwa na kwenda katika halmashauri mbalimbali hapa nchini, ili kuongeza nguvu katika shule zetu za kata ambazo Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan, amewekeza fedha nyingi zaidi ya bilioni 219 katika kuhakikisha kuna shule mpya za sekondari kwenye kata ambazo zilikuwa bado hazina shule hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda kwenye swali lake la pili la uhamisho wa kuweza kuwafuata wenza; Serikali hutoa ajira kulingana na upungufu uliopo. Tathmini hufanyika nchi nzima kuangalia maeneo mbalimbali ambayo yana upungufu wa walimu kisha ndipo kibali hutolewa kwa ajili ya kuajiri wale walimu kwenda kuziba yale mapengo. Kwa hiyo, mtu anapoomba ajira anaenda kwenye eneo kuziba pengo ni lazima atumikie kwanza mwaka mmoja kwa ajili ya kuweza kuthibitishwa kazini akiwa katika eneo lile ambalo amepangiwa. Baada ya kuthibitishwa kazini baada ya ule mwaka mmoja anatakiwa aendelee kuwepo kwenye kile kituo cha kazi kwa miaka mingine isiyopungua miwili ambayo jumla inakuwa ni miaka mitatu ndipo aweze kuona ni namna gani anahama katika kituo kile na kwenda kituo kingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ajira hizi si kwamba, ni njia tu ya kuingilia kwenye ajira ya Serikali halafu aweze kuhama na kuhamia maeneo mengine na mara nyingi wanaotaka

kuhama huwa wanahamia kwenye majiji na Manispaa, wale waliokuwa pembezoni huwa mara nyingi wanataka kuhama. Sasa tukisema mtu tu akishapata *check number* aweze kuomba uhamisho na kumfuata mwenza wake ina maana maeneo ya pembezoni mwa nchi yetu kutaendelea kuwa na upungufu wa idadi ya walimu ambao wanahitajika. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Daniel Sillo na Mheshimiwa Minza Mjika.

**MHE. DANIEL B. SILLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa kuwa, mahitaji ya walimu wa shule za msingi katika Jimbo la Babati Vijijini ni 2,349 na waliopo ni 1,379 hivyo kuwa na upungufu wa walimu 970. Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza walimu katika shule za msingi?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Sillo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka wa fedha 2021/2022 na 2022/2023 Serikali iliajiri walimu na katika ajira hizo Jimboni kwa Mheshimiwa Sillo nako walipata walimu wapya, walienda katika shule za msingi na shule za sekondari. Kama nilivyosema kwenye majibu yangu ya msingi, Serikali inaendelea kutoa ajira mpya na hivi karibuni zitatangazwa na baada ya kupatikana hawa waajiriwa wapya tutaweka kipaumbele vilevile kule kwa Mheshimiwa Sillo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Minza.

**MHE. MINZA S. MJIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naishukuru sana Serikali yangu kwa kutujengea shule nyingi za sekondari na msingi katika Mkoa wa Simiyu, lakini kuna upungufu mkubwa wa walimu. Je, ni lini Serikali italeta walimu wa kutosha katika Mkoa wetu wa Simiyu?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itapeleka walimu zaidi katika Mkoa wa Simiyu pale ambapo ajira hizi ambazo nimesema zitatangazwa hivi karibuni zitakamilika mchakato wake na wao wenyewe katika Mkoa wa Simiyu watapata mgawo wa walimu hao wapya.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hussein Amar na Mheshimiwa Saashisha niliwaona. Maswali mafupi.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona. Kwanza niipongeze Serikali kwa kuendelea kupunguza upungufu wa walimu katika Wilaya ya Nyang'hwale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, uko tayari kumuelekeza Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya ya Nyang'hwale azipitie shule zote zikiwemo za sekondari na msingi kuangalia uwiano wa walimu 'ke' na 'me' kwa sababu, kuna baadhi ya shule za msingi zina wanawake peke yake na baadhi ya shule za msingi zina wanaume peke yake, ikiwemo Shule ya Msingi ya Mama Samia.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Amar:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipo tayari kumuelekeza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'hwale kuweza kufanya tathmini hiyo na ninaomba kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kuchukua nafasi hii kumuelekeza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Nyang'hwale kuanza kufanya tathmini hii, kama alivyoshauri Mheshimiwa Amar na kuona ni namna gani anafanya msawazo wa ikama ndani ya halmashauri yake katika walimu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Saashisha.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, katika Wilaya ya Hai tunaishukuru Serikali imetujengea shule tatu mpya kwa hivyo, kuongeza mahitaji ya watumishi pamoja na kujengewa vituo vitano vya afya. Je, ni lini sasa Serikali itatuletea watumishi kwenye maeneo haya ya elimu na afya?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikirejea majibu yangu ya msingi, nikijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Saashisha Elinikyo Mafuwe:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali italeta watumishi hawa, hasa walimu katika hii ajira mpya ambayo itatangazwa hivi karibuni, basi Wilayani Hai nako mtapata mgawo katika walimu hao.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Genzabuke.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante; je, Serikali ina mpango gani mahususi wa kupeleka walimu katika maeneo ya pembezoni, ikiwa ni pamoja na Mkoa wa Kigoma?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kufanya tathmini ya upungufu wa walimu waliopo kote nchini, yakiwemo maeneo ya pembezoni, kama vile Mkoa wa Kigoma na kwenye ajira hizi mpya ambazo zitatolewa Serikali itaendelea kuweka kipaumbele hasa katika maeneo ya pembezoni ambayo yana uhitaji mkubwa wa walimu, ikiwemo Mkoani Kigoma.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwakagenda, swali fupi la nyongeza.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la uhamisho kwa walimu wanawake au wanaume kufuata wenza wao ni suala muhimu sana kwa ajili ya maadili, lakini pia, kulinda ndoa za walimu hawa. Mnaonaje Serikali kuhakikisha wale ambao wamefunga ndoa kweli, waende wakafuate wenza wao kuepukana na matatizo na maambukizi na mambo mengine kama hayo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilipokuwa nikijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Chagula, utumishi wa umma unaongozwa kwa sheria, taratibu na kanuni na miongozo mbalimbali iliyomo katika utumishi wa umma. Na mtu anapokuwa ameajiriwa katika utumishi wa umma anafuata zile sheria, taratibu na kanuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria inasema ajira mpya atafanya kazi kwa mwaka mmoja kisha atafanyiwa *assessment* na kuthibitishwa kazini. Baada ya kuthibitishwa kazini ni lazima atumikie nafasi kwa muda usiopungua miaka miwili katika lile eneo ambalo yupo, baada ya hapo anaruhusiwa kuomba uhamisho kwenda katika eneo lolote la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini hilo linategemea pia na uwepo wa nafasi kule anakotaka kwenda kwamba, ule mshahara wake ile bajeti je, imetengwa kwa muajiri yule anayetaka kuhamia.

Kwa hiyo, Serikali haikatishi mtu tamaa kuweza kuhama, lakini pia, inatakiwa kufuata sheria, taratibu na kanuni na miongozo iliyopo ya utumishi wa umma.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, Mbunge wa Viti Maalum ambalo litaulizwa na Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara.

Na. 130

**Maboma ya nyumba za walimu yaliyotelekezwa**

**MHE. DKT. THEA M. NTARA K.n.y. MHE. ASHA ABDULLAH JUMA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani kuhusu maboma ya majengo ya Nyumba za Walimu na Madarasa yaliyotelekezwa?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imefanya tathmini ya maboma ya nyumba za walimu ambapo jumla ya maboma 2,527 yamebainishwa. Ili kukamilisha maboma haya, zinahitajika shilingi bilioni 37.905 na kila boma litagharimu shilingi milioni 15.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa madarasa, jumla ya maboma ya madarasa 10,106 yanayohitaji shilingi bilioni 126.6 yametambuliwa. Serikali itatenga fedha kwa ajili ya kukamilisha maboma ya nyumba za walimu na madarasa yaliyoanzishwa na wananchi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa majibu. Swali langu la kwanza; kwa nini, Serikali isitoe fedha kwa haraka kukamilisha hayo mabima?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwa kuwa, bado kuna upungufu mwingi wa madarasa, je, Serikali inachukua mkakati gani wa kudumu kuhakikisha hali hii haijitokezi tena? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara. La kwanza, kwa nini Serikali isitoe fedha hizi kwa haraka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikumbukwe ya kwamba, katika Sera ya Ugatuaji wa Madaraka *(D-by-D)* jukumu la kujenga miundombinu yoyote ya maendeleo katika halmashauri zetu nchini ni jukumu la Halmashauri yenyewe. Serikali Kuu inafanya usimamizi na ku-*complement* jitihada za wao wenyewe katika zile halmashauri kule. Hivyo basi, ni jukumu la Mkurugenzi kuweza kufanya tathmnini katika eneo lake na kutenga fedha katika fedha za maendeleo kuweza kumalizia nguvu za wananchi zilipokwenda kama kwenye zahanati, vituo vya afya na madarasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha inayotafutwa Serikali Kuu ni kwenda kuongeza tu nguvu na kasi katika eneo husika. Hivyo, basi, Serikali Kuu inaendelea kutafuta fedha hizo kama ilivyotafuta fedha za kuweza kumalizia maboma na kuongeza madarasa katika miaka mingine kama ambavyo kila Mbunge humu ndani na halmashauri yake walipata shule mpya kupitia Mradi wa *SEQUIP* na Mradi wa *BOOST*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikkienda kwenye swali lake la pili; hali hii itaendelea kuwa hivi kwa sababu, elimu ya awali ni bure, kwa Sera ya Serikali yetu hii. Elimu ya msingi ni bure, elimu ya sekondari ni bure kwa hiyo, idadi huongezeka kadiri mwaka unavyokwenda na huwa mahitaji nayo yanaendana na wale wanaotoka huku nyuma, wanaotoka awali kwenda darasa la kwanza, wanaotoka darasa la saba kwenda *Form One*. Kwa hiyo, kila mwaka Serikali inaendelea kufanya tathmini na maoteo ya wale ambao wanamaliza na kuona ni namna gani ambavyo fedha inaweza ikapatikana kwa ajili ya kuondoa upungufu huu wa madarasa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Janejelly.

**MHE. JANEJELLY J. NTATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Suala la nyumba za walimu ni la kila watumishi, hasa kada yetu ya watendaji wa kata ambao wako vijijini kabisa na wakati mwingine maisha yao huwa hayana usalama wa kutosha. Je, Serikali ina mkakati gani kuwajengea nyumba za kuishi hawa watendaji wa kata?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itafanya tathmini juu ya mahitaji ya nyumba za watendaji wa kata kote nchini, kama ambavyo amesema Mheshimiwa Janejelly na kisha kuona ni bajeti ya kiasi gani inahitajika kwa ajili ya kuweza kujenga nyumba hizi.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Francis Isack Mtinga, Mbunge wa Iramba Mashariki.

Na. 131

**Upungufu wa walimu – Halmashauri ya Mkalama**

**MHE. FRANCIS I. MTINGA** aliuliza:-

Je, Serikali inafahamu kuna upungufu kiasi gani wa Walimu katika Halmashauri ya Mkalama na ina mpango gani kupunguza pengo hilo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Francis Isack Mtinga, Mbunge wa Jimbo la Iramba Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka 2022 Serikali iliajiri Walimu 9,800 nchi nzima na Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama ilipangiwa walimu wa ajira mpya 70, kati ya hao walimu 52 wa shule za msingi na 18 kwa shule za sekondari. Kwa mwaka 2023 Serikali iliajiri walimu 13,130 na Halmashauri ya Mkalama ilipangiwa Walimu 92, kati yao walimu hao, 65 kwa Shule za Msingi na 27 kwa Shule za Sekondari. Serikali inatambua mahitaji ya walimu katika Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama na maeneo mengine. Hata hivyo, kila mwaka Serikali inaendelea kupunguza mahitaji ya walimu katika sekta ya elimu na hivi karibuni Serikali itatangaza ajira za walimu baada ya taratibu za kibali kutoka Ofisi ya Rais – Utumishi kukamilika na kadri ya upatikanaji wa fedha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Francis Isack Mtinga, swali la nyongeza.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa upungufu wa walimu Mkalama bado ni mkubwa sana, Serikali inasema nini kuhusu upendeleo maalum kwa Mkalama kwa mgawo unaofuata wa walimu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwa kuwa, watumishi wote wa umma tayari wapo wale wanaofariki na wale wanaostaafu, tayari wapo kwenye ikama ya kibajeti ya Serikali. Serikali ina mpango gani wa haraka wa kuziba mapengo yote yanayoachwa na watumishi hawa badala ya kusubiri zile ajira ambazo Rais anatupatia kila mwaka? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Francis Isack; la kwanza, la upungufu mkubwa wa walimu Mkalama:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyokwishasema kwenye majibu yangu ya msingi, Serikali iko mbioni kuajiri, ajira mpya za walimu hivi karibuni zitatangazwa na baada ya mchakato huo kukamilika, Serikali itaweka kipaumbele katika maeneo ya pembezoni, ikiwemo jimboni au Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama kule anakotokea Mheshimiwa Francis Isack. Kwa hiyo, nikutoe mashaka katika hizi ajira mpya bado utaendelea kupata mgawao wa walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda kwenye swali lake la pili, hili la vifo, uhamisho na ile mishahara inayobaki; kwa mujibu wa Kanuni B.4(1) – (2) ya *Standing Order* ya mwaka 2009 ya Utumishi wa Umma, mshahara ule upo katika bajeti ya mwaka husika kwa sababu mshahara ni *cash budget*. Sasa, mwajiri akichelewa kuomba kibali cha ajira mbadala, ule mshahara unakuwa haupo *carried forward* kwenye mwaka mwingine wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niwatake sasa waajiri, pale wanapopata kifo katika maeneo yao ya halmashauri zao, kwa maana kuna mwajiriwa wake mmoja amefariki au amehama, waombe vibali vya ajira mbadala mara moja ili sisi tuweze ku-*compile* maombi yote yale na kuyapeleka kwa wenzetu wa Ofisi ya Rais, Utumishi, kuweza kupata vibali vya ajira mbadala, ndani ya mwaka wa fedha husika kama *Standing Order* ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2009 inavyotaka.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nusrat, swali la nyongeza.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Je, ni lini sasa Serikali itapeleka walimu katika Jimbo la Singida Mashariki, Wilaya ya Ikungi pamoja na shule za sekondari Lighwa, Mang'onyi, Shule ya Msingi Mbughantigha, Choda, kote? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itapeleka walimu kule Singida Mashariki mara baada ya mchakato huu wa ajira mpya kukamilika na Singida

Mashariki na maeneo aliyoyataja Mheshimiwa Nusrat kama Ikungi na mengineyo watapata nao mgao wa walimu hao wapya.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Benaya Liuka Kapinga, Mbunge wa Mbinga Vijijini.

Na. 132

**Sekondari ya Hagati kuwa ya kidato cha tano na sita – Mbinga**

**MHE. BENAYA L. KAPINGA** aliuliza: -

Je, ni lini Shule ya Sekondari ya Hagati itapandishwa hadhi kuwa ya kidato cha tano na sita?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Benaya Liuka Kapinga, Mbunge wa Jimbo la Mbinga Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilipeleka fedha shilingi milioni 128 kwa ajili ya ujenzi wa bweni. Ujenzi umekamilika na taratibu za usajili wa kidato cha tano unaendelea. Tayari halmashauri imeomba kibali cha kupandisha hadhi ya kuwa kidato cha tano na sita, kwa barua yenye Kumb. Na. MDC/E.80/31/150 ya tarehe 15 Januari, 2024. Hivyo shule inatarajia kuanza rasmi kwa kidato cha tano na sita Julai, 2024.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Benaya Liuka Kapinga.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na naishukuru sana Serikali kwa majibu haya mazuri ambayo yanaleta shangwe kubwa katika Tarafa hii ya Hagati. Nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na shule hii ya *Hagati Secondary*, Halmashauri ya Mbinga ina shule ya wasichana inaitwa *Mbinga Girls* na yenyewe iko katika hali nzuri. Kupitia barua yenye Kumb. Na. MDC/E.80/136/135, tumeomba kibali cha shule hii nayo ichukue kidato cha tano na cha sita. Je, Serikali iko tayari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, halmashauri hii kwa kushirikiana na wananchi tumejenga shule za *Benaya Secondary* na *Nguzo Secondary*. Shule hizi zina upungufu wa miondombinu na sasa hivi zipo kidato cha pili. Je, Serikali iko tayari kutoa fedha kwa ajili ya miundombinu ikiwemo maabara? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Benaya Kapinga; hili la kwanza kuhusu *Mbinga Girls* nayo kuweza upandishwa hadhi na kuwa *A – Level*, Serikali ipo tayari kuweza kupandisha hadhi shule hii lakini kuna taratibu zile zilizowekwa kwa ajili ya upandishaji hadhi wa shule kuweza kuwa ya *A – Level*. Hivyo basi, nimtake Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mbinga Vijijini kuweza kuanza taratibu za kupandisha hadhi shule hii, kwa mujibu wa sheria inavyotaka. Kwa maana lazima kwanza ifanyike *assessment*, pili waweze kumpeleka yule Mkaguzi wa Elimu pale na kisha waandike Wizara ya Elimu kwa ajili ya kuweza kuomba kupandisha hadhi shule hii.

Mheshmiwa Mwenyekiti, nikienda kwenye swali lake la pili la fedha kwa ajili ya kuboresha miundombinu katika shule alizozitaja ikiwemo Shule hii ya Benaya: Tutaendelea kutafuata fedha kama Serikali kwa ajili ya kuweza kuboresha miundombinu ya shule mbalimbali hapa nchini ikiwemo *Mbinga DC*. Hivyo basi, nimtake Mkurugenzi wa Halmashauri ya *Mbinga DC* kuweza kuorodhesha mahitaji yale ambayo yanahitajika katika shule hizi ili aweze kumwandikia Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, TAMISEMI na kuweza kuona namna gani Serikali itapeleka fedha kadri ya upatikanaji wake. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zuena Bushiri, Mheshimiwa Esther Matiko na Mheshimiwa Mwita Getere, maswali.

**MHE. ZUENA A. BUSHIRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Je, ni lini Serikali itapandisha hadhi Shule ya Sekondari Kwambegu iliyoko Kata ya Mahore ambalo ni hitaji la wananchi? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itapandisha hadhi shule hii iliyopo Kata ya Mahore**.** Kama nilivyokuwa nikimjibu Mheshimiwa Kapinga kwamba, ni kwa mujibu wa sheria na taratibu zile zilizopo; ni lazima kwanza iwe imekidhi vigezo ambavyo vimewekwa. Hivyo basi, nimatake Mkurugenzi wa halmashauri husika kuweza kuanza kufanya tathmini hii na kisha Mkaguzi kwenda kuona kama vile vigezo vimetimia na kuweza kuomba kwa wenzetu wa Wizara ya Elimu kuweza kupandisha hadhi shule hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, Halmashauri ya Mji wa Tarime ina shule moja tu ya kidato cha tano na cha sita ambayo ni *Tarime Secondary,* kufuatia uhitaji mkubwa wa shule za kidato cha tano na cha sita, Halmashauri ya Mji wa Tarime imeanzisha mchakato wa kuipandisha hadhi Shule ya Sekondari Mogabiri kwa kujenga mabweni mawili, madarasa mawili ya *advance* pamoja na maabara zote za sayansi.

Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka wa kuipandiisha hadhi shule hii ili iweze kusajili wanafunzi wa kidato cha tano Julai mwaka huu, ukizingatia tumeshakamilisha taratibu zote kama ambavyo umeainisha hapa na vigezo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwneyekiti, nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Esther Matiko juu ya Shule hii ya Mogabiri iliyoko kule Tarime Mjini; tutakaa na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Tarime Mjini kuona kama vigezo hivi vilishapitishwa na ni lini aliweza kuwaandikia wenzetu wa Wizara ya Elimu ili tuweze kufuatailia ndani ya Serikali na kuona tuweze kupandisha hadhi shule hii kama vigezo vyote vimefikiwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwita Getere.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kutokana na umbali mrefu wa kwenda sekondari, wakulima na wafugaji wa Kata ya Nyaburundu na Kata ya Manchimweru wameamua kujenga sekondari wenyewe kwa mikono yao na sasa hivi wameshafikisha madarasa mawili.

Je, ni nini kauli ya Serikali ya kuunga mkono? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Getere juu ya Serikali kupeleka fedha kuunga mkono juhudi za wananchi katika Kata ya Matowelo na Nyatwindu. Nimtake Mkurugenzi wa Halmashauri ya Bunda kuweza kupeleka timu kuweza kufanya tathmini juu ya mahitaji katika maeneo haya. Vilevile, nimtake Mkurugenzi wa Halmashauri hii ya Bunda kuhakikisha kwamba anatenga fedha kati ya mapato yake ya ndani, kuweza kuunga mkono juhudi za wananchi hawa wa kata hizi ambazo Mheshimiwa Getere amewataja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri Deo Ndejembi, kwa maswali hayo ya Waheshimiwa Wabunge na majibu yake. Tunaendelea na Wizara ya Afya, Mheshimiwa Sebastian Simon Kapufi, Mbunge wa Mpanda Mjini, sasa aulize swali lake. *(Makofi)*

Na. 133

**Ujenzi wa Jengo la Huduma ya Usafishaji Damu Hospitali ya Rufaa Katavi**

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI** aliuliza: -

Je, ni lini jengo la huduma ya usafishaji damu kwa wagonjwa wa figo litajengwa katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Katavi?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri ya Afya.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sebastian Simon Kapufi, Mbunge wa Jimbo la Mpanda, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2023/2024 Serikali imetenga shilingi bilioni tano kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Katavi ambapo kati ya fedha hizo, kiasi cha shilingi 224,750,000 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa jengo la huduma ya usafishaji damu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshiiwa Sebastian Kapufi.

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na nina maswali madogo mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, naishukuru Serikali kwa kutenga fedha lakini tangu mwezi wa saba mpaka leo fedha hiyo haijapelekwa.

Je, ni nini kauli ya Serikali katika kuhakikisha kwamba fedha hiyo inapelekwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Serikali inasema nini katika kuongeza mawanda ya utoaji elimu ili kuinusuru jamii na tatizo kubwa la magonjwa haya ambavyo yameendelea kuongezeka?

Ninalisema hilo kwa sababu, kwa sasa hivi ili jamii tuepuke suala la kwenda kwenye tiba, Serikali inasema nini kwa maana ya elimu ya kinga? Nakushukuru *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Kapufi, kwa kweli amekuwa akifuatilia hospitali ile na mimi na yeye tumeshakwenda zaidi ya mara nne kwenye Hospitali ya Mkoa wa Katavi. Nimwambie tu, kabla ya mwezi wa pili kuisha, fedha zitakuwa zimefika kwenye Hospitali yenu ya Mkoa wa Katavi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenykiti, swali lake la pili ni suala la magonjwa yasiyoambukiza kuongezeka, na kila mwaka matatizo hayo yanaongezeaka kwa asilimia 10. Ni kweli tunahitaji mkakati na tunaendelea. Nimuombe kila mtu tuweze kufanya hizo hamasa na zinaendelea. Tumeshaanzisha vipindi kwenye redio na kupitia makongamano mbalimbali. Nawaomba Wabunge, kile kipindi anachokiendesha Profesa Janabi, ninawaomba huo ni mkakati muhimu sana. Kwa hiyo, anachokisema Profesa Janabi naomba usikipuuze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo ukwali halisi na hicho kipindi hakiko kwa bahati mbaya. Profesa Janabi anaendesha kwa ajili ya kutunusuru na ni mkakati maalumu wa Wizara na Hospitali yenu ya Taifa ya Muhimbili ambayo ndiyo yenyewe inabeba mizigo mikubwa kutokana na hayo magonjwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Midimu, Mheshimiwa Felista Njau na Mheshimiwa Zacharia Issaay, maswali mafupi ya nyongeza.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Simiyu haina wodi za kulaza wagonjwa.

Je, ni lini Serikali itapeleka fedha za kujenga wodi hizo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namhakishia tu Mbunge, kwenye hizi hospitali zote ambazo ni mpya ambazo ziko kwenye utaratibu wa kuedelea kujengwa, zimetengewa fedha ikiwemo Hospitali yake ya Simiyu. Kabla ya mwezi Februari kwisha, fedha zitakuwa zimefika ili kuendeleza ujenzi huo ambao ulitakiwa kumalizika. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Felista nilikutaja na Mheshimiwa Zacharia Issaay.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii nami niulize swali fupi la nyongeza. Kituo cha Afya cha Uru Kusini tayari kimekamilika lakini hakuna madaktari. Ni lini Serikali itapeleka madakatari katika kituo hiki cha afya ili Wananchi wa Uru Kusini waweze kuhudumiwa? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni kweli hicho kituo kiko namna hiyo. Cha kwanza, leo leo nikienda kukaa kwenye kiti nitaongea na Katibu Tawala wa Mkoa wa Kilimanjaro ili kuona ni namna gani tunaweza ku-*switch* watendaji ndani ya mkoa au ndani ya wilaya, kupeleka kwenye eneo hili wakati tunashirikiana na wenzentu wa TAMISEMI kuhakikisha wanapatikana watumishi wa kwenda kwa ajili ya kufanya kazi hiyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zacharia Issaay nilimtaja.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, kwa kuwa gharama kubwa ya usafishaji wa figo hailingani na mapato ya Mtanzania wa ngazi ya chini au wa kipato cha chini; je, Serikali ina mpango gani sasa wa kusaidia kupunguza gharama ya usafishaji wa figo kwa wagonjwa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeweka utaratibu mzuri sana wa kuwahudumiwa wale wasio na uwezo wa kupata tiba. Kwa hiyo, kwa wale ambao hawana uwezo wa kujigharamia, kuna utaratibu wa kufuata. Pia kwa kweli ameuliza swali zuri na linagusa watu wengi. Namwomba Mheshimiwa Mbunge kwamba yeye na mimi na wengine tunakwenda kuanza mchakato wa Bima ya Afya kwa Wote. Hiyo ndiyo itakuwa suluhisho kwa wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mnakumbuka, juzi niliulizwa swali hapa. Ikaonesha kuna tiba ukiziacha tu zikaenda bure, huduma nyingine kwenye nchi zina-*collapse*. Kwa hiyo, twendelee kushirikiana kwa sababu, hata bei wanazolipa sasa hivi, watu bado wanachangia kwenye huduma hizo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Noah nilikuona, Mheshimiwa Hawa na Mheshimiwa Mpina, maswali mafupi ya nyongeza.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa magonjwa ya ini yamekuwa ni tishio hapa nchini, na gharama ya kupata chanjo ni kubwa kwa wananchi wetu ambao hawana uwezo, wa kipato cha hali ya chini; je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka kutoa chanjo hiyo kwa wananchi wote kama chanjo zingine?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimmiwa Mwenyekiti, ni kweli kama anavyosema Mheshimiwa Mbunge, tumeanza mchakato huo na muda si mrefu utakamilika kwa ajili ya kuona namna ya kutekeleza wazo zuri ambalo Mheshimiwa Mbunge unasema. Tayari tumeshaanza namna ya kuunganisha na chanjo nyingine; ionekane bajeti inapatikanaje ili kuweza kutoa hiyo huduma chanjo nyingine zinavyotolewa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hawa.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru; magonjwa ya figo yamezidi kuongezeka katika Mkoa wetu wa Tabora.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka Kitengo cha Magonjwa ya Figo katika Hospitali ya Rufaa ya Kitete ili kuwaondolea wananchi usumbufu na gharama kubwa wanazozipata katika hospitali binafsi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kama anavyosema Mheshimiwa Mbunge. Kwanza huduma hizo zipo kwenye Hospitali ya Kitete lakini haziko *strong* kuweza kutatua matatizo tuliyonayo, hasa makubwa yanayohitaji *special attention*. Kwa hiyo, kwa mwaka huu ndiyo hospitali tunazoendelea kujenga. Vifaa kwa ajili ya Hospitali yako ya Kitete kwa ajili ya masuala ya figo vimeshafika. Tunamalizia ukarabati wa baadhi ya maeneo ili hiyo shughuli iweze kuanza. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Luhaga Mpina, nilikutaja.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa kuwa gharama za matibabu ya figo watu wanapoenda kusafisha damu ni kubwa sana, takribani shilingi 540,000 kwa wiki; na kwa maana hiyo ni takribani shilingi 2,160,000 kwa mwezi, gharama ambazo ukweli ni kwamba wananchi wetu wanashindwa ku-*afford* na wengi wanapoteza maisha. Sasa haya mambo mengine ya bima tunajiandaa na bima na nini na Bunge hili lilishawahi kutoa msamaha mwingi katika maeneo mengi, kwa nini wagonjwa hawa wasitibiwe bure na tukatoa msamaha katika hili eneo na tukafidia kwa ajili ya maeneo mengine? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemsikia Mheshimiwa Mbunge, kwa kweli wazo lake lina nia njema, lakini nataka kuwaambia, juzi hapa tumeonesha kuna zaidi ya shilingi bilioni 70.4 zimesamehewa kwenye eneo hilo ambalo Mheshimiwa analisemea. Tutaendelea kuchakata, kwa sababu sasa hivi

tunaenda kwenye michakato ya bajeti na vitu vingine, watupe muda tuone. Kwa sababu, tunaweza kuahidi hapa, tukaahidi na isiweze kutekelezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wa Afya ameshafanya kazi kubwa sana ya kukaa chini na wataalamu wetu. Hizi huduma za figo zinaenda kushuka sana kwa sababu tumeshapata watu wanaoweza kutoa madawa na vile vifaa vinavyotakiwa kutoa huduma hiyo kwa bei rahisi zaidi na huduma hizo zitaenda kushuka sana. Haitakuwa kama bei aliyokuwa anaisema Mheshimiwa Mpina hapo.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Conchesta Leonce Rwamlaza, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 134

**Vifo vitokanavyo na utoaji mimba usio salama**

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA** aliuliza: -

Je, suala la vifo vitokanavyo na utoaji mimba usio salama lina ukubwa na madhara gani nchini?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Conchesta Leonce Rwamlaza, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa tafiti zilizofanywa, matatizo yatokanayo na utoaji mimba ni moja ya sababu inayochangia vifo vitokanavyo na uzazi kwa asilimia kumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madhara yanayotokana na utoaji wa mimba usio salama ni pamoja na maambukizo makali kwa mfumo wa uzazi ambao unaweza kupelekea mgonjwa kutolewa mfuko wa uzazi na wakati mwingine kupoteza maisha kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru; ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo *TBC Radio* ambacho ni chombo kikuu cha habari cha Tanzania, walikuwa wanaendesha mjadala kuhusu jambo hili. Wao wamesema ni asilimia 19, ninyi mnasema ni asilimia kumi. Naona mkasawazishe hapo kwa sababu nyote mnatoa taarifa kwa jamii.

Je, Serikali imejipangaje kupunguza hii asilimia kumi ya vifo vitokanavyo na kutoa mimba kusiko salama?

Swali la pili; Serikali iliridhia na kusaini Mkataba wa Maputo wa Nyongeza ambao mkataba huu ulikuwa unatetea haki za wanawake na afya pamoja na uzazi salama. Makubaliano hayo yalilenga kwamba mimba zitolewe zile ambazo zinapatikana kwa kubakwa, mimba ambazo zinatokana na mashambulio ya ngono na zile mimba maharimu yaani zile mimba ambazo zinatokana na ndugu. Je, Serikali sasa haioni ni wakati muafaka wakuweka makubaliano hayo katika sheria za nchi yetu ili kuwasaidia wamama ambao wanapata mimba za aina hii waweze kuzitoa kwa usalama bila kuhatarisha maisha yao? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge, kwamba eneo hilo ni muhimu lizungumziwe ili kuendelea kutoa hamasa kwamba kuna tatizo na kuna watu wanapoteza maisha kwa sababu ya mimba zisizo salama. Mheshimiwa Mbunge umesema hili la *TBC* inategemeana ni nani alikuwa anaongea na *source* yake ya *data* ni wapi, lakini sisi tuna *source* ambayo inakubalika kwa sababu tunajua duniani kwa mwaka wanawake milioni 42, mimba zisizo salama ni milioni 20 na kidunia ni asilimia 13 ambayo wanapata haya matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tutafuatilia *TBC* wametoa *source* wapi lakini *data* ambazo tunazo kwa kupitia mifumo ya hospitali zetu za Serikali na *private* inaonyesha hili ambalo tumelisema hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu tunashushaje sasa hiyo, tutaendelea kutoa hamasa kuhakikisha kwamba tunashirikiana na Wizara ya Elimu, tunashirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Jamii na nyinyi wenyewe Wabunge kila mmoja awe balozi wa kuonyesha kwamba watoto wetu kuna wakati muafaka wa kupata mimba, kuna wakati muafaka wa kuanza hayo mambo ambayo yanasababisha hayo matokeo. Wote tukiboresha na tukahamasisha maadili katika jamii yetu ni mojawapo ya sehemu yakushusha mimba kama hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili unazungumzia kwamba mikataba ya kidunia lakini pia kuruhusu sasa ili watu waweze kwenda kutoa mimba, sheria zetu ziruhusu. Hii inahitaji mchakato mkubwa kwa sababu inagusa Wizara mbalimbali lakini inagusa imani mbalimbali za watu na mambo mengine. Ninakuomba tupeni muda tuendelee kuchakata ili tusije tukajaribu kuzuia tatizo kwa namna nyingine tukazalisha tatizo lingine. Mimi ninachokuomba Serikali ipo *committed* na elimu itaendelea kutolewa na wewe uwe balozi wetu kwenye eneo lako. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel, kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge.

Sasa tunaendelea na Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa Toufiq Salim Turky, Mbunge wa Mpendae, aulize swali lake. Mheshimiwa Festo Sanga kwa Sanga kwa niaba yake.

Na. 135

**Matumizi ya Akili Mnemba nchini**

**MHE. FESTO R. SANGA K.n.y. MHE. TOUFIQ SALIM TURKY** aliuliza: -

Je, Serikali ina mkakati gani wa kudhibiti matumizi mabaya ya Akili Mnemba, kutumia Akili Mnemba kuchangia ukuaji wa uchumi nchini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Toufiq Salim Turky, Mbunge wa Mpendae, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya akili mnemba yameendelea kuongezeka siku hadi siku hapa nchini katika kuweka mazingira wezeshi ya matumizi ya akili mnemba, Serikali imechukua jitihada za kutosha kujenga uwezo wa wataalam na kuandaa miongozo ya kisera na kisheria ambayo italinda na kuchochea matumizi sahihi na salama ya teknolojia zinazoibukia ikiwemo akili mnemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa tayari Serikali imetoa ufadhiri wa masomo ya muda mrefu na muda mfupi kwa watumishi wa umma 500 kwenye maeneo ya teknolojia zinazoibukia ikiwemo eneo la matumizi ya akili mnemba. Kati ya watumishi 500, watumishi 20 tayari wameanza masomo ya kozi ya muda mrefu na nafasi 480 zilizobaki tayari Serikali imetangaza nafasi hizo na mchakato wa kupokea maombi unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeanza taratibu za ujenzi wa chuo mahiri cha TEHAMA kitakachojengwa Nala Dodoma kwa lengo la kuzalisha wataalam watakokidhi mahitaji yaliyopo kwa sasa ikiwemo hitaji la akili mnemba. Ujenzi wa chuo hiki unaenda sambamba na ujenzi wa vituo vya ubunifu vinane kwenye maeneo ya Dodoma, Dar es Salaam, Mwanza, Tanga, Mbeya, Arusha, Lindi pamoja na Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha Wizara imeboresha sera ya TEHAMA ya mwaka 2016 kwa kuandaa rasmu mpya ya sera ya

mwaka 2024 ambayo itajumuisha maeneo ya akili mnemba. Sambamba na hilo Wizara imekamilisha mkakati wa miaka 10 ya uchumi wa kidigiti unaoainisha maeneo muhimu ya matumizi ya akili mnemba katika kuchangia ukuaji wa uchumi wa kidigitali. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Festo Sanga.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza niipongeze Serikali kwa hatua hizi ambazo imeanza kuzichukua kwa ajili ya kufanikisha kupata watumishi lakini kupata vyuo ambavyo vitasaidia kwenye kuhakikisha kwamba suala la *artificial intelligence* kwa maana ya akili mnemba linapewa nafasi yake na umakini wake katika nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu ni moja tu, kwa wakati huu ambao Taifa letu na dunia imekuwa ikipitia changamoto zinazotokana na mambo ya *artificial intelligence*, tumeona kuna viongozi na tumeona kuna watumishi na watanzania na watu mbalimbali wakichafuliwa kwa kutumia teknolojia hii. Ni upi mkakati wa Serikali wa haraka ili watanzania wengi wapate elimu kuhusu hili jambo kabla ya madhara makubwa hayajawa *especial* kwa wakati huu ambapo Taifa linaelekea kwenye uchaguzi watu wasije wakatumia kitu hiki kuendelea kuchafua watu na baadaye wakakosa haki zao za kimsingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni upi mkakati wa Serikali? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Sanga, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati wa Serikali kama ambavyo nimejibu katika majibu ya msingi ni suala la kisera na la kisheria. Hata nchi za *G7* mwaka 2018 kule Quebec walikaa na kutathmini kuona madhara makubwa yatakayo sababishwa na *artificial intelligence* kwa Kiswahili akili mnemba au unaweza ukasema akili bandia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili mwaka 2018 walipitisha baada ya *IMF* kutoa taarifa ya madhara makubwa katika upande wa *cyber financial analysis* ambayo ilisababisha upotevu wa fedha takribani dola bilioni 100 mpaka dola bilioni 250. Sasa baada ya kugundua hilo ikabidi wapitie sera zao na sheria ili wajue kwamba hili kosa litatambulika vipi na ili tuchukuwe hatua gani za kisheria kwa sababu huwezi ukachukua, huwezi ukasema kwamba hili ni kosa bila ya kuliweka kwenye sera na bila kuliweka kwenye sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua zipi ambazo tunazichukua kama Serikali za dharura kuhakikisha kwamba Watanzania wanajua ili wasiingie kwenye changamoto hizo. Kazi kubwa ambayo inafanywa na Serikali ya Awamu ya Sita ya Dkt. Samia Suluhu Hassan, tunaanzisha mkakati wa kutoa elimu kwa umma ili waweze kutambua madhara ambayo yanaweza yakatokana na akili mnemba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, akili mnemba ina *offensive* na ina *defensive*. Tunachokifanya ni kuhakikisha kwamba tunawapa elimu kuhusiana na *offensive side* isije ikaleta madhara kwao. Kwa hiyo, huo ndiyo mkakati mkubwa ambao lakini unaenda sambamba sasa na kuhakikisha kwamba tunaisuka sera yetu ya TEHAMA ya mwaka 2016 ikiunganisha na teknolojia zingine zinazoibukia ikiwemo akili mnemba. Kuna *internet offence*, kuna *big data analysis* lakini pia kuna *cyber security* haya yote lazima tuyaweke kwenye sera yetu ili tukaweke sheria ambazo zitatusaidia kuchukua hatua stahiki. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Oliver Semuguruka.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kuniona. Serikali ina mpango gani wakupunguza upotevu wa fedha za mitandaoni kwa kutumia akili mnemba? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Oliver, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nimejibu katika swali la msingi, katika jibu langu la msingi. Serikali ipo katika mkakati wa kuboresha sera yake pia tunatengeneza miongozo ambayo itasaidia kwa sababu *artificial intelligence* inaweza ikatumika kwenye *cyber security, artificial intelligence* inaweza ikatumika kwenye *big data analysis, artificial intelligence* inategemea ni matumizi gani ambayo wewe unayahitaji. Serikali tunaenda kuyaangalia katika upana wake na kuyaweka kwa pamoja ili tuhakikishe kwamba *artificial intelligence* ikatumike kwa faida na siyo kwa kuleta madhara. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na sasa nimwite Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake. *(Makofi)*

Na. 136

**Mgogoro wa Shamba la Gereza Mollo**

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itamaliza Mgogoro wa Shamba la Gereza la Mollo – Rukwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika miaka ya nyuma kabla ya mwaka 2018 kulikuwepo na mgogoro wa mipaka ya ardhi kati ya gereza la kilimo Mollo na vijiji vya Msanda, Muungano, Malonje, Songambele na Sikaungu vinavyopakana na gereza hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikao cha Tarehe 24 mwezi Novemba 2023 kilichowahusisha Mheshimiwa Jerry William Silaa, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere Mkuu wa Mkoa wa Rukwa na wataalamu wa ardhi kilimaliza mgogoro uliyokuwepo kati ya Gereza la Mollo na vijiji husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kumaliza mgogoro huu ilikubalika na pande zote kwamba Jeshi la Magereza libakie na eneo lenye ukubwa wa ekari 8,989.4 na vijiji vibakie nae neo lenye ukubwa wa ekari 1,800. Baada ya makubaliano hayo Jeshi la Magereza lilipima na kubainisha mipaka ya eneo lake huku vijiji pia vikitambua maeneo yao. Hivyo kwa sasa hakuna mgogoro tena baina ya Gereza la Mollo na vijiji vinavyopakana nalo. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata.

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nishukuru kwa majibu ya Serikali lakini kimsingi mgogoro huu bado haujaisha na juzi Mwenezi wa Taifa *Comrade* Makonda, alikuja katika Mkoa wa Rukwa, wananchi wale waliandamana wakishika mabango kwamba wanaomba awaunganishe na Mheshimiwa Rais ili awasaidie kutatua mgogoro huu. Kwa hiyo mgogoro huu bado kabisa ni mbichi wananchi wamelima mashamba na wanakatazwa kwenda kupalilia mahindi yao. *(Makofi)*

Je, ni lini sasa Serikali itamaliza mgogoro huu?

Swali la pili, Mheshimiwa Waziri upo tayari kuongozana na mimi Bunge hili likiisha ili uweze kwenda kujionea hali halisi ilivyo? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nipokee malalamiko ya Mheshimiwa Mbunge, kama wapo wananchi ambao wameendelea kulalamika kwamba kuna tatizo la mpaka tutafuatilia kwa karibu ili kuona hatma yake. Kwa vile ameomba niongozane naye naweka ahadi mbele yako kwamba baada ya Bunge hili tutaongozana pamoja na wataalam wa Jeshi la Magereza ili kwenda kujiridhisha ni kitu gani kipo ili tuweze kuumaliza kabisa. Nashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nimemuona Mheshimiwa Dorothy Kilave na Mheshimiwa Yahaya Massare

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa kuwa Gereza la Keko lipo katikati ya makazi ya watu katika Jimbo la Temeke na linaleta migogoro sana kwa baadhi ya nyumba ambazo zinazunguka gereza hilo.

Je, nini mkakati wa Serikali kulihamisha gereza lile kutoka Keko? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Gereza la Keko kama lilivyo kwa sasa Dar es Salaam limezungukwa sana na wananchi na tunatambua hizo changamoto anazozisema. Kwa wakati huu ambapo bado Wilaya ya Temeke halijapata eneo lingine la kulihamishia gereza hilo na hivyo kuliingiza kwenye mpango wetu wa ujenzi wa gereza jipya. Niwaombe wananchi Jeshi la Magereza ni sehemu ya chombo cha wananchi kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya kikatiba hayo ya kuhifadhi wenzetu wanao tuhumiwa na kuhifadhiwa kule kwa makosa mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba waishi nao kwa mahusiano mema kabla hatua ya kulihamisha gereza hilo kuliweka eneo la mbali kabisa na makazi ya wananchi. Nashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Yahaya Massare.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Polisi waliopo Itigi wana mgogoro na Shirika la Reli ambalo linajiimarisha sasa na Wizara yake imekuwa na ahadi nyingi kujenga Kituo cha Polisi Itigi, Mheshimiwa Naibu Waziri, mara nyingi tumeongea kuhusu hili. Je, ni lini sasa mtaenda kujenga Kituo cha Polisi kwa ajili ya Polisi wazuri ambao wapo katika Halmashauri ya Itigi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua na nimshukuru kwa kweli Mheshimiwa Mbunge, kwa namna anavyofuatilia umuhimu wa kuwa na Kituo cha Polisi chenye hadhi ya Wilaya eneo la Itigi. Nimuahidi tu kwamba kwa vile Eneo la Itigi tayari tumeliweka kwenye mipango yetu avumilie pale Wizara ya Fedha itakapokuwa imetupatia fedha kwa ajili ya kujenga Kituo hicho cha Polisi tutakuwa tumemaliza kabisa mgogoro huo. Nashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu hayo ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, muda wetu wa maswali umefikia mwisho niwapongeze sana kwa kuuliza maswali ya nyongeza mafupi ambayo yamewapatia Wabunge wengi kupata nafasi ya kuuliza kwa wakati uleule naamini tutaendelea hivyo hivyo.

Waheshimiwa Wabunge, sasa ni wakati wa matangazo na nitaanza na matangazo ya wageni waliopo Bungeni asubuhi hii; kwanza tunaanza na wageni ambao wapo kwenye Jukwaa la Mheshimiwa Spika, kuna mgeni wa Mheshimiwa Waziri Mkuu,

Ndugu Asha Nassoro Masoud kutoka Dar es Salaam, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wanne wa Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Kagera, Viongozi wa CCM na Serikali kutoka Mkoa wa Kagera, Dkt. Toba Nguvila, Katibu Tawala Mkoa wa Kagera, Ndugu Nazir Karamagi Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Kagera; Ndugu Karim Amri, Mwenezi Mkoa wa Kagera; na Ndugu Christopher Pallangyo Katibu wa CCM Mkoa wa Kagera, karibuni sana wageni wetu kutoka Mkoa wa Kagera. *(Makofi)*

Tunaye pia mgeni wa Mheshimiwa Mbunge Zuberi Kuchauka ambaye ni Mkuu wa Wilaya ya Liwale kutoka Mkoa wa Lindi, Mheshimiwa Goodluck Mlinga, karibu sana Mheshimiwa Goodluck Mlinga Mbunge mstaafu wa Bunge la Kumi na Moja, karibu sana katika Bunge letu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni tisa wa Mheshimiwa Mbunge Janejelly Ntate kutoka Chama cha Wafanyakazi Serikalini na Afya *(TUGHE)* Taifa; tuna Dkt. Jane Madete, Ndugu Catherine Katete, Mwenyekiti wa Kamati ya Wanawake *TUGHE* Taifa; Ndugu Nsubis Mwasandende, Afisa *TUGHE* Taifa; Ndugu Dominucus Nyonyi, Mwenyekiti wa *TUGHE* Taifa; Ndugu Yunge Kanuda. Afisa Habari wa Uhusiano *TUGHE* Taifa; Maulid Kipeneku Mwenyekiti *TUGHE* Mkoa wa Dodoma; Dkt. Leonia Msafiri, Mwenyekiti wa Kamati ya Wanawake *TUGHE* Mkoa wa Dodoma; Redempta Kisima, Katibu wa Kamati ya Wanawake *TUGHE* Mkoa wa Dodoma; na Odile Juma mfanyakazi wa *TUGHE*, karibuni sana ndugu zetu kutoka *TUGHE*. *(Makofi)*

Pia leo tunao wageni wa Waheshimiwa Wabunge, kuna wageni wanne wa Mheshimiwa Mbunge George Simbachawene, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ambao ni Mwenyekiti wa UWT, Katibu wa UWT na Madiwani Viti Maalum kutoka Jimbo la Kibakwe, Mkoa wa Dodoma, karibuni sana wageni wetu wa Mheshimiwa Simbachawene. *(Makofi)*

Tuna wageni 98 wa Mheshimiwa Dkt. David Mathayo, Wenyeviti wa Matawi wa CCM kutoka Same Magharibi Mkoa wa

Kilimanjaro, karibuni sana wageni wetu kutoka Same Magharibi. Karibuni sana wageni wa Mheshimiwa David Mathayo katika Bunge letu. *(Makofi)*

Pia tuna wageni 65 wa Mheshimiwa Anne Malecela ambao ni viongozi wa Chama cha Mapinduzi kutoka Same Mashariki Mkoa wa Kilimanjaro, karibuni sana wageni wa Mheshimiwa Anne Kilango Malecela katika Bunge letu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni kumi wa Mheshimiwa Mariam Ditopile ambao ni Wajumbe wa Kamati ya Utekelezaji ya UWT Wilaya ya Kondoa - Mkoa wa Dodoma, karibuni sana wageni wetu wa Mheshimiwa Mariam kutoka Wilaya ya Kondoa huko Mkoa wa Dodoma. *(Makofi)*

Tuna wageni wa tatu wa Mheshimiwa Hussein Nassor Amar ambao ni rafiki zake kutoka *Emirates Saloon* kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana wageni wetu kutoka *Emirates Saloon* ya hapa Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Tuna wageni watano wa Mheshimiwa Rashid Shangazi ambao ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuuu cha Dodoma *(UDOM),* karibuni sana wanafunzi wetu kutoka huko *UDOM. (Makofi)*

Tuna mgeni wa Mheshimiwa Khalifa Mohamed Issa, mtoto wake kutoka Mjini Magharibi Zanzibar, karibu sana mtoto wetu kutoka huko Mjini Magharibi, Zanzibar. *(Makofi)*

Tuna wageni wawili wa Mheshimiwa Dkt. John Pallangyo, wapiga kura kutoka Meru, Mkoa wa Arusha, karibuni sana wageni kutoka huko Arusha. *(Makofi)*

Tuna mgeni wa Mheshimiwa *Bishop* Josephat Gwajima ambaye ni Mwenyekiti wa CCM Tawi la Kisauke kutoka Kata ya Wazo, Mkoa wa Dar es Salaam, karibu sana mgeni wetu wa Mheshimiwa *Bishop. (Makofi)*

Tuna wageni watano wa Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi ambao ni viongozi wa Kampuni za Kandarasi kutoka Mgodi wa Dhahabu wa Ulyanhulu uliopo Msalala, Wilaya ya Kahama Mkoa

wa Shinyanga, karibuni sana wageni hao kutoka huko Ulyanhulu. *(Makofi)*

Tuna mgeni wa Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi ambaye ni kaka yake na Mfanyakazi wa Benki ya *NMB* kutoka Tunduma, Mkoa wa Songwe, karibu sana. *(Makofi)*

Pia tuna wanafunzi 88 na walimu tisa wa Shule ya Msingi Shalom kutoka Jijijni Arusha, karibuni sana, wanafunzi wetu kutoka Jijini Arusha. *(Makofi)*

Kwa ujumla wageni wote tunawakaribisha katika Bunge letu, karibuni sana. *(Makofi)*

Katibu tuendelee.

**NDG. ZAINAB ISSA - KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA KAMATI

### Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2023

**MWENYEKITI:** Sasa ninawita Mheshimiwa wa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge Ardhi, Maliasili na Utalii kwa ajili ya kuwasilisha Taarifa ya Kamati, karibu sana Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Timotheo Mnzava. *(Makofi)*

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu ili niwasilishe Taarifa hii ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 136(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba sasa kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii…

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tutulie tumsikilize Mwenyekiti.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA – MWENYEKITI WA KAMATI YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu shughuli zilizotekelezwa na Kamati kwa kipindi cha kuanzia Februari, 2023 hadi Januari, 2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea ninaomba Taarifa yangu yote iingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge kama tulivyowasilisha leo asubuhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu nne kama ifuatavyo:-

(i) Sehemu ya Kwanza inatoa Utangulizi.

(ii) Sehemu ya Pili inafafanua namna Kamati ilivyotekeleza majukumu yake na yaliyobainika wakati wa utekelezaji huo.

(iii) Sehemu ya Tatu inatoa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati.

(iv) Sehemu ya Nne inahitimisha Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli zilizotekelezwa na uchambuzi wa yaliyobainika; katika kipindi cha kuanzia Februari, 2023 hadi Januari, 2024 Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii ilifanikiwa kutekeleza majukumu yake kama yalivyoanishwa katika kifungu cha 7(1) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yaliyotokana na Taarifa ya mwaka ya Shughuli za Kamati kwa 2022/2023; katika taarifa ya mwaka ya shughuli za Kamati iliyowasilishwa Bungeni mwezi Februari, 2023 Kamati ililiomba Bunge lako Tukufu kukubali na kuridhia mapendekezo mbalimbali kwenye sekta za Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na ile ya Maliasili na Utalii kuwa maazimio ambayo yangetekelezwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inalishukuru Bunge lako Tukufu, kwani kwa kauli moja liliridhia mapendekezo yaliyowasilishwa na hivyo kuwa maazimio ya Bunge. Kamati ilipata muda wa kufuatilia utekelezaji wa maazimio hayo na kupokea taarifa ya utekelezaji kutoka Serikalini katika sekta inazozisimamia kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Maliasili na Utalii; Bunge lilitoa maazimio kumi ambayo yalitakiwa kutekelezwa na Serikali katika Sekta ya Maliasili na Utalii. Napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba maazimio manne yalitekelezwa kikamilifu na maazimio mawili yapo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inasikitika kulitaarifu Bunge kuwa Serikali haikutekeleza kabisa maazimio manne kama ilivyoagizwa na Bunge lako Tukufu. Aidha, maazimio hayo ni pamoja na kushindwa kuandaa Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Wanyamapori Tanzania *(TAWA);* kushindwa kukamilisha mchakato wa kuipandisha hadhi Wakala wa Misitu Tanzania *(TFS*) kuwa Mamlaka; kushindwa kuanzisha mchakato wa kuhuisha sera zilizopitwa na wakati; na kushindwa kuchukua hatua za haraka kwa wawekezaji wa *lodge* na hoteli ambao wamekiuka masharti ya mikataba yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua ya Wizara ya Maliasili na Utalii kutotekeleza Azimio hili inaweza kuleta hisia kwamba wapo baadhi ya watendaji ndani ya Serikali wanaonufaika na udhaifu wa kitaasisi wa Wakala wa Misitu Tanzania *(TFS)* na Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania *(TAWA)*. Hisia hizi zinazotokana na ukweli kwamba pendekezo la kubadili, na kutunga sheria zilizoanzisha taasisi hizi linalenga kuzifanya Taasisi hizi kujitegemea na kuongeza ufanisi katika utendaji na uwajibikaji wa moja kwa moja kama zilivyo taasisi zingine zilizo chini ya Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, azimio lingine la Bunge lilitaka Serikali kuhakikisha taasisi za *TANAPA, NCAA* na *TAWA* zinabakiza kiasi cha asilimia 30 ya makusanyo yao na kiasi kingine kwenda Mfuko Mkuu wa Serikali. Msingi wa azimio hili ni kwamba hali ilivyo sasa, kiasi chote cha makusanyo ya taasisi hizi huenda Mfuko

Mkuu wa Serikali, kwa sababu hiyo, taasisi hizi hutegemea fedha za mishahara, matumizi mengineyo na miradi ya maendeleo kutoka Serikalini. Hali hii inachangia kuzorota kwa shughuli za taasisi hasa kwa aina ya kazi zake ambazo ni kazi zinazohitaji fedha kwa haraka ili kuhakikisha zinatengeneza miundombinu yao kukidhi mahitaji ya watalii nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu azimio hili, Serikali ilieleza kuwa imeona umuhimu wa hoja hii na kuanzisha akaunti maalumu *(Escrow Account)* ambayo itakuwa inatoa asilimia sita ikiwa na maana kuwa asilimia tatu kwa ajili ya uhifadhi na asilimia tatu kwa ajili ya kutangaza utalii kupitia taasisi hizi. Fedha hizi zitawekwa katika akaunti hiyo na taasisi hizi zitatakiwa kuorodhesha mahitaji yake na kuyapeleka hazina kwa ajili ya matumizi ya fedha hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uchambuzi wake Kamati ilibaini kuwa wazo hili la Serikali linatoa mwanya wa fedha za umma kuchezewa kwani halitokani na mpango wa bajeti, halitokani na sheria yoyote ile wala ushauri wa Bunge. Utaratibu wa kufungua akaunti maalum *(Escrow Account)* hufanyika pale kunapokuwa na mgogoro wa pande mbili juu ya mgawanyo wa mapato ya fedha zao ambapo pande hizo hutunza fedha hizo katika akaunti hiyo hadi pale suluhu ya mgogoro huo itakapopatikana. Swali la kujiuliza, je, kuna mgogoro wa mgawanyo wa mapato kati ya taasisi hizi na Hazina? Na kama hakuna, kwa nini Hazina waje na wazo la kufungua *Escrow Account?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Ardhi, Nyumba na Makazi**;** katika sekta hii, Kamati ilitoa mapendekezo nane ambayo Bunge lako Tukufu liliridhia na kuwa Maazimio ya Bunge. Katika maazimio hayo, Kamati inapenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa Serikali imetekeleza kwa ukamilifu maazimio manne na maazimio mengine manne yapo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Aidha, maazimio yaliyo katika hatua mbalimbali za utekelezaji ni kama yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, kushughulikia mchakato wa kutokuwepo kwa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba katika kila

Wilaya nchini; pili, taasisi na mashirika ya umma kutokulipa kodi ya pango; tatu, kuhuishwa kwa sera mbalimbali zilizopitwa na wakati; na nne, kuanzishwa kwa Mamlaka ya Kusimamia Sekta ya Nyumba nchini *(Real Estate Regulatory Authority)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inapenda kuisisitiza Serikali kukamilisha mchakato huo ili maazimio yawe yametekelezwa kwa ukamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo; ili kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii ilipata nafasi kufanya ziara ya kukaguzi wa miradi ya maendeleo ipatayo sita katika mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kushughulikia bajeti za Wizara; Kamati ilitekeleza jukumu hili la kuchambua na kupitia bajeti za Wizara zote mbili na taasisi zake. Jukumu hili ni kwa mujibu wa Kanuni ya 117(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa Bajeti kwa kipindi cha nusu mwaka; Kamati ilipata fursa ya kuchambua utekelezaji wa bajeti za Wizara zote mbili kwa kipindi cha nusu mwaka kuanzia Julai hadi Disemba, 2023. Katika uchambuzi huo, Kamati ilijikita katika kuangalia ukusanyaji wa maduhuli na fedha zilizopokelewa na Wizara na Taasisi zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Wizara ya Maliasili na Utalii - Fungu Namba 69; hadi kufikia tarehe 30 Disemba, 2023 Wizara na taasisi zake ilikuwa imefanikiwa kukusanya kiasi cha shilingi 572,905,619,470.92 sawa na asilimia 64.88 ya lengo la makusanyo kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande mwingine hadi kufikia tarehe 30 Disemba, 2023 Wizara na taasisi zake ilikuwa imepokea kiasi cha shilingi 272,657,107,509.68 ikiwa ni fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Kiasi hicho ni sawa na asilimia 41.51 ya bajeti yote iliyoidhinishwa na Bunge lako

Tukufu kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Katika fedha hizo kiasi cha shilingi bilioni 242 ni fedha za matumizi ya kawaida sawa na asilimia 49.83 na fedha za maendeleo zilizopokelewa ni shilingi 30,226,324,003 tu sawa asilimia 17.97 ya lengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaomba Wizara ya Fedha kuhakikisha inaongeza kasi ya kutoa fedha za miradi ya maendeleo kwa Wizara na Taasisi zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi - Fungu Namba 48; Wizara ilipanga kukusanya maduhuli kiasi cha shilingi bilioni 300 kutoka vyanzo vyake vya ndani. Hadi kufikia Disemba, 2023 Wizara ilikuwa imekusanya shilingi 76,642,421,871.02 sawa na asilimia 26 tu ya lengo la makusanyo. Mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli ni wa kusuasua na hauridhishi kabisa katika fungu hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yaliyobainika wakati wa ufuatiliaji wa sekta; katika kipindi cha kuanzia Januari, 2023 hadi Februari, 2024 Kamati ilipokea na kujadili taarifa 46 ambapo taarifa 14 ni za Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na taarifa 32 ni za Wizara ya Maliasili na Utalii. Lengo la kupokea na kujadili taarifa hizi ni kuiwezesha Kamati kulisaidia Bunge kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Ibara ya 63(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio na changamoto katika Sekta ya Maliasili na Utalii; Sekta ya Maliasili na Utalii ni sekta mtambuka ambayo imekuwa na mchango mkubwa katika uhifadhi wa mazingira hivyo kutunza ikolojia, uoto wa asili na viumbe hai ambao wapo katika hatari ya kutoweka duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa taarifa uliofanywa na Kamati, umewezesha kubaini mafanikio na changamoto katika utekelezaji wa majukumu ya Sekta ya Maliasili na Utalii kwenye miradi na taasisi zake kama ifuatavyo:-

(a) Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro; Kamati imeridhika na uratibu mzuri wa zoezi hili ambalo ni la hiari na

linalozingatia haki za binadamu ambapo Serikali inawapa huduma zote muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa zoezi hili limeonyesha mwitiko mkubwa toka kwa wakazi wa Ngorongoro kutokana na uhamasishaji uliofanywa na Serikali, ni rai ya Kamati kuwa Serikali ihakikishe inaongeza kasi katika kutekeleza mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori *(TAWA);* Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania *(TAWA)* ilianzishwa ili kusimamia mapori ya akiba, mapori tengefu, jumuiya za hifadhi ya wanyamapori na maeneo ya ardhi oevu ambapo mamlaki hii inasimamiwa na Bodi ya Ushauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania *(TANAPA);* hadi sasa shirika linasimamia hifadhi za Taifa 21 zikiwa na ukubwa wa eneo la kilometa za mraba 96,908.88 sawa na takribani asilimia 10.2%.  ya eneo lote la nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio makubwa ya shirika hili, shirika linakabiliwa na changamoto ya ufinyu wa bajeti ya uendeshaji kwani bajeti ya hifadhi 16 za awali ndio inatumika kuendeshea hifadhi 21, pamoja na kanda nne, vituo vitano vya malikale na ofisi mbili Kiunganishi zilizopo Dar es Salaam pamoja na Dodoma. Hali hii ya ufinyu wa bajeti imechangia kushuka kwa ubora wa huduma zinazotolewa na shirika pamoja na kudorora kwa shughuli za uhifadhi hivyo kupunguza ufanisi katika utendaji wa shirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania *(TAWIRI);* lengo kuu la uanzishwaji wa *TAWIRI* ni kufanya, kuratibu na kusimamia tafiti za wanyamapori hapa nchini. Hata hivyo, taasisi hii inakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa rasilimali fedha inayotokana na ufinyu wa bajeti hali inayoathiri utekelezaji wa majukumu yake kwa ufanisi. Taasisi hii haina jengo la makao makuu tangu ilipoanzishwa mwaka 1980, inakabiliwa na changamoto ya uchakavu wa miundombinu, uhaba wa vifaa vya kisasa katika utafiti na ukosefu wa fedha za sensa za wanyamapori.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya utalii nchini; Sekta ya Utalii imepata takwimu ambazo hazijawahi kufikiwa nchini tangu nchi yetu ipate Uhuru. Watalaamu wa sekta hii nchini wanakiri kuwa hii imetokana na juhudi za Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kuchukua jukumu la kuitangaza sekta hii yeye mwenyewe kwa kuandaa filamu *Tanzania the Royal Tour*. Hadi kufikia mwezi Disemba, 2023 kwa taarifa za hali ya uchumi za robo ya mwisho ya mwaka 2023 *(Quarterly Economic Review)* kutoka Benki Kuu ya Tanzania *(BOT)* watalii waliongia nchini walikuwa takribani 1,790,301 ikiwa ni kiwango cha juu kabisa kuwahi kufikiwa katika sekta hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta hii imeliingizia Taifa fedha za kigeni zaidi ya Dola za Marekani bilioni 3.3 sawa na asilimia 25. Imetoa ajira kufikia 1,600,000 sawa na asilimia 11 ya ajira nchini. Ili kuhakikisha mafanikio haya yanakuwa endelevu, hatuna budi kama Taifa kuwekeza zaidi kwenye sekta ya uhifadhi na kutangaza vivutio vyetu vya utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya Utalii ya nchini; Kamati ilipata nafasi ya kupitia na kuchambua mkakati wa kutangaza vivutio vya utalii nchini, ikiwa ni kufuatilia utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2020/2025 ya kuhakikisha Taifa linafikia lengo la watalii milioni tano kwa kwa mwaka 2025 na fedha za kigeni zaidi ya Dola za Marekani bilioni sita. Kama zilivyo taasisi zingine za Wizara, Bodi ya Utalii inakabiliwa na changamoto ya ufinyu wa bajeti kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jumuiya za Hifadhi za Jamii *(WMAs);* Jumuiya za Hifadhi za Jamii *(WMA)* ni eneo kwenye ardhi ya kijiji au vijiji iliyokubalika na kutengwa kwa misingi ya kuhifadhi wanyamapori na kwa ajili ya biashara inayotokana na uhifadhi huo. Katika Taifa letu, usimamizi wa shughuli za jumuiya hizi unaratibiwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania *(TAWA)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilibaini kuwa baada ya Serikali kuanzisha mfumo wa kupeleka moja kwa moja katika Mfuko Mkuu mapato ya taasisi mbalimbali ikiwemo taasisi za

uhifadhi, mapato ya yatokanayo za *WMAs* nayo yamekuwa yakiingia moja kwa moja katika Mfuko Mkuu wa Serikali na Serikali imekuwa ikuchukua muda mrefu kurejesha kiasi kinachostahili kwenye jumuiya hizo. Hali hii inazorotesha shughuli za uhifadhi katika maeneo hayo kwani, jumuiya hizo huingia gharama katika uhifadhi wa maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio na changamoto katika Sekta ya Ardhi; katika nadharia ya uchumi duniani moja ya nyanja kuu za uzalishaji kwa asili ni ardhi. Ardhi ni rasilimali ya msingi kabisa isiyoweza kuzalishwa kwa jitihada za mwanadamu hata katika mapinduzi makubwa ya teknolojia ambayo dunia imeyashudia. Ardhi ndio inayoanza kujenga familia, jamii na hata Taifa. Ardhi ndio inatafsiri mipaka ya Taifa lolote lile na ndio msingi wa neno nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya ardhi ikiboreshwa itapunguza migogoro ya ardhi kwa kiasi kikubwa na itachangia ufanisi katika sekta zingine za uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio na changamoto katika taasisi na sekta mbalimbali ndani ya Wizara ya ardhi; Tume ya Taifa ta Mipango ya Matumizi ya Ardhi; pamoja na mafanikio haya, Tume hii inakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo upungufu wa rasilimali fedha kuweza kufikia malengo yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Uboreshaji Usalama wa Milki za Ardhi *(LTIP);* Wizara inaendelea kutekeleza Mradi wa *LTIP* ambao unatekelezwa na fedha za mkopo wa Dola za Marekani milioni 150 kutoka Benki ya Dunia katika kipindi cha miaka mitano (2022/2023 - 2027/2028).

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa kupitisha bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Kamati liitoa maoni kuwa Serikali ipitie upya mpango wa matumizi ya fedha za mradi ili kuiwezesha Wizara kutekeleza mpango wa matumizi bora ya ardhi na kuboresha mfumo wa Usimamizi wa ardhi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inapenda kuipongeza Serikali kwa kuzingatia ushauri wake, ambapo iliongeza vijiji kutoka vijiji 500 katika kipindi chote cha utekelezaji wa mradi hadi kufikia vijiji 700 kwa mwaka huu wa fedha. Aidha, jumla ya mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji 404 imeandaliwa kati ya lengo la vijiji 700 vilivyopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ni mafinikio makubwa kwa Wizara na Watanzania na ushahidi wa mchango wa Bunge lako Tukufu na ni kielelezo kuwa kama Serikali itatekeleza vyema ushauri unaotolewa na Bunge lako Tukufu tunaweza kuleta mapinduzi makubwa na kuondoa migogoro katika sekta ya ardhi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maboresho ya mfumo wa usimamizi wa ardhi; Wizara imeanza kuboresha mfumo wa usiamamizi wa ardhi kidijitali ili kuleta ufanisi katika utoaji huduma, kupunguza malalamiko na kutenda haki miongoni mwa wananchi. Hadi Disemba, 2023 mfumo unaojengwa ulikuwa umekamilika kwa asilimia 88 na unatarajia ifikapo mwezi Juni, 2024 mikoa mitano ya Arusha, Tanga, Mbeya, Mwanza, na Dodoma itakuwa imefikiwa na mfumo huo. Mikoa mingine inatarajiwa kufikiwa kwa mwaka wa fedha unaokuja. Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha inatenga fedha za kutosha ili mfumo huu uweze kuanza kazi nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na mapendekezo; maoni ya jumla kuhusu shughuli zitokanazo na Kamati kuanzia mmwezi Februari, 2023 mpaka Januari, 2024 kwenye ukurasa 50 mpaka ukurasa wa 51 wa Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo, maboresho ya eneo la Hifadhi ya Ngorongoro:-

Kwa kuwa, Serikali imepiga hatua nzuri katika kuhakikisha kuwa inainusuru Hifadhi ya Ngorongoro ambayo ilikuwa katika hatari ya kutoweka kutokana na ongezeko kubwa la watu na shughuli zao kinyume na lengo la uanzishwaji wake;

Na kwa kuwa, zoezi linaloendelea la kuhamisha kwa hiari wakazi wanaoishi ndani ya hifadhi hii kuwapeleka maeneo mengine nje ya hifadhi limeonesha mafanikio makubwa baada ya wakazi wengi kukubali kuhama kwa hiari;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba:-

(i) Serikali iongeze kasi katika ujenzi wa nyumba na miundombinu wezeshi ikiwa ni pamoja na kuongeza kasi ya ujenzi wa majosho, malambo na maandalizi ya vitalu ya malisho ya mifugo ili kukamilisha zoezi la kuhamisha wakazi wa Ngorongoro kwa hiari kwa wakati.

(ii) Serikali ihakikishe inaunda timu ya wataalaamu kutoka katika Wizara za kisekta ili kufanikisha uratibu wa zoezi la kuhamisha wakazi wa Ngorongoro kwa hiari.

(iii) Serikali ihakikishe inaendesha zoezi la ujenzi wa miundombinu yote iliyopangwa kwenye maeneo ya Msomera, Kitwai na Saunyi kwa kutumia Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) ambao wameonesha ufanisi wa hali ya juu katika zoezi la ujenzi wa nyumba 5,000 linaloendelea kwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utekelezaji wa bajeti kwenye miradi ya maendeleo kwa Wizara ya Maliasili na Utalii:-

Kwa kuwa, hadi kufikia Disemba, 2023, Wizara na Taasisi zake zilikuwa zimepokea kiasi cha shilingi bilioni 30.2 sawa na asilimia 17.7 tu;

Na kwa kuwa, hali hii inachangia kuzorota na kusuasua kwa utekelezaji wa miradi ya maendeleo, ikiwa ni pamoja na kushindwa kufanya ukarabati wa miundombinu kwenye vivutio vya utalii, kushindwa kutangaza utalii kwenye masoko mapya, kushindwa kukuza na kuendeleza mazao ya utalii;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba, Serikali ihakikishe inaongeza kasi ya kutoa fedha za miradi ya maendeleo

iliyoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Wizara na Taasisi zake ili kutekeleza miradi ya maendeleo iliyopagwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzishwa kwa akaunti maalum *(Escrow Account)* kwa ajili ya kuimarisha uhifadhi na kutangaza utalii:-

kKwa kuwa, kwa kuwa hakuna mgogoro wowote ule wa mgawanyo wa fedha kati Hazina na Wizara ya Maliasili na Utalii na Taasisi zake, ambao ungesababisha kuanzishwa kwa akaunti hii;

Na kwa kuwa, kuanzishwa kwa akaunti hii kutapalekea matumizi ya fedha za umma kushindwa kufanyiwa ukaguzi na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa utaratibu wa kawaida;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba: -

(i) Serikali isitishe mara moja kuanzishwa kwa akaunti hiyo hali inayoweza kupelekea fedha za umma kutumika bila usimamizi na uwajibikaji;

(ii) Serikali ifanye Marekebisho ya Sheria ya Fedha Na. 8 ya mwaka 2020 kwa lengo la taasisi hizi kubaki na sehemu ya makusanyo yake ili kuzisadia taasisi hizi kutekeleza majukumu yake ya uhifadhi kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu changamoto za wanyamapori wakali na waharibifu:-

Kwa kuwa, muingiliano baina ya binadamu na wanyamapori katika kushindania rasimali za asili ikiwa ni pamoja na chakula na maji umekuwa mkubwa;

Na kwa kuwa, muingiliano huo unaathiri shughuli za wananchi na kupelekea uharibifu wa mazao na mali nyingine, ulemavu, na hata kupoteza maisha;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba: -

(i) Serikali ihakikishe inaongeza kasi ya ujenzi wa vituo vya udhibiti wa wanyama wakali na waharibifu nchini ikiwa ni pamoja na kuongeza askari wa uhifadhi ili kupunguza athari kwa wananchi; *(Makofi)*

(ii) Serikali kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii na *TAWIRI* ihakikishe inatafuta teknolojia ya kudhibiti na kukabiliana na changamoto za wanyama wakali na waharibifu;

(iii) Serikali ihakikishe inakamaliisha zoezi la kuongoa Shoroba za Wanyama wakali na waharibifu 18 ilizojipangia katika mwaka wa fedha 2023/2024 ili kupunguza muingiliano wa shughuli za wananchi na wanyama;

(iv) Serikali ihakikishe inafanya marejeo ya Kanuni za Malipo ya Kifuta Jasho na Machozi ya Mwaka 2011 ili kuboresha viwango kwa aliyeathirika na wanyama wakali na waharibifu ili kuendana na hali maisha ya sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutungwa kwa Sheria ya Uendeshaji wa Mamlaka ya Wanyamapori *(TAWA)* na mchakato wa kupandisha hadhi *TFS*:-

Kwa kuwa, Taasisi hizi za Uhifadhi zinaongozwa na Bodi za Ushauri, ambazo zina nguvu ndogo ya uwajibikaji;

Na kwa kuwa, hali hii inaathiri utendaji wa taasisi hizi wa kukokosa nguvu ya kisheria katika kutekeleza majukumu yake;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba: -

(i) Serikali ihakikishe inaandaa na kuleta Bungeni Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Wanyamapori Tanzania *(TAWA)*;

(ii) Serikali iharakishe mchakato wa kuipandisha hadhi Wakala wa Misitu Tanzania *(TFS)* kuwa Mamlaka ili kuipa nguvu ya kisheria ya kusimamia na kudhibiti matumizi ya rasilimali za misitu yote nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutangaza vivutio vya utalii:-

Kwa kuwa, Sekta ya Utalii ina mchango mkubwa katika Uchumi wa Taifa, kwa kuchangia zaidi ya asilimia 25 ya mauzo yote ya nje, huku ikichangia takribani asilimia 20 ya Pato la Taifa na kutoa takribani asilimia 11 ya ajira nchi;

Na kwa kuwa, sekta hii ilianguka kwa kiasi kikubwa kutokana na mlipuko wa janga la UVIKO – 19, huku ikikabiliwa na ushindani mkubwa toka nchi jirani;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba: -

(i) Serikali itekeleze mikakati ya kutangaza utalii chini ya Bodi ya Utalii Tanzania ili idadi ya Watalii izidi kuongezeka na kufikia lengo;

(ii) Serikali ianzishe Mfuko wa Maendeleo ya Utalii *(Tourism Development Fund)* ambao utachangiwa na asilimia moja ya mauzo yote ya nje yanayoingia nchini kutokana na shughuli za utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto za Taasisi za Utafiti za *TAFORI* na *TAWIRI*:-

Kwa kuwa, Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania *(TAFORI)* na Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori *(TAWIRI)* zinakabiliwa na changamoto ya ufinyu wa bajeti na changamoto ya upungufu wa wafanyakazi na vitendea kazi;

Na kwa kuwa, changamoto hizi zinaathiri ufanisi wa taasisi hizo katika kufanya na kusimamia shughuli zake;

Hivyo basi, Bunge linaazimia kwamba: -

(i) Serikali ihakikishe Taasisi hizi zinaongezewa bajeti na kupelekewa fedha kwa wakati ili ziweze kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria;

(ii) Serikali ihakikshe inatoa kibali cha kuajiri kwa taasisi hizi ili kuziba pengo wafanyakazi lililopo kwa sasa hali itakayoongeza ufanisi na tija katika utendaji wa taasisi hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Azimio la Bunge la Kuridhia Mapendekezo ya kurekebisha Mpaka wa Hifadhi ya Taifa ya Ruaha:-

Kwa kuwa, Taifa linahitaji uhifadhi wenye tija ambao ni endelevu usiokuwa na migogoro ya mipaka kati ya maeneo ya hifadhi na ardhi za vijiji;

Na kwa kuwa, utekelezaji wa Azimio hili la Bunge ulilenga kusaidia kulinda mifumo ya ikolojia katika Bonde la Usangu ili kurejesha uoto wa asili kwenye Hifadhi ya Taifa ya Ruaha na kuimarisha mtiririko endelevu wa maji katika Mto Ruaha Mkuu ambao unategemewa katika uzalishaji wa umeme wa maji katika Vituo vya Mtera, Kidatu na Mwalimu Nyerere;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba: -

(i) Serikali itekeleze Azimio la Bunge na masharti yake kama yalivyowasilishwa na Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii na taarifa ya utekelezaji huo iwasilishwe Bungeni kama ambavyo Serikali iliahidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Usimamizi wa Maliasili Endelevu na Ukuaji wa Utalii Kanda ya Kusini:-

Kwa kuwa, mradi umeelekezwa katika Hifadhi za Taifa za Ruaha, Mikumi, Udzungwa, Nyerere na Hifadhi ya Msitu wa Asili wa Kilombero;

Na kwa kuwa, lengo la mradi ni kuhakikisha kuna usimamizi wa Maliasili endeleu na Utalii wa Kanda nzima ya Kusini;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba: -

(i) Katika awamu ya pili ya mradi, Serikali ihakikishe inapanua wigo kwa kuongeza idadi ya hifadhi katika Eneo la

Kusini ili kuchochea utalii katika Kanda ya Kusini ili kuchochea utalii katika Kanda ya Kusini kama lilivyo lengo la mradi;

(ii) Serikali ihakikishe miradi yote inayotekelezwa kupitia *REGROW* inakamilika ndani ya muda ili kukuza utalii wa Eneo la Kusini, kuongeza mapato ya Serikali na kuinua uchumi wa watu wanaoishi kuzunguka karibu na hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori:-

Kwa kuwa, *WMAs* zinafanya kazi kubwa katika uhifadhi kwa kudhibiti ujangili wa wanyamapori na kutatua changamoto ya muingiliano wa binadamu na wanyama;

Na kwa kuwa, utekelezaji wa jukumu hilo unahitaji fedha ambazo zinatokana shughuli zinazofanywa katika *WMAs* ambazo hukusanywa moja kwa moja na Serikali na Serikali imekuwa ikichelewesha kurejesha fedha hizo kwenye *WMAs*;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba: -

(i) Serikali ihakikishe inarejesha kiasi chote za fedha kinachostahili kurejeshwa kwenye *WMAs* kwa mujibu wa Kanuni ili kuziwezesha katika utendaji kazi wake;

(ii) Serikali iandae mpango wa ukusanyaji wa mapato ambao utatofautisha mapato ya Serikali na yale ya *WMAs* ili fedha za Jumuiya hizi ziende moja kwa moja kwenye akaunti zao; *(Makofi)*

(iii) Serikali ishughulikie na kutatua migogoro ya mipaka kati ya maeneo ya hifadhi na *WMAs* mbalimbali nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Mipango ya Matumizi bora ya Ardhi:-

Kwa kuwa, migogoro mingi ya ardhi nchini inasababishwa na ardhi kutokupangiwa matumizi, ambapo hadi sasa ni vijiji 3,681

tu vilivyopangiwa matumizi ya ardhi kati ya vijiji 10,744 vilivyopimwa nchini;

Na kwa kuwa, Kasi ndogo ya upangaji inatokana na ufinyu wa bajeti inayotengwa kwa Tume ya Taifa ya Matumizi ya Ardhi ambayo imepewa jukumu la kupanga matumizi ya ardhi nchi nzima;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba: -

(i) Serikali iongeze kasi ya kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi katika vijiji vyote vilivyopimwa nchini;

(ii) Serikali iendelee kuongeza fedha za maendeleo kwa Tume ili kuhakikisha kila kipande cha ardhi nchini kinapangiwa matumizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maboresho ya Mfumo wa Usimamizi wa Ardhi Nchini:-

Kwa kuwa, Serikali imedhamiria kuboresha mfumo wa Usimamizi wa Ardhi Nchini ikiwa ni utekelezaji wa Azimio la Bunge;

Na kwa kuwa, lengo la kuboresha mfumo huo ni kuhakikisha Serikali inaongeza kasi ya kuwahudumia wananchi, kupunguza migogoro ya ardhi nchini na kupunguza malalamiko ya wananchi katika kupokea huduma toka kwa Watumishi wa Sekta ya Ardhi nchini;

Hivyo basi, Bunge linaazimia kwamba: -

(i) Serikali kuhakikisha Mfumo huo unakuwa rafiki kwa watumiaji na uzinduliwe haraka ili kutimiza malengo yaliyokusudiwa;

(ii) Serikali inatoa elimu ya matumizi ya mfumo kwa wananchi kupitia vituo vya Televisheni, radio na njia mbadala za habari ikiwemo mitandao ya kijamii ili wananchi wengi waufahamu mfumo na kuutumia kwa urahisi hali itakayosababisha lengo la maboresho ya mfumo kufikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Nyumba la Taifa:-

Kwa kuwa, lengo la kuanzishwa kwa Shirika ni kujenga nyumba za makazi na biashara kwa ajili ya kuwauzia wananchi wenye kipato cha hali zote;

Na kwa kuwa, Kumekuwa na malalamiko toka kwa wananchi kuwa Shirika linajenga nyumba zenye gharama za juu bila kuzingatia utofauti wa kipato miongoni mwa wananchi ambayo yanatokana na kodi ya ongezeko la thamani *(VAT)* katika miradi ya Shirika;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba: -

(i) Serikali ilisaidie Shirika kutimiza adhma yake kwa kuondoa kodi ya ongezeko la thamani *(VAT)* kwa nyumba zinauzouzwa kwa bei isiyozidi shilingi milioni 100 badala ya shilingi milioni 50 ya sasa;

(ii) Shirika kuhakikisha linaandaa mpango wa kutoa elimu kwa umma juu ya fursa mbalimbali zitakazowawezesha wananchi wa vipato vya kawaida kumiliki nyumba kupitia miradi ya Shirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupanga, kupima na Kumilikisha Ardhi Nchini:-

Kwa kuwa, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi iliona ni vyema kuzishirikisha Mamlaka za Serikali za Mitaa kurahisisha zoezi hili;

Na kwa kuwa, lengo la Wizara kuzikopesha halmashauri ilikuwa ni kuhakikisha fedha hizi zinazunguka katika halmashauri zote nchini ili kusaidia katika kupanga, kupima na kumilikisha ardhi kwa wananchi;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba: -

(i) Serikali kupitia Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais – TAMISEMI, ihakikishe inazisimamia halmashauri zote kurudisha kiasi cha shilingi bilioni

28.3 walizokopeshwa kwenye mradi huu ili ziweze kutumiwa na Wizara kusaidia maeneo mengine;

(ii) Serikali kupitia Wizara ya Ardhi ihakikishe inakamilisha utekelezaji wa Mfuko wa Mzunguko wa Maendeleo ya Ardhi *(Plot Development Revolving Fund)* ili kuratibu namna bora ya matumizi ya fedha katika Mfuko katika utekelezaji wa Programu ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ukusanyaji wa Maduhuli ya Serikali kupitia Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:-

Kwa kuwa, Serikali iliamua ukusanyaji wa kodi ya pango la ardhi *(Land Rent)* ufanywe na Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini ili kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato yatokanayo na pango la Ardhi;

Na kwa kuwa, uamuzi huo umetoa matokeo hasi hadi kufikia nusu ya kwanza ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2023/2024, kwani hadi kufikia Januari, 2024 hakuna halmashauri yoyote nchini iliyokuwa imekusanya;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba: -

(i) Serikali irudishe jukumu la ukusanyaji wa Kodi ya Pango la Ardhi katika Wizara ya Ardhi, ambayo ndio ina nyezo za kisheria na kimfumo katika kutekeleza jukumu hilo;

(ii) Serikali iiwezeshe kifedha Wizara ya Ardhi ili itimize vyema jukumu la kukusanya kodi hii kwani hadi kufikia Januari, 2024, Wizara imekuwa ikutumia fedha zake za *OC* kwa ajili ya ukusanyaji wa maduhuli;

(iii) Serikali kupitia Wizara ya Ardhi ihakikishe inaongeza nguvu katika kukusanya maduhuli kwani hali ya sasa ya ukusanyaji wa mapato siyo ya kuridhisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ya kulipa fidia katika Ardhi inayotwaliwa na Serikali na wawekezaji:-

Kwa kuwa, nia ya Serikali na wawekezaji katika kutwaa ardhi ni nzuri, kwani inahusisha ujenzi na upanuzi wa miradi ya maendeleo kwa ajili ya wananchi;

Na kwa kuwa, ni takwa la kisheria kuwa wananchi wanaokutwa na miradi ya maendeleo katika ardhi inayotwaliwa ni lazima walipwe fidia stahiki baada ya uthamini kuwa umeidhinishwa na Mthamini Mkuu wa Serikali;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba: -

(i) Serikali ihakikishe kuwa kunakuwa na uthibitisho wa uwepo wa fedha za kulipa fidia ambao utatolewa na Wizara, taasisi mtwaaji au mwekezaji anaekusudia kutwaa ardhi husika. Hii itasadia kuweka msisitizo kuwa kama hakuna fedha za kulipa fidia basi zoezi la utwaaji ardhi lisubiri mpaka fedha za kulipa zitakapopatikana;

(ii) Serikali ihakikishe kuwa kwa kushirikiana na wadau wote muhimu wa utwaaji inafanya Uhakiki kabla ya Mthamini Mkuu kuidhinisha majedwali ya fidia, na kabla ya hatua ya Uoneshaji majedwali hayo kwa wananchi *(Disclosure Stage)* kufanyika, hii itasaidia kurekebisha dosari zote ndani ya muda sahihi na kuhakikisha wananchi wanalipwa kwa wakati; *(Makofi)*

(iii) Serikali ihakikishe mfuko wa Fidia ya Ardhi unasimamiwa na Wizara ya Fedha ili kuwe na mtiririko sahihi wa upatikanaji wa fedha kwa miradi yote inayohusisha Serikali kwa ajili ya fidia hali itakayompa nafasi Mlipaji Mkuu wa Serikali kuweza kuzitaarifu taasisi zote za umma zinazokusudia kutwaa ardhi hakikisho la uwepo wa fedha za fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utatuzi wa migogoro ya ardhi nchini:-

Kwa kuwa, kumekuwa na malalamiko katika utendaji wa Kamati ya Mawaziri nane wa Kisekta katika utatuzi wa migogoro katika vijiji na mitaa 975;

Na kwa kuwa, malalamiko hayo yanaathiri utekelezaji wa utatuzi wa migogoro katika vijiji hivyo na utekelezaji wake umechukua muda mrefu;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba: -

(i) Serikali ihakikishe Kamati hiyo inashirikisha wananchi na wawakilishi wao ili kutatua migogoro katika vijiji na mitaa 975;

(ii) Serikali ihakikishe inakamilisha utekelezaji wa zoezi la kutatua miggogoro hiyo ndani ya wakati uliokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho, kwa namna ya kipekee napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Mafanikio ya Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii katika kutekeleza Shughuli zake kwa kipindi cha Februari 2023 hadi Januari, 2024. Ni wazi kwamba, ufanisi wa utendaji wa Kamati hii unatokana zaidi na mchango mkubwa wa Ofisi ya Bunge, kuwajengea uwezo Wabunge na kuwapa msaada stahiki wa kitaalam na wa kiushauri wakati wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima kubwa ningependa kuwataja majina ya Wajumbe wa Kamati yetu. Hata hivyo, kutokana na ufinyu wa muda naomba majina yao yote yaingizwe kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Naibu wake, Waziri wa Maliasili na Utalii na Naibu wake, Makatibu Wakuu, Naibu Makatibu Wakuu pamoja na Watendaji wote wa Wizara hizo kwa ushirikiano waliouonyesha katika kipindi chote ambacho Kamati imekuwa ikitekeleza majukumu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kueleza shughuli zilizotekelezwa na Kamati, uchambuzi wa matokeo ya utekelezaji shughuli hizo, pamoja na maoni na mapendekezo ya Kamati, sasa naomba kutoa hoja kwamba, Bunge sasa lipokee, lijadili na hatimaye kuikubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya

Ardhi, Maliasili na Utalii pamoja na maoni na mapendekezo yaliyomo katika taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII KUHUSU SHUGHULI ZA KAMATI KWA MWAKA 2023 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**SEHEMU YA KWANZA**

**1.0 UTANGULZI**

**Mheshimiwa Spika**, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu ili niwasilishe taarifa hii ya Kamati. Aidha nitumie nafasi hii, kuwashukuru wajumbe wa Kamati kwa namna walivyojitoa kikamilifu kutekeleza majukumu yao kwa moyo na weledi mkubwa na hivyo kuwezesha Kamati kukamilisha taarifa kwa wakati na ufanisi.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 136 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba sasa kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2023. Taarifa hii inawasilisha Shughuli zilizotekelezwa na kamati kuanzia Februari 2023 hadi Januari, 2024.

**Mheshimiwa Spika**, taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu nne (4) kama ifuatavyo:-

i) Sehemu ya Kwanza inatoa Utangulizi wenye kueleza Muundo na Majukumu ya Kamati, na kuanisha shughuli zilizotekelezwa na Kamati;

ii) Sehemu ya Pili inafafanua namna Kamati ilivyotekeleza Majukumu yake na yaliyobainika wakati wa utekelezaji huo;

iii) Sehemu ya Tatu inatoa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati; na

iv) Sehemu ya Nne inahitimisha taarifa.

### 1.1 Muundo na Majukumu ya Kamati

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii ni miongoni mwa Kamati za Kisekta za Bunge lako Tukufu. Muundo wa kamati hii unajumuisha aina mbalimbali za Wabunge kama inavyoelekezwa na kanuni ya 135(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023.

Aidha, Kwa mujibu Kifungu cha 6(8) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, Kamati hii ina jukumu la kusimamia shughuli za Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi pamoja na Wizara ya Maliasili na Utalii.

**Mheshimiwa Spika,** Majukumu ya Kamati za Kisekta, yamebainishwa katika Kifungu cha 7 (1) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Majukumu hayo ni kama ifuatavyo: -

a) Kushughulikia Bajeti za Wizara au Taasisi inazozisimamia;

b) Kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara inazozisimamia;

c) Kushughulikia Taarifa za Utendaji za kila Mwaka za Wizara hizo; na

d) Kufuatilia Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara hizo.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kulijulisha Bunge lako tukufu kwamba Kamati yangu imetekeleza kikamilifu wajibu wake katika kuzingatia matakwa ya Kanuni hiyo.

### 1.2 Msingi wa Utekelezaji wa Shughuli za Kamati

**Mheshimiwa Spika,** msingi wa utekelezaji wa majukumu ya Kamati umejengwa katika dhana ya Kikatiba kupitia ibara ya 8(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977. Kwa mujibu wa ibara hiyo, lengo kuu la Serikali ni ustawi wa

wananchi. Ibara ya 62 na 63 zinasisitiza juu ya Wananchi kushiriki katika shughuli za Serikali yao kupitia chombo chao cha Uwakilishi ambacho ni Bunge. Katika ibara ya 96, Katiba inaelekeza Bunge kuunda Kamati mbalimbali ili kurahisha majukumu yake ya kuisimamia na kuishauri Serikali. Hivyo, basi Kamati inapotekeleza majukumu yake inafanya kwa niaba ya Bunge zima na wananchi kwa ujumla katika kuhakikisha Serikali inatimiza wajibu wa kuleta ustawi wa watu wake.

### 1.3 Njia na Mbinu Zilizotumika

**Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha shughuli za Kamati, zinatekelezwa kikamilifu, kwa ufanisi na kwa mujibu wa Katiba, huku tukizingatia Kanuni za Kudumu za Bunge na kuhakikisha ustawi wa wananchi ambao ndio tunaowawakilisha, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii ilitumia mbinu na njia mbalimbali katika kutekeleza majukumu yake. Njia hizo ni kama zifuatavyo: -

i) Vikao vya kupokea, kuchambua na kujadili Taarifa za Wizara na Taasisi zake kwa lengo la kufahamu utendaji wao, mafanikio na changamoto zinazowakabili wakati wa utekelezaji wa majukumu yao;

ii) Ziara za ukaguzi wa maeneo na miradi ya maendeleo kwa lengo la kujiridhisha hatua mbalimbali zilizofikiwa katika utekelezaji wake kwa kulinganisha na taarifa iliyowasilishwa katika vikao vya Kamati; na

iii) Kushiriki mafunzo, semina na warsha mbalimbali kwa lengo la kujifunza na kubadilishana uzoefu na Wizara, Mashirika ya Umma, Taasisi Binafsi, Asasi za Kiraia na wadau wengine katika Sekta zinazosimamiwa na Kamati hii.

**Mheshimiwa Spika**, lengo la kutumia mbinu hizi tofauti ni kuwawezesha wajumbe wa Kamati kujielimisha kwa kiwango cha kutosha katika sekta ambazo wanawajibika kuzisimamia na kuishauri Serikali kwa niaba ya Bunge na wananchi kwa ujumla.

## SEHEMU YA PILI

### 2.0 SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA NA UCHAMBUZI WA YALIYOBAINIKA

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha kuanzia Februari, 2023 hadi Januari, 2024, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii ilifanikiwa kutekeleza majukumu yake kama yalivyoanishwa katika Kifungu cha 7(1) cha Nyongeza ya nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023. Miongoni mwa Shughuli ambazo zilitekelezwa na Kamati katika kipindi hicho ni hizi zifuatazo: -

i. Kufanya Ziara za ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023;

ii. Kupokea, kuchambua na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa bajeti kwa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 na mwelekeo wa bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024;

iii. Kupokea, kuchambua na kujadili Taarifa za Utendaji wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Wizara ya Maliasili na Utalii na Taasisi zinazosimamiwa na Wizara hizo;

iv. Kushughulikia Azimio la Bunge la kuridhia kufutwa kwa Hifadhi ya Taifa ya Kigosi ili kuruhusu kuanzishwa kwa hifadhi ya msitu wa Kigosi;

v. Kushughulikia Azimio la Bunge la kuridhia Kurekebisha Mpaka wa Hifadhi ya Taifa ya Ruaha;

vi. Kukutana na Wadau wa Sekta za Maliasili, Uhifadhi, Utalii, Ardhi na Miliki;

vii. Kushiriki Semina na warsha za Mafunzo; na

viii. Kufuatilia utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yaliyotokana na taarifa ya mwaka ya kamati.

## 2.1 Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yaliyotokana na Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati kwa 2022/2023

**Mheshimiwa Spika,** katika taarifa ya mwaka ya shughuli za Kamati iliyowasilishwa Bungeni mwezi Februari, 2023 Kamati ililiomba Bunge lako Tukufu kukubali na kuridhia mapendekezo mbalimbali kwenye sekta za Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na ile ya Maliasili na Utalii kuwa maazimio ambayo yangetekelezwa na Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inalishukuru Bunge lako Tukufu, kwani kwa kauli moja, liliridhia mapendekezo yaliyowasilishwa na hivyo kuwa maazimio ya Bunge. Kamati ilipata muda wa kufuatilia utekelezaji wa maazimio hayo na kupokea taarifa ya utekelezaji kutoka Serikalini katika sekta inazozisimamia kama ifuatavyo: -

### 2.1.1 Sekta ya Maliasili na Utalii

**Mheshimiwa Spika**, Bunge lilitoa maazimio kumi (10) ambayo yalitakiwa kutekelezwa na Serikali katika Sekta ya Maliasili na Utalii. Napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba, maazimio manne (04) yalitekelezwa kikamilifu na maazimio mawili (02) yapo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inasikitika kulitaarifu Bunge kuwa Serikali haikutekeleza kabisa maazimio manne (4) kama ilivyoagizwa na Bunge lako Tukufu. Aidha, maazimio hayo ni pamoja na Kushindwa kuandaa Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Wanyamapori Tanzania (TAWA); Kushindwa kukamilisha mchakato wa kuipandisha hadhi Wakala wa Misitu Tanzania (TFS) kuwa Mamlaka; Kushindwa kuanzisha Mchakato wa kuhuisha Sera zilizopitwa na wakati; na Kuchukua hatua za haraka kwa wawekezaji wa Loji na Hoteli ambao wamekiuka masharti ya mikataba ikiwa ni pamoja na kuharakisha mchakato wa kuzirejesha Serikalini na kuzitafutia wawekezaji wenye uwezo wa kuzihudumia.

**Mheshimiwa Spika,** huko nyuma katika vikao vya Kamati na Wizara ya Maliasili na Utalii, mara kadhaa Serikali imekuwa ikiiambia Kamati kuwa wapo katika hatua mbalimbali za kubadili sheria, kutunga sheria mpya na kuhuisha sera ambazo hata wao

kama Wizara wanakiri zimepitwa na wakati. Wakati wa kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa maazimio ya Bunge, Kamati ilipohoji kwanini Azimio hili halikutekelezwa, Serikali kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii iliitarifu Kamati kuwa bado inaamini sheria na sera zilizopo zinafaa kwa mazingira ya sasa, hivyo Azimio la Bunge litaendelea kuzingatiwa kwa kadiri ya mahitaji ya wakati, kinyume na msimamo wao wa awali.

**Mheshimiwa Spika,** hatua ya Wizara ya Maliasili na Utalii kutotekeleza Azimio hili inaweza kuleta hisia kwamba wapo baadhi ya watendaji ndani ya Serikali wanaonufaika na udhaifu wa Kitaasisi wa Wakala wa Misitu Tanzania (TFS) na Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA). Hisia hizi zinazotokana na ukweli kwamba pendekezo la kubadili, na kutunga sheria zilizoanzisha Taasisi hizi linalenga kuzifanya Taasisi hizi kujitegemea na kuongeza ufanisi katika utendaji na uwajibikaji wa moja kwa moja kama zilivyo taasisi zingine za Uhifadhi chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii kama vile Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) na Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (NCAA).

**Mheshimiwa Spika,** azimio lingine la Bunge lililitaka Serikali kuhakikisha taasisi za TANAPA, NCAA na TAWA zinabakia (retain) na kiasi cha **asilimia 30** ya makusanyo yao, na kiasi kingine kwenda mfuko mkuu wa Serikali. Msingi wa azimio hili ni kwamba hali ilivyo sasa, kiasi chote cha makusanyo ya taasisi hizi huenda mfuko mkuu wa Serikali. Kwa sababu hiyo, Taasisi hizi hutegemea fedha za mishahara, matumizi mengineyo (OC) na miradi ya maendeleo toka Serikalini. Hali hii inachangia kuzorota kwa shughuli za taasisi hasa kwa aina ya kazi zake ambazo ni kazi zinazohitaji fedha kwa haraka ili kuhakikisha zinatengeneza miundombinu yao kukidhi mahitaji ya watalii.

**Mheshimiwa Spika,** Kuhusu Azmio hili, Serikali ilieleza kuwa imeona umuhimu wa hoja hii na kuanzisha akaunti maalumu **(escrow account)** ambayo itakuwa inatoa **asilimia 6** ikiwa na maana kuwa **asilimia 3** kwa ajili ya uhifadhi na **asilimia 3** kwa ajili ya kutangaza utalii kupitia taasisi hizi. Fedha hizi zitawekwa katika akaunti hiyo na taasisi hizi zitatakiwa kuorodhesha mahitaji yake na kuyapeleka hazina kwa ajili ya matumizi ya fedha hizi.

**Mheshimiwa Spika,** katika uchambuzi wake Kamati ilibaini kuwa wazo hili la Serikali linatoa mwanya wa fedha za umma kuchezewa kwani halitokani na mpango wa bajeti, sheria yoyote ile wala ushauri wa Bunge. Utaratibu wa kufungua akaunti maalum (Escrow account) hufanyika pale kunapokuwa na mgogoro wa pande mbili juu ya mgawanyo wa mapato ya fedha zao, ambapo pande hizo hutunza fedha hizo katika akaunti hiyo hadi pale suluhu ya mgogoro huo itakapopatikana. Swali la kujiuliza, Je, kuna mgogoro wa mgawanyo wa mapato kati ya taasisi hizi na Hazina? Na kama hakuna, kwa nini Hazina waje na wazo hili?

**Mheshimiwa Spika,** fedha zinazokuwa kwenye akaunti hii maalumu hata ukaguzi wa matumizi yake huwa sio wa kawaida. Kamati inaona suluhu pekee ya kushughulika na matatizo ya taasisi hizi za Uhifadhi, ni kuhakikisha wanabaki na sehemu ya fedha wanazokusanya kwa ajili ya taasisi hizi kujiendesha kwa ufanisi kwa kuzingatia aina na mazingira ya kazi zao. Hii itahakikisha kuwa matumizi ya fedha hizi ambazo ni fedha za Umma zinakaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

**2.1.2 Sekta ya Ardhi, Nyumba na Makazi**

**Mheshimiwa Spika,** Katika sekta hii, Kamati ilitoa mapendekezo nane (8) ambayo Bunge lako Tukufu liliridhia na kuwa maazimio ya Bunge. Katika maazimio hayo, Kamati inapenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa Serikali imetekeleza kwa ukamilifu maazimio manne (4) na maazimio mengine manne (4) yapo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Aidha, maazimio yaliyo katika hatua mbalimbali za utekelezaji ni kama yafuatayo; kutokuwepo kwa mabaraza ya ardhi na nyumba katika kila Wilaya nchini, taasisi na mashirika ya umma kutokulipa kodi ya pango, kuhuishwa kwa sera mbalimbali zilizopitwa na wakati na kuanzishwa kwa mamlaka ya kusimamia sekta ya Nyumba nchini (Real Estate Regulatory Authority).

**Mheshimiwa Spika,** hadi sasa Serikali imefanikiwa kuanzisha mabaraza **96** ya ardhi na nyumba nchini huku kukiwa na ongezeko la mabaraza **11** tangu Bunge lilipotoa azimio la kuanzisha mabaraza ya ardhi na nyumba katika Wilaya zote

nchini. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuanza kutekeleza azimio hili ambalo linalengo la kusaidia katika kutatua migogoro ya ardhi nchini na kuwahudumia wananchi kwa karibu bila kufuata huduma mbali. Hata hivyo, Kamati inapenda kuisisitiza Serikali kuendelea na utekelezaji wa azimio hili hadi kufikia mabaraza **139** katika Wilaya zote nchini.

**Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi iliijulisha kamati kwamba Sera ya Ardhi ya Mwaka 1995 inahuishwa ili kuendana na wakati wa sasa na tayari ilikwisha ridhiwa na Baraza la Mawaziri huku Sera ya Nyumba na Maendeleo ya Makazi mchakato wake ukiwa umefikia hatua ya kujadiliwa na Kamati ya Wataalam ya Makatibu Wakuu (IMTC). Aidha, mchakato wa kuanzishwa kwa sheria ya Miliki (Real Estate Act) umeanza na upo katika hatua ya Wizara kukusanya maoni ya wadau.
Kamati inapenda kuisisitiza Serikali kukamilisha mchakato huo ili maazimio yawe yametekelezwa kwa ukamilifu.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Disemba 2023, Wizara ilikuwa imefanikiwa kukusanya takribani kiasi cha **Shilingi bilioni 32** kati ya **Shilingi bilioni 123** ambazo taasisi na mashirika mbalimbali ya umma zinadaiwa kama pango la ardhi (Land Rent) nchini. Kamati kuipongeza Wizara kukusanya kiasi hicho ambacho ni sawa na **asilimia 26** ya deni lote. Aidha, Kamati inazitaka taasisi na mashirika yote ya umma nchini yanayodaiwa kulipa kodi ya pango la ardhi.

**2.2 Ziara za Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo**

**Mheshimwa Spika,** ili kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii ilipanga kufanya ziara ya ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo ipatayo Sita (06) iliyopo katika Mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro. Miradi iliyotembelewa na kukaguliwa ni pamoja na:-

a) Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Kushuka Ndani ya Kreta (Seneto Descend Road) katika eneo la Ngorongoro;

b) Mradi wa Kiwanja cha Ndege na Jengo la kupokelea Wageni katika Hifadhi ya Taifa Tarangire;

c) Mradi wa Ukarabati wa Maonesho na Maktaba katika eneo la Azimio la Arusha na Elimu Viumbe;

d) Utekelezaji wa Shughuli za Chuo cha Viwanda vya Misitu (FITI);

e) Mradi wa Kupanga, Kupima na Kumilikisha ardhi (KKK); na

f) Mradi wa Uimarishaji wa Mipaka Kimataifa.

**2.2.1 Utekelezaji wa Miradi ya Sekta Maliasili na Utalii**

***a) Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Kushuka Ndani ya Kreta (Seneto Descend Road) Katika eneo la Ngorongoro***

**Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa mradi huu ulilenga kuhakikisha kuwa vivutio vya utalii katika eneo la Ngorongoro Kreta vinafikika wakati wote wa mwaka, hivyo kuongeza idadi ya watalii na ongezeko la mapato yatokanayo na Utalii.
Mradi huu ulitekelezwa kwa kutumia teknolojia ya mawe ambayo ni rafiki katika uhifadhi wa mazingira.
Kamati ilijulishwa kuwa mradi huu umetekelezwa kwa sehemu nne ambazo ni ukaguzi na upimaji wa barabara, usanifu, uchongaji wa mawe ya kujengea barabara na ujenzi wa barabara. Mradi huu umekamilika kwa asilimia 100 na tayari umeanza kutumika.

***b) Mradi wa Kiwanja cha Ndege na Jengo la Kupokelea Wageni katika Hifadhi ya Taifa ya Tarangire***

**Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa mradi huu unalenga kuboresha miundombinu ya uwanja ili uweze kukidhi matakwa ya viwanja vya Kimataifa (ISO 9001:2015). Hadi Kamati inatembelea na kukagua mradi huu ulikuwa umetekelezwa kwa **asilimia 60**, huku kukiwa na kusimama kwa mradi kulikosababishwa na Mkandarasi kucheleshewa malipo yake.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inashauri Serikali kuhakikisha kuwa inachukua hatua za haraka ili mradi huu uweze kukamilika kwa

wakati na kuanza kutumika, hivyo kuboresha mazingira ya kupumzika wageni wanaoingia na kutoka hifadhini kupitia kiwanja kidogo cha ndege cha Kuro.

***b) Mradi wa Ukarabati wa Maonyesho na Maktaba katika eneo la Azimio la Arusha na Elimu Viumbe***

**Mheshimiwa Spika,** Mradi huu unalenga kuongeza idadi ya Watalii katika eneo la Makumbusho ya Taifa hadi kufikia lengo la Watalii milioni mbili katika eneo hilo mahsusi.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kamati inaenda kutembelea na kukagua utakekelezaji wa mradi huu, mradi ulikuwa umefikia asilimia 93 ikiwa imehusisha ujenzi wa vyoo, mfumo wa TEHAMA, mfumo mpya wa umeme na ujenzi wa ukumbi mkubwa wa maonyesho na maktaba.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inashauri Serikali ihakikishe upatikanaji wa kangavuke (generator) na tenki la kuhifadhi maji ili kukidhi dharula ya umeme na maji kwenye kituo ikiwa ni pamoja na kununua gari la shughuli za vituo vya makumbusho ya Taifa.

**2.2.2 Utekelezaji wa Miradi ya Sekta ya Ardhi**

***a) Mradi wa Kupanga, Kupima na Kumilikisha (KKK) katika Shamba la Valeska***

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu unatekelezwa kwa utaratibu wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa kutoa Mikopo ya fedha isiyo na riba kwa halmashauri nchini. Katika mwaka wa fedha 2022/2023 Wizara iliidhinishiwa na Bunge kiasi cha **Shilingi 5,358,166,155.56** kwa ajili ya utekelezaji mradi huu kwenye halmashauri mbalimbali nchini.

Kamati ilitembelea na kukagua utekelezaji wa mradi wa KKK katika shamba la Valeska lililopo Halmashauri ya Wilaya ya Meru, Mkoani Arusha.

***b) Mradi wa Uimarishaji wa Mipaka Kimataifa***

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu ni wa uimarishaji wa mipaka ya kimataifa kati ya Tanzania na Kenya hususani eneo la Namanga. Kwa ujumla mpaka wa Kenya na Tanzania unakabiliwa kuwa na urefu wa kilomita 818 ambapo kilomita 758 ni eneo la nchi kavu

na kilomita 60 ni eneo la maji. Mradi huu uliidhinishiwa **Shilingi 2,495,830,550/=** kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Kamati ililiridhishwa na hali ya uimarishaji wa mpaka na usalama katika eneo hilo.

### 2.2.3 Maoni ya jumla kutokana na yaliyojitokeza wakati wa ukaguzi wa miradi

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inapenda kutoa maoni ya jumla katika eneo la ukaguzi wa miradi kama ifuatavyo:-

a) Fedha za miradi ya maendeleo ziwe zinapatikana kwa wakati na kwa kiwango kilichopangwa ili kuwezesha utekelezaji sawia wa miradi ya maendeleo;

b) Bajeti iongezwe kwa ajili ya uimarishaji wa mipaka ya kimataifa ili kukamilisha miradi hiyo;

c) Wananchi waelimishwe kuhusu umuhimu wa kulinda alama za mpaka kwa kuepuka kuendesha shughuli za kilimo na za kijamii;

d) Kutengeneza miundombinu ya barabara katika maeneo ya mipaka ili kuwezesha usafirishaji wa vifaa na utekelezaji wa kazi kikamilifu;

e) Serikali ihakikishe inatumia teknolojia ya ujenzi wa barabara za maeneo ya hifadhi kwa kutumia mawe kwani ni wa gharama nafuu, rafiki kwa mazingira na uhifadhi na barabara zitadumu kwa muda mrefu;

### 2.3 Kushughulikia Bajeti za Wizara

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitekeleza jukumu hili la kuchambua na kupitia bajeti za Wizara zote mbili na taasisi zake. Jukumu hili ni kwa mujibu wa fasili ya 117 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023.

### 2.3.1 Mpango wa Makadirio wa Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2023/2024

***i) Wizara ya Maliasili na Utalii (Fungu 69)***

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara ilitengewa na kupitishiwa na Bunge lako Tukufu kiasi cha Shilingi 654,668,208,000/= ikiwa ni ongezeko lako asilimia 2.7 kulinganisha na mwaka wa fedha 2022/2023 ambapo Wizara ya Maliasili na Utalii ilitengewa Shilingi 624,142,732,000/=. Aidha, fedha zilizoidhiishwa na Bunge lako Tukufu kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ni Shilingi 168,166,759,000/=, kati ya hizo Shilingi 109,879,593,000/ = sawa na asilimia 65 ya fedha zote za maendeleo ni fedha za ndani na Shilingi **58,287,166,000/=** sawa na **asilimia 35** ni fedha za nje.

***ii) Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (Fungu 48)***

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara iliidhinishiwa na Bunge lako Tukufu kiasi cha Shilingi 163,169,880,000/=. Aidha, katika fedha hizo, kiasi cha Shilingi 82,126,645,000/= kilikuwa ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo ambapo Shilingi bilioni 14,006,000,000/= ni fedha za ndani na Shilingi bilioni 68,120,645,000/= zikiwa ni fedha za nje.

***iii) Tume ya Matumizi bora ya Ardhi (Fungu 03)***

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2022/2023, Tume iliidhinishiwa Shilingi 4,867,704,000/= tu kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Aidha, katika mwaka wa fedha 2023/204, Bunge lako Tukufu lilifanya uamuzi wa kuiongezea bajeti Tume hadi kufikia Shilingi 8,202,628,000/= ikiwa ni ongezeko la zaidi ya asilimia 68 baada ya kupokea ushauri wa Kamati na kuzingatia umuhimu wa Tume katika kupima na kupanga ardhi ya nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inapenda kulishukuru Bunge lako Tukufu na Serikali kwa kuona na kuzingatia ushauri wa Kamati. Katika fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya Tume ya Mipango ya Matumizi bora ya Ardhi, kiasi cha **Shilingi 3,410,000,000/=** zilikuwa ni fedha za miradi ya maendeleo ikiwa ni ongezeko la zaidi ya asilimia 140 ya fedha za maendeleo kulinganisha na mwaka wa fedha 2022/2023 ambapo zilikuwa **Shilingi 1,410,000,000/=** tu.

**2.3.2 Utekelezaji wa Bajeti kwa kipindi cha nusu mwaka kati ya Julai-Desemba 2023**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipata fursa ya kuchambua utekelezaji wa bajeti za Wizara zote mbili kwa kipindi cha nusu Mwaka kuanzia Julai hadi Disemba, 2023. Katika uchambuzi huo, Kamati ilijikita katika kuangalia ukusanyaji wa maduhuli na fedha zilizopokelewa na Wizara na Taasisi zake.

***i) Wizara ya Maliasili na Utalii (Fungu 69)***

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa maduhuli hadi kufikia tarehe 30 Disemba, 2023, Wizara na taasisi zake ilikuwa imefanikiwa kukusanya kiasi cha **Shilingi 572,905,619,470.92** sawa na **asilimia 64.88** ya lengo la makusanyo kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia tarehe 30 Disemba, 2023, Wizara na taasisi zake ilikuwa imepokea kiasi cha **Shilingi 272,657,107,509.68** ikiwa ni fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Kiasi hicho ni sawa na **asilimia 41.51** ya bajeti yote iliyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

**Mheshimiwa Spika,** katika fedha hizo kiasi cha **Shilingi 242,430,783,506.68** ni fedha za matumizi ya kawaida ikiwa ni pamoja na mishahara na matumizi mengino sawa na **asilimia 49.83** ya lengo. Kwa upande mwingine, fedha za maendeleo zilizopokelewa ni **Shilingi 30,226,324,003/=** tu sawa **asilimia 17.97** ya lengo.

**Mheshimwa Spika,** Kamati inaomba Wizara ya Fedha kuhakikisha inaongeza kasi ya kutoa fedha za Miradi ya Maendeleo kwa Wizara na Taasisi zake kwani Wizara hii ni Wizara inayoongoza katika kuchangia fedha za kigeni nchini. Miradi ya Maendeleo katika Wizara hii inahusisha ukarabati wa miundombinu katika maeneo ya hifadhi ambayo ndio vivutio vya utalii nchini.

**Mheshimiwa Spika,** kwa jinsi hali ya miundombinu ilivyo katika maeneo ya hifadhi zetu zikiwemo mbuga za wanyama, eneo la Ngorongoro na maeneo mengine ya uhifadhi, na ukizingatia juhudi na mipango ya Kutangaza Utalii nchini ilivyo, itafika mahali maeneo yetu ya vivutio na yatashindwa kuhudumia ongezeko

kubwa la idadi ya Watalii wanaoingia nchini. Hivyo, kuna haja ya kufanya jitihada za makusudi katika kuhakikisha kuwa Wizara na Taasisi zake wanapewa fedha zote za miradi ya maendeleo kama ilivyoidhinishwa na Bunge kwa wakati.

***ii) Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (Fungu 48)***

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ilipanga kukusanya maduhuli kiasi cha **Shilingi 300,000,000,000/=** kutoka vyanzo vyake vya ndani. Hadi kufikia Disemba, 2023 Wizara ilikuwa imekusanya Shilingi **76,642,421,871.02** sawa na **asilimia 26** tu ya lengo la makusanyo. Mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli ni wa kusuasua na hauridhishi kabisa katika Wizara hii.

**Mheshimiwa Spika,** Katika kujadili, Wizara ilieleza Kamati kuwa kusuasua kwa makusanyo ya maduhuli kumechangiwa na uamuzi wa Serikali kupitia Sheria ya Fedha kuhamisha makusanyo ya Kodi ya pango la ardhi (Land Rent) kukusanywa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na nia nzuri ya Serikali, Kamati ilibaini kuwa kuna changamoto kadhaa ambazo zimefanya zoezi la ukusanyaji wa pango la ardhi (Land Rent) kusuasua kwani hadi kufikia Disemba, 2023, hakuna Halmashauri iliyokuwa imekusanya mapato hayo. Changamoto zilizochangia ni halmashauri kutokuwa na nguvu ya kisheria ya kuchukua hatua kwa wadaiwa na kukosekana kwa mfumo mahsusi wa ukusanyaji katika ngazi za halmashauri kwani halmashauri zinatumia mfumo wa TAUSI wakati Wizara ya Ardhi wanatumia mifumo ya MORIS na ILMIS ambayo ina kanzidata za maeneo yote yanayotakiwa kulipiwa pango la ardhi.

**Mheshimiwa Spika,** hii ilipelekea Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kuendelea kukusanya kodi hii kwa kuchelewa kwani walitegemea halmashauri zingeanza kukusanya mara moja baada ya mwaka wa fedha 2023/2024 kuanza. Hata hivyo, Wizara imekumbana na changamoto ya kukosa fedha za kugharamia shughuli za ukusanyaji (facilitation fund) kwa ufanisi kama ilivyokuwa awali.

**Mheshimiwa Spika, Aidha,** Wizara ilipokea kiasi cha **Shilingi 140,030,291858.20** ikiwa ni fedha kwa ajili ya kulipa madeni mbalimbali za Wizara. Kamati inapenda kuipongeza Serikali kupitia Hazina kwa kuhakikisha Wizara inapokea fedha hizi ili kulipa madeni yakiwemo ya wazabuni, wakandarasi na watumishi wake. Ongezeko la kiasi hiki cha fedha, kinafanya jumla ya Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2023/2024 kuwa kiasi cha **Shilingi 303,200,171,858.20.**

**Mheshimiwa Spika, hadi** kufikia Disemba, 2023 Wizara ilipokea kiasi cha **Shilingi 194,854,758,623.52**. Katika fedha zilizopokelewa kiasi cha **Shilingi 160,132,526,394.72** zilizokuwa ni fedha za Maendeleo. Kiasi hiki kilichopokelewa ni sawa na **aslimia 64** ya bajeti yote kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Aidha, Wizara na taasisi zake ilikuwa imetumia asilimia **95** ya fedha zote ilizokuwa imezipokea toka hazina.

**Mheshimiwa Spika,** hali hii inaonyesha dhamira ya dhati na utashi wa kisiasa (political will) ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kushughulikia migogoro ya ardhi kwa kuiwezesha Wizara kifedha ili kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi hivyo kuhakikisha Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2020 inatekelezwa kwa vitendo hasa kufikia lengo la kupima viwanja 500,000 hadi kufikia mwaka 2025.

***iii) Tume ya Mipango ya Matumizi bora ya Ardhi (Fungu 03)***

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Disemba, 2023 Tume ya Mipango ya Matumizi bora ya Ardhi ilikuwa imepokea kiasi cha **Shilingi 4,729,337,930** sawa na **asilimia 57.65** ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu .Vile vile Tume iliendelea kupokea **Shilingi 927,722,500** kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (AFDB) kwa ufadhili wa Mfuko wa Ushirikiano wa Kiuchumi wa Korea na Afrika (KOEFEC) ambazo zimetokana na kuandika andiko kwa ajili ya kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi ; na **Shilingi 1,691,128,150** ni michango ya wadau ambayo imetokana na uhamasishaji wa matumizi bora ya ardhi.

**2.4 Kufuatilia Utekekelezaji wa Shughuli zinazotekelezwa na Wizara**

**Mheshimiwa Spika,** fasili ya 7(1)(d) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, inazitaka Kamati za Kisekta kufanya ufuatiliaji wa shughuli mbalimbali zinazotekelezwa na Wizara zinazosimamiwa na Kamati. Kwa kuzingatia sharti hilo la kikanuni, Kamati imetekeleza shughuli mbalimbali za ufuatiliaji wa shughuli zinazotekelezwa na Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Wizara ya Maliasili na Utalii. Shughuli hizo zinajumuisha ufuatiliaji wa utekelezaji wa Bajeti kama ilivyoainishwa hapo mwanzo, kwa dhumuni la kujiridhisha kuwa malengo yaliyokusudiwa na bajeti hizo yanafikiwa. Shughuli hii ilitekelezwa kwa kupokea taarifa za utekelezaji wa bajeti kutoka Wizara zote mbili za kisekta zinazosimamiwa na Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati pia ilifanya ufuatiliaji wa Utendaji wa Wizara na Taasisi zake kwa kupokea taarifa mbalimbali za utendaji katika vikao mbalimbali vya Kamati. Lengo la shughuli hii ni kujiridhisha kwamba dhima ya ustawi wa wananchi kupitia sekta zinazosimamiwa na Wizara hizi inafikiwa kikamilifu.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati pia ilifanya ziara za ufuatiliaji kwa lengo la kujiridhisha na tija inayopatikana katika miradi na program zinazotekelezwa na Wizara zinazosimamiwa na Kamati. Kutokana na Ziara hizo Kamati iliweza kuwianisha taarifa zinazotolewa na Serikali kuhusu tija na mafanikio na hali halisi iliyopo kwenye maeneo husika. Kamati ilitembelea Pori la Akiba Wami-Mbiki katika Mikoa ya Morogoro na Pwani kwa ajili ya kuona miradi inayotekelezwa kwa fedha za Mpango wa maendeleo kwa ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO-19, Eneo la Msomera –Tanga kuona maendeleo na hatua zilizofikiwa katika kuhamisha kwa hiari wananchi toka eneo la Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, Hifadhi ya Taifa Mikumi kuona moja ya Mradi wa Kuboresha Usimamizi wa Maliasili na Kukuza Utalii Kusini mwa Tanzania (REGROW), Kijiji cha Mwadela Wilayani Maswa Mkoa wa Simiyu kuona na kukagua utekelezaji wa Mradi wa Uboreshaji wa Usalama wa Milki za Ardhi (LTIP) na Jijini Arusha kuona mradi wa Maboresho ya Mfumo wa Usimamizi wa Ardhi nchini.

**Mheshimiwa Spika,** kabla ya uchambuzi wa bajeti za Wizara kwa Mwaka 2022/2023 Kamati ilitembelea na kukagua miradi sita (6) iliyotekelezwa na wizara hizi pamoja na taasisi zilizo chini yake kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Tolea la Februari, 2023. Aidha, Kamati pia ilipata fursa ya kuchambua taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2023/2024 kwa kipindi cha nusu mwaka kati Julai na Disemba kama ilivyoonyeshwa hapo awali kwenye taarifa hii.

### 2.4.1 Yaliyobainika wakati wa ufuatiliaji wa Sekta

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha kuanzia Januari, 2023 hadi Februari, 2024, Kamati ilipokea na kujadili taarifa 46 ambapo taarifa 14 ni za Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na taarifa 32 ni za Wizara ya Maliasili na Utalii. Lengo la kupokea na kujadili Taarifa hizi ni kuiwezesha Kamati kulisaidia Bunge kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Ibara ya 63 (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo imelipa Bunge mamlaka ya kuisimamia na kuishauri Serikali.

#### 2.4.1.1 Mafanikio na Changamoto katika Sekta ya Maliasili na Utalii

**Mheshimiwa Spika,** Sekta ya Maliasili na Utalii ni sekta mtambuka ambayo imekuwa na mchango mkubwa katika uhifadhi wa mazingira hivyo kutunza ikolojia, uoto wa asili na viumbe hai ambao wapo katika hatari ya kutoweka duniani. Sekta hii ina mchango mkubwa katika ustawi wa wananchi, ukuaji wa uchumi na sekta inayohakikisha uchumi wa nchi yetu unakuwa stahimilivu kwa wakati wote kwa kuchangia kiasi kikubwa cha fedha za kigeni kuliko sekta zote za uchumi nchini. Uchambuzi wa taarifa uliofanywa na Kamati, umewezesha kubaini mafanikio na changamoto katika utekelezaji wa majukumu ya sekta ya Maliasili na Utalii kwenye miradi na taasisi zake kama ifuatavyo;

#### *a) Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro*

**Mheshimiwa Spika,** Sheria ya Mamlaka ya Hifadhi ya eneo Ngorongoro (1959) iliweka msingi wa matumizi ya ardhi ya eneo la Ngorongoro kama eneo la matumizi mseto (Multiple Land use) kwa shughuli za Uhifadhi na shughuli za binadamu zinazozingatia uhifadhi ili kulinda ikolojia ya eneo la Ngorongoro ikiwa ni pamoja na mimea, wanyama na vyanzo vya maji katika eneo la hifadhi.

**Mheshimiwa Spika**, hata hivyo kutokana na ongezeko la watu na shughuli za binadamu ikiwemo ufugaji na kilimo ambapo inapelekea ushindani wa rasilimali (resources competition) kati ya wakazi wa Eneo la hifadhi na viumbe hai wengine kwenye hifadhi, eneo hili ambalo ni moja ya eneo la urithi wa dunia lipo hatarini kupoteza ikolojia yake, hali iliyopelekea Kamati kuishauri Serikali kuchukua hatua za kuhamisha wakazi wa Ngorongoro kwa hiari kutoka eneo la hifadhi.

**Mheshimiwa Spika,** zoezi la kuwahamisha wakazi wa Ngorongoro kwa hiari lilianza Februari, 2022 ikiwa ni awamu ya kwanza ya zoezi hili na kukamilika mwezi Julai, 2023. Utekelezaji wa Mradi wa kuhamishawananchi waishio eneo la Hifadhi ya Ngorongoro awamu ya pili ulianza Mwezi Julai, 2023. Vipengele vya mradi katika awamu hii vinahusisha; ujenzi wa nyumba 5000, ujenzi wa miundombinu ya huduma za kijamii, kutoa elimu na uhamasishaji, kuwezesha uthamini wa mali na kuhamisha kaya zilizojiandikisha kuhama kwa hiari kwenda Msomera, Kitwai, Saunyi na maeneo mengine watakayochagua wananchi wenyewe. Awamu yakwanza Serikali ilijenga nyumba 503 katika kijiji cha Msomera na kuwezesha kaya 551 kuhamia zikiwa na jumla ya watu 3,010, mifugo 15,521.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imeridhika na uratibu mzuri wa zoezi hili ambalo ni la hiari na linalozingatia haki za binadamu ambapo Serikali inawapa huduma zote muhimu kama vile chakula, nyumba, elimu na afya, miundombinu ya maji, mawasiliano, umeme, majosho, na vitalu vya malisho ya mifugo.

**Mheshimiwa Spika**, Pamoja na mafanikio makubwa yaliyopatikana katika utekelezaji wa mpango huu, Kamati ilibaini kuwepo kwa changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na; upotoshwaji unaofanywa na baadhi ya Taasisi zisizo za kiserikali pamoja na baadhi ya watu waliopo ndani na nje ya nchi; na watu wasiokuwa na sifa za kuhamishwa kutaka kutumia fursa hii ili wahamishwe kinyume na taratibu. Kamati inapenda kuipongeza Serikali kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii pamoja na Jeshi la Wananchi Tanzania kwa namna wanavyoendelea na utekelezaji wa mradi huu.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa zoezi hili limeonyesha muitiko mkubwa toka kwa wakazi wa Ngorongoro kutokana na uhamasishaji uliofanywa na Serikali, ni rai ya Kamati kuwa Serikali ihakikishe inaongeza kasi katika kutekeleza mradi huu.

***b) Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori (TAWA)***

**Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA) ilianzishwa kwa Amri ya Serikali (establishment order) kupitia Kifungu cha 8 cha Sheria ya Kuhifadhi Wanyamapori Na. 5 ya Mwaka 2009 na kutangazwa kwa kuchapishwa kwenye Gazeti la Serikali Na. 135 la tarehe 09 Mei 2014, pamoja na marekebisho yaliyochapishwa katika gazeti la Serikali Na. 20 la tarehe 23 Januari 2015. TAWA ilianzishwa ili kusimamia mapori ya akiba, mapori tengefu, jumuiya za hifadhi ya wanyamapori na maeneo ya ardhi oevu ambapo Mamlaki hii inasimamiwa na Bodi ya Ushauri.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na majukumu mengine, Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori (TAWA) imekasimiwa jukumu la usimamizi wa Uwindaji wa Kitalii nchini. Uwindaji wa kitalii hufanyika kwa madhumuni ya kupata burudani (sport) na kupata nyara (trophies) ambazo ni sehemu ya mnyama aliyewindwa kama vile mifupa, meno, damu, manyoya, ngozi, fuvu, pembe, kucha na nyama.

**Mheshimiwa Spika**, Uwindaji huu hufanyika kwa kuzingatia Sheria ya Uhifadhi Wanyamapori, Sura 283 mapitio ya mwaka, 2022 na Kanuni za Uwindaji wa Kitalii za mwaka 2015 na marekebisho yake na mikataba ya kimataifa (Mkataba wa kusimamia biashara ya wanyamapori na mimea iliyo hatarini kutoweka - CITES) ambayo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeridhia.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 67(a)(i) ya ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi - CCM ya mwaka 2020-2025, imeelekeza Serikali kuhakikisha inakuza na kuimarisha uwindaji wa wanyamapori ili kuongeza mchango wa sekta katika uchumi wa Taifa. Hapa nchini, uwindaji huu huchangia fedha za kigeni. Serikali hukusanya takribani **Dola za Marekani Milioni 12.8** kwa mwaka kutokana na uwindaji wa kitalii. Vilevile huchangia zaidi ya asilimia sitini (60%) ya mapato ya TAWA. Pamoja na utekelezaji wa

jukumu hilo, TAWA bado inaendeshwa kwa tamko la uanzishwaji wake huku ikiwa na bodi ya ushauri badala ya bodi tendaji.

***c) Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA)***

**Mheshimiwa Spika,** Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA) ni Taasisi ya Umma yenye dhamana ya kusimamia na kuendeleza maeneo yaliyoanzishwa kisheria kuwa Hifadhi za Taifa. Shirika lilianzishwa Mwaka 1959 kupitia Sheria ya Hifadhi za Taifa Sura ya 412 (kwa sasa Sura ya 282). Hadi sasa Shirika linasimamia hifadhi za Taifa ishirini na moja (21) zikiwa na ukubwa wa eneo la kilometa za **mraba 96,908.88** sawa na takribani **asilimia 10.2%.**

**Mheshimwa Spika,** pamoja na Hifadhi za Taifa 16 zilizokuwepo awali, Shirika limeendelea kusimamia maeneo ya Hifadhi mpya za Taifa tano (5) zilizoongezeka Mwaka 2019 (Burigi-Chato, IbandaKyerwa, Rumanyika-Karagwe, Mto Ugalla na Nyerere) kwa weledi mkubwa ili kuhakikisha yanakuza utalii na kuimarisha uhifadhi.

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi kati ya Januari na Disemba, 2023, Shirika lilifanya shughuli mbalibali ikiwa ni pamoja na Kulinda na Kuimarisha Mipaka ya Hifadhi, kupunguza matukio ya ujangili ndani na pembezoni mwa Hifadhi za Taifa Kwa kuwezesha doria dhidi ya ujangili kufanyika katika hifadhi zote na kuimarisha mahusiano yake na jamii zinazoishi kwenye Vijiji vinavyopakana na hifadhi za Taifa kwa kutoa elimu ya uhifadhi na kuchangia shughuli za maendeleo kupitia miradi ya ujirani mwema (support for community initiated projects-SCIP na TANAPA Income Generating Project-TIGP).

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio hayo hapo juu, Shirika linakabiliwa na changamoto ya ufinyu wa Bajeti ya uendeshaji kwani bajeti ya hifadhi 16 ndio inatumika kuendeshea hifadhi 21, pamoja na kanda nne, vituo 5 vya Malikale na ofisi mbili Kiunganishi zilizopo Dar es Salaam na Dodoma. Hali hii ya ufinyu wa bajeti imechangia kushuka kwa ubora wa huduma zinazotolewa na Shirika pamoja na kudorora kwa shughuli za uhifadhi hivyo kupunguza ufanisi katika utendaji wa Shirika.

***d) Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania (TAFORI)***

**Mheshimiwa Spika,** TAFORI ilianzishwa mwaka 1980 kwa Sheria Na. 5 iliyopitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muun-gano wa Tanzania. Kupitia Sheria hiyo Taasisi ilipewa jukumu la kufanya, kusimamia, na kuratibu tafiti na kutoa ushauri wa kitaalamu kuhusu matumizi ya teknolojia bora na uendelezaji wa misitu nchini.

**Mheshimiwa Spika,** Taasisi hii inafanya Utafiti wa rasilimali za Misitu katika kanda saba za Wizara ya Maliasili na Utalii. hadi sasa kanda nne tu, ambazo ni Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Kanda ya Magharibi, Kanda ya Kati na Kanda ya Ziwa ndio zimekamilisha na kuchapicha matokeo ya tafiti zao. Aidha tathmini ya rasilimali za Misitu imeonyesha kuwa kuna misitu kiasi cha **hekta 266,457.98** za miti ya kupandwa katika mikoa ya Kanda hizo. Utafiti utaendelea katika kanda tatu zilizobaki (Kanda ya Mashariki, Kusini na Kaskazini).

**Mheshimiwa Spika,** Serikali ilielekeza TAFORI kuratibu utafiti wa uhasibu wa kijani *(Green Accounting)* ili kuainisha mchango utolewao na sekta ya misitu kupitia mazao ya misitu ambayo mchango wake si wa moja kwa moja kwenye pato la Taifa. Hadi sasa, watafiti wamekusanya takwimu za msingi katika utafiti huu wa uhasibu wa kijani kutoka Mikoa 16 ya Tanzania Bara.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na utendaji wake, bado taasisi hii inakabiliwa na changamoto kadhaa ikiwemo ufinyu wa Bajeti na upungufu wa wafanyakazi kwa zaidi ya **asilimia 55%.**

***e) Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania (TAWIRI)***

**Mheshimiwa Spika,** Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania (TAWIRI) ilianzishwa kwa Sheria ya Bunge ya Na. 4 ya mwaka 1980, na marekebisho ya sheria kama ilivyo Na. 10 ya mwaka 1999 na (Sura 260), mwaka 2002 na mwaka 2021. Lengo kuu la uanzishwaji wake ni Kufanya, kuratibu na kusimamia tafiti za wanyamapori hapa nchini.

**Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha mwaka 2022/2023, Taasisi hii ilifanya tafiti zinazoigusa jamii (*Public Interest*) ikiwa ni pamoja na Tathmini ya sababu zinazozuia urejeshwaji wa chura wa Kihansi katika mazingira yake ya asili na Sababu za kijamii, kiuchumi,

kiikolojia na kimazingira zinazosababisha migongano ya watu na tembo nchini Tanzania.

**Mheshimiwa Spika,** katika kufanya tathmini ya sababu zinazozuia urejeshwaji wa chura wa Kihansi katika mazingira yake ya asili, matokeo ya awali yanaonyesha kuwa ubora wa maji (water quality) katika bonde la Kihansi yana kiwango kikubwa cha amonia ambacho kinaweza kuwa chanzo cha ustawi hafifu wa vyura katika eneo hilo. Utafiti, unaendelea wa vinasaba kubaini endapo kuna mabadiliko ya vinasaba (genetics) yanayosababisha kufifia kwa ustawi wa vyura.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Sababu za kijamii, kiuchumi, kiikolojia na kimazingira zinazosababisha migongano ya watu na tembo Nchini, utafiti ulipitia mifumo ya ikolojia kati ya watu na wanyama hao ili kusaidia upatikanaji wa njia za kutatua migongano hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** katika maeneo ya Magharibi tafiti zimeonesha kuna ongezeko la shughuli za kibinadamu, ikiwemo kilimo, mifugo na makazi kama visababishi vya migogoro. Kwa upande wa Kaskazini ongezeko la idadi ya binadamu na tembo; mabadiliko ya tabianchi na mabadiliko ya tabia za ulaji wa tembo "Changes in feeding behavior" kama visababishi vya migogoro.

**Mheshimiwa Spika,** Taasisi hii kama ilivyo TAFORI ndio tegemeo katika sekta ya Uhifadhi na Utalii nchini. Hata hivyo, taasisi hii inakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa rasilimali fedha inayotokana na ufinyu wa bajeti hali inayoathiri utekelezaji wa majukumu yake kwa ufanisi. Taasisi hii haina jengo la Makao Makuu tangu ilipoanzishwa mwaka 1980, inakabiliwa na changamoto ya uchakavu wa Miundombinu, Uhaba wa vifaa vya kisasa katika Utafiti na Ukosefu wa fedha za Sensa za wanyamapori.

***f) Hali ya Utalii Nchini***

**Mheshimiwa Spika,** Sekta ya Utalii imepata takwimu ambazo hazijawahi kufikiwa nchini tangu nchi yetu ipate Uhuru. Watalaamu wa sekta hii nchini wanakiri kuwa hii imetokana na juhudi za Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan, kuchukua jukumu la kuitangaza sekta hii yeye mwenyewe kwa kuandaa filamu ''*The Royal Tour*''. Hadi kufikia mwezi Disemba, 2023 kwa taarifa za hali ya Uchumi za robo ya mwisho ya mwaka 2023 (*Quartely Economic Review*), kutoka Benki kuu ya Tanzania (BOT), Watalii walioingia nchini walikuwa takribani 1,790,301 ikiwa ni kiwango cha juu kabisa kuwahi kufikiwa katka sekta hii.

**Mheshimiwa Spika,** Sekta hii imeliingizia Taifa fedha za kigeni zaidi ya **dola za Marekeni bilioni** 3.3 sawa na zaidi ya asilimia 25 ya mauzo yote ya nje nchini hadi kufikia tarehe 31 Disemba, 2023 ikiwa ni sekta iliyoongoza katika kuingiza fedha za kigeni nchini, huku ikiwa imechangia zaidi ya asilimia 20 ya pato ghafi la Taifa (GDP). Kwa upande wa ajira, sekta imeongeza ajira za moja kwa moja kufikia hadi ajira **1,600,000** ikiwa ni sawa na **asilimia 11** ya ajira nchini.

**Mheshimiwa Spika,** ili kuhakikisha mafanikio haya yanakuwa endelevu, hatuna budi kama Taifa kuwekeza zaidi kwenye sekta ya Uhifadhi na kutangaza vivutio vyetu vya Utalii. Mathalani, Miongoni mwa wageni waliotembelea Tanzania kwa lengo la kutalii, **asilimia 58** huvifikia vivutio vya Hifadhi za Taifa na **asilimia 42** hutembelea maeneo mengine ya utalii ikiwemo Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro na fukwe za Zanzibar, lakini hali miundombinu katika hifadhi zetu nchini ni mbaya na tukizingatia hali ya neema ya mvua tuliyoipata mwaka huu, inaweza kupelekea kupoteza sehemu kubwa ya watalii nchini kwani hawatakuwa na nia ya kurejea tena nchini.

***g) Bodi ya Utalii Tanzania (TTB) na Mkakati wa Kutangaza Vivutio vya Utalii Nchini***

**Mheshimiwa Spika,** Bodi ya Utalii Tanzania (TTB) ilianzishwa kwa Sheria ya Bodi ya Utalii Tanzania Sura ya. 364 ya Sheria za Tanzania (R.E 2002), baada ya kufanyiwa marekebisho sheria ya awali ya utalii kuliko endana na kuvunjwa kwa lililokuwa Shirika la Utalii Tanzania (TTC). Sheria iliyounda Bodi ya Utalii, imeainisha majukumu makuu ambayo ni pamoja na Kutumia mbinu mbalimbali za utangazaji ili kuifanya Tanzania iwe kituo kimojawapo mashuhuri cha utalii duniani; Kuhamasisha uendelezaji wa miundombinu ya utalii; Kufanya tafiti kwa ajili ya

kuboresha Sekta ya Utalii nchini; na Kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa Sekta ya Utalii na manufaa yake kiuchumi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipata nafasi ya kupitia na kuchambua mkakati wa kutangaza vivutio vya Utalii nchini, ikiwa ni kufuatilia utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2020/2025 ya kuhakikisha Taifa linafikia lengo la Watalii **milioni 5** kwa kwa mwaka 2025 na fedha za kigeni zaidi ya dola za Marekani **bilioni 6.**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilichambua mikakati mahsusi ikiwa ni pamoja na Kupanua wigo wa Masoko ya Utalii ya Kimkakati ikiwemo Nchi za Brazil, Russia, India, China na South Africa (BRICS). Hili likifanyika litakuwa na matokeo chanya hasa katika mazao mbadala ya Utalii ikiwa ni pamoja na utalii wa kihistoria, utamaduni na utalii wa fukwe ambapo nchi yetu imeabarikiwa rasilimali hizo.

**Mheshimiwa Spika,** Mikakati mingine kama vile Kutangaza utalii kupitia Watu Mashuhuri kutoka kwenye masoko yetu. Mfano China tunatarajia kuwatumia Lu Han (10.9m Instagram followers), Jing Dong (15k Instagram followers), Priyanka Chopra (89.9m Instagram followers), Kazi ambayo inatarajiwa kuwa itafanyika katika mwaka wa fedha 2024/25-2025/2026, kutaongeza idadi ya watalii wa nje wanaofuatilia vivutio vyetu.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na matokeo mazuri ya kushangaza (Mirraculaous Results) ya Filamu ya ***"The Royal Tour"*** iliyofanywa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Bodi ya Utalii Tanzania inapanga Kuratibu uzalishaji wa filamu 4 za kimataifa: ikiwemo mbili (2) za mwendelezo wa Royal Tour na Makala mbili (2) za video (documentaries) za kimataifa kutoka kwa wazalishaji wa viwango vya Hollywood. Filamu hizo moja itaitwa ***"Kijiji cha Milele"*** au ***"Presidential Tour"*** iliyomshirikisha Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, na mwigizaji maarufu wa Filamu Bw. Jing Dong kutoka Nchini China, na nyingine ni maandalizi ya ***Documentary*** inayohusu mchango wa Mwalimu Julius K. Nyerere katika harakati za ukombozi wa Bara la Afrika. Mikakati yote hii ni mikakati inayohitaji fedha za kutosha.

Kwa bahati mbaya, bado kama Taifa hatujafanya juhudi za makusudi katika kutangaza Utalii ili tupate matokeo yanayotarajiwa.

**Mheshimiwa Spika**, kama zilivyo taasisi zingine za Wizara, Bodi ya Utalii inakabiliwa na changamoto ya ufinyu wa bajeti kwa kiwango kikubwa.

***h) Usimamizi wa Maliasili Endelevu na Ukuaji wa Utalii Kanda ya Kusini (REGROW)***

**Mheshimiwa Spika,** Mradi wa REGROW ni mradi wa miaka sita (28 Novemba 2017 hadi 28 Septemba 2023) ambao Serikali ya Tanzania inautekeleza kwa mkopo wa masharti nafuu (credit) kiasi cha Dola za Kimarekani milioni 150 (TZS. 345 Bilioni) kutoka Benki ya Dunia. Mradi ulipangwa kukamilika mwezi Septemba, 2023, kutokana na changamoto mbalimbali mojawapo ikiwa ni UVIKO 19 mradi uliongezewa muda wa miezi 17 na hivyo utakamilika Februari 28, 2025.
Mradi unatekelezwa kwenye maeneo ya kipaumbele yaliyohifadhiwa kusini mwa Tanzania ambayo ni Hifadhi za Taifa Ruaha, Mikumi, MilimaUdzungwa na Nyerere na Hifadhi ya Msitu Asili wa Kilombero.

**Mheshimiwa Spika,** Mradi unasimamiwa na Wizara ya Maliasili na Utalii na kutekelezwa na Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA), Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania (TAWIRI), Bodi ya Utalii Tanzania (TTB), Tume ya Taifa ya Umwagiliaji (NIRC), na Bodi ya Maji Bonde la Rufiji (RBWB).

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipata nafasi ya kufuatilia utekelezaji wa mradi wa REGROW Hifadhi ya Taifa Mikumi na kubaini kuwa kabla ya Mradi wa REGROW, miongoni mwa changamoto zilizokabili hifadhi ya Taifa ya Mikumi ilikuwa ni pamoja na Miundombinu duni kama vile barabara, njia za kurukia ndege na za miguu za watalii, Huduma za utalii zisizotosheleza (malazi, maeneo ya stoo, vituo vya habari, nk), Uendelezaji na utangazaji usioridhisha wa mazao ya utalii, Kaya zisizo na uwezo wa kufanya shughuli mbadala za kiuchumi, Utegemezi wa jamii katika maliasili ikiwa ni pamoja na ujangili, Kiwango kidogo cha ufahamu wa

uhifadhi wa jamii, Kiwango kidogo cha ushiriki wa jamii katika uhifadhi na utalii na Uwepo wa migogoro baina ya binadamu na wanyamapori wakali na waharibifu.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia tarehe 31 Desemba 2023, Mradi umepokea jumla ya fedha kiasi cha **Dola za Marekani 73,850,933.71** sawa na **Shilingi 169,857,147,533.00,** ambayo ni **asilimia 66** ya jumla ya fedha zilizotengwa na mradi kiasi cha **Dola za Marekani 111,364,488.00** sawa na **Shilingi 256,138,322,400**. Matumizi yote kutoka mwanzo wa Mradi hadi sasa ni Dola za **Marekani 37,042,410.68 (Shilingi 85,197,544,565.91).** Salio lisilotumika limetengwa kwa ajili ya malipo ya ujenzi wakati yanapohitajika.

**Mheshimiwa Spika,** miradi iliyotekelezwa ni pamoja na uboreshaji wa miundombinu ya ndani ya hifadhi ikiwa ni pamoja na ununuzi wa mitambo, kuboresha Kiwanja cha Ndege Kikoboga, Malazi kwa watalii na wafanyakazi, Uendelezaji na utangazaji wa vivutio vya utalii kupitia TTB na kuanzishwa miradi ya kuwainua kiuchumi wakazi wa maeneo yanayozunguka hifadhi ya Mkimu Maarufu kama COCOBA (Conservation Community Banks) ikiwa ni pamoja na Kuwezesha askari wa uhifadhi wa Vijiji "Village Game Scout" (VGS) 113 (kundi la tatu) kujiunga katika mafunzo ya miezi mitatu katika Chuo cha Wanyamapori cha Likuyu SekaMaganga.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio ya mradi huu, hata hivyo, Kamati inaliona changamoto katika ucheleweshaji wa miradi kukamilika kwa wakati na miradi kujikitika katika Hifadhi chache katika eneo la Kusini mwa Tanzania.

**i) *Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge ya Kuridhia Kurekebisha Mpaka wa Hifadhi za Taifa za Kigosi na Ruaha***

**Mheshimiwa Spika,** tarehe 27 Juni, 2023, Serikali kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii iliwasilisha ndani ya Bunge lako maazimio ya kubadili hadhi ya hifadhi ya Taifa ya Kigosi na Mipaka katika Hifadhi ya Taifa ya Ruaha. Bunge lako Tukufu lilipata nafasi na kusikia maoni ya Kamati inayosimamia sekta hiyo ikiwa ni Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii. Baada ya maoni ya Kamati na michango ya Waheshimiwa Wabunge, hatimae Bunge liliridhia na

kukubali kubadili hadhi ya Hifadhi ya Taifa ya Kigosi na kuwa Hifadhi ya Misitu ya Kigosi bila masharti yoyote.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa kubadili mipaka ya Hifadhi ya Taifa ya Ruaha, Bunge lako Tukufu lilikubali kubadili mipaka ya hifadhi kwa masharti kuwa Serikali itatekeleza mapendekezo ya Kamati ikiwa na lengo la kuhakikisha wananchi wanaoishi pembezoni wa eneo linatotakiwa kufanyiwa marekebisho ya Mipaka wanatendewa haki lakini pia, hifadhi inalindwa. Kauli ya Serikali kupitia kwa aliyekuwa Waziri wa Maliasili na Utalii Mhe. Mohamed Mchengerwa siku hiyo ilikuwa ni kukubaliana na Maoni ya Kamati na kuahidi kuyafanyia kazi maoni hayo na kuwasilisha taarifa ya utekelezaji kwenye Kamati katika vikao vya Kamati vya mwezi Agosti, 2023.

**Mheshimwa Spika,** hadi tunawasilisha taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu, mapendekezo yote yaliyotolewa na Kamati hajatekelezwa kama Serikali ilivyoahidi. Hali ya kushangaza ni kuwa kila tulipokutana na Wizara katika vikao mwezi Agost, 2023, Oktoba, 2023 na Januari, 2024, Wizara imeshindwa kabisa kutoa majibu ya kuridhisha juu ya jambo hili.

**Mheshimiwa Spika,** Bunge lako Tukufu ni chombo cha Uwakilishi wa wananchi, sisi wabunge tunawakilisha matakwa ya wananchi kwa mujibu wa Ibara ya **62** na **63** za Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 katika kuhakikisha Serikali inatenda shughuli zake zote. Kwa hiyo, Kamati inaomba Bunge lako Tukufu kuiagiza Serikali kutekeleza maagizo iliyoyatoa na kuyaridhia ndani ya Bunge.

***j) Changamoto za kuzibwa kwa Shoroba za Wanyama***

**Mheshimiwa Spika,** Maeneo ya hifadhi na mifumo ikolojia ya wanyamapori yanaunganishwa na shoroba ambazo huruhusu wanyamapori kuhama kutoka hifadhi au eneo moja kwenda nyingine kwa malengo mbalimbali ikiwemo kujihami, kuzaliana, maeneo ya mtawanyiko na maeneo muhimu kwa ajili ya kupata chakula na maji wakati wa msimu kiangazi wa mwaka.

**Mheshimiwa Spika,** kuziba kwa shoroba hizi kumepelekea changamoto nyingi hususani migongano baina ya binadamu na

wanyamapori inayosababishwa na Wananchi wanaoendesha shughuli zao za kijamiii na kiuchumi katika maeneo ya shoroba ambapo wanakabiliwa na athari za kujeruhiwa; kuuawa; mazao kuharibiwa na mifugo kuuawa na hivyo kuongeza kiwango cha umaskini kwa wananchi; na wanyamapori kushindwa kubadilishana vinasaba (genetic exchange) na hivyo kusababisha kupotea kwa vizazi kwa baadhi ya wanyamapori ambao hawaruhusu inbreed.

**Mheshimiwa Spika,** ni wakati sasa wa Serikali kuweka alama za kudumu kwenye maeneo yaliyoanishwa kama shoroba ili kudhibiti uvamizi wa shughuli za kibinadamu. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongoa shoroba 5 kati 18 ambazo zilipangwa kuongolewa hadi Juni, 2024. Pia, Serikali ihakikishe inaandaa mpango kabambe wa kuongoa shoroba zote 61 ili kupunguza mgongano kati ya binadamu na wanyama wakali na waharibifu.

***k) Jumuiya ya Hifadhi za Wanyamapori (WMAs)***

**Mheshimwa Spika,** Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori (WMA) ni eneo kwenye ardhi ya kijiji au vijiji iliyokubalika na kutengwa kwa misingi ya kuhifadhi wanyamapori na kwa ajili ya biashara inayotokana na uhifadhi huo. Katika Taifa letu, usimamizi wa shughuli za Jumuiya hizi unaratibiwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA).

**Mheshimiwa Spika,** Katika maeneo yanayopakana na hifadhi za Taifa, Serikali imeruhusu jamii kuanzisha hifadhi za wanyamapori hususan kwenye maeneo yanayozunguka hifadhi za taifa au hifadhi nyingine, na kwenye ushoroba (njia maalum za wanyama) ambapo wanyama wanasafiri kutoka hifadhi moja kwenda nyingine kwa ajili ya kutafuta chakula, maji na mahitaji mengineyo.

**Mheshimiwa Spika,** ni muhimu kukumbuka kuwa, WMA SIYO hifadhi ya Taifa na Wala SIYO muendelezo wa hifadhi za Taifa, au ardhi inayomilikiwa na mtu binafsi. Vijiji vinaweza kutoa leseni kwa wawekezaji binafsi ili kujenga miundombinu ama kuendesha shughuli zao ndani ya maeneo ya WMA mfano kujenga kambi na kuendesha uwindaji.

**Mheshimiwa Spika,** Sera ya Wanyamapori ya mwaka 1998 inabainisha kuwa jamii itakuwa na mamlaka yote ya kusimamia na kupata manufaa kutokana na juhudi zao za uhifadhi, ingawa umiliki wa rasilimali za wanyamapori unabaki kwa Serikali. Hata hivyo kanuni za WMA za mwaka 2018 zinaeleza kuwa mgawanyo wa manufaa utaelezwa 'na waraka utakaokuwa ukitolewa mara kwa mara'. Waraka wa mwaka 2020, unaeleza kuwa mapato yatokanayo na shughuli za uhifadhi yaende moja kwa moja kwa Serikali, ambayo itarudisha sehemu ya mapato hayo kwenye WMAs kama inavyoonekana katkka jedwali hapa chini.

**Jedwali Na 1:** ***Mchanganuo wa mgawanyo wa mapato yatokanayo na shughuli za uwindaji wa kitalii kwenye WMAs***

| Na. | CHANZO CHA MAPATO | TAWA | WMA | H/WILAYA | HAZINA |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Ada ya Kitalu | 25% | 75% | 0.00 | 0.00 |
| 2. | Ada ya Uwindaji | 25% | 55% | 10% | 10% |
| 3. | Ada ya Uhifadhi | 25% | 45% | 5% | 25% |
| 4. | Ada ya Watazamaji | 25% | 60% | 5% | 10% |
| 5. | Ada ya Kibali | 25% | 30% | 5% | 40% |

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilibaini kuwa baada ya Serikali kuanzisha mfumo wa kupeleka moja kwa moja katika mfuko mkuu mapato ya taasisi mbalimbali ikiwemo taasisi za uhifadhi, mapato ya yatokanayo za WMAs nayo yamekuwa yakiingia moja kwa moja katika mfuko mkuu wa Serikali na Serikali imekua ikuchukua muda mrefu kurejesha kiasi kinachostahili kwenye Jumuiya hizo. Hali hii inazorotesha shughuli za Uhifadhi katika maeneo hayo kwani, Jumuiya hizo huingia gharama katika uhifhadhi wa maeneo hayo.

### 2.4.1.2 Mafanikio na Changamoto katika Sekta ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

**Mheshimiwa Spika**, katika nadharia ya Uchumi duniani moja ya nyanja kuu za uzalishaji kwa asili ni ardhi. Ardhi ni rasilimali ya msingi kabisa isiyoweza kuzalishwa kwa jitihada za mwanadamu hata katika mapinduzi makubwa ya teknolojia ambayo dunia imeyashudia. Ardhi ndio inayoanza kujenga familia, jamii na hata Taifa. Ardhi ndio inatafsiri mipaka ya Taifa lolote lile na ndio msingi wa neno Nchi.

**Mheshimiwa Spika,** nimeanza na sababu hizo hapo juu ili kuonyesha umuhimu wa sekta hii adhimu katika uzalishaji ndani ya Taifa letu. Ardhi ni msingi mkuu katika shughuli za uzalishaji ikiwa ni pamoja na kilimo, ufugaji, madini, utalii, biashara, ujenzi, uchukuzi na mawasiliano. Hata shughuli zetu nyingi za kijamii kama Taifa tunazifanya juu ya ardhi iwe ni ibada, matambiko, sherehe na mazishi. Kwa sababu hiyo, kama Taifa sekta ya ardhi inatakiwa kuwa moja ya sekta ya kipaumbele kwa maana ya bajeti na elimu ya umiliki na utunzaji wa ardhi.

**Mheshimiwa Spika,** sekta ya ardhi ikiboreshwa itapunguza migogoro ya ardhi kwa kiasi kikubwa na itachangia ufanisi katika sekta zingine za uzalishaji. Kamati imebaini mafanikio na changamoto katika sekta ya ardhi kwa miradi na taasisi kama ifuatavyo: -

***a) Tume ya Taifa ta Mipango ya Matumizi ya Ardhi***

**Mheshimiwa Spika,** Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi inatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia sheria ya Upangaji wa Matumizi ya Ardhi, Sura Na. 116, Mpango Mkakati wa Tume (2020-2025), Ilani ya Chama cha Mapinduzi (2020-2025), Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka mitano (2021/222025/26) na maelekezo mbalimbali ya Serikali. Majukumu ya Tume yameainishwa katika Sura Na. 116 ambayo ni pamoja na kuwezesha, kuratibu, kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Mipango ya Matumizi ya Ardhi.

**Mheshimiwa Spika,** Katika kutekeleza majukumu yake ya msingi, Tume imewajengea uwezo wadau mbalimbali wa sekta ya ardhi wapatao **15,843** ambao walipewa mafunzo na kushiriki katika

kuandaa, kusimamia na kutekeleza mipango ya matumizi ya ardhi. Mafunzo haya yalihusu sheria, taratibu na masuala mbalimbali yanayohusu sekta ya ardhi. Vilevile, washiriki wamejengewa uwezo wa namna ya kusoma jira za nukta, picha za anga, kutatua migogoro ya mipaka na usimikaji wa alama za ardhi (beacon).

**Mheshimiwa Spika,** Aidha, kupitia Mfumo wa Mipango ya Matumizi ya Ardhi (NLUIS) Tume imeweza kutoa Hati za Hakimiliki za Kimila na kupakia Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Vijiji **534** na kufanya jumla ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Vijiji iliyohifadhiwa kwenye mfumo kuwa **1,252** kati ya Mipango **3,277** iliyoandaliwa hadi sasa nchini.

**Mheshimiwa Spika,** Tume imesaidia kutatua migogoro ya Kiutawala nchini, ambapo jumla ya mipaka ya Vijiji 194 imehuishwa, kupimwa na kuidhinishwa. Aidha, migogoro ya ardhi 178 inayotokana na mipaka ya kiutawala na ile ya matumizi imetatuliwa.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio haya, Tume hii inakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo Upungufu wa Rasilimali Fedha kuweza kufikia malengo ya uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji 826 na Wilaya 11 na mipango kina 175 kwa mwaka kwa mujibu wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (2020 – 2025) na Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2021/22 – 2025/26).

**b) Taasisi za Mafunzo zilizochini ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.**

**Mheshimiwa Spika,** Wizara hii ina taasisi mbili za elimu ikiwa ni pamoja na Chuo cha Ardhi Tabora (ARITA) na Chuo cha Ardhi Morogoro (ARIMO). Vyuo hivi vilianzishwa kwa lengo la kuzalisha wataalamu wa sekta ya ardhi ngazi ya mafundi sanifu (Technicians) kutokana na kuongezeka kwa uhitaji wao nchini.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na majukumu yake ya msingi, vyuo hivi katika mwaka huu wa fedha vimeendelea kutekeleza shughuli mbalimbali ikiwa ni pamoja na Kuendelea kutoa huduma za ushauri wa kitaalam na kufanya kazi za upimaji wa viwanja na

uthamini wa ardhi na mali (zinazohamishika na zisizohamishika) katika Mashirika, Idara za Serikali, Taasisi za umma na binafsi pamoja na Mamlaka ya zSerikali za Mitaa nchini, Kuendelea kuzalisha machapisho mbalimbali ya nyaraka zinazotumiwa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa ajili ya kumilikisha ardhi na usajili kwa ujumla na Kuandaa mtaala wa mafunzo ya kuwajengea uwezo viongozi wa vijiji na mitaa kuhusu usimamizi na utawala wa ardhi katika maeneo yao ya uongozi ili kupunguza au kuondoa migogoro ya ardhi nchini.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilibaini kuwa katika utekelezaji wa majukumu ya vyuo hivi, bado vinakabiliwa na changamoto ya upungufu wa watumishi, baadhi ya miradi kutokamilika kwa wakati kutokana na kuchelewa kwa upatikanaji wa fedha za maendeleo. Vilevile ufinyu wa bajeti umesababisha vyuo kushindwa kutekeleza majukumu yao ya msingi kwa tija na ufanisi.

***c) Shirika la Nyumba la Taifa (NHC)***

**Mheshimiwa Spika,** Shirika la Nyumba la Taifa linatekeleza majukumu yake kupitia Sheria ya Bunge Na. 2 ya mwaka 1990 pamoja na marekebisho yake ya mwaka 2005 na kupewa jukumu la kujenga nyumba za makazi na biashara kwa ajili ya matumizi ya wananchi.

**Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza jukumu hilo, Shirika kwa sasa linatekeleza miradi kadhaa ya Ujenzi wa Nyumba ambayo ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji kama ifuatavyo:-

- Mradi wa **Samia Housing Scheme (SHS)** ambao unahusisha ujenzi wa nyumba **5000** katika maeneo mbalimbali nchini. Asilimia 50 ya nyumba hizi zitajengwa Mkoa wa Dar es Salaam, asilimia **20** katika mkoa wa Dodoma na asilimia **30** zitajengwa katika mikoa mingine. Mradi huu utakaotekelezwa kwa awamu na utagharimu takriban Shilingi **bilioni 466.** Ujenzi wa nyumba 560 ulianza mwezi Februari, 2023 katika eneo la Kawe, Dar es Salaam ambapo muitikio wake umekua mzuri kwani takribani asilimia **96** zimekwishapata wateja na utagharimu kiasi cha Shilingi **bilioni 48.**

- Mradi wa **Kawe 711(Seven – eleven)** ambao ulikadiriwa kugharimu shilingi **bilioni 105**, ambapo mkandarasi amesharejea kazini ili kukamilisha mradi; na

- Mradi wa **Golden Premium Residence (GPR)** wenye thamani ya shilingi **bilioni 71.1** nao utakamilishwa baada ya kukamilika kwa mazungumzo ya Shirika na Mkandarasi yanayotokana na madai ya gharama zili zotokana na kusimamishiwa mradi.

**Mheshimiwa Spika,** Shirika limekamilisha utekelezaji wa miradi kadhaa ikiwemo mradi wa **Morocco Square** uliokuwa umesimama kwa kukosa fedha. Shirika liliomba kibali cha kukopa kutoka Serikalini na kuruhusiwa kukopa kiasi cha **Shilingi billion 44.7** ajili ya kukamilisha mradi huo ambao umekamilika kwa sasa. Kamati inapenda kumshukuru na Kumpongeza **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassani**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuruhusu Shirika kukopa na kuukwamua mradi huo uliokuwa umesimama toka mwaka 2016. Pamoja na mradi huo, pia Ujenzi wa nyumba **303** eneo la Iyumbu na nyumba **101** Chamwino Mkoani Dodoma umekamilika na mauzo yanaendelea.

**Mheshimiwa Spika,** mafanikio hayo yanaambanatana na changamoto katika uendeshaji wa Shirika, ikiwa ni pamoja na Shirika kushindwa kujenga nyumba za bei nafuu kwa wananchi wengi wa kipato cha chini na kipato cha kati. Hii imekua ikichangiwa na kodi ya ongezeko la thamani (VAT) katika bei za nyumba zinazouzwa na Shirika.

***d) Mradi wa Uboreshaji Usalama wa Milki za Ardhi (LTIP)***

**Mheshimiwa Spika,** Wizara inaendelea kutekeleza Mradi wa LTIP ambao unatekelezwa na fedha za Serikali pamoja na mkopo wa **Dola za Marekani Milioni 150** kutoka Benki ya Dunia katika kipindi cha miaka mitano (2022/23 - 2027/28). Mradi huu unalenga katika maeneo mahsusi manne ambayo ni:-

i. Kuimarisha usalama wa taarifa za miliki za ardhi ambapo **Shilingi bilioni 167.1** zimepangwa kuandaa hati za kimila, leseni za makazi na seleni za mijini kwa ajili ya kupima vijiji **500;**

ii. Ujenzi wa mfumo wa kuhifadhi taarifa za miliki za ardhi kwa ununuzi wa vifaa kwa ajili ya mfumo na kukarabati na kuweka samani katika ofisi za ardhi wilaya na mikoa ambapo zitatumika takribani **Shilingi bilioni 76.93;**

iii. Ujenzi wa Ofisi za ardhi za mikoa 25, ukarabati wa Ofisi za ardhi za wilaya 40 na kusimika vifaa vya mfumo wa ILMIS utakaogharimu kiasi cha **Shilingi bilioni 55;** na

iv. Uendeshaji, uratibu na dharula kwa gharama ya **Shilingi bilioni 46.86** ikiwa na mgawanyo wa **Shilingi bilioni 2.4** kwa ajili ya uendeshaji, **Shilingi bilioni 29.46** kwa ajili ya uratibu na **Shilingi bilioni 17.41** kwa ajili ya dharula.

**Mheshimiwa Spika,** tangu mradi kuanza kuna shughuli mbalimbali ambazo zimetekelezwa ikiwa ni pamoja na Urasimishaji wa makazi **3,640** umefanyika katika zoezi la majaribio lililofanyika katika Halmashauri ya Jiji la Dodoma kwenye mitaa mitatu (3) ya Bihawana, Mapinduzi na Mkwawa. Baada ya majaribio hayo, mradi umeendelea kufanya urasimishaji katika Halmashauri za Jiji la Dodoma, Manispaa za Kahama na Kigoma na Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze ambapo jumla ya vipande vya ardhi **35,785** vimetambuliwa. Kati ya viwanja hivyo, viwanja **23,508** vimepimwa na hatua za umilikishaji zinaendelea. Aidha, jumla ya hati **6,247** zimetolewa katika mkoa wa Dar es Salaam kupitia mpango wa ukwamuaji miradi ya urasimishaji mkoa wa Dar es Salam (Kliniki za Ardhi).

**Mheshimiwa Spika,** wakati wa kupitisha bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Kamati iitoa maoni kuwa Serikali ipitie upya mpango wa matumizi ya fedha za mradi ili kuiwezesha Wizara kutekeleza mpango wa matumizi bora ya ardhi na kuboresha mfumo wa Usimamizi wa ardhi nchini. Kamati inapenda kuipongeza Serikali kwa kuzingatia ushauri wake, ambapo iliongeza vijiji kutoka vijiji **500** katika kipindi chote cha utekelezaji wa mradi hadi kufikia vijiji **700** kwa mwaka huu wa fedha pekee. Aidha, jumla ya mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji **404** imeandaliwa kati ya lengo la vijiji **700** vilivyopangwa katika mwaka 2023/24 ikiwa ni sawa na asilimia **58** ya lengo.

**Mheshimiwa Spika,** haya ni mafinikio makubwa kwa Wizara na Watanzania na ushahidi wa mchango wa Bunge lako Tukufu nani kielelezo kuwa kama Serikali itatekeleza vyema ushauri unaotolewa na Bunge lako Tukufu tunaweza kuleta mapinduzi makubwa na kuondoa migogoro katika sekta ya ardhi nchini. Pamoja na pongezi hizo, bado Kamati inaendelea kusisitiza kuwa Serikali ihakikishe fedha nyingi zaidi zinatengwa kutoka kwenye maeneo mengine ya mradi kwenda kwenye mpango wa matumizi bora ya ardhi ili kuhakikisha inapunguza na kumaliza kabisa migogoro ya ardhi katika maeneo ambayo mradi unatekelezwa.

***e) Programu ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi (KKK)***

**Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kutekeleza Programu ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi kwa kuzikopesha Taasisi na Halmashauri mbalimbali nchini na miradi ya Wizara. Hadi kufikia Disemba, 2023, Viwanja **1,017** vimepimwa katika Halmashauri ya Jiji la Dodoma, Viwanja **7,945** na mashamba **46** vimemilikishwa kati ya viwanja **246,136** vilivyopimwa mwaka 2022/23.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilijulishwa kuwa kumekuwa na kusuasua katika kurejesha fedha za mikopo kwa halmashauri nyingi ili kuhakikisha proramu hii inakuwa endelevu. Hata hivyo, Wizara imeandaa mwongozo wa utekelezaji wa Mfuko wa Mzunguko wa Maendeleo ya Ardhi (Plot Development Revolving Fund) ambao utatoa utaratibu wa namna ya fedha katika Mfuko huu utakavyotumika ili kutekeleza program ya KKK.

**Mheshimwa Spika,** katika kurejesha fedha ambazo halmashauri zilipewa kwa ajili ya kutekeleza program hii, **Shilingi bilioni 21.7** zimerejeshwa kati ya **Shilingi bilioni 50** zilizotolewa kwa halmashauri sawa na **asilimia 43.** Aidha, halmashauri **12** za Ofisi ya ardhi Mkoa wa Iringa zimerejesha fedha zote, halmashauri **44** zimerejesha sehemu ya fedha huku halmashauri za Manispaa ya Shinyanga na Musoma DC zikiwa hazijarejesha kabisa. Kamati inaitaka Wizara kushirikiana na Ofisi ya Rais-TAMISEMI kuhakikisha wanazibana Halmashauri zilizobaki ziweze kurejesha fedha zote ili ziende zikasaidie Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi katika maeneo mengine ya nchi yetu.

*f) Uboreshaji makazi yaliyoharibiwa na maporomoko Wilaya ya Hanang*

**Mheshimiwa Spika,** usiku wa kuamkia siku ya Jumapili ya tarehe 3 Disemba, 2023, nchi yetu ilikumbwa na janga la asili ambapo kutokana na mvua iliyonyesha usiku mzima, ilisababisha sehemu ya Mlima Hanang kumomonyoka, tope lake kushuka chini na kuathiri nyumba na makazi ya watu wa mji mdogo wa Kateshi na kuchukua uhai wa baadhi ya Watanzania wenzetu.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na janga hilo, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan** alitoa agizo kwa mamlaka zote za Serikali kwenda eneo la Hanang chini ya uratibu wa Ofisi ya Waziri Mkuu ili kuweza kuhakikisha maisha ya Watanzania wenzetu yanaokolewa na kurejesha hali ya kawaida ikiwa ni pamoja na kuhakikisha watu waliopata madhara hayo wanajengewa nyumba.

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya kazi kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais-TAMISEMI, kupitia kwa Ofisi ya Ardhi Mkoa wa Manyara na Halmashauri ya Wilaya Hanan'g ilipima viwanja **270** katika eneo la ekari **100** lililomegwa kutoka katika eneo la Jeshi la Magereza lililoko katika Kijiji cha Gidagamowd Wilayani Hanang' Mkoa wa Manyara ikiwemo viwanja **269** vya wahanga wa maporomoko ya ardhi katika mlima Hanan'g na kiwanja kimoja cha eneo la jeshi la magereza vilipimwa na kusajiliwa. Viwanja vilivyopimwa ni viwanja vya makazi, makazi na biashara, eneo la Soko, Shule, Zahanati, Kituo cha Polisi, Kituo cha Zimamoto, maeneo ya wazi, uwanja wa michezo na eneo la Kanisa na Msikiti.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati kupitia Bunge lako Tukufu inatoa pole kwa Mheshmiwa Rais **Dkt. Samia Suluhu Hassan**, Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Mkuu wa Wilaya ya Hanang, Mbunge wa Jimbo la Hanang na wananchi wote wa Wilaya ya Hanang kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inampongeza Mheshimwa Rais, **Dkt. Samia Suluhu Hassani**, Waziri Mkuu Mhe. **Majaliwa Kassim Majaliwa Mb**, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, **Mhe. Jenisther Mhagama Mb,** na Serikali kwa ujumla kwa jinsi walivyoitikia kwa haraka kuoko maisha ya ndugu zetu waliothirika

na janga hilo. Aidha**, K**amati inapongeza Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa namna iliyochukua hatua za haraka katika kupima na kusajili viwanja hivyo.

***g) Maboresho ya Mfumo wa Usimamizi wa Ardhi***

**Mheshimiwa Spika,** Wizara imeanza kuboresha Mfumo wa usiamamizi wa Ardhi kidijitali ili kuleta ufanisi katika utoaji huduma, kupunguza malalamiko na kutenda haki miongoni mwa wananchi. Hadi Desemba, 2023 Mfumo ulikuwa umekamilika kwa asilimia 88 na unatarajia ifikapo mwezi Juni, 2024 mikoa mitano (5) ya Arusha, Tanga, Mbeya, Mwanza, na Dodoma itakuwa imefikiwa na Mfumo huo. Mikoa mingine inatarajiwa kufikiwa kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na maboresho mengine yatakayokuja kutokana na mahitaji, mfumo huo unategemea kumuwezesha mwananchi Kujisajili na kuomba huduma wenyewe kupitia Mfumo (online) bila kulazimika kwenda Ofisi za Ardhi kuomba huduma hizo; Kufahamu muda ambao huduma inayoombwa itakamilika.

**Mheshimiwa Spika,** uboreshaji huo wa mfumo utawapa wananchi uwezo wa kutoa taarifa endapo watacheleweshewa huduma; Mfumo utaondoa changamoto ya upotevu wa nyaraka zinazowasilishwa na wananchi kuomba huduma, kwani zitakuwa zinawasilishwa kupitia mfumo (online); na Mfumo utaongeza uoni (visibility) kwa viongozi wa ngazi mbalimbali wa Wizara kuona utendaji wa majukumu unavyoendelea katika ngazi mbalimbali.

**Mheshimiwa Spika,** Mfumo huu unakusudia kuanzisha Ardhi Kiganjani App itakayomuwezesha mwananchi anayeomba huduma inayotakiwa kulipiwa atapata Namba ya Malipo (Control Number) kwenye dashboard au simu yake ya kiganjani bila kuhitaji kwenda Ofisini kuipata.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha inatenga fedha za kutosha ili mfumo huu uweze kuanza kazi nchi nzima.

***h) Changamoto katika Kulipa Fidia ya Ardhi kwenye maeneo yanayotwaliwa kwa ajili ya Miradi ya Serikali na Uwekezaji***

**Mheshimiwa Spika,** Fidia ni malipo yanayotolewa kwa mtu au taasisi kama mbadala wa mali yake au kutokana na kuondolewa kwenye eneo lake linalotwaliwa kwa manufaa ya umma au kupangiwa matumizi mengine tofauti na yale yaliyopo kwa sasa. Ili kukadiria kiasi cha fidia kitakacholipwa kwa mwananchi ambaye mali zake zimetwaliwa kwa manufaa ya umma, sheria inaelekeza kuwa thamani ya mali hizo zinapaswa kukadiriwa na mthamini aliyesajiliwa na bodi ya wathamini.

**Mheshimiwa Spika,** uthamini wa fidia kwa miradi mbalimbali yenye manufaa kwa umma inayotekelezwa na Serikali inasimamiwa na sheria mbalimbali ikiwemo Sheria ya utwaaji ya Mwaka 1967, Sheria ya Ardhi Na. 4 ya Mwaka 1999 na kanuni zake za mwaka 2001, Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na. 5 vya Mwaka 1999 na Sheria ya Uthamini na Usajili wa Wasajili ya Mwaka Na. 7 ya mwaka 2016 na kanuni zake za mwaka 2018.

**Mheshimwa Spika,** Aidha, Waraka wa Fidia namba 1 wa mwaka 2015 uliweka hitaji la kikanuni kuwa kila mamlaka inayotwaa Ardhi inapaswa kuthibitisha kwa barua kuwa inao uwezo na iko tayari kulipa kiasi cha fidia kilichooneshwa katika jedwali la fidia ili kuhakikisha kuwa fidia ya mali za wananchi inalipwa kwa wakati na kuipunguzia Serikali au mwekezaji riba na gharama za kurudia kufanya uthamini.

**Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 7 cha sheria ya Uthamini Sura 138 pamoja na kanuni ya 51 ya sheria hiyo imempa Mthamini Mkuu mamlaka ya kufanya Uhakiki wa Uthamini wa ardhi na maendelezo yake kabla Serikali au mwekezaji kuitwaa Ardhi hiyo. Hata hivyo, Kamati inatambua mamlaka ya Taasisi nyingine za Serikali katika kujiridhisha na taarifa za uthamini kabla ya kufanya malipo (Financial Verification). Changamoto iliyopo ni utaratibu wa ufanyaji uhakiki huo ambapo Wizara ya Fedha huwa wanafanya uhakiki baada ya majedwali ya fidia kuidhinishwa na Mthamini Mkuu na wananchi kuonyeshwa majedwali ya fidia (Disclosure).

**Mheshimiwa Spika,** Kamati iligundua kuwa ili kukabiliana na changamoto hiyo hapo juu, Kifungu cha 173 cha Sheria ya Ardhi Na. 4 ya mwaka 1999 ilianzisha Mfuko wa Fidia ya Ardhi kwa madhumuni ya kulipa fidia kwa mtu au Taasisi iliyopoteza haki au maslahi katika ardhi kutokana na kutwaliwa kwa Ardhi yake kupisha shughuli za Maendeleo zinazofanywa na Serikali au Uwekezaji wa taasisi au mtu binafsi. Aidha, Mfuko huu upo chini ya Wizara ya Ardhi na umekosa tija kwani Taasisi zinazotwaa ardhi haziweki fedha za kulipa fidia kwenye huu mfuko kwa mujibu wa Sheria, hivyo kupelekea mfuko huu kutokufanya kazi iliyokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika,** hali hii inachangia katika kuzalisha migogoro kati ya wananchi na Serikali au muwekezaji, kulipa riba kutokana na kuchelewesha kulipia fidia, mlundikano wa kesi za Ardhi katika mabaraza ya Ardhi na Mahakamani na kuwafanya wananchi kuwa masikini kinyume na kusudio la Serikali la kuhakikisha ustawi katika maisha ya wananchi wake.

***i) Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi Nchini***

**Mheshimiwa Spika,** kumekuwa na migogoro ya matumizi ya ardhi nchini ambayo inahusisha ama wananchi wenyewe au wananchi na Serikali katika maeneo mbalimbali nchini. Migogoro hiyo imekuwa chanzo cha uvunjifu wa amani na kusababisha madhara kwa wananchi na mali zao kwa upande mmoja na uharibifu wa miundombinu, mazingira, hifadhi na vyanzo vya maji kwa upande mwingine.

**Mheshimiwa Spika,** katika kutatua changamoto hiyo, pamoja na juhudi zingine, Serikali iliamua kuunda Kamati Maalum ya Mawaziri nane (8) wa kisekta ambapo ilibainisha uwepo wa vijiji na mitaa 975 vyenye migogoro ya matumizi ya ardhi nchini. Kamati inatambua juhudi na kuipongeza Serikali kwa hatua inazochukua katika kutatua migogoro hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** katika kujadili na kuchambua taarifa ya utendaji ya Kamati ya Mawaziri 8, Kamati ilibaini kuwa kumekuwa na changamoto kadhaa katika utendaji wa Kamati hiyo ikiwa ni pamoja na malalamiko kutoka kwa wananchi na wawakilishi wao kwamba hawashirikishwi kikamilifu katika utekelezaji wa maazimio

ya Serikali kuhusiana na utatuzi wa migogoro iliyobainika katika maeneo hayo.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

### 3.1 Maoni ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, yafuatayo ni maoni ya Kamati kuhusu shughuli zilizotekelezwa katika kipindi cha kuanzia Februari 2023 hadi Januari 2024 ambayo yanabainisha mtazamo wa kile kilichojiri wakati Kamati ikitimiza majukumu yake.

#### 3.1.1 Wizara ya Maliasili na Utalii

i) Serikali iweke mikakati ya kulinda maeneo yaliyohifadhiwa na kuweka alama za kudumu na zenye kuonekana ili kudhibiti uvamizi wa shughuli za kibinadamu;

ii) Serikali ichukue hatua madhubuti za kutoa elimu na kuwashirikisha Wananchi katika shughuli za uhifadhi wa rasilimali za misitu ili kunusuru misitu yetu nchini;

iii) Serikali iweke mkakati wa kuvitambua, kuviendeleza na kuvitangaza vivutio vyote vya utalii nchini ikiwa ni pamoja na utalii wa malikale, utalii wa fukwe za bahari, uvuvi, utamaduni na maeneo mengine;

iv) Serikali iajiri Askari Uhifadhi wa kutosha ili kuimarisha doria na kukabiliana na ujangili pamoja na kuzuia athari za wanyama wakali na waharibifu;

v) Serikali ione umuhimu wa kuwatumia Mabalozi wetu katika nchi mbalimbali duniani kutangaza na kuhamasisha utalii ili kuongeza idadi ya watalii na mapato yatokanayo na utalii.

vi) Wizara kwa kushirikiana na Wizara za Ardhi iandae mpango wa matumizi bora ya ardhi ili kupunguza migogoro baina ya hifadhi na wananchi;

vii) Kuweka mikakati ya kuchimba mabwawa na visima vya maji kwa ajili ya wanyamapori kwenye maeneo ambayo yana

upungufu wa maji ili kupunguza kasi ya wanyama hao kuvamia maeneo ya makazi ya wananchi kutafuta maji; na

viii) Elimu itolewe kwa wananchi kuhusu maeneo ya shoroba za wanyamapori ili kupunguza muingiliano kwa wanyama na binadamu hali inayoathiri wananchi wanaoishi maeneo hayo katika shughuli zao za kiuchumi, kuwasababishia umasikini, njaa na wakati mwingine ulemavu au kupoteza maisha.

### 3.1.2 Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

i) Kutokuwepo kwa mabaraza ya Ardhi na Nyumba kila wilaya nchini kumesababisha baadhi ya wananchi kulazimika kusafiri umbali mrefu kufuatilia mashauri yao. Serikali iharakishe kuanzisha mabaraza haya katika Wilaya 43 zilizobaki ili kusogeza huduma kwa wananchi;

ii) Serikali ibuni mbinu mbalimbali za kuhamasisha wananchi kulipa kodi za ardhi, kama vile kufanya matangazo kwenye mikusanyiko mbalimbali;

iii) Serikali iendelee kutoa elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu wa kuzingatia mpango wa matumizi ya ardhi sambamba na ushirikishwaji wa wananchi;

iv) Serikali ihakikishe inaendelea kubuni kutekeleza mipango mbalimbali itakayoendelea kupunguza migogoro ya Ardhi nchini; na

v) Serikali kupitia Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) ihakikishe inabuni na kujenga nyumba za bei nafuu kwa wananchi wa kipato cha chini na cha kati.

## 3.2 MAPENDEKEZO

### 3.2.1 Maboresho ya eneo la hifadhi ya ngorongoro

**KWA KUWA**, Serikali imepiga hatua nzuri katika kuhakikisha kuwa inainusuru Hifadhi ya Ngorongoro ambayo ilikuwa katika hatari ya kutoweka kutokana na ongezeko kubwa la watu na shughuli zao kinyume na lengo la uanzishwaji wake;

**NA KWA KUWA**, zoezi linaloendelea la kuhamisha kwa hiari wakazi wanaoishi ndani ya hifadhi hii kuwapeleka maeneo mengine nje ya hifadhi limeonesha mafanikio makubwa baada ya wakazi wengi kukubali kuhama kwa hiari;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba;

(i) Serikali iongeze kasi katika ujenzi wa nyumba na miundombinu wezeshi ikiwa ni pamoja na kuongeza kasi ya ujenzi wa majosho, malambo, na maandalizi ya vitalu ya malisho ya mifugo ili kukamilisha zoezi la kuhamisha wakazi wa Ngorongoro kwa hiari;

(ii) Serikali ihakikishe inaunda timu ya wataalaamu kutoka katika Wizara za Kisekta ili kufanikisha uratibu wa zoezi la kuhamisha wakazi wa Ngorongoro kwa hiari; na

(iii) Serikali ihakikishe inaendesha zoezi la ujenzi wa miundombinu yote iliyopangwa kwenye maeneo ya Msomera, Kitwai na Saunyi kwa kutumia Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) ambao wameonyesha ufanisi wa hali ya juu katika zoezi la ujenzi wa nyumba 5000 linaloendelea kwa sasa. Hii itachangia miundombinu yote kukamilika kwa ujumla, kupunguza gharama za utekelezaji wa mradi na kurahisha zoezi la kuhamisha wakazi wa Ngorongoro kwa hiari.

### 3.2.2 Utekelezaji wa bajeti kwenye miradi ya maendeleo kwa Wizara ya Maliasili na Utalii

**KWA KUWA**, hadi kufikia Disemba, 2023, Wizara na Taasisi zake ilikuwa imepokea kiasi cha takribani **Shilingi bilioni 30.2** sawa na **asilimia 17.7** tu ya fedha za miradi ya maendeleo iliyoidhishiwa na Bunge lako Tukufu;

**NA KWA KUWA**, hali hii inachangia kuzorota na kusuasua kwa utekelezaji wa miradi ya maendeleo, ikiwa ni pamoja na kushindwa kufanya ukarabati wa miundombinu kwenye vivutio vya utalii, kushindwa kutangaza utalii kwenye masoko mapya, kushindwa kukuza na kuendeleza mazao mapya ya Utalii,

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba, Serikali ihakikishe inaongeza kasi ya kutoa fedha za miradi ya maendeleo

iliyoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Wizara na Taasisi zake ili kutekeleza miradi ya maendeleo kutoka **aslimia 30** ya sasa hadi kufikia **asilimia 100** katika mwisho wa mwaka huu wa fedha hali itakayochangia kukuza uchumi wa nchi kupitia sekta ya Utallii.

**3.2.3 Kuanzishwa kwa Akaunti Maalumu (Escrow Account) kwa ajili ya kuimarisha Uhifadhi na Kutangaza Utalii**

**KWA KUWA**, kwa kuwa hakuna mgogoro wowote ule wa mgawanyo wa fedha kati Hazina na Wizara ya Maliasili na Utalii na Taasisi zake, ambao ungepelekea kuanzishwa kwa akaunti hii;

**NA KWA KUWA,** kuanzishwa kwa akaunti hii kutapalekea matumizi ya fedha za umma kushindwa kufanyiwa ukaguzi na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa utaratibu wa kawaida;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba: -

i. Serikali isitishe mara moja kuanzishwa kwa akaunti hiyo hali inayoweza kupelekea fedha za umma kutumika bila usimamizi na uwajibikaji; na

ii. Serikali ifanye Marekebisho ya Sheria ya **Fedha Na.8 /2020** kwa lengo la taasisi hizi kubaki na sehemu ya makusanyo yake (retention) ili kuzisadia Taasisi hizi kutekeleza majukumu yake ya Uhifadhi kwa ufanisi.

**3.2.4 Changamoto za Wanyamapori Wakali na Waharibifu**

**KWA KUWA**, muingiliano baina ya binadamu na wanyamapori katika kushindania rasimali za asili ikiwa ni pamoja na chakula na maji;

**NA KWA KUWA**, muingiliano huo unaathiri shughuli za wananchi na kupelekea uharibifu wa mazao na mali nyingine, ulemavu, na hata kupoteza maisha; **KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba: -

(i) Serikali ihakikishe inaongeza kasi ya ujenzi wa vituo vya udhibiti wa wanyama wakali na waharibifu nchini ikiwa ni

pamoja na kuongeza askari wa Uhifadhi ili kupunguza athari kwa wananchi;

(ii) Serikali kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii na TAWIRI ihakikishe inatafuta teknolojia ya kudhibiti na kukabiliana na changamoto za wanyama wakali na waharibifu;

(iii) Serikali ihakikishe inakamaliisha zoezi la kuongoa Shoroba za Wanyama wakali na waharibifu 18 ilizojipangia katika mwaka wa Fedha 2023/2024 ili kupunguza muingiliano wa shughuli za Wananchi na Wanyama hao; na

(iv) Serikali ihakikishe inafanya marejeo ya Kanuni za Malipo ya Kifuta Machozi/Jasho ya Mwaka 2011 ili kuboresha viwango kwa aliyeathirika na wanyama wakali na waharibifu ili kuendana na hali maisha ya sasa.

**3.2.5 Kutungwa Kwa Sheria ya Uendeshaji wa Mamlaka ya Wanyamapori Tanzania (TAWA) na Mchakato wa kupandisha hadhi Wakala wa Misitu Tanzania (TFS)**

**KWA KUWA**, Taasisi hizi za Uhifadhi zinaongozwa na Bodi za Ushauri, ambazo zina nguvu ndogo ya uwajibikaji;

**NA KWA KUWA**, hali hii inaathiri utendaji wa taasisi hizi wa kukokosa nguvu ya kisheria katika kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba,

i. Serikali ihakikishe inaandaa na kuleta Bungeni Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Wanyamapori Tanzania (TAWA) ; na

ii. Serikali iharakishe mchakato wa kuipandisha hadhi Wakala wa Misitu Tanzania (TFS) kuwa Mamlaka ili kuipa nguvu ya kisheria ya kusimamia na kudhibiti matumizi ya rasilimali za misitu yote nchini

### 3.2.6 Kutangaza vivutio vya Utalii Nchini

**KWA KUWA**, sekta ya utalii ina mchango mkubwa katika uchumi wa Taifa kwa kuchangia zaidi ya **asilimia 25** ya mauzo yote ya nje, huku ikichangia takribani **asilimia 20** ya pato la Taifa na kutoa takribani **asilimia 11** ya ajira nchi; **NA KWA KUWA,** sekta hii ilianguka kwa kiasi kikubwa kutokana na mlipuko wa janga la UVIKO – 19, huku ikikabiliwa na ushindani mkubwa toka nchi jirani;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba: -

(i) Serikali itekeleze mikakati ya kutangaza Utalii chini ya Bodi ya Utaii Tanzania ili idadi ya Watalii izidi kuongezeka na kufikia lengo lililowekwa katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2020-2025; na

(ii) Serikali ianzishe Mfuko wa Maendeleo ya Utalii **(Tourism Development Fund-TDL)** ambao utachangiwa na asilimia moja (1%) ya mauzo yote ya nje yanayoingia nchini kutokana na shughuli za Utalii.

### 3.2.7 Changamoto za Taasisi za Utafiti za (TAFORI & TAWIRI)

**KWA KUWA**, Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania (TAFORI) na Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori (TAWIRI) zinakabiliwa na changamoto ya ufinyu wa bajeti na changamoto ya upungufu wa wafanyakazi na vitendea kazi;

**NA KWA KUWA**, changamoto hizi zinaathiri ufanisi wa taasisi hizo katika kufanya, kusimamia, kuratibu tafiti na kutoa ushauri wa kitaalam katika sekta husika ya Uhifadhi na Utalii nchini;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba: -

(i) Serikali ihakikishe Taasisi hizi zinaongezewa bajeti na kupelekewa fedha kwa wakati ili ziweze kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria; na

(ii) Serikali ihakikshe inatoa kibali cha kuajiri kwa taasisi hizi ili kuziba pengo wafanyakazi lililopo kwa sasa hali itakayoongeza ufanisi na tija katika utendaji wa taasisi hizi**.**

### 3.2.8 Azimio la Bunge la kuridhia mapendekezo ya kurekebisha mpaka wa Hifadhi ya Taifa ya Ruaha

**KWA KUWA,** Taifa linahitaji uhifadhi wenye tija ambao ni endelevu usiokuwa na migogoro ya mipaka kati ya maeneo ya hifadhi na ardhi za vijiji;

**NA KWA KUWA,** utekelezaji wa azimio hili la Bunge ulilenga kusaidia kulinda mifumo ya ikolojia katika Bonde la Usangu ili kurejesha uoto wa asili kwenye Hifadhi ya Taifa ya Ruaha na kuimarisha mtiririko endelevu wa maji katika Mto Ruaha Mkuu ambao unategemewa katika uzalishaji wa Umeme wa Maji katika vituo vya Mtera, Kidatu na Mwalimu Nyerere;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba, Serikali itekeleze Azimio la Bunge na masharti yake kama yalivyowasilishwa na Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii na taarifa ya utekelezaji huo iwasilishwe Bungeni kama ilivyoahidi.

### 3.2.9 Mradi wa Usimamizi wa Maliasili Endelevu na Ukuaji wa Utalii Kanda ya Kusini (REGROW)

**KWA KUWA,** mradi umeelekezwa katika Hifadhi za Taifa za Ruaha, Mikumi, Udzungwa, Nyerere na Hifadhi ya Msitu wa Asili wa Kilombero,

**NA KWA KUWA,** lengo la mradi ni kuhakikisha kuna usimamizi wa Maliasili endeleu na Utalii wa Kanda ya Kusini unakuwa endelevu na wenye tija,

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba,

i. Katika awamu ya pili ya mradi ihakikishe inapanua wigo kwa kuongeza idadi ya Hifadhi katika eneo la Kusini ili kuchochea Utalii katika kanda ya Kusini kama ilivyolengo la mradi; na

ii. Serikali ihakikishe miradi yote inayotekelezwa kupitia REGROW inakamilika ndani ya muda ili kukuza utalii wa eneo la kusini, kuongeza mapato ya Serikali na kuinua uchumi wa watu wanaoishi kuzunguka hifadhi zinazotekeleza mradi huo.

### 3.2.10 Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori (WMAs)

**KWA KUWA,** WMAs zinafanya kazi kubwa katika uhifadhi kwa kudhibiti ujangili wa wanyamapori na kutatua changamoto ya muingiliano wa binadamu na wanyama wakali na waharibifu;

**NA KWA KUWA,** utekelezaji wa jukumu hilo unahitaji fedha ambazo zinatokana shughuli zinazofanywa katika WMAs ambazo hukusanywa moja kwa moja na Serikali, na Serikali imekuwa ikichelewesha kurejesha fedha hizo kwenye WMAs;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba: -

i. Serikali ihakikishe inarejesha kiasi chote za fedha kinachostahili kurejeshwa kwenye WMAs kwa mujibu wa Kanuni ili kuziwezesha katika kuendesha na kuratibu shughuli zao kwa ufanisi;

ii. Serikali iandae mpango wa ukusanyaji wa mapato ambao utatofautisha mapato ya Serikali na yale ya WMAs ili fedha za Jumuiya hizi ziende moja kwa moja kwenye akaunti zao; na

iii. Serikali ishughulikie na kutatua migogoro ya mipaka kati ya maeneo ya hifadhi na WMAs mbalimbali nchini.

### 3.2.11 Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi

**KWA KUWA**, migogoro mingi ya ardhi nchini inasababishwa na ardhi kutokupangiwa matumizi, ambapo hadi sasa ni vijiji **3,681** tu vilivyopangiwa matumizi ya ardhi kati ya vijiji **10,744** vilivyopimwa nchini,

**NA KWA KUWA**, Kasi ndogo ya upangaji inatokana na ufinyu wa bajeti inayotengwa kwa Tume ya Taifa ya Matumizi ya Ardhi ambayo imepewa jukumu la kupanga matumizi ya ardhi nchi nzima,

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba: -

(i) Serikali iongeze kasi ya kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi katika vijiji vyote vilivyopimwa Nchini; na

(ii) Serikali iendelee kuongeza fedha za maendeleo kwa Tume ili kuhakikisha kila kipande cha ardhi nchini kinapangiwa matumizi hali itakayochochea ukuaji wa uchumi kwa kuongeza uzalishaji na kupunguza migogoro ya Ardhi

**3.2.12 Maboresho ya Mfumo wa Usimamizi wa Ardhi Nchini**

**KWA KUWA,** Serikali imedhamiria kuboresha mfumo wa Usimamizi wa Ardhi Nchini ikiwa ni utekelezaji wa Azimio la Bunge;

**NA KWA KUWA**, lengo la kuboresha mfumo huo ni kuhakikisha Serikali inaongeza kasi ya kuwahudumia wananchi, kupunguza migogoro ya ardhi nchini na kupunguza malalamiko ya wananchi katika kupokea huduma toka kwa watumishi wa sekta ya ardhi nchini;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba: -

(i) Serikali kuhakikisha Mfumo huo unakuwa rafiki kwa watumiaji na uzinduliwe haraka ili kutimiza malengo yaliyokusudiwa; na

(ii) Serikali inatoa elimu ya matumizi ya mfumo kwa wananchi kupitia vituo vya Televisheni, radio na njia mbadala za habari ikiwemo mitandao ya kijamii ili wananchi wengi waufahamu mfumo na kuutumia kwa urahisi hali itakayopelekea lengo la maboresho ya mfumo kufikiwa.

**3.2.13 Shirika la Nyumba la Taifa (NHC)**

**KWA KUWA,** lengo la kuanzishwa kwa Shirika ni kujenga nyumba za Makazi na Biashara kwa ajili ya kuwauzia wananchi wenye kipato cha hali zote;

**NA KWA KUWA**, Kumekuwa na malalamiko toka kwa Wananchi kuwa Shirika lina jenga nyumba zenye gharama za juu bila kuzingatia utofauti wa kipato miongoni mwa wananchi ambayo

yanatokana na kodi ya ongezeko la thamani (VAT) katika miradi ya Shirika;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba: -

i. Serikali ilisaidie Shirika kutimiza adhma yake kwa kuondoa kodi ya ongezeko la thamani (VAT) kwa nyumba zinauzouzwa kwa bei isiyozidi **Shilingi milioni 100** badala ya **Shilingi milioni 50** ya sasa; na

ii. Shirika kuhakikisha linaandaa mpango wa kutoa elimu kwa umma juu ya fursa mbalimbali zitakazowawezesha wananchi wa vipato vya kawaida kumiliki nyumba kupitia miradi ya Shirika.

### 3.2.14 Mradi wa Uboreshaji Usalama wa Milki za Ardhi (LTIP)

**KWA KUWA,** Serikali ya Tanzania imepata mkopo kutoka Benki ya Dunia wa **Shilingi Bilioni 345** kwa lengo la kuimarisha usalama wa taarifa za ardhi, kuimarisha miundombinu ya upimaji na kujenga majengo ya Ofisi nchini;

**NA KWA KUWA**, fedha hizi za kama Mkopo utatakiwa kulipwa kwa riba;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba: -

i. Serikali ihakikishe inaendelea kuongeza fedha za mradi katika eneo la kupanga matumizi bora ya ardhi ili kupunguza na kuondoa migogoro ya ardhi katika maeneo ambayo mradi unatekelezwa; na

ii. Serikali ihakikishe inatoa elimu kwa wananchi ambao mradi unatekelezwa ili waweze kuchukua hati zao za kimila, hatimiliki na leseni za makazi hali itakayowawezesha kuwa na umiliki rasmi wa ardhi hivyo kuwawezesha kupata huduma na faida zinazoambana na umiliki rasmi wa ardhi nchini.

### 3.2.15 Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi Nchini

**KWA KUWA,** Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi iliona ni vyema kuzishirikisha Mamlaka za Serikali za Mitaa kurahisisha zoezi hili;

**NA KWA KUWA**, lengo la Wizara kuzikopesha ilikuwa ni kuhakikisha fedha hizi zinazunguka katika Halmashauri zote nchini ili kusaidia katika kupanga, kupima na kumilikisha ardhi wananchi;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba: -

i. Serikali kupitia Wizara ya Ardhi kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais-TAMISEMI ihakikishe inazisimamia Halmashauri zote kurudisha kiasi cha **Shilingi bilioni 28.3** walizokopeshwa kwenye mradi huu ili ziweze kutumiwa na Wizara ya sekta katika kuendelea Kupanga, Kupima na Kumilikisha ardhi kwenye Halmshauri zingine;

ii. Serikali kupitia Wizara ya Ardhi ihakikishe inakamilisha utekelezaji wa Mfuko wa Mzunguko wa Maendeleo ya Ardhi (Plot Development Revolving Fund) ili kuratibu namna bora ya matumizi ya fedha katika Mfuko katika utekelezaji wa Programu ya KKK.

### 3.2.16 Ukusanyaji wa Maduhuli ya Serikali kupitia Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

**KWA KUWA,** Serikali iliamua ukusanyaji wa kodi ya pango la ardhi (Land Rent) ufanywe na Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini ili kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato yatokanayo na pango la Ardhi;

**NA KWA KUWA**, uamuzi huo umetoa matokeo hasi hadi kufikia nusu ya kwanza ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2023/2024, kwani hadi kufikia Januari, 2024 hakuna halmashauri yoyote nchini iliyokuwa imekusanya kodi hii;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba: -

i. Serikali irudishe jukumu la ukusanyaji wa kodi ya pango la ardhi katika Wizara ya Ardhi ambayo ndio ina nyezo za kisheria na kimfumo katika kutekeleza jukumu hilo; na

ii. Serikali iiwezeshe kifedha Wizara ya Ardhi ili itimize vyema jukumu la kukusanya kodi hii kwani hadi kufikia Januari, 2024, Wizara imekuwa ikutumia fedha zake zenyewe yaani OC katika kuhakikisha zoezi la ukusanyaji wa kodi ya pango la ardhi nchini haukwami;

iii. Serikali kupitia Wizara ya Ardhi ihakikishe inaongeza nguvu katika kukusanya maduhuli kwani hali ya sasa ya ukusanyaji wa mapato sio ya kuridhisha.

### 3.2.17 Changamoto ya Kulipa Fidia katika Ardhi inayotwaliwa na Serikali na Wawekezaji toka kwa Wananchi

**KWA KUWA,** nia ya Serikali na Wawekezaji katika kutwaa Ardhi ni nzuri kwani inahusisha ujenzi na upunuzi wa miradi ya maendeleo kwa ajili ya wananchi;

**NA KWA KUWA,** ni takwa la kisheria kuwa wananchi wanaokutwa na miradi ya maendeleo katika Ardhi inayotwaliwa ni lazima walipwe fidia stahiki baadha ya uthamini kuwa umeidhinishwa na Mthamini Mkuu wa Serikali;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba: -

i. Serikali ihakikishe kuwa kunakuwa na uthibitisho wa uwepo wa fedha za kulipa fidia ambao utatolewa na Wizara/ taasisi mtwaaji au mwekezaji anaekusudia kutwaa ardhi husika. Hii itasadia kuweka msisitizo kuwa kama hakuna fedha za kulipa fidia basi zoezi la utwaaji ardhi lisubiri mpaka fedha za kulipa zitakapokuwepo;

ii. Serikali ihakikishe kuwa kwa kushirikiana na wadau wote muhimu wa utwaaji inafanya Uhakiki kabla ya Mthamini Mkuu kuidhinisha majedwali ya fidia, na kabla ya hatua ya Uoneshaji majedwali hayo kwa wananchi (Disclosure Stage) kufanyika, hii itasaidia kurekebisha dosari zote ndani ya muda sahihi na kuhakikisha wananchi wanalipwa kwa wakati; na

iii. Serikali ihakikishe mfuko wa Fidia ya Ardhi unasimamiwa na Wizara ya Fedha ili kuwe na Mtiririko sahihi wa upatikanaji wa fedha kwa miradi yote inayohusisha Serikali kwa ajili ya fidia hali itakayompa nafasi Mlipaji Mkuu wa Serikali kuweza kuzitaarifu taasisi zote za umma zinazokusudia kutwaa ardhi hakikisho la uwepo wa fedha za fidia.

**3.2.18 Utatuzi wa migogoro ya Ardhi nchini**

**KWA KUWA** , kumekuwa na malalamiko katika utendaji wa Kamati ya Mawaziri nane (8) wa kisekta katika utatuzi wa migogoro katika vijiji na mitaa 975;

**NA KWA KUWA,** malalamiko hayo yanaathiri utekelezaji wa utatuzi wa migogoro katika vijiji hivyo na Utekelezaji wake umechukua muda mrefu;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kuwa;

i. Serikali ihakikishe Kamati hiyo inashirikisha wananchi na wawakilishi wao ili kutatua migogoro katika vijiji na mitaa 975 na uwe shirikishi na wa kudumu; na

ii. Serikali ihakikishe inakamilisha utekelezaji wa zoezi la kutatua miggogoro hiyo.

**SEHEMU YA NNE**

**4.0 HITIMISHO NA KUFUNGA HOJA**

**4.1 Hitimisho**

**Mheshimiwa Spika**, Kwa namna ya kipekee napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Taarifa hii mbele ya Bunge lako mafanikio ya Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii katika kutekeleza Shughuli zake kwa kipindi cha Februari 2023 hadi Januari, 2024 yametokana na juhudi, weledi pamoja na umahiri mkubwa wa Wajumbe katika kushiriki na kutoa maoni yenye tija wakati wote ambapo Kamati imekuwa ikiisimamia Serikali. Ni wazi kwamba, ufanisi wa utendaji wa Kamati hii unatokana zaidi na Ofisi yako kuwajengea uwezo Wabunge na kuwapa msaada stahiki wa kitaalam, na kiushauri wakati wote. Kwa heshima kubwa ningependa kuwataja majina yao. Hata hivyo, kutokana na ufinyu wa muda naomba majina yao yaingizwe kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge (Hansard). Majina hayo ni haya yafuatayo: -

1. Mhe. Timotheo P. Mnzava, Mb - **Mwenyekiti**
2. Mhe. Najma Murtaza Giga, Mb -**/Mwenyekiti**
3. Mhe. Alaudin Hasham Salim, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Cecilia Daniel Paresso, Mb - Mjumbe

| | | |
|---|---|---|
| 5. | Mhe. Asia Abdulkarimu Halamga, Mb | - Mjumbe |
| 6. | Mhe. Khalifa Salum Suleiman, Mb | - Mjumbe |
| 7. | Mhe. Askofu Josephat M. Gwajima, Mb | - Mjumbe |
| 8. | Mhe. Neema William Mgaya, Mb | - Mjumbe |
| 9. | Mhe. Innocent Bilakwate, Mb | - Mjumbe |
| 10. | Mhe. Maida Hamadi Abdallah, Mb | - Mjumbe |
| 11. | Mhe. Oliver Daniel Semuguruka, Mb | - Mjumbe |
| 12. | Mhe. Taska Restituta Mbogo, Mb | - Mjumbe |
| 13. | Mhe. Lucy Thomas Mayenga, Mb | - Mjumbe |
| 14. | Mhe. Suleiman Haroub Suleiman, Mb | - Mjumbe |
| 15. | Mhe. Munira Mustafa Khatibu, Mb | - Mjumbe |
| 16. | Mhe. Dkt Florence G. Samizi, Mb | - Mjumbe |
| 17. | Mhe. Emmanuel A. Mwakasaka, Mb | - Mjumbe |
| 18. | Mhe. Festo Richard Sanga, Mb | - Mjumbe |
| 19. | Mhe. Josephine Thabita Chagula, Mb | - Mjumbe |
| 20. | Mhe. Shaban Omari Shekilindi, Mb | - Mjumbe |
| 21. | Mhe. Ester Lukago Midimu , Mb | - Mjumbe |
| 22. | Mhe. Mussa Omar Salim, Mb | - Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mhe. Jerry W. Silaa (Mb), na Naibu wake Mhe. Geofrey M. Pinda, (Mb) Waziri wa Maliasili na Utalii Mhe. Angela J. Kairuki (Mb) na Naibu wake Mhe. Dunstan L. Kitandula, (Mb) Makatibu Wakuu, Naibu Makatibu Wakuu pamoja na watendaji wote wa Wizara hizo kwa ushirikiano waliouonesha katika kipindi chote ambacho Kamati imekuwa ikitekeleza majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika**, mwisho lakini sio kwa umuhimu, nawashukuru Watunishi wote wa Bunge chini ya uongozi thabiti wa Katibu wa Bunge Ndg. Nenelwa J. Mwihambi, *ndc* kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo wakati wote.

### 4.2 Hoja

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kueleza shughuli zilizotekelezwa na Kamati, uchambuzi wa matokeo ya utekelezaji shughuli hizo, na pia maoni na mapendekezo ya Kamati, sasa naomba kutoa hoja kwamba, Bunge sasa lipokee, kujadili na hatimaye kuikubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii pamoja na maoni na mapendekezo yaliyomo katika taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

Timotheo P. Mnzava, Mb
**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII**
08 Februari, 2024.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maliasili na Utalii, hoja imeungwa mkono. Sasa tunaendelea na uchangiaji. *(Makofi)*

Tutaanza na Mheshimiwa Askofu Josephat Gwajima, atafuatiwa na Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi. Mheshimiwa Munira Mustapha Khatib na Mheshimiwa Dkt. Florence George Samizi, wajiandae. Mnaweza kuchangia kwa dakika 15. Mheshimiwa Josephat Gwajima.

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kukushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nichangie kwenye hii taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maliasili na Utalii. Kwanza nakushukuru wewe na pia namshukuru Mwenyekiti wa Kamati yetu ndugu Mnzava pamoja na wewe ambaye ni Mwenyekiti lakini ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuanza na Wizara ya Maliasili, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Wizara hii iliidhinishiwa kiasi cha shilingi bilioni 163 na katika fedha hizo Bunge liliidhinisha kiasi cha shilingi bilioni 82 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kwenye hizo fedha za miradi ya maendeleo kuna kiasi kama shilingi bilioni 14 ni fedha ya ndani na kuna shilingi bilioni *68.1* ni fedha ya nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ilikuwa na makusudio ya kukusanya shilingi bilioni 300 lakini mpaka kufikia Desemba 2023, Wizara hii imekusanya shilingi bilioni 76 peke yake. Ambayo ni asilimia 26 tu ya malengo yake ya kukusanya mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni *disaster*, tena ni *disaster* kweli kweli; lakini bado wizara hii imetumia fedha. Yenyewe imekusanya shilingi bilioni 76 lakini yenyewe tayari imepokea fedha shilingi bilioni 194.8. Imepokea kutoka wapi kama yenyewe haina uwezo wa kukusanya? Ni kitu gani kinafanya hii wizara *giant* ambayo ardhi yote ya Tanzania iko chini yake, nyumba zote za Tanzania ziko chini yake na ishindwe kukusanya mapato; lakini tayari imepokea shilingi bilioni 194. Hii fedha imetoka wapi? Kwenye hii fedha iliyopokea imelipa madeni, imelipa fidia na imetatua migogoro. Tayari fedha hii iliyopokea imeshatumia tayari asilimia 95 ya hizi fedha. Yaani yenyewe haikukusanya vizuri, imepokea na imeshatumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Bunge lako linisikilize, shida ya nchi yetu ni kukosa mipango. Naipongeza sana Serikali kwa kuiongezea Tume ya Bajeti ya matumizi bora ya ardhi kutoka kuwa na bajeti ya shilingi bilioni 4.8 mwaka jana *2022/2023* kufikia mpaka shilingi bilioni 8, 2023/2024. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuongea mambo, Wizara ya Ardhi na Maendeleo na Makazi *is a sleeping giant*. Ni wizara ambayo inaweza kuiletea nchi yetu fedha nyingi sana, Nchi ya Tanzania ina karibu *square kilometer* za mraba 945,000. Nchi yetu ina idadi ya vijiji 12,318, Kata 3,564, Tarafa 570 na kati ya hii vijiji vilivyopimwa hadi kufikia sasa ni vijiji 10,744.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijiji vilivyoandaliwa Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi ni vijiji 3,681. Vijiji ambavyo havijaandaliwa Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi ni vijiji 8,637 na eneo ambalo limekwisha kupimwa na kupangwa la mjini ni asilimia 30 tu ya mijini imekwisha kupangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha sana kuona mahali ambapo Mwenyezi Mungu ametupa ardhi kubwa ili kwamba kupitia ardhi hiyo tupate mapato; lakini hatuwezi kukusanya mapato na matokeo yake tunaishia kuwa tunakopa mahali ambapo sisi wenyewe tungeweza ku-*run* nchi yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikupe mfano, kama ardhi yote ya Tanzania ikapimwa, kila kipande cha ardhi ya Tanzania

kikapimwa na kikawa na hati, hii inamaana kwamba kila kipande cha ardhi ya Tanzania kiwe kinamilikiwa na mtu binafsi au taasisi au na shirika, kitalipiwa kodi ya ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ardhi yote ya Tanzania ikapimwa, kila kipande cha ardhi ya Tanzania kikapimwa na kikawa na hati. Hii ina maana kwamba kila kipande cha ardhi ya Tanzania, kiwe kinamilikiwa na mtu binafsi au na taaasisi au na shirika kitalipiwa kodi ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano mifumo ya Kiserikali ikaunganishwa, Wizara ya Mheshimiwa Nape wakaamua kuunganisha mifumo na Wizara ya Ardhi; kwamba kila kipande cha ardhi kikawa na hati na wakatengeneza mfumo ambao kila ukifikia wakati fulani ule mfumo una-*generate control number,* unamtumia mtu mahala popote alipo na fedha inalipwa kutokea popote pale alipo. Fedha itaanza kuingia kupitia Wizara ya Ardhi kwa namna ambayo huwezi ku-*emagine*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni aibu kubwa tena kubwa sana *a giant Ministry* kama Wizara ya Ardhi inaweza kukusanya shilingi bilioni 76 kwenye malengo yake ya shilingi bilioni 300. Hili ni jambo tunahitaji kuliangalia tena na tena. Kwa hiyo ningeomba sana hii Tume ya Matumizi Bora ya Ardhi iongezewe fedha ili hatimaye nchi yetu yote tuipime, narudia tena, nchi yote ipimwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna faida za kupima nchi yote. Kwanza, tunaepuka migogoro ya ardhi, mbili tunaipa ardhi thamani na kuwasaidia wananchi wetu waweze ku-*mortage* ardhi yao wajipatie mapato yao. Tatu itatusaidia sana kwenye kukusanya mapato ya nchi. Ardhi ni mali ambayo kila mwaka utakuwa unategemea fedha na itakuwa inaingia kila wakati. Lakini leo ardhi yetu imekuwa *a sleeping giant*. Kwa sababu ya kutokupanga kwa ardhi yetu imesababisha kuwa na changamoto za wanyama waaribifu

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye taarifa ya Kamati hii wameazimia, naomba nisome kidogo kwenye changamoto za wanyama wakali na waaribifu. Kamati inaazimia kwamba, Serikali ihakikishe inakamilisha zoezi la kuondoa shoroba za wanyama

wakali na waharibifu 18 ilizojipangia katika mwaka 2023 mpaka mwaka 2024 ili kupunguza mwingiliano wa shughuli za wananchi na wanyama hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shoroba ni nini? Shoroba ni njia ambazo wanyama huwa wanapita *traditionally*. Wanyama kama tembo wana kumbukumbu ya ajabu sana. Tembo akipita barabara fulani akaenda baada ya miaka mitatu anarudia kwenye barabara hizo hizo. Zipo njia ambazo wanyama wanapita *traditionally* ambazo zinaitwa shoroba au njia za wanyama. Sababu mojawapo inayofanya wanyama tembo wanatoka kwenye hifadhi wanaingia kwenye nyumba za watu na kuharibu maisha ya watu ni kwa sababu kwenye maeneo ya shoroba ambazo wanyama wangepita Serikali yenyewe imejenga nyumba maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na inashangaza sana wanaposema kwamba wanataka kuondoa shoroba 18. Nikupe mfano. Moja kati ya maeneo ambayo ni shoroba zimejengwa. Halmashauri ya Mvomero imejenga ghorofa kwenye shoroba ya wanyama. Leo wanaposema hapa wanakwenda kuondoa shoroba, utakwenda kubomoa Halmashauri ya Mvomero? Mojawapo ya maeneo ambayo ni shoroba zimejengwa kuna Chuo Kikuu kimojawapo kimejengwa kwenye shoroba. Mojawapo ni *airport* moja imejengwa kwenye shoroba ya wanayama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo mkituambia kwamba mtakwenda kuondoa hizo shoroba huwezi kutushawishi utakwenda kuharibu Halmashauri ya Mvomero au uharibu *airport*…

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa Mheshimiwa.

**TAARIFA**

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na namuunga mkono Mheshimiwa Askofu Josephat

Gwajima kwa mchango mzuri. Ameeleza kwa habari ya *airport* iliyojengwa kwenye shoroba ni *airport* ya Kilimanjaro. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Josephat Gwajima umepokea hiyo taarifa?

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napokea taarifa ya ndugu yangu Mheshimiwa Kunambi. Kwa hiyo hizi ni Taarifa za Wizara sio taarifa za kwangu. Sasa kitu gani kinachosababisha Halmashauri iwe na *building permit* ya kujenga kwenye shoroba? Kitu gani kinachosababisha *airport* iwe *building permit* ya kujenga kwenye shoroba? Kitu gani kinachosababisha university iwe na *building permit* ya kujenga kwenye shoroba?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kukosa mipango ya muda mrefu ya matumizi bora ya ardhi. Kama nchi yote ingepangwa tayari pangejulikana eneo hili ni shoroba, eneo hili ni mbuga ya wanyama, eneo hili ni kijiji; na kwa namna hiyo wanadamu wasingefanya shughuli za wanadamu kwenye shoroba za wanyama na tukaingia kwenye haya tuliyonayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila mpango tunaojaribu kuufanya wa kuwaokoa wananchi wetu wa wanyama waaribifu hautafanikiwa kama hatujaingia kwenye mipango bora ya ardhi. Nashukuru sana Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan kwa kuamua kwa makusudi kuongeza fedha kwenye Tume ya Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi mwaka huu, angalau itasaidia lakini niseme jambo moja. Kama tusipoipanga nchi yote tutapata matatizo. Kwa sababu leo hii mwananchi mmoja anahamia mahala fulani, anafika pale anajenga nyumba yake, akijenga nyumba yake anavuta na umeme wananchi wenzake nao wanamuona wanajenga karibu wanaanza kuongezeka inakuwa Kijiji lakini tungekuwa tumepanga vijiji vyote, tumepanga nchi yote hii ingetusaidia sana kama taifa tusingekuwa na migogoro ya ardhi tuliyonayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumbuka hii fedha shilingi bilioni 194 iliyotolewa inatatua migogoro hiyo hiyo, inalipa fidia hizo hizo, inajaribu kulipa madeni yale yale lakini nakuomba sana tuisaidie

Serikali, tuazimie kwa nguvu zetu zote kuwa mipango ya muda mrefu, nchi yote ipangwe. Kila kipande cha ardhi ya Tanzania iwe kichuguu, iwe barabara, iwe njia panda, ipangwe ili iwe sehemu ya kuipa Serikali fedha. Tutasaidia sana nchi yetu kupata fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ambalo ningependa kulikazia sana. Hebu tuone ukweli uliopo kati ya hii fidia inayolipwa kwa wananchi walioshambuliwa na wanyama waharibifu, ni kidogo sana. Ni kweli *there is no value for human life, there is no amount that can be paid for human life it is true*. Hakuna kiwango kinachoweza kulipwa kwa maisha ya mwanadamu lakini angalao wale wanaoshambuliwa na wanyama wawe na faraja fulani. Naomba sana hayo maazimio ya Kamati Serikali iyazingatie sana na iyafanye vizuri. Lakini nchi lazima ipangwe. Nchi isipopangwa tunajiandaa tena kutengeneza migogoro mingine tena, tutakuwa tunalipa migogoro tena na tena na hatutafika mwisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, sasa Tanzania yote ipangwe; na Wizara ya Ardhi msipokuja na bajeti ya kupanga Tanzania yote kwenye Bunge lijalo nitashika shilingi mpaka mwisho kwa ajili ya maslahi mapana ya nchi yetu Tanzania. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Askofu Josephat Gwajima. Tunaendelea na Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, Mheshimiwa Munira Mustapha Khatibu ajiandae.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia fursa na mimi leo kuchangia. Kwanza kabisa nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema lakini pia nimshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoendelea kuifanya lakini pia niipongeze Kamati hii ya Ardhi, Nyumba, Maliasili na Utalii kwa kazi kubwa ya uchambuzi ambayo imefanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi leo nilitaka nichangie mambo machache sana. Nianze kwa kusema yafuatayo. Sekta ya Ardhi ama Wizara ya Ardhi tukubaliane ya kwamba ndiyo uti wa mgongo wa uchumi wetu wa nchi yetu hii ya Tanzania. Sekta ya

Ardhi imebeba mambo mengi sana. Tunapozungumzia habari ya maendeleo ya ukuaji wa uchumi hatuwezi kuacha kuizungumzia Sekta ya Ardhi. Tunapozungumzia habari ya uwekezaji ni lazima tuguse ardhi. Tunapozungumzia habari ya kilimo ni lazima tuguse ardhi. Sasa ni namna gani hii Wizara ya Ardhi imejipanga kikamilifu kuhakikisha ya kwamba inatumia ardhi hii katika kuonesha ya kwamba inaleta mchango mkubwa wa uchumi kwenye taifa letu hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Ardhi katika nchi yetu nadhani imekuwa ni tofauti kidogo, na hasa ukiangalia namna ya mipango ya matumizi bora ya ardhi katika nchi hii umeona kuna changamoto kubwa. Mheshimiwa Gwajima amezungumza hapa, ametaja ukubwa wa nchi yetu hii, kwamba ina ardhi kubwa, *square meter* za mraba zaidi ya 940 na zaidi lakini tukubaliane tu, kwa hali tuliyofikia kwa sasa nikitazama namna Sekta ya Ardhi ilivyojipanga kwenye nchi yetu hii, mimi naona kama hatuna ardhi kwa sasa. Kwa nini nasema kwamba hatuna ardhi, ni kwa sababu ya mipango ambayo Wizara ya Ardhi imechelewa kuhakikisha ya kwamba inaleta mipango mizuri ya matumizi bora ya ardhi kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii utaona Waziri Bashe ana mipango mizuri sana ya kuinua Sekta ya Kilimo kwenye nchi hii. Lakini swali la kujiuliza hapa, hiyo ardhi ambayo Mheshimiwa Waziri wa Kilimo anatamani anyanyue Sekta ya Kilimo ipo wapi? Utaona kwamba mipango mibovu ya ardhi ambayo huko nyuma imeweza kuchukuliwa, hawakuweka mipango mizuri ya kutenganisha maeneo kwenye nchi hii. Ndiyo maana umeona tukijaribu kuangalia uwekezaji wa mashamba makubwa kwenye nchi hii hatuwezi kupata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii ukienda kwenye maeneo yetu hakuna matumizi na mipango mizuri ya ardhi. Kwamba wapi ardhi ya mifugo, wapi ardhi imetengwa ya wafugaji? Ipo wapi ardhi imetegwa kwa ajili ya shughuli za kilimo, ipo wapi ardhi imetengwa kwa ajili ya uwekezaji wa viwanda? Hakuna, ni *vise versa*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ukienda kwenye maeneo yetu utaona hakuna sheria ambayo imewekwa inayom-*protect* mtu na inamzuia mtu kuwekeza kitu chochote kwenye maeneo yoyote; na ndiyo maana umeona leo hii ukienda kwenye ardhi, kwenye ardhi kwa mfano kwenye Jimbo la Msalala, hatuna maeneo ambayo tumeyapanga kwamba maeneo haya yatakuwa mahususi kwa ajili ya kilimo tu peke yake; na hakuna mtu yeyote yule atakayeweza kupewa *permit* ya ujenzi *either* wa nyumba za kudumu kwenye maeneo hayo. Tuyaache yawe ni maeneo ya kilimo tu. Itatuwezesha kumwezesha Waziri wa Kilimo kuja na mkakati wa kuja na mkakati wa kuhakikisha ya kwamba anawezesha sekta ya kilimo kwenye eneo lile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo yake ni nini? Kwenye eneo hilo hilo tulilotenga la mashamba ndiko kunakojengwa nyumba, eneo hilo hilo la makazi ndiko kunakojengwa viwanda, eneo hilo hilo la makazi ndiko shughuli zozote zile zinaendelea kwenye maeneo hayo. Matokeo yake ni nini; tunapokuja kwenye kuanza kutafuta maeneo ya uwekezaji katika maeneo ya kilimo na maeneo mengine tunakosa maeneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niombe sana, Wizara ya Ardhi ni wakati sasa umefika wa kukaa na kujitadhimini ni namna gani bora ya kukaa na kujifumbia kuanza kuweka matumizi bora na kupanga mipango bora ya matumizi ya ardhi kwenye maeneo yetu ili tuweze kuwa na ardhi itakayotuwezesha kuwekeza kwenye maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii kuna wawekezaji walitoka nje ya nchi wakaja kwenye Jimbo la Msalala, wakawa wanahitaji eneo la uwekezaji wa kilimo hekta elfu kumi tulikosa. Leo kuna wawekezaji wanakuja wanataka kuwekeza kwenye mashamba makubwa lakini hatuna mashamba hayo, ni kwa sababu hatukuwa na mipango mizuri ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ninaomba nizungumzie suala la migogoro ya ardhi. Kwanza kabisa nichukue nafasi hii kumpongeza Katibu Mwenezi wa Chama cha Mapinduzi, Ndugu Makonda kwa kazi kubwa anayoendelea kuifanya. Niombe Wizara ya Ardhi, hebu iangalieni Wizara

anayofanya Katibu Mwenezi Ndugu Christian Paul Makonda, migogoro mikubwa, changamoto kubwa kwenye mikutano ile ni migogoro ya ardhi. Mimi jimboni kwangu tuna migogoro ya ardhi mingi sana. Ukienda kwenye Kata yangu moja ya Jana tumekuwa na migogoro ya ardhi watu wanaporwa ardhi zao, wanadhulumiwa ardhi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia utaratibu wa namna ya kutatua migogoro hii hasa kupitia mabaraza haya imekuwa ikiwanyima haki ya wamiliki wa ardhi na wadai wa ardhi kupatiwa haki zao kwa wakati. Ni wakati sasa Wizara ya Ardhi kupitia upya mabaraza haya; na ikiwezekana tutenge fedha kuyawezesha mabaraza haya yawe yanakaa mara kwa mara ili kuweza kutatua matatizo ya ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini leo utaona mtu anapeleka kesi yake kwenye Baraza la Ardhi la Kata, linakaa labda mara mbili kwa mwaka na wakati mwingine hawana bajeti linaweza lisikae. Maana yake ni nini? Mgogoro wa ardhi ambao walipaswa kupata hati mapema inamchukua ndani ya miaka minne hadi mitano mpaka kupata hati yake ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni uwekezaji kwenye maeneo ya madini. Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri naomba mnisikilize vizuri. Ni wakati sasa umefika wa Mtanzania ambaye Mwenyezi Mungu amemjalia kumpa neema ya kumiliki ardhi kwenye eneo hilo, na kupitia umiliki wake wa ardhi kwenye eneo hilo akamjalia uwepo wa madini chini ya ardhi hiyo anayoimiliki. Sasa kumekuwa na changamoto ya fidia kwenye maeneo hayo. Pindi muwekezaji anapopatikana kwenda kuwekeza kwenye maeneo hayo, utaratibu wa fidia unaotumika hauzingatii kwa kuangalia thamani ya ardhi kwenye eneo hilo. Pia imeenda kwa kuzingatia thamani ya kuangalia maeneo haya yapo vijijini bila kuangalia mali iliyo kwenye eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa leo utaona; kuna mgogoro mmoja, na naomba sana Mheshimiwa Naibu Waziri huu mgogoro ukatatuliwe. Tuna mgogoro kwenye Kata moja ya Mwakata. Kuna mwekezaji alikuja akakuta kijiji kipo pale anaitwa Kanuck, akawakuta wananchi wanaishi pale na wanaishi pale na

wanaendeleza shughuli zao pale, akapata leseni ya uchimbaji wa madini kwenye eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa sheria zetu ni kweli amemiliki leseni na anahitaji kulipa fidia lakini kwa mara ya mpaka tunavyozungumza hivi leo, bado wananchi wa Mwakata hawajapatiwa fidia ya maeneo yao. Hata tathmini waliyofanyiwa mwanzoni, tathmini inafanyika lakini pia kumekuwa na watumishi ambao si waaminifu. Mwekezaji anawapa dhamana Wizara ya Ardhi kwenda kufanya tathmini, tathmini inayofanyika inafanyika bila kuzingatia thamani ya madini; na thamani ya mali zilizopo pale. Alipaswa kulipwa milioni kumi, anaambiwa alipwe milioni moja laki tano wakati ardhi ile inamiliki zaidi ya mabilioni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo kutokana na kile ambacho kimeshafanyiwa udhamini bado ucheleweshaji wa malipo unachukua muda. Mathalani unakuta kuna kesi moja Bulyanhulu, toka mwaka 2006 tunazungumza, watu wamefanyiwa tathmini mwaka huu malipo yao yanakuja kulipwa mwaka unaokuja, sheria imeshabadilika, ardhi imepanda thamani, wananchi wanagoma. Leo mnakuja kulazimisha kulipa fidia kipindi ambacho uthamini umefanyika lakini sio kipindi ambacho malipo yamefanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niombe sana, Wizara muweze kuweka msukumo pindi muwekezaji au mtu yeyote anaenda kufanya uthamini wa ardhi, malipo ya ardhi (fidia) ahikikishe ya kwamba analipa kwa wakati ili kuondokana na ucheleweshaji ambao utampelekea hasara mmliki wa ardhi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kule Mwakata mpaka tunavyozungumza leo wananchi bado hawajapatiwa malipo yao, fidia ya maeneo hayo; na Wizara ya Madini imeenda kuzuia shughuli za wananchi lakini wananchi wale hawajapatiwa fidia. Lakini cha kushangaza mwekezaji huyu ame…

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa inatoka wapi?

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mtaturu karibu.

**TAARIFA**

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, nataka nimpe taarifa mchangiaji anayechangia vizuri kwamba ardhi ndiyo urithi pekee wa mwananchi. Sasa maeneo ambayo anaeleza yamekuwa yakijitokeza, wananchi wanafanyiwa tathmini na hakuna shughuli zinazoendelea kwa muda mrefu. Kwa hiyo mwananchi aendelee na shughuli na wakati huo mwekezaji aendelee na shughuli. Kwa hiyo ninataka nimpe taarifa kwamba anachosema ni sawa, kuna haja ya kuangalia sheria upya. Kwamba anayepewa leseni akishindwa katika muda fulani wananchi waendelee na shughuli zao ili wananchi waendelee kutumia ardhi hiyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Iddi unaipokea hiyo taarifa?

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea taarifa hii ya ndugu yangu Mheshimiwa Mtaturu kwa mikono miwili na niongeze kwa kusema kwamba ikiwezakana basi Wizara ya Ardhi mtoe tamko, muwekezaji huyu kama hajalipa fidia asianze kufanya shughuli zake kwenye eneo hilo mpaka ahakikishe kwamba malipo yote yamefanyika kwenye eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa leo huyu anamiliki ardhi ya juu, huyu anamiliki leseni ya madini lakini kwa kuwa huyu anatakiwa amlipe anamwambia wewe unamiliki eneo la juu, wewe endelea na shughuli zako za juu halafu yeye anachimba chini kwa chini. Wakati huo huo huyu anaishi na nyumba zake na familia, milipuko inafanyika, yeye akiwa juu na huyu anafanya milipuko chini. Sasa swali langu linakuja; hivi Serikali, Wizara ya Ardhi, Wizara ya Madini kwa nini msikae pamoja mkaona namna gani ya kuwasaidia wananchi hawa wanyonge kuhakikisha na kwamba wanapewa fidia zao? Ili kuhakikisha ya kwamba muwekezaji analidwa lakini pia na wananchi wenye haki zao wanalindwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala jingine ni kesi kubwa ambayo inaendelea. Bulyanhulu tuna kesi nyingi sana. Tuna kesi moja ya toka mwaka 1996 mpaka leo bado haijapatiwa mwafaka lakini tuna kesi nyingine ya mapunjo ambayo tunasema ni haya haya kuchelewesha malipo. Uthamini ulifanyika na wakati unafanyika malipo ya ardhi yalikuwa bado hayatambuliki, yalikuwa yanatambulika malipo ya vitu vilivyomo kwenye ardhi peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kucheleweshwa malipo yao, mwaka ambao wanaenda kulipwa fedha zile tayari sheria imeshabadilika na inatambua sasa ardhi inaweza ikalipwa. Maana yake hawa watu wakaja wakadai walipwe ardhi yao upya lakini mgodi wa Bulyanhulu ulikaa chini na ukasema sawa, ukapitia upya na kuona sasa tutalipa; na wanakubali kulipa; lakini bado kuna watumishi ambao sio waaminifu ndani yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha ambayo imetolewa na mgodi walipwe wananchi malipo yao ya ardhi, fedha ile ikaenda kwa watu wajanja na fedha ikalipwa kwa watu ambao hawastahili na migogoro ikaendelea kubaki palepale na wananchi bado tunaendelea kulaumu Mgodi wa Bulyanhulu wakati Mgodi wa Bulyanhulu hauna matatizo kwa sababu wenyewe wamekubali kweli ardhi hii ni ya wananchi na ikatenga fungu kutoka milioni 300 ikaongeza milioni 200 ikawa milioni 500 kwamba wananchi walipwe; lakini Kamati zilizoundwa zimeenda kufanya ndivyo sivyo na zikalipa watu ambao hawastahili, na wadai mpaka leo wanaendelea kulia na ardhi zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakuomba Mheshimiwa Waziri, ni wakati sasa umefika wa kwenda kumaliza migogoro kwenye Jimbo la Msaala, kwenye Kata ya Bulyanhulu. Wadai hawa wanadai toka muda mrefu sana, toka mwaka 2003 wengine wanadai toka mwaka 1996. Niombe ni wakati sasa umefika wa Wizara kwenda kutatua migogoro hii, migogoro ya ardhi ni mingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niombe, amezungumza Mwenyekiti wa Kamati, hapa kuna Tume iliundwa ya Mawaziri Nane kwenda kushughulikia migogoro, ikikupendeza hebu Bunge lako hili tunaomba taarifa ile ije iletwe hapa ili watuambie

wamefikia wapi, kwa sababu sisi ndiyo tunaishi na wananchi na wananchi wanatarajia majibu kutoka kwao na sisi tuwapelekee majibu, migogoro hii imefikia wapi. Wakati mwingine migogoro hii haiishi kwa sababu bado inasubiri Kamati hii, imalize kazi yake. Kila mwaka tunasomewa hapa Kamati ile bado inaendelea. Kwa hiyo, niombe sana ikiwezekana basi Kamati ile ya Mawaziri iliyoundwa ilete taarifa hapa tujadili ili tuone imefikia wapi na tuweze kushauri kwenye maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jingine ni suala zima la upimaji wa ardhi. Alizungumza mwaka jana Mheshimiwa Kunambi, akasema Wizara ya Ardhi ikitumia ardhi yake vizuri inaweza kuchangia pato kubwa sana kwenye Pato la Taifa. Mimi nakubaliana naye kwa asilimia 100 nakuunga mkono leo Mheshimiwa Kunambi, kwamba kama Wizara ya Ardhi itajipanga vizuri inaweza ndiyo ikawa sekta ambayo inachangia mchango mkubwa kwenye Pato letu la Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nitatoa mfano mmoja. Hapahapa Dodoma toka 2020 Miganga *North*, tayari wananchi eneo lile lilipimwa na baada ya kupimwa tukaambiwa tulipie fedha na wananchi wakalipia fedha, baada ya kulipia fedha mpaka leo toka 2020 bado wananchi wale hawajapatiwa hati zao. Tumefuatilia tukaambiwa kwamba bado Halmashauri imekosa kiasi cha shilingi milioni 50 tu, kwenda ku-*approve* ramani ili basi *procedure* za hati ziendelee. Maana yake ni nini? maana yake ni kwamba kukosa milioni 50 kunaikosesha mapato Serikali zaidi ya mabilioni kwenye eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana Mheshimiwa Naibu Waziri, hebu nendeni mkaone namna gani manaweza kuonyesha ya kwamba mnatatua migogoro hii na mnasimamia vizuri kwenye maeneo haya; lakini nimshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, baada ya kuona kuna umuhimu mkubwa wa kupanga maeneo yetu alitoa fedha kuzipeleka kwenye baadhi ya Halmashauri, hata Halmashauri yangu ilipatiwa kiasi cha shilingi bilioni moja na milioni mia sita kwa ajili ya matumizi kupanga ardhi kwenye maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nikajiuliza hivi hizi pesa tulizopeleka kule kwa ajili ya kupanga ardhi, tulijipanga vizuri. Tumepokea kiasi cha shilingi bilioni moja na milioni mia sita lakini namna ya uandaaji wa maeneo yale mimi wananishangaza mpaka leo, nilienda kufanya ziara kwenye maeneo mengine nimeona wenzetu wanapotaka kupanga maeneo, moja wanahakikisha kwamba wanapeleka miundombinu kwenye maeneo yale, kama ni barabara wanatengeneza barabara kwenye maeneo yale, kama ni maji wanapeleka maji, kama ni umeme unapelekwa umeme halafu baada ya hapo wanaanza *advertisement* ya viwanja vile ili viweze kuuzika na ile fedha iweze kurudi na wananchi waweze kupata kwenye maeneo yale, lakini kilichofanyika ni tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeenda kutumia zile fedha, tumeenda kufanya malipo kwenye maeneo yale lakini hatujapeleka miundombinu na wala hata kutangaza hatutangazi, matokeo yake vile viwanja haviuziki na Serikali inahitaji fedha zirudishwe. Sasa najiuliza huu mpango wakwenda kupanga miji kwenye maeneo hayo hivi mmejipanga kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana Wizara ya Ardhi hebu pitieni fedha ambazo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, amezipeleka kwenye Halmashauri hizo muone nini kinakwamisha kuhakikisha kwamba viwanja vile vinauzika kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine …*(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa muda wako umeisha.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie la mwisho. Mheshimiwa Waziri hili alichukue, kumekuwa na uporaji wa maeneo ya wananchi hasa kwa Wakurugenzi wa Miji. Kuna eneo moja liko eneo la Nyamagana, eneo hili mmiliki anaitwa Mzee yuko pale, yule Mzee anamiliki lile eneo toka enzi za uhuru lakini leo hii Halmashauri ya Jiji la Mwanza imekuja pale na kutaka kulichukua eneo lile kwa nguvu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kulichukua kwa nguvu Mzee yule kaenda Mahakamani, Mahakama ikaamuru yule Mzee arudishiwe eneo lake liko Makongoro *opposite* na Benki Kuu, Mkurugenzi amekataa kumrudishia eneo hilo. Sasa niombe Mheshimiwa Naibu Waziri, haya mambo siyo mpaka Katibu Mwenezi, siyo mpaka Mheshimiwa Waziri Mkuu, siyo mpaka Mheshimiwa Rais, aende ninyi mnaweza kuyamaliza. Hebu wasilianeni na Wakurugenzi hawa muwaulize, Mkurugenzi wa Jiji la Mwanza shida yake ni nini, kwa nini anataka kupora eneo la mwananchi ambaye amalihangaikia kwa muda mrefu? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi. Nilimtaja Mheshimiwa Munira Mustapha Khatib na Mheshimiwa Dkt. Florence Samizi, ajiandae.

**MHE. MUNIRA MUSTAPHA KHATIB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi ya kuchangia taarifa hii ya Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii. Kwanza kabisa niunge hoja mkono Taarifa hii ya Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais, Mama yetu Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa ambayo aliifanya kwa kuitangaza nchi kupitia filamu yake ya *Royal Tour*, nadhani matokeo makubwa tumeyaona. Hapo awali tulikuwa tunaingiza watalii milioni moja lakini baada ya filamu hii ya *Royal Tour* tumeona tumeanza kuingiza watalii 1,790,000 hii ni hatua kubwa sana kwa hiyo nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa filamu yake hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeongeza pato kubwa la Taifa, tumeweza kuingiza fedha za Kimarekani bilioni 3.3, hiki kitu hakijawahi kutokea toka Uhuru wa Tanzania upatikane. Niiombe sana Serikali iweze kuongezea fedha Wizara ya Utalii kupitia Bodi ya Utangazaji, ili waweze kutangaza zaidi kuweza kupata fedha za kigeni lakini watalii waweze kuongezeka nchini kwetu, niiombe sana Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti ya Ardhi, Maliasili na Utalii kupitia Wizara ya Maliasili hadi sasa imepatiwa asilimia 17 tu katika miradi yake ya maendeleo, hii fedha ni kidogo. Niiombe sana Wizara iangalie namna ya kuweza kutoa fedha kwa wakati katika Wizara ya Maliasili, kwa sababu hii fedha sasa hivi kama ukiangalia *TANAPA* imeongezewa hifadhi 21. Kwa hiyo, wana mzigo mkubwa wa kuweze kupambana na kutangaza hifadhi zetu za utalii, niwaombe sana Wizara waweze kuongeza fedha hzi kama zilivyopangwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la wanyama wakali na waharibifu. Waheshimiwa Wabunge, wamekuwa mashahidi kwenye Majimbo yao kila Mbunge anayeinuka hapa aliyekuwa anazungumzia suala la wanyama wakali na waharibifu, hili suala limeongelewa Bungeni kwa muda mrefu. Niiombe Serikali na Wizara itafute teknolojia ambayo inaweza kudhibiti wanyama hawa wakali na waharibifu kwa sababu hiki kimekuwa kilio cha Wabunge cha muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wamekuwa wakiathirika na mazao yao lakini wanachi wamekuwa wakiuliwa na Wanyama hawa, lakini hata nyumba zao zimekuwa zikibomolewa na wanyama hao waharibifu, tutafute teknolojia ambayo itakuja kudhibiti wanyama hao waharibifu. Hili suala limekuwa la muda mrefu na changamoto kubwa kwa wananchi wetu lakini ukiangalia kifuta machozi hebu Serikali ituambie ni lini italeta Bungeni Sheria hizi mpya kuja kuzipitia, kuangalia namna ya ulipaji fidia kwa wananchi hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wanalipwa fidia ndogo sana, niiombe Serikali, niiombe Wizara iangalie kwa jicho la huruma namna ya kuwasaidia wananchi wetu hawa kwa ulipaji fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Kaka yangu Mheshimiwa Jerry Silaa, tumekuwa tukimuona jinsi anavyopambana kutatua migogoro ya ardhi, amekuwa akijitahidi sana lakini bado migogoro ya ardhi imekuwa changamoto kwenye nchi yetu. Bado tuna migogoro mingi sana na migogoro

hii taweza kuondoka pale tu Serikali itakapoamua kuweka wazi taarifa ya Mawaziri Nane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuiombe sana Wizara na Serikali kwa ujumla waweze kuleta ripoti ya Mawaziri nane, kwa sababu wananchi mpaka muda huu hawajielewi nani anaondoka, nani anabakia katika vituo vyao lakini hata ukiangalia hawawezi kulima, hawawezi kufanya miradi yoyote ya maendeleo wananchi wamekuwa na taharuki kila kiongozi anayepita anazungumzia, utasema nchi yetu ina migogoro mingi wakati haina migogoro mingi ya kiasi hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuiombe sana Wizara, tuimbe sana Serikali iweze kuleta taarifa hii ndani ya Kamati lakini pia ndani ya Bunge lako, ije ituambie lini italeta taarifa hii ya Mawaziri nane ndani ya Bunge lako hili Tukufu. Tumeshuhudia mgogoro wa Ruaha na wananchi, niombe sana Wizara ya Maliasili, iweze kwenda kumaliza mgogoro ule wa Ruaha ili wananchi wale wajue, wananchi hawana shida lakini wanataka kujua wanaobakia wabakie, wanaoondoka waondoke. Kwa sababu haya Maazimio tumeyapitisha toka Bunge la mwezi wa saba Bunge la Bajeti, lakini mpaka muda huu hakuna kitu kilichoendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe Serikali ituambie ni lini itamaliza mgogoro wa Ruaha na Maazimio yetu ambayo tuliyaleta Bunge la mwezi wa tisa ni kauli gani Serikali inaweza kutuambia kupitia ahadi ambayo Mheshimiwa Waziri, aliahidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo niunge mkono taarifa ya Kamati na niseme ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Munira. Tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. Florence Samizi na Mheshimiwa Godwin Emmanuel Kunambi, ajiandae.

**MHE. DKT. FLORENCE G. SAMIZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi na mimi niweze kuchangia taarifa ya Kamati iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nianze kwa kuwapongeza Mawaziri wa Wizara hizi husika kwa jinsi ambavyo wanaendelea kutekeleza majukumu lakini kipekee nimpongeze Mheshimiwa Rais wetu kwa jinsi ambavyo ameendelea kuelekeza pesa katika hizi Wizara ili kuweza kuzikwamua. Nitaendelea kuchangia pale kwenye kupanga, kupima na kumilikisha ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Gwajima ameshasema na akionyesha dhahiri kwamba nchi yetu haijapimwa, ni asilimia 30 tu ya nchi yetu ambayo imepimwa, lakini viko Vijiji 1,500 bado havijapimwa hata mipaka hii inaashiria kabisa kama Vijiji vyetu na ardhi yetu bado haijapimwa basi migogoro ya ardhi itaendele sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe mfano mdogo katika Mkoa wangu wa Kigoma. Mkoa wa Kigoma, wenye Kata 306 ni Kata 112 tu zilizopimwa ambazo ni asilimia 36, lakini yako Majimbo ya Buhigwe na Kibondo, kama Kakonko hamna hata Kijiji kimoja ambacho kilichopimwa, Muhambwe Vijiji 50 ni Vijiji tisa tu ndiyo vimepimwa! Hii ina maana gani? Ina maana kwamba ndiyo maana kule kwenye Vijiji vyetu migogoro inashindikana. Kila siku watu wanagombea ardhi, kila siku wavamizi, mkiamka asubuhi hapa ng'ombe mkiamka asubuhi hapa mbuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuna njia nyingine zaidi ya kupima ardhi ya nchi hii na njia pekee ni kuendelea kuwezesha Tume ya Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi, kwa kuiongezea pesa. Katika hili nimshukuru Mheshimiwa Rais, kwa kuridhia kuongeza pesa kutoka bajeti ya bilioni 1.4 mpaka bilioni nane na wote tumekuwa mashahidi mpaka Disemba wameshapokea asilimia 56 ya hii pesa bilioni nne lakini wameweza kuandaa mipango 3,000. Mipango asilimia 50 imeandaliwa kwa huu mwaka mmoja ambapo Mheshimiwa Rais ameamua kwa dhati kabisa kuweka pesa kwa kuongeza bajeti lakini na kupitia mradi wetu wa miradi ya kuboresha usalama wa umiliki ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo, ni dhahiri kabisa Tume yetu ya Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi, ikiongezewa pesa tunaweza tukaipanga nchi yetu. Tukizingatia Ilani yetu ya

Uchaguzi tumesema tutaandaa mipango kina 10,000 lakini mpaka sasa tumeandaa mipango kina 3,000, kwa hiyo tuna kazi ya kufanya katika hii miezi 17, lakini kazi hii inawezekana, Tume ya Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi, wameshatuambia wakipata bilioni 20 kwa mwaka wanao uwezo wa kuipanga hii nchi kwa kuiandalia mipango kina na huku Halmashauri zikiendelea kupaga katika *level* zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote tumeona Halmashauri zimepewa pesa lakini kama Tume ya Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi, haijandaa Mipango kina kwenye hizi Halmashauri zetu, basi hizi Halmashauri zetu hazitoweza kufanya hivi. Maadam Tume ya Mpango ya Matumizi Bora ya Ardhi, ndiyo tumewapa kazi ya kuanda hii mipango kina lazima tuiwezeshe kwa dhati kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiipatia bilioni 20 hii Tume itaenda kutusaidia sana ili tuendane na kasi ya kupanga hii nchi yetu kama ambavyo tumeelekeza kwenye Ilani ya Uchaguzi. Hili linawezekana kabisa, huku tukiwa tunalia na nchi yetu haijapimwa ziko Taasisi na Mashirika ya Serikali ambayo hayalipi pango la ardhi. Taarifa yetu imeeleza, taasisi zilikuwa zinadaiwa deni la bilioni 123 na Wizara kwa hapa niipongeze sana imefanikiwa kukusanya bilioni 32, sawa na asilimia 26 tunazo bilioni 91 ziko kwenye Mashirika, Mashirika yamejengwa kwenye ardhi yetu na hayataki kulipa pango ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ridhaa yako leo nitawataja wale ambao wanadaiwa pesa nyingi sana. *National Development Cooperation (NDC)* wanadaiwa bilioni 15 kama pango la ardhi, lakini *Mbeya Cement* wanadaiwa bilioni nne pango la ardhi, *National Bank of Commerce* wanadaiwa bilioni 12 kama *land rent*, Msajili wa Hazina anadaiwa bilioni tano, *TAMESA* wanadaiwa bilioni mbili, *Tanzania Airport Authority* wanadaiwa bilioni 11, naweza kuendelea *list* hapa ni ndefu sana kuweza kuona kwamba watu gani wanadaiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mashirika yetu na Taasisi zetu zikiweza kuzilipa hizi pesa ninyi wenyewe mnaona Tume ya Mipango inahitaji bilioni 20 tu lakini kuna taasisi zimekalia bilioni 91. Tunaiomba Serikali ije na mpango mkakati wa kuzipata hizi pesa

ambazo Mashirika yameshindwa kulipa ili Wizara yetu ya Ardhi na kupitia Tume ya Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi iweze kupanga nchi hii ili tuweze kupunguza hii migogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa ni mashahidi tunaona kila siku tuongeze mabaraza. Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, tunamuona Mheshimiwa Jerry Silaa, kila siku anaenda kutatua migogoro, tumeona viongozi wakubwa wa nchi wakitembelea migogoro ya ardhi inaongoza. Hatuna sababu ya kuendelea kupoteza pesa nyingi kwenye hiyo migogoro hebu tuwekeze kwenye kupanga, kupima na kumilikisha ili nchi yetu iweze kuwa na matumizi bora ya ardhi na hii migogoro itaisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi pesa tunazopeleka kule basi ziweze kupanga na kupima. Lakini tunafahamu kabisa tukiweza kupanga nchi yetu wananchi wetu wanakuwa na uhakika. Tumetembelea miradi ya kupanga na kupima, tumeenda kule Meru, tumeenda Simiyu, wananchi wanafuraha kabisa na Serikali yao kwa sababu sasa wana hati zao, wana uhakika wa kwenda benki lakini wameondoa migogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kuwa tumewamilikisha hawa watu na kuwapatia hati basi tunaendelea kupoteza kwanza mapato lakini migogoro hatutaimaliza. Tunaomba mikakati ya dhati ya kuongezea Wizara yetu kupitia Tume, pesa ya kupanga na kupima lakini na mikakati ya kuikomboa hii hela ambayo Mashirika ya Serikali na Taasisi yameshindwa kulipa tunaitaka hii *land rent* iweze kutusaidia kupanga nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakwenda kuchangia kwa upande wa Maliasili. Kwanza kabisa nimpongeze Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuwa yeye ndiye Mtalii namba moja ambaye ameonesha kwa vitendo jinsi ambavyo utalii unaweza kufanyika. Katika hili jukumu letu ni kuendelea kumuunga mkono kuendeleza kile alichokifanya. *Royal Tour* imeanza lakini tunapaswa kuendeleza kile ambacho Mheshimiwa Rais, amekianzisha. Tumeona jinsi gani Wizara yetu ya Maliasili, imepokea pesa kidogo kwa ajili ya miradi ya maendeleo asilimia 17, lakini tumeiona *TANAPA* ambavyo ina mzigo wa hifadhi hifadhi 21 kutoka 16 lakini bajeti yake bado ipo chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii maana yake ni nini? maana yake hii nguvu kubwa tuliyoiweka kwenye *Royal Tour*, kama tusipoiendeleza kwa kuendeleza kuboresha miundombinu na hasa ya kwenye hifadhi zetu basi hatutaweza kufanikiwa. Niiombe Serikali iongezee bajeti *TANAPA* ili iweze kukabiliana na hizi hifadhi ambazo tumeiongezea, lakini ipeleke pesa kwa wakati za miradi ya maendeleo kwenye Wizara yetu ya Maliasili ili iendelee kuboresha miundombinu iliyopo katika hifadhi zetu ili watalii waendelee kuja katika hifadhi zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko Azimio ambalo limeshindwa kutekelezeka kama ambavyo Mwenyekiti amesoma katika taarifa yetu la kupandisha hadhi Wakala wa Misitu na kuwa Mamlaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala wa Misitu ana Bodi ya Ushauri; wote tunashuhudia misitu yetu inavyoangamia katika nchi hii, tunashuhudia jinsi uchomaji wa miti ovyo ulivyo, tunashuhudia uchochoro wa kujificha kwa uvunaji endelevu, ambapo tukienda kuona kiuhalisia hakuna uvunaji endelevu, wanavuna lakini hawapandi huku Wakala wa Misitu Tanzania akiendele kuwa Wakala wa Misitu na siyo Mamlaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inasababisha haya madhara yaendelee kwa sababu huyu *TFS* hana bodi ya mamlaka, ana bodi ya ushauri tu. Ili kuendana na mabadiliko ya tabianchi ambayo yote tumeshuhudia nchi yetu inavyoingia kwenye majanga kutokana na ukataji wa miti hovyo, kutokana na moto kichaa, kutokana na uvunaji wa miti ambao siyo unaostahili kwenye mazingira yetu, sasa ni muda muafaka mamlaka hii kupandishwa hadhi na kuwa mamlaka kamili, kutoka kuwa Wakala wa Misitu na kuwa Mamlaka ili tuendelee kuokoa misitu yetu katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwenyekiti wa Kamati yetu amesema jinsi ambavyo tumetembelea miradi ya maliasili, kwa kweli kwa hapa tumpongeze Mheshimiwa Rais sana na maliasili kwa jinsi walivyotekeleza. Tumetembelea viwanja vya ndege kwenye hifadhi zetu, tumetembelea barabara za mawe kwenye hifadhi zetu, tumeona jinsi gani ambavyo nia ya Serikali kuboresha zile hifadhi. Kwa hiyo, jukumu letu sasa, tusimamie zile sheria

ambazo tunatakiwa tubadilishe na hasa ile ya *TAWA* ambapo tunaona sheria ile imekuwa na changamoto, imeshindwa kutekelezeka. Tunahitaji *TAWA* sheria yao ipitishwe ili sasa waweze kujengewa uwezo, wawe na nguvu ya kusimamia hili jambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenzangu amesema, wanyama wakali na waharibifu ni tatizo katika nchi yetu. Pia tumeona ambavyo Kanuni ya kifuta jasho imechukuwa muda kuweza kubadilishwa na kutekelezeka, tumeona jinsi ambavyo kifuta jasho kinachelewa kupelekwa kwa walioathirika. Yote haya yanatakiwa *TAWA* kama *TAWA* iweze kufikishwa kwenye hadhi ya kuwa mamlaka kamili ili iwe na mamlaka ya kuweza kusimamia hizo kazi ambazo wamepewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kusisitiza kwamba ili tuweze kufanikiwa lazima tuwe na mipango madhubuti. Kwa kumalizia tu, nikumbushie lile ambalo Mwenyekiti pia amelisema kuhusu kuhamisha kukusanya mapato ya *land rent* kupeleka mamlaka ya Serikali za Mitaa na kuitoa Wizara ya Ardhi, imechangia ukusanyaji wa mapato ya *land rent* kwa kipindi cha mwaka 2023/2024 kwenda chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu gani? Serikali imehamisha ukusanyaji wa mapato kutoka ardhi na kupeleka Serikali za Mmlaka za Mitaa bila kuwa na mifumo. Serikali za Mamlaka za Mitaa hazina mifumo na kwa bahati nzuri Serikali imeshawekeza sana kupitia Wizara ya Ardhi kutengeneza mifumo ya ukusanyaji wa mapato. Tulikuwa tumeshafikia tumesema tunataka kwenda kuonyesha sasa; tutakuwa mpaka tunaleta meseji kwenye simu zenu kuonesha kiwanja cheko kinadaiwa shilingi ngapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tumeshafikia hatua hiyo, tena *system* hiyo inataka ihamishwe ipelekwe mamlaka ya Serikali za Mitaa. Tunaishauri Serikali na kuiomba, kwa vile tumeshatumia fedha nyingi kuboresha mifumo ya Wizara ya Ardhi ili iweze kukusanya mapato vizuri, tunaiomba Serikali iliangalie upya hilo tena, makusanyo hayo ya pango na ardhi basi yaendelee kukusanywa na Wizara ya Ardhi ili Wizara ya Ardhi iweze

kukusanya mapato na iweze kujitosheleza na kusimamia, kwa sababu tumeona umuhimu wa kupanga na kupima na kumilikisha ardhi ya nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Florence Samizi. Nilimtaja Mheshimiwa Godwin Emmanuel Kunambi atafuatiwa na Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga na Mheshimiwa Zacharia Paul Issaay ajiandae.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nianze mchango wangu kwanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema aliyenijalia afya njema hata siku ya leo nikawepo hapa. Pia, niendelee kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayoifanya kulijenga Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu nimeingia hapa Bungeni, mchango wangu mkubwa katika michango mingine ambayo nimekuwa nikichangia, kwa kiasi kikubwa nimekuwa nikichangia sekta hii ya ardhi. Kwa nini sekta ya ardhi? Kwa sababu ya umuhimu wake kwa Taifa letu. Nimeamua kugawanya michago yangu hapa Bungeni, tangu nilipoanza mpaka nitakavyomaliza Ubunge wangu kwa kipindi hiki cha miaka mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimegawanya michango yangu hasa kwenye sekta ya ardhi kwa mfumo wa *episode*. Nilikuwa na *episode one*, ikaja *episode two* na hii sasa ni *episode three*. Hii inatokana na namna ya Mawaziri kwenye sekta hiyo wanavyobadilishwa. *Episode one, episode two*, sasa nakwenda kwenye *episode three,* yuko kaka yangu Mheshimiwa Jerry Silaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nirejee maneno ya Hayati Baba wa Taifa. Alisema maneno haya, wengi wamezungumzia fedha, fedha, fedha. Baba wa Taifa alisema fedha siyo msingi wa maendeleo, bali fedha ni matokeo ya maendeleo. Baba wa Taifa aliendelea kusema kwamba nchi yoyote ili iweze kuendelea duniani; nchi yoyote iliyopiga hatua za maendeleo na inayotaka

kupiga hatua za maendeleo, jambo la kwanza lazima liwe na ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu ina ardhi yenye kilomita za mraba takribani 945,000. Ardhi tunayo ambayo hatuitumii ipasavyo. Jambo la pili, watu tunao idadi ya takribani Watanzania milioni 60. Jambo la tatu ni uongozi bora na la mwisho, siasa safi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeeleza haya kabla sijaenda kwenye mchango wangu, lengo ni kwamba nataka nitoe darasa kidogo hapa. Marcus Garvey alisema, ukitia hofu au shaka kwenye jambo lolote ambalo unataka kulifanya, umeshindwa. Changamoto tuliyonayo sisi kama Watanzania hasa Serikali, ni fikra *(mindset)*, kwamba tunachowaza siku zote ni kwamba tutashindwa, tusaidiwe, tunashindwa. Nchi yetu inaweza kufanya kila kitu. Changamoto ni fikra. Jambo la pili ni *commitment*. Hali ya utayari wa kuamua kufanya jambo na mwisho ni uzalendo. Tulio wengi Watanzania hasa tuliokuwa kwenye majukumu haya ya nchi yetu, sio wazalendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa najaribu kuangalia hapa na nitaanza na hoja ya kupanga, kupima na kumilikisha ardhi. Ili uweze kupanga, kupima na kumilikisha ardhi, lazima uwe na mpango kabambe *(master plan)*. Nilikuwa nafuatilia takwimu za sekta ya ardhi nchi nzima na sina hakika sana kama ni kweli zimefika, naambiwa katika halmashauri zote 184, kuna *Master Plan* 25, sina hakika sana. Katika hizi 25 ambayo nina uhakika ambayo imetekelezwa kwa asilimia kama 90, ni Dodoma, lakini hizi 24 zote hazijatekelezwa. Mfano mzuri ni Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dar es Salaam *is a squatter city,* na hatuwezi tena, tumeshachelewa. Ili uipange Dar es Salaam na kuipima, ni lazima tuache miradi yote ya maendeleo kwenye bajeti ya mwaka mzima wa fedha, shilingi trilioni zote 15 ziende Dar es Salaam, ndiyo uipange Dar es Salaam. Tumeshashindwa, sasa tusishindwe na mikoa mingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutaenda taratibu, kwa sababu tulitaka tuivunje Vingunguti yote, uvunje ile Buguruni yote, yaani

uivunje Manzese sijui wapi kote. Sasa hiyo kitu, na Baba Askofu hapa anatusaidia. Kwa hiyo, Dar es Salaam twende taratibu, tumeshachelewa na hili siyo kosa lenu, ni jambo lamuda mrefu sana, huko nyuma hatukuanza vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa najaribu kuangalia hapa, Mheshimiwa Askofu Gwajima ameeleza kwa habari ya takwimu za vijiji ambavyo vimepimwa na kadhalika. Tuna vijiji takribani 12,318. Katika vijiji hivi vilivyopimwa kwa maana vimepangwa kwa utaratibu mzuri wa ardhi ni takribani 3,681. Nikafanya hesabu ndogo tu, Tume ya Taifa ya Mipango na matumizi bora ya ardhi inasema, inaweza kupima kila Kijiji kimoja kwa Shilingi milioni 15. Hesabu ya kawaida tu ya kujumlisha na kutoa, katika vjiji vilivyobaki 8637 ukizidisha kwa milioni 15, tunahitaji tuipelekee Tume shilingi bilioni 129.5 tu kumaliza kazi ya vijiji vyote. Leo hii mnawapelekea shilingi bilioni mbili, bilioni nne, hii safari ni ndefu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, (Naibu Waziri unanisikiliza, wewe ni mtu rahimu sana, ndiyo maana nikasema leo nitakuwa *lenient* kidogo). Ukipeleka hizi fedha, shilingi bilioni 129 Tume, zile fedha shlingi bilioni 345, mimi mpaka leo nasikitika, au sipati usingizi, hivi zile hela jamani! Tumwombe kibali Mheshimiwa Rais. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani sana naku-*address* wewe. Naiomba Wizara ya Ardhi imwombe kibali Mheshimiwa Rais kubadilisha mpango wa matumizi ya fedha zile za mkopo wa Benki ya Dunia shilingi bilioni 345 waje kwenye mipango yenye tija. Wewe unapeleka shilingi bilioni 47 kwenye dharura kweli, katika nchi hii ambayo haijapimwa! Sijui, lakini Mheshimiwa Naibu Waziri na Waziri ambaye nadhani anasikia, naomba umshauri aende kwa Mheshimiwa Rais aombe kibali, inawezekana. Kubadilisha mpango wa shilingi bilioni 345 waje na mpango wa kupima nchi yetu, inawezakana. Ndiyo maana nikasema ni *mindset*, *commitment* na uzalendo *that is all,* hamna kitu kingine. Hatuhitaji zaidi ya hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nataka nilieleze hapa ni eneo la kukosekana kwa uratibu mzuri wa sekta

ya ardhi na TAMISEMI. Mheshimiwa Waziri TAMISEMI yupo na ningependa unisikilize kaka yangu. Tume-*paralyze* sekta ya ardhi sisi wenyewe. Leo hii ukisoma Sheria ya Mipango Miji (Na. 8) ya mwaka 2007, inatambua mpaka leo mamlaka ya upangaji ni halmashauri, na tumevunja sheria. Bunge hili hatukuwahi kufanya mabadiliko ya Sheria ya Mipango Miji kukabidhi kazi kwa Wizara ya kisekta. Hatukuwahi Bunge hili, *and I stand to be corrected*. Ilikuja tu hapa Kanuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikwambie tu, unajua ni kwa nini? Ah, bwana wee, siwezi kusema zaidi, Mheshimiwa Naibu Waziri ukinitafuta na wenzako nitawasaidia. Alitokea mtu mmoja akaenda kushawishi kwamba unajua hawa Madiwani hawana uwezo wa kuwasimamia watumishi wa ardhi, niletee mimi huku; lakini hakukuwa na nia njema kwa Taifa letu. Ukifanya hivi, maana yake unapoka majukumu ya Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa jambo hili nadhani Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI akishirikiana na Waziri wa Ardhi, hebu mtengeneze hapa hii mifumo isomane; sekta ya ardhi na TAMISEMI. Kwa mfano, leo hii Mkurugenzi wa Halmashauri ndio anayesimamia utendaji kwenye mamlaka ya upangaji. Anamwagiza Afisa Ardhi ambaye yupo kwenye ofisi yake akafanye kazi fulani, Kamishina wa Ardhi naye anamwagiza kwa wakati huo huo, anamtii nani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesha-*paralyze* watumishi hawa. Ni mfano mdogo tu, Kamishina wa Ardhi ngazi ya mkoa yupo pale anamwambia sasa wewe Afisa Ardhi nenda kafanye jambo hili, Mkurugenzi Halmashauri, yupo ofisini kwangu nenda kafanye hili, anaenda kwa nani? Kuna ombwe. Mnaliona ombwe hilo? Sasa naomba, kwanza tumevunja sheria. Serikali imevunja Sheria Na. 8 ya 2007 ya Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi. Sasa tusiendelee kuvunja sheria, wale watumishi warudi TAMISEMI. Kwa sababu, kama hakuna uratibu, kwa sababu Wizara ya Ardhi kazi yake ni sekta, yeye ni msimamizi wa sekta tu. Yeye siyo Mamlaka ya Upangaji, ni msimamizi wa sekta na sera. Sasa sijui kama tunaeleweka! Ndiyo maana nikasema hii ni *episode three* na *episode four* itakuja mpaka nione jambo langu linakubaliwa. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni mfumo wa *ILMIS (Integrated Land Management Information System)*. Nawapongeza Wizara ya Ardhi, *all starts well ends well*. Mmeanza vizuri katika eneo hili, nimesikia hapa Taarifa ya Kamati kwamba sasa mnakwenda kwenye mikoa mitano katika mkoa mmoja wa Der es Salaam, na Mkoa wa Dar es Salaam nadhani wilaya zote karibu zina *ILMIS* na ndiyo maana migogoro ya ardhi Kinondoni haipo leo hii. *ILMIS* ni mfumo wa kuhifadhi taarifa za sekta ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Afisa Ardhi mmoja na nilikuwa sijui gharama inatoka wapi, Mheshimiwa Naibu Waziri utanisaidia, kwa sababu ninachojua kwenye *ILMIS* hamna jambo jipya. Kuna *computer,* kuna *printer* na kuna *sever* unampa Afisa Ardhi mmoja moja *that is all.* Sasa tunashindwa nini? Ni jambo la kawaida tu, hatuhitaji ku-*invest a will* hapa, tumsaidie Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni suala zima la migogoro ya ardhi. Nampngeza Waziri lakini atachoka, yaani hata Yesu akirudi hapa Tanzania migogoro ya ardhi itaendelea kuwepo. Kwa kweli juzi nimemwona ana mvi kidogo, kashaanza kuchoka, mvi zimeanza. Namwonea huruma sana kaka yangu Mheshimiwa Jerry Silaa, lakini yeye ana-*deal* na jawabu la tazizo, anaacha ku-*deal* na tatizo. Lazima u-*deal* na tatizo, siyo jawabu la tatizo. Ana *clean* tembezi zile, *well and good*. Hivi Waziri unaweza kutembea Halmashauri zote 184 na vijiji vyote, si utakufa kesho tu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashauri Wizara, tengenezeni mfumo. Kauli ya Waziri ikitoka pale juu, hawa wengine wote wanasema shikamoo, halafu yeye anasema marahaba. *Very simple, very simple!* Yaani wakati mwingine, *anyway!* Nasikitika lakini... *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama sekta nawaomba, nawashauri mka-*deal* na chanzo cha tatizo, msi-*deal* na jawabu la tatizo, hamtafanikiwa kamwe. Migogoro ya ardhi ni matokeo ya *failure* ya sekta, *that is all.* Hamna hamna jambo jipya hapa. Jamani eeh, mnajua ninyi mna bahati sana, lakini hizo bahati haziwapati wengine. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kusema nini? Kwa nini nimewaeleza haya jamani? Mheshimiwa Naibu Waziri, wewe ni kaka yangu, unanisikiliza, tunashauriana; na Mheshimiwa Waziri juzi umeona tunazungumza vizuri, nia yetu ni njema, na ninakushukuru. Chukueni michango yangu *positively*. Mimi bado kijana mdogo, ndiyo kwanza nina miaka 38 hapa, huko mbele nitafika tu. Sina nia nyingine zaidi ya kuishauri Serikali hii nzuri ya Mheshimimwa Rais Samia Suluhu Hassan. Nia yake njema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nashauri kitu kwa watumishi wote wa umma nchini...

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa inatoka wapi? Haya Mheshimiwa Gwajima.

**TAARIFA**

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumpa taarifa mwongeaji, ndugu yangu kwamba ni kweli anachosema, pamoja na mapafu yote ya Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, lakini migogoro anayokimbiza kutatua ni matokeo ya tatizo ya kushindwa kupima nchi yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye jimbo langu unakuta hati moja ya mtu halafu ndani yake kuna hati nyingine 100 ndani ya hati moja lakini yote imetolewa na Serikali. Kwa hiyo, kutokupima na kupanga kama anavyosema ndugu yangu Mheshimiwa Kunambi, ndiyo hasa chanzo cha mgogoro. Tusishughulike na matokeo, tushughulike na chanzo cha mgogoro. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kunambi, unaipokea hiyo taarifa?

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepokea kwa mikono miwili. Niseme tu kwa dhati, hata ufike mwisho wa dunia, nchi yetu kamwe kama hatuta-*deal* na chanzo

cha migogoro ya ardhi, tukaendelea ku-*deal* na majawabu ya migogoro ya ardhi, nchi hii migogoro ya ardhi itaendelea kukithiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijikite kwenye enelo lingine la umuhimu la sekta ya ardhi. Wenzetu Walatini, kuna usemi mmoja wa Kilatini unasema, "*Quicquid plantatur solo, solo cedit.*" Maana yake nini? *Anything attached to the land from part of it, permanent attached,* na kuna masuala ya *fixture* huko na *fitting,* hilo ni somo lingine nitatoa siku nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa umuhimu wa sekta ya ardhi, ukizungumzia madini yako sekta ya ardhi; ukizungumzia kilomo, ni sekta ya ardhi. Kwa hiyo, niwaambie, sekta zote kama hamjashirikiana na Wizara ya Ardhi huko, aah, tunatwanga maji kwenye kinu. Namwona Mheshimiwa Bashe anakimbia kweli kweli, lakini namwangalia, kaka utafika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu Watanzania wenye hatimiliki hata za mashamba, ukifuatilia hata 1% hawafiki. Anakopeshekaje. Unakuwaje na kilimo biashara? Unamchukua mwekezaji huko, Mama anafanya kazi kubwa sana, Mheshimiwa Rais kuhamasisha wawekezaji ndani ya nchi, lakini tufanye hesabu kwenye kilimo, kuna wawekezaji wangapi wamewekeza kwenye…

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Karibu. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Ndiyo.

**TAARIFA**

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda tu kumpa taarifa mzungumzaji kwa mchango mzuri ambao anaendelea nao kwamba hata hii migogoro inayotokea ya wakulima pamoja na wafugaji chanzo chake ni hicho hicho kwamba hakuna mipango halisia iliyowekwa vizuri. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Unaipokea Taarifa Mhehsimiwa Kunambi?

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sana, kwa mchumi bobezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wakati nazungumza, nasema, hivi nasikilizwa hapa? Ila wajibu wangu ni kusema, nitasema tu. Hii ni *episode three,* nitaenda *episode five,* mpaka nimalize Ubunge wangu. Wananchi wa Malinyi wamesema wamenipa *guarantee* nitarudi tena hapa ili nifanye kazi yao vizuri. Kwa hiyo, nitaendelea mpaka Mungu atakapochukua uhai wangu, mpaka nione Tanzania imepangwa na kupimwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nihitimishe, nirudi jimboni kidogo, nimezungumza kwa niaba ya watanzania wote sasa nazungumza kwa wananchi wangu wa Jimbo la Mlimba, pale Mlimba, Kata ya Namawala, tuna mgogoro wa ardhi uliochukua takribani miaka 20 na Naibu Waziri tulizungumza, kwa kweli nakusifu sana Kaka yangu, *keep it up* unafanya vizuri. Hizi changamoto zote, ninyi ni wapya mmekuta zimerundikana lakini *anyway* tutawasaidia tu, huu mgogoro wa Kambenga kesi yake ni ndogo tu na nitawasaidia kutatua. Huyu bwana Kambenga alipata ardhi hekari mia moja akaongeza sifuri wakati wa miaka ya tisini akapata hekari elfu moja lakini makubaliano ya kijiji ni heka mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombe Mheshimiwa Naibu Waziri kama tulivyokubaliana na ikiwezekana tuambatane na Mheshimiwa Waziri kadri mtakavyoona inafaa. Twende kule tukatatue tatizo, ni tatizo dogo sana, lakini niwaambie nimekuwa mtu laini sana leo kwa sababu nimeona mmeanza vizuri. Niwaahidi kama hamjatatua ule mgogoro wa Kambenga nina shilingi ambayo mpaka leo sijairudisha. Kwenye bajeti yenu inayokuja mwezi wa tatu, hii ambayo ninayo nitaongeza tena na ya pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ile nyingine ninayo mpaka sasa sikuirudisha sasa sitaki nifike huko kwa sababu najua ninyi ni watu *Rahm* na Waziri wako twendeni mkatatue migogoro hasa ule wa Kambenga ili wananchi wangu wapate nafuu ya maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana ubarikiwe. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Godwin Kunambi, nilimtaja Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga, Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay na Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo ajiandae.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi. Nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya na nimeweza kusimama na kuchangia kwenye Taarifa hii ya Kamati ya Ardhi, Msaliasili na Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja Taarifa ya Kamati ya Ardhi na Maliasili, kwanza kabisa nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, ndugu yangu Jerry Silaa kwa kazi kubwa ambayo anaifanya ya kwenda kutatua migogoro iliyopo kwa hekima na nidhamu ya ari ya juu kwa sababu migogoro mingi iliyopo inahitaji hekima jinsi ambavyo migogoro inaendelea katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Jerry na Naibu wake kwa kazi kubwa ambayo wanafanya ya kuhakikisha kwamba tunakwenda kuwa salama lakini nimwambie Mheshimiwa Waziri tu kwamba hii migogoro anayokwenda kuitatua leo kesho itazuka migogoro mingine na mingine, kama Taifa hatujaamua kupanga matumizi bora ya ardhi. Kila itwapo kesho tutakwenda kuwa na migogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii inahitaji kupangiwa matumizi ya ardhi. Mimi nilikuwa mjumbe wa Kamati hii, nilitembea kwenye baadhi ya maeneo ambayo yamepangiwa matumizi bora ya ardhi. Watu hawagusi kwenye eneo ambalo sio la kwao, kama hautapanga matumizi bora ya ardhi hatutafanya kitu. Mheshimiwa Jerry atatatua mgogoro huu leo na kesho utazalika mwingine kule. Hii migogoro haitakwisha kama hatujafanya maamuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na Askofu Gwajima, safari hii kama hakutakuwa na bajeti ya kutosha ya Tume ya

Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi na mimi nitakuwa mmoja kati ya watu ambao hatutapitisha bajeti ya Wizara ya Ardhi safari hii. Lazima humu ndani kieleweke, kwa sababu haiwezekani tuwe tunashauri Serikali, tunapiga kelele. Sisi ndio wenye changamoto huko, tunatokanazo kwa wananchi wetu. Haya tunayozungumza sio ya kwetu, haya tunatumwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni Mbunge wa Viti Maalum, lakini nina Mkoa ambao ninatokea, Mkoa wa Tabora ndio Mkoa mkubwa kwa sasa hivi wenye eneo kubwa katika mikoa yote ya Tanzania na hata tunapozungumza kwamba Mkoa wa Tabora uwe ni miongoni mwa Mikoa ambayo itapunguzwa ili wananchi wetu waweze kupata maendeleo, tunaomba sana hili jambo litekelezwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ukubwa wake, ndio umekuwa Mkoa mkubwa pia hata kwenye hii migogoro. Nimwombe sana Mheshimiwa Waziri, katika *clinic* ambazo anaendelea nazo, naomba Mkoa wa Tabora upewe kipaumbele ili mwende kupunguza matatizo na changamoto za ardhi kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro inachosha, pale Tabora ardhi iliyopo ni kubwa sana kiasi kwamba matajiri wachache wanakwenda kununua ardhi sasa wanainunua wanahodhi ile ardhi, hata kama inatokea una jambo ambalo linataka lifanyike, hata kama kuna mwekezaji ni lazima umwone yule mtu ili yeye aweze kukuuzia ile ardhi. Sasa jambo hili ni baya, kama tungekuwa tumeshapanga matumizi ya ardhi kwenye maeneo yetu, tungejua hapa itajengwa shule, hapa hospitali, hapa kituo cha afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Wizara ya TAMISEMI, Mheshimiwa Rais anashusha fedha nyingi sana kwa ajili ya miradi ya hospitali, zahanati na miradi ya shule, lakini unakuta kuna maeneo mengine hatuna maeneo ya kujenga shule kwa sababu tu kuna watu wachache wanahodhi hayo maeneo, kwa hiyo watu wanashindwa kujenga kwa sababu kuna mtu fulani amechukua yale maeneo na anayauza kwa bei anayotaka yeye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo inasababisha migogoro na mtu anapoona kwamba lile eneo liko wazi anakwenda kufanya shughuli zake na yeye anajimilikisha matokeo yake unakuta tunaanza kukatana mapanga na kuuana. Kwa hiyo, niombe Serikali, tunashauri na kushauri sana tunaomba sana nchi hii ipangiwe matumizi bora ya ardhi ili tuweze kwenda sawa, vinginevyo Mheshimiwa Waziri mtahangaika sana, mnatatua mgogoro, halafu mgogoro mwingine unazaliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie Mabaraza ya Ardhi, hili jambo bado ni kero kwa wananchi, na mimi nafurahi sana jamani uletwe tu huo utaratibu wa kuondoa mabaraza ya ardhi ama wenyeviti. Huko ni rushwa tupu, hakuna lolote wanalofanya, wanasababisha migogoro tu kila uchwao. Mtu ana haki, ana hati, ana kila kitu, anahangaika mahakamani zaidi ya miaka mitano sita, kwa sababu tu ya Mwenyekiti wa Baraza la Ardhi aliyehukumu tofauti na hukumu ilivyokuwa inatakiwa. Na hii ni kwa sababu ya kukosa elimu ya ile kazi ambayo yanaifanya pelekeni haya mambo kwenye Mahakama zetu ili kule kuweze kwenda kufanyika vizuri na ili mambo yaweze kwenda sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumze kwenye suala zima la maliasili, Mkoa wa Tabora ni moja kati ya Mikoa ambayo ni ya kihistoria katika nchi hii. Mkoa wa Tabora katika mapambano ya kupigania uhuru ni moja kati ya mkoa ambao umetoa mchango mkubwa kwa nchi hii katika mapambano ya uhuru wa Taifa hili, lakini cha ajabu mpaka sasa nimekuwa nikizungumza sana maeneo yote yaliyopo Tabora ambayo yangeweza kufanywa kama makumbusho kwa ajili ya vitukuu vyetu watakaokuja wajue kwamba hapa jambo gani lilitokea na lipi lilitokea yametelekezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa mfano mmoja na hili nililizungumza hata kwenye mkutano wa hadhara niulipozungumza Tabora. Tuna eneo moja la taasisi pale Tabora, lipo katikati ya mji. Pale kuna sanamu ya Mwalimu Nyerere pale mwaka 1958, Mwalimu Nyerere alilia machozi akiomba uhuru wa

nchi hii, aliombea pale katika eneo lile amepiga magoti analia machozi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiona eneo lile ni changamoto kubwa, halina umeme, majengo yamechakaa, hiyo sanamu yenyewe ya Mwalimu Nyerere imechakaa. Unajiuliza ninyi kama watu wa Wizara ya Maliasili mna mambo ya makumbusho, mna mambo ya mali kale, mnashindwa hata kututengenezea eneo ambalo Mwalimu Nyerere alilia machozi wakati akiomba uhuru wa Taifa hili? Mnashindwa kuweka kwenye mazingira ya kufanya liwe ni eneo la makumbusho, mnafanya nini kwenye Wizara? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeongea kwa uchungu na nimeongea kwa ukali kwa sababu sio jambo ambalo nimelisema leo, hata Wabunge wenzangu baadhi wamekuwa wakilizungumza hili jambo, linatuchosha Mkoa wetu mnaufanya unazidi kuwa mkongwe. Sasa hivi Mkoa wa Tabora umefunguka. Tuwekeeni ili Wananchi wa Tanzania, watoto wetu, vitukuu na wajukuu waje wajue kwamba Mkoa wa Tabora ni moja kati ya Mikoa ambayo ilichangia katika uhuru wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwashukurusana *TAWA* na niseme kwamba, hapa nilizungumza na leo ninaomba. Watu hawa wameongezewa maeneo lakini pamoja na kuongezewa maeneo hawana *power* ya kutosha yaani hawana watendaji wa kutosha lakini hata waliopo malipo wanayolipwa hayaendani na kazi kubwa wanayofanya. Hali ni mbaya katika taasisi hii na ndio maana tuliomba hapa hawa *TAWA, TFS* wapewe mamlaka ili waweze kufanya majukumu yao. Mazingira yao ya kazi ni magumu na hata zile ela wanazopata ni kidogo sana haziendani na kazi kubwa wanayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwashukuru *TAWA* kwamba pamoja na Tabora kuwa na maeneo makubwa ya mapori lakini wameweza kutengeneza maeneo ya vivutio katika Mkoa wetu wa Tabora ili hata mtu anapokuja asikutane na mapori sana ili mwisho wa siku watu waende na waweze ku-*enjoy* na kuona hali na mazingira ya Tabora jinsi yalivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana, sasa hivi tunayo *zoo* pale Tabora, zamani ilikuwa ni pori kweli kweli, wadudu wote wakali walikuwa pale lakini leo ukifika Tabora utakutana na *zoo* ambayo iko pale eneo la *game* ambapo ni kivutio kizuri nani kivutio kikubwa. Ukifika Tabora unahitaji kupumzika unakwenda pale Tabora *zoo* na mambo yanakuwa mazuri kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tabora imefunguka, tunazo barabara, ni Mkoa ambao ni wa kihistoria. Tumechoka kuwa mji mkongwe na sisi tunataka maendeleo ikiwepo vitu vya kihistoria, viwekwe katika mazingira mazuri ili hata na sisi tunapotangaza watalii, watalii waweze kufika katika Mkoa wetu wa Tabora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niombe sana, Wizara hii haijapelekewa fedha. Fedha zilizopelekwa nimeangalia hapa *is almost 17%, 17%* kwa Wizara ya Maliasili unafanya nini? Leo ninavyozungumza Watalii wamekuja wengi kweli kweli lakini hizo barabara zinazopita kwenye hifadhi zetu umeziona? Hali ya barabara katika hifadhi zetu ni mbaya, kwa hiyo tunaomba Serikali ipeleke fedha haraka sana ili tuweze kupata fedha lazima tutoe fedha. Mtu hawezi kuja akakutana na hali mbaya namna ile ya barabara akakubali kwenda kufanya utalii wowote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe sana hizi barabara zitengenezwe haraka, watalii waendelee kuja ili tuweze kuendelea kuingiza pato ambalo tunalitarajia kutoka katika Wizara hii ya Maliasili. Fedha ndio kila kitu Wizara ikipewa fedha kazi zinaweza zikafanyika vizuri na mambo yakaenda sawasawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nirudi tena kwenye hili suala zima la ardhi na changamoto zake. Changamoto za ardhi zimekuwa ni nyingi sana. Niliona nikimbilie kwanza kwenye Wizara ya Maliasili ili niweze kuzungumzia Mkoa wangu kwa sababu natoka kwenye Mkoa huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyotangulia kusema, ardhi ndio kila kitu. Ardhi haiongezeki lakini sisi binadamu tunaongezeka, kwa hiyo, kwa sababu sisi binadamu tunaongezeka ni lazima tutengeneze mazingira ili kila mmoja

anapokuja awe ana eneo ambalo atalipata kuliko mtu mmoja kuhodhi ardhi zaidi ya hekari 1,000, 2,000, 10,000, hii kwa kweli sio sawa. Ni lazima mfike mahali mfanye maamuzi kwamba sasa hivi Mtanzania wa kawaida ardhi anayotakiwa kuwa nayo ni kiasi hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu watanzania tunaongezeka na hii ardhi iko vilevile na kila siku watu wanazaliwa, kila siku watu wanakufa lakini bado watu wanazidi kuongezeka na sisi tupo vilevile. Kwa hiyo, ili tuweze kuondoa changamoto hii ni lazima tufike mahali tuamue kwamba, mtanzania unatakiwa uhodhi ardhi kwa kilomita kadhaa ama hekari kadhaa ili mtu mwingine akija, kwa sababu tayari imeshapimwa na imeshawekewa matumizi ataambiwa pale mnaweza mkampimia raia anayetaka ama pale ni kwa ajili ya maeneo ya msingi ambayo tunataka kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana Wizara ya Ardhi na Wizara ya Maliasili wanahitaji sana fedha kwa ajili ya kuweza kutekeleza haya majukumu yao lakini niwaambie Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, kwamba kazi bado ni ngumu pamoja na kazi kubwa ambayo wanaifanya lakini mwisho wa siku changamoto ni nyingi kuliko hizo ambazo tayari zimeshatatuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Hawa Mwaifunga, nilimtaja Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay na badae atafuatiwa Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kuungana na wenzangu wote kumshukuru sana Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu wa Rehema ametupa nafasi hii leo kuweza kujadiliana masuala mbalimbali kwa ajili ya watanzania wetu. Pia, niipongeze Serikali kwa kazi kubwa inayofanya kupitia Wizara hizi zilizo chini ya Kamati hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nichukue nafasi hii kwa ujumla kutoa na kuchangia kwa sehemu Taarifa ya Kamati. Kwanza nizungumze tu kwamba ni karibu miaka kadhaa sasa tukisubiri hizi

Kanuni za Mwaka 2011 zilitwe Bungeni ili tuzitazame upya. Kanuni hizi ambazo zinazungumzia fidia pamoja na kifuta machozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni karibu miaka saba, kanuni hizi sio rafiki kwa watanzania kwa sababu unapozungumza kifuta machozi shilingi laki tano na fidia ama tunasema fidia kwa wale waliopoteza maisha kile kiasi cha shilingi milioni moja. Hebu tutazame kwa upana, kwanza hakuna fidia wala hakuna kifuta machozi kwa mtu ambaye tayari amepoteza maisha. Mimi ushauri wangu ni kwamba jambo hili lifanyiwe kazi na Serikali halafu mtuletee tulijadili tutazame kwa upana wake na athari zake kwa jinsi ambavyo tunapata madhara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni madhira makubwa kwa wananchi kwa sehemu hii ya fidia ya wanyama wakali, lakini pia wanaokuja kuleta madhara makubwa katika maisha ya watanzania. Hali hii inafanya Serikali kulalamikiwa lakini pia watanzania kuona kwamba sisi tunathamini zaidi wanyama kuliko maisha ya watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini eneo hili linakabiliwa sana na changamoto nyingi hasa kwa sisi tunaopakana na hifadhi. Mojawapo ni ile ya wanyama kutoka kwenda kuharibu mali za watanzania kwa muda mrefu na hakuna namna ya kuwazuia wala kuwarudisha kwenye yale maeneo. Pia hatua za haraka zinashindikana kwa sababu eneo hili linakabiliwa na changamoto kadhaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto mojawapo ni ukosefu wa wa wataalam, wale askari *game* lakini pia na vitendea kazi. Ni hali ambayo inasikitisha sana pale ambapo tunashindwa kuchukua hatua za makusudi ili kunusuru usalama wa wananchi na mali zao na hatimaye madhara yanakuwa makubwa. Pia, mahusiano ambayo sio mazuri kati ya wenzetu wa *TANAPA* na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Mbulu mji sio mji kama tunavyozungumza, lenyewe lina kata saba ziko mjini na kumi ziko vijijini, na kule kwenye kata za vijijini kuna hifadhi za *TANAPA* za Manyara na Mara, ambako kuna wanyama wakali na wanyama

waharibifu, lakini unakuta Tembo anatoka msituni anaharibu mazao ya mwananchi, matokeo yake yule mwananchi anaambiwa tutakufidia laki tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa akili ya kawaida ama hali ya kawaida, hatua ya kwanza ni kuwazuia na hatua ya pili ni kuchukua namna ya kuweza kuzuia majanga yanayotokea. Lakini unapozungumza madhara ya laki tatu wakati ng'ombe tu akiingia msituni ni shilingi laki moja, laki mbili. Hebu jambo hili litazamwe na tukijifunza kwa umbali zaidi tunaona madhira makubwa pengine wale wanyama wanafuata maji na chakula na kwa asilimia kubwa chakula huwa kipo msituni na suala kama ni maji si twendeni Serikali yetu ikafanye tafiti maeneo ya kujenga mabwawa ili kuweza kupatikana huduma ya maji katikati ya hifadhi zetu kuliko ambavyo wanatoka nje wanaharibu mazao ya wananchi, usalama wa wananchi na maisha ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia hali hiyo imesababisha mahusiano ya wenzetu wa *TFS* na wale wa *TANAPA* kuwa mabaya sana na wananchi katika maeneo ya vijiji, hali ambayo baadaye Serikali ndiyo inalaumiwa, kumbe sisi ndio tunatakiwa kuchukua hatua, na kadri tunavyochelewa kuchukua hatua basi wananchi wanaichukia Serikali, ningeomba yale yanayowezekana yawekwe kwenye mpango na utaratibu ufanyike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna matumizi makubwa na yasiyorafiki kati ya Askari wa *TANAPA* na wananchi wetu hasa katika hifadhi hizi ambazo zinapakana na wananchi. Nini kifanyike? Vikao vya ujirani mwema, mahusiano mazuri, kuweza kutafsiriana majanga yanayotokea na namna ya kukabiliana nayo na uwazi kwa mambo yanayotokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mambo mengine ni magumu, ya wananchi kupotea msituni na hata hawafahamiki walipo. Mheshimiwa Waziri wa Maliasili nilikusihi sana ufanye ziara Mbulu. Mbulu siyo salama kama tunavyofikiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niombe, mimi kama mwakailishi wa wananchi siwezi kuzungumza kitu ambacho

hakina ukweli ama hali ikoje. Kwa hiyo, mimi naomba sana kama inawezekana, upande wa Serikali na upande wa wachaguliwa wote tunajenga nyumba moja. Nia yetu ikiwa ni kujenga taswira nzuri ya wananchi kuipenda Serikali yao. Kwa hiyo, mimi nadhani jambo hili lina umuhimu mkubwa, ulichukulie hatua na uweze kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichangie eneo la upimaji; hii KKK kwa maana ya kupanga, kupima na kumilikisha. Nia ya Serikali ilikuwa njema sana, na tunaipongeza sna Serikali kwa kuja na mpango huu, lakini mpango wowote unapoanzishwa inafika mahali tuje tukae chini ili tufanye tathimini ya mapungufu yaliyoonekana na namna ya kuyarekebisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo hili fedha zinatumwa halmashauri, unakuta halmashauri hatuna wataalamu, kampuni inatafutwa inakwenda kufanya upimaji, inafanya upimaji ambao haujakamilika. Pengine eneo fulani limepimwa lakini upimaji haujaainishwa kwa mipaka halisi na malalamiko ya wananchi hayajafanyiwa kazi. Matokeo yake yale makusanyo ya fedha yanakosekana, na hata uendelezaji wa ule mpango unakwama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa na ushauri, kama itawezekana tukubaliane na baadhi ya wajumbe waliochangia, kwamba tuangalie sasa suala la kupanga, kupima na kumilikisha liwe suala la Wizara ya Ardhi. Pia, lifanywe na maafisa wa ardhi kwenye ngazi za halmashauri, kama hawapo waazimwe kwenye halmashauri nyingine. Wakati huo ukusanyaji wa maduhuli yale ya upimaji, pia ufanywe na maafisa wa ardhi. Ni kazi ngumu sana inapokuwa anayepima ni mwingine, anayekusanya fedha ni mwingine, mpango kabambe wa *master plan* unaandaliwa na mwingine. Matokeo yake mradi huu na mpango huu utakwama na mwisho wa siku hautakuwa na tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini napendekeza jambo hili? Majukumu ya upimaji, upangaji na umilikishaji, sasa hivi tumekwenda kufanya tathmini katika nchi nzima hakuna hati zilizotolewa inagawa tunazungumza ni KKK. Je, kama "K" ya kwanza ya kupanga ilifanywa na afisa ardhi, "K" ya pili ikafanywa na afisa ardhi, kwa maana ya kupima, na "K" ya tatu ya

kumilikisha anatakiwa afanye afisa ardhi; na fedha za makusanyo katika eneo hili inatakiwa ikusanywe na afisa ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yanawezekana. Niipongeze sana Serikali kwa hatua hizi inazochukuwa. Kuna athari kubwa sana sasa hivi kwenye maeneo ya miji na yale maeneo ambayo yanafikiwa na upimaji, hasa yale ya miji. Tunakosa maeneo ya vituo vya afya, tunakosa maeneo ya ujenzi wa shule, tunakosa maeneo ya huduma nyingine mpaka za mazishi kwa sababu mipango ya ardhi, au ule mpango kabambe wa *master plan* haujaweza kuingiza hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini kifanyike? Ni kwamba mipango hii iwekwe wakati wa kupanga *master plan* (mpango kabambe wa eneo linalokusudiwa kwa mradi huu) ili uweze kukidhi mahitaji ya wakati huo na kwa jinsi ambavyo itawezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia tuna maeneo, kwa mfano watu wa Wizara ya Ardhi. Waziri wa Ardhi na timu yake hebu tuangalie sasa hivi. Kwa mfano *National housing* wanajenga kwenye miji mikubwa lakini kwenye miji ya halmashauri kuna nyumba zao zilikwishakuwa chakavu, kama kule Mbulu, hzaifai hata kuona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini waipange kwa mwaka kwa yale maeneo ambayo yana nyumba zao zilizo chakavu, wakatenga fedha wakajenga hata ghorofa moja, wafanyakazi na watu wengine wakanunua majengo kwenye yale maghorofa na mengine yakapangishwa kwa watu wenye uhitaji, ili kuweza kujenga miji yenye taswira nzuri lakini pia kwa miji ambayo hatima yake inakuwa imepangika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi nilikuwa nadhani wafanye tathimini katika maeneo ya miji ambayo tayari ni miji kongwe ya zamani na wamekwishakuwa na maeneo. Hayo maeneo yajengwe nyumba za kuuzia wananchi, watumishi lakini pia kujenga majengo yale na kuibadilisha sura za miji. Vilevile waweze kutembelea hayo maeneo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mpango kabambe wa upimaji wa vijiji. Huu mpango tusipouchukua kwa mfano Mkoa kama wa Manyara una kesi nyingi za ardhi. Maana upimaji ungekuwa umepima Kijiji, tukatoka ngazi ya upimaji wa Kijiji, tukasogea upimaji hata wa kila mwananchi kote nchini, itawezekana kuondoa migogoro ya ardhi, vile vile wananchi wanaomiliki zile ardhi watakuwa na manufaa makubwa na thamani ya zile ardhi itakuwa imeonekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mpango huu ambao tunakwenda tu tunaanzisha mabaraza ya ardhi siyo njia ya kuzuia kesi za ardhi. Maana yake baadaye tutapata mabaraza ya ardhi ngazi ya kata na gharama za kuyahudumia kwa sababu mahitaji yatakuwa makubwa kulingana na hali halisi ambayo tatizo linazidi kujitanua na linakuwa kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi nilikuwa nashauri, kama itawezekana, katika bajeti tuwe walau tunatoka katika ngazi za upimaji wa mipaka ya vijiji halafu, ndipo tuje na mpango wa kwenda kwenye upimaji wa mwananchi mmoja mmoja. Na kwa kuwa sehemu kubwa wananhi ndio wanaogharamia, na hata hizo za vijiji wanaweza kugharamia baadhi ya gharama, tuangalie namna ya kuingia ubia wa hizo gharama ili kuipunguzia Serikali gharama kubwa ya upimaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije tena kwenye eneo lingine ambalo nataka nilizungumzie kwa namna ya pekee sana; eneo la mapato; fedha hazikusanywi kwa nini? Tunapozungumza asilimia 22, sasa hivi tumebakiza miezi minne. Hebu kwa akili ya kawaida hatupaswi kukaa chini na kutafakari kama Serikali? Ina maana miezi minne iliyobaki tuta-*cover* hiyo asilimia 76. Hatuoni kuwa hata tukipambana kwa vyovyote vile tna kwa namna yoyote ile hatuwezi kukusanya hizo fedha asilimia 70 na kitu katika miezi minne iliyobaki kuelekea mwaka mpya wa bajeti?

Mheshimiwa Mwenyekiti, na hali hii inasbababishwa kwanza na mkanganyiko uliopo wa upungufu wa watumishi kwenye kada hiyo pamoja na uwajibikaji usiokidhi haja. Watu tuko katika nafasi hizo kwa kukaa tu bila kufanya majukumu yetu ya kila siku na usimamizi ambao unakidhi haja na kuweza kufikia hatua ambayo

inastahili na itafanikisha sana kwa jinsi ambavyo fedha hizo zinahitaji kukusanywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi ama mamlaka yoyote ile inayoshindwa kukusanya, itakaposhindwa kukusanya ni lazima itashindwa kutoa huduma bora kwa wananchi kwa kadri ilivyokusudiwa na hii inachangiwa na wachache ambao pengine hawazitendei haki nafasi zao lakini pia kufanikisha na kufanya kazi kubwa inayoweza kuleta tija ya kuwahudumia wananchi na jamii kwa ujumla. Vilevile kwa upande wa majukumu yetu tuliyoomba kwa wananchi, iwe mtumishi au mchaguliwa kwa kadri ambavyo kila mmoja tunatakiwa atimize wajibu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho niishukuru Serikali, na niombe sana katika ajira zinazokuja tuangalie zile kada muhimu kwenye halmashauri, hasa Wizara ya Ardhi lakini pia kwenye halmashauri. Kwa sababu ukizunbgumza Wizara ya Ardhi na Wizara ya TAMISEMI ni wizara mbili zinazoshabihiana katika majukumu ya kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa unapokuta katika halmashauri huna watumishi wa idara ya ardhi katika eneo lile la halmashauri huwezi kutekeleza mipango hii kabambe inayokusudiwa na Serikali. Kwa hiyo, niishukuru Serikali lakini kwenye bajeti tusi-*base* tu upande mmoja wa kuajiri sekta moja na tunaacha upande wa pili tunakwama na mwisho wake hatuna vitendea kazi lakini pia hatuna watumishi ambao wataweza kutufanyia hizo kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Zacharia. Nilimtaja Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo.

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Kwanza kabisa napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuwa mwaka huu 2024 leo ndiyo siku ninachangia mara ya kwanza; namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uhai. Napenda nichukue nafasi hii kwanza kabisa kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri ambazo anazifanya

za kuwatumikia Watanzania. Watanzania wote wameona kazi ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, inavyofanyika kuanzia kijijini mpaka mijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiwa kama Mjumbe wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii, napenda kuunga mkono Maazimio yote ya Kamati yaliyosomwa na Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Timotheo Mnzava.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana tulikuwa hapa, Bunge likatoa maagizo na maazimio yakapitishwa. Kati ya maazimio hayo, Wizara ya Maliasili na Utalii ilikuwa na maazimio 10. Maazimio manne yametekelezwa, mawili yanaendelea kufanyiwa kazi lakini manne hayajatekelezwa. Naomba niyasome.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maazimio ya mwaka 2023 tuliyokuwa tumeazimia yameshindwa kutekelezwa:-

(a) Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Wanyamapori T*AWA*.

(b) Kushindwa kutekeleza mchakato wa kupandisha hifadhi ya misitu Tanzania *TFS*.

(c) Kushindwa kuanzisha mchakato wa sera zilizopitwa na wakati.

(d) Kushindwa kuchukua hatua za haraka kwa wawekezaji wa hoteli na *lodge* ambao walikiuka masharti ya mikataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maazimio hayo tuliyoyatoa mwaka 2023 hapa Bungeni na hayajatekelezwa. Sasa ninaanza pale kwenye kushindwa kuchukua hatua madhubuti kwenye hoteli zilizoshindwa kutekeleza mikataba yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliazimia na tukatoa maazimio ndani ya Bunge hili ambayo ni maazimio ya Bunge, kwamba Serikali irudishe zile hoteli ambazo watu walibinafishiwa lakini

hawakuweza kuendeleza. Nini maana yake? Kuna hoteli ambazo toka zimebinafisishwa hazijawahi kufanya kazi. vilevile, kuna hoteli ambazo zimebinafisishwa lakini zina-*operate* kwa kiwango cha chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baba wa Taifa Hayati, Mwalimu Nyerere, alijenga hoteli kila mkoa. Kulikuwa na *Mbeya Hotel, Tabora Hotel, Dodoma Hotel, Musoma Hotel.* Hoteli hizi zote zina-*operate* kwa kiwango cha chini. Ni bora zilivyokuwa kabla hazijabinafisishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipitia azimio kwamba, Serikali irudishe hoteli hizo kwa sababu waliopewa wamevunja mkataba na hawakuweza kutimiza masharti ya mikataba. Hata hivyo, azimio hilo halijatekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziko *hotel* kama *Embassy Hotel, Kunduchi Beach Hotel,* Mikumi na *Lodge* nyingi kule Manyara, zote hizo zipo na zilikuwa za Serikali, zilibinafisishwa na zinafanya kazi kwa kiwango cha chni sana. Embassy imefungwa na ninafikiri takribani miaka 14 sasa pana uzio pale na iko katikati ya Dar es salaam. Vile vile, kuna *Agip Hotel* pale ziko nyingi. Hivyo, ninaomba Bunge hili labda lije na utaratibu wa kuunda Kamati ambayo itakwenda kufuatilia Mazimio ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumzia hapa ni kusisitiza kwamba, katika hizo hoteli tulimwita *TR* wa wakati huo kabla ya huyu wa sasa alikuja kwenye Kamati na tukampa maagizo ya kulifanyia kazi hilo suala. Tunamuomba *TR* wa sasa alifanyie kazi suala la hoteli ambazo zilibinafsishwa na hazifanyi kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo ningependa kulizungumza kwenye Wizara ya Maliasili na Utalii ni suala la miundombinu mibovu iliyopo kwenye mbuga zetu za wanyama. Mheshimiwa Hawa Mwaifunga, amezungumza hapa lakini na mimi napenda nizungumzie hapo. Mbunga zetu za wanyama zinatuingizia pato la Taifa kama alivyosema Mwenyekiti hapa takribani asilimia 25. Hata hivyo, mbunga hizo za wanyama barabara zake ni mbovu. Nachelea kusema kwamba ni mbovu.

Katika mvua hizi za masika tumeona magari yakizama kule Serengeti na watalii wakishuka na kusukuma magari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, madaraja yaliyopo kwenye mbunga zetu za wananyama, kama derava hajui kuendesha vizuri gari linatumbukia kwenye maji. Niombe basi, hii Wizara ya Maliasili na Utalii washirikiane na Wizara ya Ujenzi ili waweze kuweka miundombinu mizuri kwenye Hifadhi zetu za Taifa. Tukianzia na hiyo Serengeti ambayo inafahamika duniani kote, lakini pia Ngorongoro na hifadhi nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo madaraja ya Serengeti siyo kwamba ninazungumza kwa kusoma kwenye karatasi tu, tulikwenda Serengeti na nilishuhudia jinsi magari yalivyokuwa yanazama. Ni kitu ambacho nilikiona na ninaweza kuchelea kusema kwamba, vilevile, vidaraja ni vidogo na havifai kuwa kwenye hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Wizara ishirikiane na iangalie itatoa wapi pesa au itafanyaje ili iweze kujenga barabara zetu zilizoko kule kwenye hifadhi zetu, na ukiangalia kwamba Pato la Taifa asilimia 25 linatokana na wageni wanaokuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi hapo hapo kwenye Wizara ya Maliasili na Utalii. Mheshimiwa Rais alitusaidia kuitangaza nchi hii kwa filamu yake ya *Royal Tour.* Sasa hivi wageni wanaokuja kwenda kwenye hifadhi wanakosa vitanda, nikiwa na maana kwamba hoteli hazitoshi. Ndiyo maana natoa msisitizo kwamba, hoteli ambazo zimeshindwa kutekeleza masharti ya mkataba Serikali izichukue. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo ningependa kulizungumzia kwenye Wizara ya Maliasili na Utalii ni utangazaji wa hifadhi zetu. Hifadhi zetu za Tanzania zinapaswa zipewe uwiano mzuri wa kutangazwa. Nikiwa namaanisha kwamba, tusitangaze Ngorongoro kila siku, Serengeti kila siku, ziko na hifadhi nyingine. Nitoe mfano hifadhi ya kule kwetu Katavi nayo pia inahitaji kutangazwa. Hii ni kwa sababu nayo ni hifadhi nzuri lakini pia ina Wanyama wazuri; ina twiga mpaka mweupe ambaye hapatikani

kwenye hifadhi nyingine yoyote. Sasa iwenje unapofungua ile *channel* ya Tanzania ambayo inatangaza unakuta inarudia hifadhi Serengeti, *Serengeti shall never die,* Ngorongoro hiyo hiyo, wakati kuna hifadhi nyingine. Tuweke uwiano kama ni mwezi mzima unatangaza Serengeti, mwezi ujao tangaza *Katavi National Park* mwezi mwingine tangaza Saadani, mwezi mwingine tangaza Gombe ili kuwe na uwiano. Nafikiri hawa waratibu wa haya matangazo wamenisikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo ningependa kulizungumzia kwenye Wizara ya Maliasili na Utalii ni suala la kuweka mazingira rafiki kati ya wale wageni wanaokuja na hoteli zilizopo kwenye mbuga zetu. Kuna hoteli katika mbuga zetu ambazo *charge* usiku mmoja ni takribani dola 1400 kwa siku. Ina maana mtalii analala kwa dola 1400. Hivyo basi, muone kama mtu binafsi anaweza kujenga hotel akatengeneza dola 1400 kwa siku ni kwa nini Serikali isitengeneze hoteli ya aina hiyo hiyo ikatengeneza dola 1400 kwa siku? Zipo hoteli kama *Four Seasons* kule Serengeti na nyingine nyingi. Kwa hiyo, kwenye Wizara ya Maliasili na Utalii ninapenda kulisisitizia hilo na lifanyiwe kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakwenda kwenye Wizara ya Ardhi. Kwenye Wizara ya Ardhi nitakuwa na machache ya kusisitiza, hususani suala la zile fedha, dola bilioni 150 sawa na takribani bilioni 346 ya hela za Kitanzania. Kati ya fedha hizo kuna suala la ujenzi wa ofisi za ardhi katika kila mkoa. Niombe basi, wakati watakapokuwa wanatoa hizi pesa za kujenga hizo Ofisi, basi kwanza ningeomba ile ramani ya jengo ifanane, kwa sababu katika ripoti yao walisema watajenga ofisi za ardhi katika mikoa 25. Niombe, ili kuwe na uwiano wa pesa na ili ile pesa iweze kutumika vizuri na isionekane kuna upendeleo kwa fulani na fulani; kwanza ramani iwe moja ambayo itajengwa hiyo ofisi ya ardhi kwenye kila mkoa. Pili, yale matumizi ya pesa, kama Mkoa wa Tabora utapewa bilioni kadhaa, labda *let say* bilioni 80, basi na Mkoa wa Katavi upewe bilioni hiyo hiyo na ramani iwe moja ili isije ikaonekana Mkoa mwingine kwamba umeongezewa pesa kwa sababu ramani yake ni kubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitoka kwenye Wizara ya Ardhi, naomba nirudi kwenye Wizara ya Maliasili niende niizungumzie

*TAWIRI, TAWIRI* ni taasisi ya Serikali. Hii *TAWIRI* ni *Tanzania Wildlife Research Institute* ambayo inafanya *Research* kwa ajili ya wanayama wetu nchini Tanzania, kuangalia kama kuna magonjwa Wanyama wamepata lakini pia kuangalia mambo yote ya wanyamapori nchini Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taasisi hii ilianzishwa tangu mwaka 1980, lakini cha kushangaza ndiyo taasisi ambayo inafanya *research* kwa wanayama wote, sijui kiboko, sijui tembo ameugua, sijui pundamilia wamekufa, sijui nini, wote hao ndiyo wanafanya *research* kuangalia ni kwa nini wamekufa. Maana yake ni *scientific research* lakini cha kushangaza taasisi hii haina jengo tangu mwaka 1980. Taasisi hii inapewa bajeti ndogo. Pia, niliona jengo la *research* kule Serengeti ni kama vinyumba nyumba fulani hivi vimekaa pale ambavyo vimeachwa kwa muda mrefu bila kupakwa rangi. Halafu eti unategemea taasisi kama hii ije na *research* ambayo itaweza kuboresha mambo ya wanayamapori nchini Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kweli tunataka kuboresha mambo ya wanayamapori na kupata *research* nzuri kutoka kwenye hii taasisi ya *Tanzania Research institute (TAWIRI)* ambayo ipo Arusha tuna wajibu wa kuwapa bajeti ya kutosha, kujenga makao makuu ya taasisi hii pamoja na kwenda kurekebisha yale majengo yaliyopo Serengeti ambayo kwa kweli nachelea kusema ni majengo ambayo yako kwenye kiwango cha chini kabisa; nimeyaona kwa macho yangu. Hivyo, basi nilikuwa naiomba Serikali itilie mkazo suala hili la hii *research* ya *TAWIRI*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiweza kuboresha taasisi hii, tutajua ni jinsi gani tunakwenda kupandisha utalii wetu nchini Tanzania kwa faida yetu sisi lakini pia kwa faida ya kizazi kinachokuja. Haiwezekani taasisi mwaka 1980 mpaka sasa ni *almost 40 years* taasisi haina jengo eti tunasubiri kupata *results* nzuri kutoka kwenye taasisi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi hii. Naomba tu niseme kwamba ninaunga mkono hoja zote za Kamati na Maazimio yote yaliyotolewa na Kamati na ninaomba maazimio ya mwaka jana na maazimio ya mwaka huu Serikali

isipoyatekeleza mwakani tutayaleta, na hata mwaka 2030 tutayaleta tena. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Taska.

Waheshimiwa Wabunge, muda wetu wa mchana huu kwa ratiba yetu umeishia hapa. Kabla sijasitisha shughuli za Bunge kuna tangazo hapa la wageni ambao wapo muda huu wa mchana ambao ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge.

Wageni wawili wa Mheshimiwa Exaud Kigahe, Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara ambao ni Wananchama wa Chama cha Wafanyabiashara wa Madini Tanzania (CHAMATA) kutoka Jijini Arusha, wale pale; karibuni sana. *(Makofi)*

Pia kuna wageni ambao wametembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo ambao ni wanafunzi 90 na walimu kumi kutoka Shule ya Msingi *St. Monica* ya Jijini Arusha, karibuni sana wageni au wanafunzi wetu katika Bunge letu kutoka huko Arusha. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijasitisha naomba nitaje majina ya ambao watachangia jioni; tutaanza na Mheshimiwa Festo Richard Sanga, Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah, Mheshimiwa Edward Olelekaita, Mheshimiwa Aida Khenani, Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta na Mheshimiwa Ezra John Chiwelesa.

Baada ya kusema hayo nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 asubuhi.

*(Saa 7.04 Mchana Bunge lilisitishwa hadi saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA KAMATI

### Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2023

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano yetu, tutaanza na Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah, Mheshimiwa Edward Olelekaita ajiandae.

**MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi kuweza kuchangia taarifa ya Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii, nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Mwenyekiti Ndugu Mnzava pamoja na Kamati kwa ujumla kwa utayarishaji mzuri wa taarifa hali kadhalika na uwasilishaji wa taarifa yenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu *Allah Subhanahu Wa Taala* kwa kutujalia uzima na kutupa kibali cha uhai na wale ambao kidogo afya zao zina mgogoro basi allah awajalie wapone haraka ili waungane na Watanzania wenzao kuja kulijenga Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu kwanza ningependa kumshukuru sana na kumpongeza Mama Samia kwa juhudi zake ambaye ni mwanamazingira na mhifadhi nambari moja ambaye amejitolea siku yake ya kuzaliwa kwenda kupanda miti katika eneo la Donge Muhanda, hii inatupa sisi wanajamii wa Tanzania kwamba kama kiongozi mkubwa kama yeye amejitolea siku yake kubwa ya kuzaliwa kwenda kupanda miti, na siku hiyo amepanda miti karibu miti 5,400, sasa kama ingekuwa kwa viongozi wetu wote kuanzia ngazi za Taifa, ngazi za Mkoa, Wilaya hadi Vijiji basi kama siku zao za kuzaliwa wanapanda miti namna alivyofanya Mheshimiwa Rais basi sijui Tanzania ingekuwa na miti kiasi gani. Hali kadhalika nafikiri tunafahamu kwamba Watanzania tupo milioni 60, sasa kama kila mtanzania siku yake ya kuzaliwa angepanda miti basi ingekuwa kila mwaka tunakwenda kupanda miti milioni 60 mbali zile jitihada za *TFS* na jitihada za wadau wengine katika kupanda miti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiria tu hii iwe ni chachu kwa viongozi hali kadhalika na kwa wadau wengine kufuata nyayo za Mheshimiwa Rais kuweza kutukuza siku zao za kuzaliwa kwa kwenda kuhifadhi mazingira. Nafikiri wale wasanii akina Diamond, Harmonize, kina Nandy, akina Ali Kiba na kadhalika sasa badala ya kwenda kwenye majukwaa kama kwenda *Serena Hotel* kwenda kusheherekea siku zao za kuzaliwa basi nafikiri wameshapewa mafunzo mazuri ya mazingatio sasa walekeze siku zao za kuzaliwa katika kuhifadhi mazingira na itaacha *legacy* katika maisha yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu pia ni utangulizi nafikiri Mheshimiwa Rais ametoa dira kwamba hali ya uhifadhi, hali ya misitu yetu Tanzania siyo nzuri sana, kwa sababu wataalam wanatuambia kwamba kila mwaka tunapoteza karibu hekta zaidi ya laki tatu za misitu. Hii inatujulisha kitu gani? Hii inaonyesha kwamba maji ambayo yallitakiwa yatiririke kutoka katika misitu yetu ya jamii au misitu yetu ya asili kwa uharibifu wa misitu inakwenda kupungua, lakini nishati ambayo inategemea sana maji katika maeneo tofauti ya misitu yetu inakwenda kuathirika, hata shughuli za utalii ambazo vivutio vingi vinapatikana katika maeneo ya misitu vinakwenda kuathirika, hii nafikiria tunaweza tukapima Tanzania tunaathirika kiasi gani kwa uharibifu au upoteaji wa misitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama jitihada hazikuongezeka za kupanda na kuhifadhi misitu yetu ya asili na tukaelekeza jitihada zetu katika kulaumu zaidi na katika kuji-*defend,* kwa sababu utaona kuna hali halisi ambayo inajitokeza mara nyingi kwamba oooh wananchi wanataka eneo la kulima, wananchi wanataka eneo la mifugo, wananchi wanataka maeneo tofauti tofauti kwa shughuli mbalimbali lakini bila kuangalia thamani ya mazingira yetu, thamani ya misitu yetu kama ikitoweka hizi sekta nyingine za kilimo, mifugo, uvuvi, nishati na kadhalika zitakwenda kuathirika kwa kiasi gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ningependa kutoa wito kwa maliasili lakini hata kwa Mheshimiwa Rais, nafikiri sasa ilishafika hatua kwamba tuje na semina elekezi ambayo

itajumuisha watendaji wote wakubwa wakiwemo Mawaziri, Makatibu Wakuu na vyombo vingine mbalimbali ili tuje tujadili hali halisi ya uharibifu wa mazingira, hali halisi ya uharibifu wa misitu Tanzania na kila mtu aondoke na jukumu lake pale. Kwa sababu tunajua kwamba kuna jitihada mbalimbali zimefanyika au zimewekwa, kwa mfano wenzetu wa mazingira wamekuja na mpango kabambe ambao unategemea kila sekta i-*play its part, our part.* Ukiangalia uhalisia kila sekta imejifungia upande wake haifanyi vya kutosha, sasa nafikiria katika semina elekezi itatusaidia kuweza kila taasisi kuweza kuelekezwa upande gani ikafanye shughuli zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ningeomba nichangie kidogo kuhusu suala zima la bajeti, nafikiri Kamati imetufahamisha hapa kwamba bajeti hasa upande wa maendeleo, nafikiri mpaka sasa hivi kuna asilimia 17. Tumebakisha nafikiri kama miezi mitano ama sita hivi tuweze kufika mwisho wa utekelezaji wa bajeti hii. Sasa hii inatoa picha gani? Kwamba hali ya mtiririko wa fedha hauko vizuri. Ningependekeza turejee katika maazimio ya miaka miwili iliyopita. Tumezungumza hapa kwamba ni vema suala la *retention* ambalo lilikuwepo huko nyuma tulirejeshe, yaliwekwa maazimio mwaka juzi, mwaka jana lakini azimio hili halijatekelezwa katika hali yake ya ukamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeliomba tu kwamba Wizara ya Fedha hivi kuna kigugumizi gani kuweza kupanga *retention* au kurudisha *retention* ya asilimia 30 siyo asilimia 100 ni asilimia 30 na asilimia 70 tuka-*retain* tukafanya kazi za maendeleo katika mambo mengine. Kwa sababu dunia nzima masuala ya uhifadhi basi yanaendeshwa kwa *retention*, kwa kutegemea fedha za *OC,* fedha zitoke kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali ndiyo zitumike zirudi si rahisi, kwa sababu mambo mengi ya uhifadhi ni mambo ya dharura. Moto ukitokezea hausemi utatokezea kesho, keshokutwa, hali kadhalika uvamizi umetokezea hausemi utatokea lini. Sasa kama hatukuweka *retention* jamani wa *are very hypothetical,* hatuhifadhi maliasili katika hali ya kisayansi tunahifadhi katika hali tunayojua sisi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri wa Fedha ningeliomba hili nasikia kwamba tumeanzisha utaratibu wa *escroll* kwamba kutakuwa na *account* maalum ambayo tutaweka fedha asilimia sita, na asilimia sita hii asilimia tatu

itakwenda kwenye hifadhi na asilimia tatu itakwenda kwenye masuala mengine ya kutangaza utalii lakini mimi naona hili siyo suluhisho ambalo lina afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeliomba Waziri wa Fedha akafuata maelekezo ya Bunge lako Tukufu ya kwamba tuende tukaweke *retention* ambayo itakwenda kusaidia hizi hifadhi *TANAPA, WMA* na wenzao kuweza ku-*retain* hizo fedha na kutumia katika maeneo mbalimbali badala ya kutegemea ruzuku kutoka Serikalini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka hapa kipindi kile Mheshimiwa Mchengerwa alikuwa nafikiri alikuwa ndiyo Waziri, aliahidi kwamba kila mwanzo wa mwaka basi watatenga bajeti mbili zitapelekwa kwa miezi miwili ili hizi bajeti hizo moja ikae kama *standby* na moja ndiyo itumike, hata hilo halikufanyika! Tutakuwa tunakaa hapa tunapitisha mambo halafu wenzetu wa Serikali wakishafika Wizarani huko wanayafumbia macho nafikiri hili halina afya na ningeliomba likafanyiwa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala jingine kuna maazimio ambayo wenzetu hapa mwaka jana tuliyapitisha unakumbuka wewe, kuna maazimio kumi tuliyapitisha na tumeambiwa kuna maazimio manne yametekelezwa kwa vizuri na maazimio mawili yako kwenye mchakato, maazimio manne hayakutekelezwa kabisa, maazimio haya ukiangalia ndiyo afya ya uhifadhi wa maliasili zetu. Mfano, kama Azimio la kuweza kuipandisha hadhi taasisi ya *TFS* kuwa mamlaka, tumelipigia kelele sana lakini naona katika Azimio ambalo limefeli kutekelezwa ni hili la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, azimio la kuweza kuhuisha sheria ambazo zimeshapitwa na wakati au sheria ambazo zilishakaa muda mrefu na ni sera lakini mpaka hilo nalo halikufanyiwa kazi na inasemekana kwamba wenzetu wa Serikali wamejitetea kwamba hizi sera ziko vizuri. Jamani nafikiri mwezi mmoja uliopita tulikuwa huko Dubai tumeona mabadiliko ya sayansi, mabadiliko ya teknolojia, mabadiliko ya kidunia yanavyokwenda kwa kasi, ndani ya miaka 15 tunasema kwamba sera hii bado iko rafiki na inafaa kwa mazingira ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiria siyo haki wenzetu wa Serikali hawalifanyii haki hili Bunge kwa sababu kama kuna mambo tunayapitisha tu pamoja halafu tena wakishajifungia Wizarani huko wanasema Hapana, tunakwenda hivi ni vyema tukaa kitako wakati tunakubaliana kwenye Kamati na tunakuja kupitisha hapa basi haya maazimio yatekelezwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna azimio la *WMA* kutayarisha sheria yake *independent* badala ya kuongozwa na Bodi mpaka leo nafikiri ni zaidi ya miaka saba Wabunge wanapiga kelele, sheria hii haijaja bado hapa, hili ni tatizo, kwa hiyo ningeliomba wenzetu hawa tunapokaa pamoja tukapanga basi ni vyema tukafanya mambo kwa pamoja na makubaliano yakatekelezwa kinyume chake inakuwa hawalipi heshima Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala jingine ni suala zima la Jeshi la Uhifadhi. Tumekuwa tukizungumza mara nyingi hapa kwamba Jeshi la Uhifadhi maslahi yake bado yako duni. Vijana hawa wanafanya kazi nyingi ambazo zinahatarisha maisha yao, kwa hiyo ningeliomba tu tuende tukawasaidie kutayarisha maslahi mazuri, *package* nzuri kama yalivyo Majeshi mengine Jeshi la Uhifadhi nalo waweze ikiwezekana kupata mishahara na marupurupu yanayofanana Majeshi mengine ili kuwatia moyo na mazingira magumu wanayofanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kengele imelia naunga mkono hoja *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah. Nilimtaja Mheshimiwa Edward Olelekaita, Mheshimiwa Aida Khenani na Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, wajiandae

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi. Kwanza kwa sababu ya muda nichukue muda huu kupongeza Kamati ya Ardhi, Maliasili, Mazingira na Utalii kwa kazi nzuri ambayo wameifanya hapa, nipongeze pia Serikali Wizara ya Ardhi na Maliasili kwa kazi wanazojaribu kufanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaongelea kidogo kuhusu migogoro. Tumeona *data* hapa kwamba vijiji viko 12,318 hivi, halafu vijiji vilivyopimwa na kuwa na matumizi bora ya ardhi ni 3,681, halafu ambazo bado ni karibu 8,638 hivi, sasa hii inatisha kidogo, kwamba migogoro ambayo imekuwepo kwa muda mrefu baina ya vijiji na hifadhi, Wilaya - Wilaya, Kijiji kwa Kijiji, lakini kubwa zaidi migogoro inaondoa raha sana kutoka kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema Wizara na *specifically* Tume hii Taifa matumizi bora ya ardhi kama walivyosema Kamati wapewe pesa nyingi sana ili tukiondokana na migogoro haya mengine yote tunayapanga itawezekana, bila kupima vijiji kwanza, mipaka ikafahamika na matumizi ya ardhi yakawekwa vizuri migogoro inaweza ikaendelea kwa miaka na miaka. Kwa hiyo ni vema pesa zikatengwa za kutosha kwa ajili ya Tume hii ya Taifa ya Mipango na Matumizi bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukifanya hivyo itaondoa migogoro na migogoro nadhani ndiyo *easiest* kuliko kutafuta pesa za barabara. Hilo ni rahisi kuliko yote, tuliambiwa hapa kwamba Kijiji sijui milioni 15, kama ndiyo Tume inasema hivyo, sasa tutashindwaje kutafuta bilioni 300 kweli ili tumalizane na migogoro ili haya mengine yote tunayoyapanga iwezekane, hilo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulibadilisha sheria hapa ya kuondoa mamlaka kwa Mabaraza yale ya Kata, sasa tunataka ije kwenye Mabaraza ya Wilaya na nadhani *thinking* ni kwa sababu sheria hawa wanafahamu zaidi. Tunatarajia Wizara ya Ardhi sasa muanze kuajiri hawa ili sasa migogoro isirundikane bure. Kwa mfano, Kiteto Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi nakumbuka na nawapongeza sana kwa kuja Kiteto na timu yenu mnahangaika sana, mnakwenda kila mahala na Waziri wako, ndio maana Waziri wako karibu nywele kichwa chote kinakuwa nyeupe na wewe kila siku mnapishana, lakini Jimbo la Kiteto ambalo kila siku nazungumza hapa migogoro ni mingi mikubwa kuliko Mkoa halafu bado mnatuletea Mwenyekiti anayetembelea sijui anatoka wapi? Mheshimiwa Waziri mtuletee Mwenyekiti wa

Balaza la Ardhi Kiteto awe pale *full time* ili migogoro ishughulikiwe na kwingine kote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo jingine Wizara ya Ardhi kuna *clip* ya Mheshimiwa Rais Mstaafu ilikuwa inatembea hapa siku za hivi karibuni kusema hii Wizara yenu bwana kuna watu wagumu kwelikweli, sasa sijui ni changamoto na hiyo imegeuka kuwa nayo ni changamoto ama ni *confusion* iliyopo kwamba wale Maafisa Ardhi waliopo Wilayani hawajulikani kama wako Halmashauri ama wako kwenu ni kama wana-*hang* tu hivi, ni vyema mkaweka hili sawa ili na wale waanze kufanya kazi huko Wilayani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nirudi Maliasili na Utalii, kwanza nimpongeze Waziri na Naibu Waziri kwa kuja na huu mpango wa kukutana na Wabunge Mikoa, nadhani itawajengea fursa ya kufahamu changamoto nyingi kutoka kwa watu wanowakilisha wananchi hapa ambao ndiyo wanatupa kura hapa. Sasa mkichanganya na ripoti zile za wataalam wenu na nyinyi mkapata na picha huku nadhani mtatengeneza majawabu ambayo ni mazuri kwa watu na uhifadhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nitajikita kwenye *WMA* zaidi na *WMA* nchini kuna *WMA* karibu 38 hivi, lakini 22 ndio ziko *active* kidogo na Kiteto tuna *WMA*, Mahakama ya *WMA* lakini kuna Waheshimiwa Wabunge wengi sana hapa wana *WMA*, Mwenyekiti wa Bunge Mheshimiwa Baran Sillo ana *WMA* ya Bunge Mheshimiwa Mpakate ana *WMA*, Mheshimiwa Kuchauka, kuna Wabunge zaidi kama 30 hivi, Dkt. Steven Kiruswa kule Longido.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *WMAs* zilianzishwa na Sera ya Wanyamapori ya mwaka 1998 na nia ilikuwa ni kwamba pamoja na kwamba tuna maeneo ya hifadhi *(core protected areas);* maeneo mengine ya kufanya uhifadhi bila kubugudhana na watu ni kushawishi watu washiriki kwenye suala la uhifadhi. Kwa hiyo, wananchi wanatenga ardhi zao, halafu wanapewa mamlaka ya kuingia mikataba na wawekezaji. Kwa hiyo, nimependa sana Kamati walivyoweka hapa kwamba *WMA* siyo Hifadhi za Taifa wala siyo *extension* ya *National Parks*, siyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama walivyosema Kamati, *WMA* siyo Hifadhi ya Taifa wala siyo mwendelezo wa Hifadhi za Taifa, hizi ni ardhi za vijiji, ambacho wanachofanya ni wanafanya mnachofanya ninyi, kuhifadhi. Sasa nadhani ingekuwa ni jambo jema kama Hifadhi za Taifa za hizi za kijamii zikafanya kazi pamoja na mkashindana kibiashara bila kusumbuana, kwa sababu lengo ni lile lile. *Data* hapa zinatuambia pamoja na mbuga zote ishirini na ngapi sijui, asilimia 65 mpaka 70 ya wanyamapori wako nje ya hizi tunazoziita *core protected areas* na *logic* ni *simple* tu, mnyama wala hajui kwamba eti ndio na *cross* Serengeti sasa kwa hiyo anaanza ku-*vibrate* kwamba navuka mpaka wa Serengeti, *no these are free agents,* wanakwenda kila mahali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo *unless* tu-*improve* mahusiano zaidi na watu ndio itafanya uhifadhi uwe *complete*. Itakuwa ni kujidanganya sana kama mnafikiri mtafanya uhifadhi bila ku-*involve* watu, hiyo haitowezekana. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri *task* kubwa ni kuangalia mahusiano, mahusiano ya wananchi na hifadhi na wanyamapori. Siku mkitengeneza *balance* nzuri sana uhifadhi utakuwa umekamilika vizuri sana na utakuwa na manufaa makubwa zaidi kwa nchi na kwa wananchi wenyewe. Tutaongea mengi zaidi tukikutana kwenye Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kilichonifurahisha sana leo ni Maazimio ya Bunge kuhusu pesa za *WMA*; *WMA* wamepewa Madaraka, wanasaini mikataba na wawekezaji, mwekezaji kalipa hela halafu hela haziji. Hawa wanashindwa kulipa mishahara, wanashindwa kufanya kazi za uhifadhi, wanashindwa ku-*control* majangili kwa sababu pesa zimekwama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hii kwa kweli Kamati kwa kweli shikamoo Kamati, kama ndio Mwenyekiti ndio anapokea kwa niaba yenu. Mmefanya jambo ambalo limetusumbua kwa muda mrefu kidogo. Azimio lenyewe; Serikali ihakikishe inarejesha kiasi chote cha fedha kinachostahili kwenda *WMA* na naambiwa na watu wa *WMA* wanadai kama *four point something billion* sasa. Kwa hiyo, mlete hiyo haraka kama lilivyosema azimio hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine zuri sana mtengeneze mpango wa kuhakikisha kwa sababu tumeshakubaliana kikanuni, kila mtu anapata nini hapa, *WMA percent* ngapi, Serikali, wilaya na wawekezaji na wao wako tayari, kwani akiandika *cheque* tatu kila mtu akapata kwa wakati kuna shida gani? Kwa hiyo, kama azimio hili lilivyoweka vizuri tunataka hela za *WMA* ziende *directly,* hizi za kwenu zinazokwenda Hazina kwanza ziende huku, hiyo vita ni yenu wenyewe kwa wenyewe lakini hizi za wananchi angalau ziende *straight* ili mambo ya uhifadhi na pia isilete migogoro kati ya *WMAs* na wawekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu leo *you can imagine an investor* ana-*sign* mkataba na *WMA* hela haziji, halafu anaye-*hold* hela siyo sehemu ya mkataba, anaye-*hold* hela ana-*frustrate* ile *agreement* kwa sababu ya ku-*hold* hela. Kwa hiyo, sheria kama ilivyokuwa inasema hizi hela ziende, kwa kweli hapa Kamati mmetufanya sisi ambao tunatoka maeneo haya, tumefurahi sana na *WMA* nchi nzima leo nadhani zinafuatilia sana hili na wamefarijika sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la mwisho, narudi kwenye mahusiano, mimi nawaambia wananchi wangu wa Kiteto, hizi fidia hizi tunazozungumza hapa, kanuni hizi ambazo mmesema kifuta jasho, sijui ni kifuta nini, halafu haziji na zinachelewa. Mimi Kiteto pekee yake wananchi wameleta *forms* zaidi ya 223 lakini kesi za mifugo 21, majeruhi wanne, vifo vinavyotokana na wanyamapori.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *is very unfair*, leo tembo anavuruga shamba lote na wananchi wale hawalali kila siku wako mashambani. Halafu tembo au wanyamapori anakuja anavuruga, halafu mnaniambia shilingi 500,000 na shamba lote eka mia, mia mbili lote limevurugwa.

Kwa hiyo, kati ya vitu ambavyo kwa kweli ningetamani hii kanuni mmelete haraka sana ili turekebishe ili wananchi hawa wasivunjike moyo ambao hawalali usiku na mchana wakijaribu kulima ili wanufaishe nchi na Taifa kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nafurahi na nashukuru sana, ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Edward Olelekaita.

Nilimtaja Mheshimiwa Aida Khenani, Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta na Mheshimiwa *Engineer* Ezra ajiandae.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi na mimi nianzie alipoishia Mjumbe aliyepita kwa kuwapongeza sana Kamati kwa kazi kubwa ambayo mmeifanya, lakini naunga mkono maazimio yote yalioletwa na Kamati kwa maslahi mapana ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza na kwenye eneo la kifuta jasho au kifuta machozi. Kwanza nianze kwa kutoa pole tarehe 27 Januari, 2024 jimboni kwangu mwananchi aitwaye Shija Machenga, mwananchi wa Kijiji cha Itete, Kata ya Itete akiwa anaenda kukamua maziwa alipata changamoto ya kukutana na tembo akakanyaga mguu wake ukawa kama chapati. Ni kwa neema ya Mungu tu kwamba hakufa, lakini mpaka sasa anaendelea na matibabu Hospitali ya Rufaa Mbeya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeanza kwa kutoa pole, mwaka jana tulizungumza kwenye Bunge hili hapa kipindi cha bajeti na kwenye maazimio ya Kamati wameleta tena hilo jambo. Waziri mwaka jana alikuwa Mheshimiwa Mchengerwa ambaye Waziri wa sasa alikuwa TAMISEMI, ukiona changamoto zilizopo tunaamini kutoka kwake hapa migogoro iliyopo huko kwenye vijiji wakisharikiana na Waziri wa Maliasili kuna sehemu tunaamini wanakwenda kufanya utatuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo eneo la kifuta machozi nilizungumza karibia dakika 10 mwaka jana na nitarudia hapa. Kanuni za mwaka 2011 ni kanuni ambazo zinaleta doa kwenye Taifa letu, zinaleta sifa mbaya kwenye Taifa letu, kwa mfano, kwa binadamu pekee yake kwenye hilo eneo la kifuta machozi, mwananchi akipata majereha kutokana na wanyama wakali na waharibifu, akijeruhiwa anatakiwa kulipwa kifuta machozi shilingi 200,000; mkono au mguu ukikatika kabisa analipwa shilingi 500,000

na huyo mtu hawezi kufanya kazi tena; akifa yaani hayupo jamii yake imemkosa kifuta machozi ni shilingi milioni moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa letu leo tunaangalia thamani ya mwanadamu ni sawa na shilingi milioni moja, halikubaliki. Tumeshafanya mabadiliko ya vitu vingi sana, kuna shida gani kwenye kanuni hizi? Kuna shida gani? Ukitoka kwa binadamu, njoo kwenye mazao ambayo leo ndio changamoto kubwa. Hawa wanyama wakali na waharibifu, huyu mwananchi ambaye amelima mita 500 kutoka eneo la hifadhi, eka moja…

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa

**MHE. AIDA J. KHENANI:** … hawa wanyama wakila…

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** …analipwa shilingi 25,000 kwa eka moja.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**TAARIFA**

**MWENYEKITI:** Taarifa inatoka wapi? Mheshimiwa.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe taarifa mzungumzaji kwamba akipoteza maisha imepangwa alipwe shilingi milioni moja pamoja na hiyo milioni moja kuna watu ambao wamepoteza maisha leo zaidi ya miaka mitatu hawajalipwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Aida unaipokea hiyo taarifa?

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea taarifa kutoka kwa baba yangu na ninaamini hiki ninachozungumza hatutegemei kuja kwenye Bunge la Bajeti tena mwaka huu kukiwa hakujafanyiwa mabadiliko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ekari moja ambayo leo tunajua mfuko mmoja wa mbole ni shilingi 75,000; shilingi 70,000 mpaka shilingi 69,000 inategemea ni aina gani ya mbolea. Huyu ekari moja ambaye angevuna gunia zaidi ya 25 ambayo maandalizi yake mpaka anakuja kuvuna inakaribia shilingi 750,000 halafu Serikali inasema itamlipa shilingi 25,000. Serikali ituambie ni wapi wataenda kununua gunia 25 kwa shilingi 25,000? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kanuni zenyewe zinawapa umaskini Watanzania, ukitoka kuanzia mita 501 mpaka kilometa moja kama eneo lake liko mbali kutoka eneo la hifadhi, mita 500 mpaka kilometa moja anatakiwa alipe shilingi 50,000 kwa ekari. Hizi kanuni walitunga Watanzania? Tuliwatungia Watanzania? Kweli lengo letu ni kuwasaidia Watanzania? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutoka kilometa moja eneo la hifadhi mpaka kilometa nne, huyu mwananchi endapo kama hao wanyama wameenda kula mazao yake analipwa shilingi 75,000. Wote tunajua unapozungumzia kilometa nne ni umbali gani kutoka eneo la hifadhi, lakini kilometa nne mpaka tano ikitokea kwamba eneo lake lina umbali kutoka eneo la hifadhi atalipwa kwa ekari moja shilingi 75,000; akitoka shilingi 75,000 kama amekidhi vigezo wanaweza wakampa shilingi 100,000. Halafu ikaenda mbali zaidi, hii kanuni inasema eneo lake lisizidi ekari tano. Kwa hiyo, tunataka Watanzania uwezo wao wa kulima isizidi ekari tano ndio maana yake, haiwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi kanuni tumezungumza mwaka jana ziko ndani ya Wizara, Waziri mwenyewe ana mamlaka nayo, kwa nini toka mwaka jana mpaka leo tunazungumzia kanuni hizo hizo zinazowakandamiza Watanzania, zinaleta sura mbaya kwenye Taifa letu, bado tunarudia kuzungumza. Haifurahishi na haipendezi, yaani leo tunataka tuseme hizi kanuni walitunga wakoloni? Hizi kanuni yawezekana zilikuwa zinafaa kipindi hicho kwa sasa zimepitwa na wakati. Mambo yanaendelea kwenye Taifa letu, haya mambo hayafai na hayana sababu ya kuendelea kuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kanuni hizi zikiendelea kuwa hivi ina maana tunawaambia watu, tunaiambia dunia kwamba Taifa letu

linathamini wanyama kuliko binadamu. Huyu mwanadamu huyu, huyu Mtanzania anapopambana na huyo myama mkali tunayemwita, akimuua tu shilingi milioni 30 inategemeana alikuwa anajihami alikuwa anafanya nini? Kwa nini thamani ya mnyama iwe kubwa kuliko ya binadamu? Haiwezekani, ni aibu kuendelea kujadili kanuni kama hizi ndani ya hili Bunge. Tumejadili mwaka jana vizuri kabisa, tukamwambia Waziri kaanze na hili eneo halileti sifa nzuri kwenye Taifa letu. Toka mwaka jana mpaka leo tunazungumzia kanuni ingekuwa ni sheria ingekuwaje? Na hizi kanuni zipo ndani ya mamlaka ya Waziri mwenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu naamini na sitaki kuamini kwamba Taifa letu tunaamini wanyama kuliko binadamu, tunategemea Serikali itaenda kulichukua hili jambo kwa umuhimu mkubwa. Najua hata watu hawa wa *TAWA* kuna wakati wanasema sisi hatuwezi kuvuna hawa tembo, wanakuja wanawasukuma tu wanawaswaga wanawapeleka wanawarudisha hifadhini. Leo tembo anaenda mpaka kwenye makazi ya watu, ndani, halafu huyu mtu akiuawa nyumbani kwake, Serikali yetu ya Tanzania tunasema tutamlipa milioni moja, kweli? Halifurahishi, linatia huzuni, linatia aibu kwa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nishauri; la kwanza ni lazima mabadiliko ya hizi kanuni yapitiwe haraka ili kuendelea kulinda sifa ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili kwa sababu tulikuwa na mpango mwaka jana wa kufuta kifuta jasho, kwamba fedha ambazo zinatumika ni zaidi ya zile ambazo tunapitisha kama Bunge kwa kuwa matukio ni mengi, na mimi natamani, Serikali itakapokuja angalau kipindi cha bajeti watuambie ni matukio mangapi yameripotiwa kwao na mangapi yamefanyiwa kazi, kwa sababu pamoja na kwamba hiyo fedha ni kidogo ya kifuta machozi, kwanza inachelewa na wakati mwingine hawa watu wanaikosa hiyo haki ambayo siyo haki kwa namna nyingine, hili jambo si zuri. Kwa hiyo, Serikali ije itueleze ni kesi ngapi zimeripotiwa na kesi ngapi zimefanyiwa kazi kwa Watanzania hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine niliwatolea mfano nchi ya Kenya jirani tu hapo waliweka *fence* na Serikali inaweza kufanya hivyo, Serikali inasema wafugaji inabidi waanze kufuga kisasa, Serikali lazima tuwe mfano na sisi tuanze kuhifadhi kisasa. Eneo dogo lakini uhifadhi ambao una manufaa kwa Taifa letu. Lazima tuwe mfano sisi kama Serikali, hili jambo halikubaliki hata kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine wakati tunafikiri kufuta hicho kifuta machozi ni lazima Serikali iongeze vituo vya askari wa wanyamapori kwenye maeneo yote ambayo yana changamoto na ikipeleka hao askari wawape na magari. Wakati mwingine wale askari ni wachache tembo wamevamia kituo *A* mpaka waende kule *TARI* imeshatokea madhara. Kwa hiyo lazima tuwawezeshe tukienda na hili jambo kwa vitendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni hii migogoro inayoendelea, migogoro kati ya hifadhi na maeneo ya wananchi. Huwezi kutumia mfumo uliotengeneza tatizo kumaliza tatizo, nasema hivyo kwa nini? Leo ukiangalia maeneo mengi yenye migogoro yale maeneo wanakuja baadaye kuna makazi ya watu wanasema wamejenga katikati ya hifadhi, wamejenga ndani ya hifadhi. Hilo eneo linakuwa na Mwenyekiti wa Serikali, zimepelekwa taasisi za Serikali, anayehusika na uchaguzi ni Waziri wa TAMISEMI, ni Serikali hiyo hiyo. Wanachagua Mwenyekiti wa Serikali, wanaamua kupeleka shule anayehusika ni Waziri wa TAMISEMI; anakuja Waziri wa Maliasili na Utalii anasema hili eneo ni eneo la hifadhi. Sasa mtueleze hivi kweli hilo eneo linahitaji Malaika Gabriel kuja kutatua tatizo hilo? Lazima tunapoanzisha jambo tushirikiane na taasisi nyingine, hapa unataka kwenda kusajili kijiji lazima tujue ni eneo sahihi? tunakwenda kuanzisha shule mpaka ina sajiliwa ni eneo sahihi? Na wakati mwingine unakuta ina hati, hati miliki hiyo shule halafu unakuja kuwaambiwa wananchi kwamba hilo eneo ni eneo la hifadhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua kwamba kuna taasisi za Serikali ziko kwenye maeneo ambayo tunaita sijui maeneo ya wanyamapori, hamjawahi kubomoa lakini wananchi tunawaondoa, tuache hizo tabia. Tuanze kuonesha mfano kama Serikali, kama tumejenga Taasisi za Serikali ziko kwenye maeneo

ambayo ni mapito ya wanyamapori tuanze sisi kama mfano. Tunapowaambia wananchi tuwe tumeonesha mfano sisi moja kwa moja, kinachoendelea leo ni uonevu na haukubaliki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hiyo ni vizuri leo maeneo yanayoanzishwa, shule zinazoanza kujengwa zipimwe kwanza kwa mawasiliano ya hizi taasisi zote kujua hili eneo ni sahihi au siyo sahihi; kwa sababu pale mpaka miundombinu ya Serikali inapelekwa pale inakuaje mnakuja kuambiwa baadaye kwamba hili ni eneo ambalo liko ndani ya hifadhi. *(Makofi)*

Mimi naamini haya mambo yanaanzishwa kuanzia nyumba ya kwanza, ya pili mpaka inajenga shule, anapatikana Mwenyekiti, Serikali haiko likizo Serikali ipo. Tusisubiri matatizo kama hayo, halafu unataka umezalisha matatizo ukienda kwenye huo mgogoro tukupigie makofi, ulianzisha mwenyewe umekwenda mwenyewe, unataka tukushangilie kwa nini? Wakati wewe ndio chanzo cha mgogoro, haiwezekani tusipoteze muda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na hizi tume/tume zinazoundwa hizi zinatumia fedha za Serikali. Ukiangalia mimi nimekaa hapa sijawahi kuona majibu ya hizo tume yanapokwenda. Ni matumizi mabaya ya fedha za Serikali, haiwezekani mtu ambaye amesababisha tatizo akalimalize tatizo hilo na tunataka tuone tunapoona mabadiliko ya Mawaziri tunategemea kuna kitu Rais amekiona muende mkafanye mabadiliko, mumshauri Rais mambo ya msingi, haiwezekani turudie mambo hayo kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mambo tunapozungumza tunategemea tuone mabadiliko na mabadiliko hayo yanawezekana tu kama tunaelewana. Leo tunajua idadi ya vijiji, kama tunajua idadi ya vijiji tuna tume ambayo inatakiwa ihusike, hiyo tume ipo shida ni nini ni dhamira ya dhati. Tumekubaliana hapa kama Bunge fedha ziende, hiyo tume ikafanye kazi ya upimaji, shida iko wapi? Shida ni nini? Ni kwamba hatuna kipaumbele? Ni kwamba hatuoni umuhimu wa mambo haya? Ni kwamba hatuoni umuhimu wa watu wetu wanavyopoteza maisha? Haya mambo hayakubaliki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi na nuanga mkono hoja ya Kamati. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Aida Khenani, nilimtaja Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, Mheshimiwa *Engineer* Ezra Chiwelesa ajiandae.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hoja iliyoko mezani. Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu amenipa uhai wa kufika siku leo, lakini pia nawashukuru wapiga kura wangu wa Urambo ambao wamenipa ushirikiano kila wakati na hali kadhalika naishukuru pia familia yangu, naishukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kuipongeza Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii kwa kazi nzuri waliowasilisha kwa kazi nzuri waliowasilisha leo asubuhi mezani, hongera sana Kamati, Mwenyekiti hongera sana na Wajumbe wote hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali yetu inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kweli kwa kazi kubwa inayofanya kuleta maendeleo ikiwemo pia kutanganza nchi yetu sasa hivi tunapata watalii wengi, hongera Mheshimiwa Rais wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya Kamati ilikuwa nzuri na nimefuatilia maazimio yao, nayaunga mkono hongereni sana na Kamati hii nimshukuru sana Mwenyekiti kwa sababu nimeshaenda kuonana nao zaidi ya mara mbili kwa suala hili ambalo nalizungumzia sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Urambo sasa na sisi pia tuna hifadhi ya msitu ambayo inaitwa Hifadhi ya Taifa ya Mto Ugalla na niishukuru Serikali kwa sababu walipitisha maazimio hapa ya hifadhi za aina mbalimbali ikiwemo mojawapo ya kwetu ya Urambo inayoitwa Hifadhi ya Taifa ya Mto Ugalla Kaskazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna ambaye asingeshukuru kupata hifadhi kwa sababu tunajua yako manufaa

yanayotokana na hifadhi kama vile *TANAPA* sasa hivi wanatusaidia ukiomba madawati unapata tunashukuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na shukrani yetu Wananchi wa Urambo walikuwa wananiuliza, mbona ilitokea ghafla sana? Kwa sababu wao walitegemea pamoja na kufurahia hiyo *TANAPA* lakini walikuwa wanategemea kwamba watashirikishwa kwenye maamuzi hayo ili wajue sasa ufanyaji kazi utakuwaje, ushirikiano, kulinda msitu wenyewe itakuwaje? Kwa sababu Urambo sisi katika zao mojawapo ambalo tunalithamini sana ni asali na hata marafiki zangu mliomo humu mkitaka kunituma asali ninawaletea tu kutoka Urambo. Ni nzuri sana na watu wanaitaka pamoja na Wamarekani walikuja kuifuata Urambo asali yetu tunayoizalisha pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, walipoanzisha tu Hifadhi ya Taifa ya Mto Ugalla; la kwanza ni kuzuia marufuku kuingia, marufuku hata kufuata ile mizinga ambayo waliiweka tangu zamani na sisi miaka yote huwa tunauza asali kwa kuweka mizinga kwenye msitu huo. Sasa ghafla ikaonekana kwamba hawawezi kuingia, kama kuna pigo mojawapo ambalo tulilipata; hilo ni mojawapo ni kubwa ambalo limetuathiri sana sisi kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua tunatumbaku lakini huwezi kutegemea zao moja tu, tunategemea na mazao mengine mojawapo likiwa ni zao la asali. Nilikwenda kuiona Kamati nikazungumzia suala hili; la kwanza kwamba mlipokwenda kugeuza kuwa Hifadhi ya Taifa mliongea na wananchi husika? Mliwaelimisha? Mliwaambia wajibu wao ni nini? Mabadiliko yao katika kutumia msituo huo itakuwaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakukuwa na ushirikiano wa aina yoyote wala elimu yoyote. Sasa kata nne zinazozunguka hapo mojawapo ikiwa Kata ya Ugalla, Kata ya Ukondamoyo, Kata ya Nsenda na Kata ya Kasisi wanalia, vijiji kumi hawaruhusiwi kuingia mle kufuga (kuweka mizinga yao) wala kuchukua hata asali ambayo walishaweka mizinga miaka mingi na ng'ombe hawawezi kuwalisha pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukumbuke kwamba jinsi miaka inavyokwenda watu wanazidi kuongezeka na cha ajabu kimojawapo walipokuwa wanaweka ile mipaka sasa wakachukua mpaka na maeneo ya vijiji. Tukumbukue kwamba hivi vijiji vilipimwa na wao wanajua hata kama ni kesho twende na Waziri muhusika, wao wala hawahitaji jembe wanafukua na vidole tu wanakwambia mawe yetu haya hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kwanza mipaka mipya iliingilia mipaka ya zamani lakini pia ikawa kama nilivyosema hawaruhusiwi kuingia kabisa. Hili ni pigo kubwa kwetu sisi na hili suala silizungumzii hapa kwa mara ya kwanza, nililizungumzia tarehe 3 Juni, 2023 nilizungumzia humu Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hivyo tu, walipounda ile Kamati ya Mawaziri nane nilipeleka barua rasmi na Serikali hii pia nilitegemea kwamba baada ya kuwatuma Naibu Mawaziri; Mheshimiwa Ramo Makani alikuwa Naibu Waziri Maliasili alikuja lakini pia Mheshimiwa Josephat Hasunga alikuwa Naibu Waziri alikuja lakini pia Mheshimiwa Dkt. Kigwangala ambaye alikuwa Waziri alikuja lakini bahati mbaya mvua ilinyesha sana akashindwa na Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula aliyekuwa Waziri wa Ardhi pia naye alihusika lakini hatujapata jibu lolote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina imani na Serikali yetu kwamba itazingatia maoni ya Kamati lakini pia na ya Wabunge kama hivi ninavyosema sasa hivi. Tuliomba sisi na ninarudia tena kuomba kwa heshima na taadhima Serikali ninayoiamini turudishiwe angalau siyo chini ya eka sita kuzunguka zile kata ili wapate mahali pa kuendelea kuweka mizinga, waendelee kufuga nyuki lakini pia waendelee na kupeleka mifugo yao kuchunga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba tena kurudia ombi kwa niaba ya Wananchi wa Urambo kata hizo nne kwamba turudishiwe eneo. Sasa ninachoshangaa mimi nitashukuru kama kuna mtu atanipinga hapa; wengine wameomba wamerudishiwa, mimi nimeomba wee sijui mwaka wa ngapi huu. Wanarudishiwa siyo hiyo tu, na sisi tunashukuru kuwa na *TANAPA*

lakini turudishiwe kama nilivyosema siyo chini ya kilometa sita wananchi wetu waendelee kufuga nyuki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais alipokuja Tabora nakumbuka tarehe 30 Machi, 2022 nililizungumzia hili suala na wenzangu wakaniunga mkono kwamba bado tunahitaji kuweka mizinga kule na kuvuna asali; Mheshimiwa tusaidie. Jambo la ajabu ni kwamba Mheshimiwa Waziri nadhani atakuwepo hapa na aliyekuwa Waziri muda uliopita. Wananchi wa Urambo hawa wafugaji wa nyuki wameunda umoja wao kuna eneo tayari wameshaandaa la kuchenjua asali. Mimi kwa niaba yao na wao wenyewe pia waliandika barua; mimi niliandika barua na wao wakaandika barua tukapeleka Maliasili na Utalii kwenye Wizara. Wakakubali wakamtuma na Naibu Mkurugenzi wa nyuki akaja Urambo akaona lile jengo la wafugaji nyuki akalipenda akaahidi kwamba mimi hapa nitaleta maji na nitaleta umeme na nitaleta mashine; tukashangilia, tukapiga vigelegele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, najisikia vibaya kwamba Serikali yetu tunayoithamini na kuiamini iliahidi itatoa mashine ya kuchenjua asali na waliahidi kwamba watatuchimbia kisima na kutuvutia umeme. Sasa hivi imekuwa kimya. Sasa nabaki unauliza; hivi ni mabadiliko ya Mawaziri au ni kitu gani hiki lakini Serikali ni moja? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kwa heshima na taadhima, Serikali inisikilize tupewe ile mashine tuliyoahidiwa tuchimbiwe kisima cha maji kama walivyoahidi na kutuvutia umeme kama walivyoahidi tuendelee kuheshimu Serikali yetu, Serikali ya Mama Dkt. Samia inaheshima yake. Halafu haya mawili ndiyo ninayasisitizia; kwanza turudishiwe eneo, tunakubali kabisa kuwa na hifadhi lakini turudishiwe eneo ili wanaofuga nyuki ambao wameunda umoja wao waendelee na kufuga nyuki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kwa sababu ya ongezeko la watu waweze kufuga mifugo yao watugawie sehemu hiyo, tunathamini azimio, tunathamini *TANAPA* lakini na sisi tunaomba maombi yetu hayo mawili; kurudishiwa eneo na kuletewa vile vifaa walivyokubali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo napongeza tena Kamati husika imefanya kazi nzuri; ahsanteni sana kwa kunisikiliza na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Margaret Sitta; nilimtaja Mheshimiwa *Engineer* Ezra Chiwelesa, Mheshimiwa Mwita Getere ajiandae.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kukushukuru lakini kipekee niipongeze Kamati kwa taarifa hii nzuri ambayo wameitoa kwa niaba yetu na yale mambo ambayo wameyabainisha. Tuisihi tu Serikali iweze kuyafanyia kazi hususani suala la kushindwa kutekeleza mchakato wa kuifanya *TFS* kuwa mamlaka na kuitoa kwenye uwakala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia suala la zile sera ambazo zimepitwa na wakati *even though* kwenye taarifa inaonekana upande wa Serikali au upande wa wasimamizi wao wanasema hazijapitwa na wakati lakini Bunge ambalo ndiyo wawakilishi wa wananchi wanasema zimepitwa na wakati. Sasa saa nyingine najiuliza hawa watu wanamuwakilisha nani? Maana sisi ndiyo wawakilishi wa wananchi; tunaposema kwamba hili jambo linashida na limepitwa na wakati ni vizuri wakasikiliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nimeanza na hii? Nataka tu leo niende kwa *style* ya tofauti kidogo ninataka ku-*refer* maandiko matakatifu katika Biblia. Ukisoma Mwanzo1: 25 inasema hivi; "Basi Mungu akafanya aina zote za wanyama wa porini, wanyama wa kufugwa na viumbe vyote vitambaavyo, Mungu akaona ni vyema." Mstari wa 26 unasema, "Kisha Mungu akasema; tumfanye Mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu akatawale samaki wa baharini, ndege wa angani, wanyama wa kufugwa, dunia yote na viumbe vyote vitambaavyo." Mwisho wa kunukuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nimekuwa najiuliza hata maandiko tu yalimpa *power* mwanadamu dhidi ya hawa wanyama lakini huko tulipo labda kwa sababu Wabunge ni

wawakilishi wa wananchi na wananchi wako tofauti na wote tunakutana humu kwenye Bunge kwa sababu tunawakilisha watu tofauti. Ukienda Ilala pale kwa Mheshimiwa Naibu Spika huwezi kusikia Naibu Spika anaomba josho humu ndani hata siku moja. Maana yeye anawakilisha watu tu ila mimi ninayetoka Biharamulo ninawakilisha wanyamapori maana ninahifadhi, ninawakilisha mifugo maana ninawafugaji na ninawakilisha wananchi sawa na nyie wengine ambao mnatoka kwenye majiji au maeneo mengine makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tulikuwa tunaomba pale tunapoleta mawazo na maoni yetu kama wawakilishi wa makundi haya matatu au makundi zaidi ya nyie ambao mnawakilisha kundi moja moja tupewe nafasi ya kusikilizwa kwa sababu hata maandiko yameelekeza hivyo. Kwa sababu inaumiza sana mimi kwangu sasa hivi wananchi wamekuwa wananyanyaswa. Mtu anakutwa na kuni tu, hivi kweli hata gesi ndiyo tumeanza kugawiwa juzi Wabunge; gesi si ndiyo tunagawana sasa hivi na tunazipeleka kule? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbolea ya ruzuku tumepiga kelele hapa kwamba mbolea zinaishia wilayani hata kule vijijini hazifiki. Gesi tulipewa mitungi hapa sisi wa vijijini nilivyosema tunawakilisha makundi huenda wale tuliowapa baada ya ile gesi kwisha, hawajaenda ku-*refill* tena maana hata sehemu ya ku-*refill* hawana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa unakuta mwananchi ana kuni tu ya kawaida unamnyang'anya baiskeli mwanamke, unamnyang'anya zile kuni; hivi kweli mnataka wapikie nini? Labda nyie mliozaliwa mjini mnajua *alternative*. Sasa sisi Wabunge wa vijijini tungeomba Serikali mtupe *alternative,* kwa mwananchi ambaye yuko kijijini ambaye leo hata kituo cha afya au zahanati hana anatembea kilometa tisa, kilometa 10 kutafuta ile lakini anakutwa na kuni ananyang'anywa zile kuni, mnataka hawa watu waende wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inaumiza *and if we are here truly representing people* tulione hili. Tumepeleka watu wamesoma wamekuja na sera zao lakini hizi sera mnazoenda huko shuleni

mkasoma hebu basi zi-*reflect* maisha ya watu tunaowawakilisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawafugaji kwangu wananyanyasika kila siku tunaongelea habari za wafugaji. Biharamulo leo ndiyo Jimbo namba 20 kwa wingi wa watu katika Taifa hili, Jimbo namba moja kwa wingi wa watu kwa Mkoa wa Kagera. Nimezungukwa na Hifadhi ya Burigi hiyo sina shida nayo lakini tuna maeneo mengi ya *TFS* yako pale yale mapori yamehifadhiwa. Watu wangu ng'ombe wanakamtwa kila siku wengine wanalalamika kwamba ng'ombe wanaswagwa wanaingiza mle wanatozwa. Hatukatai hapa Waziri atatetea kwa sababu analetewa ripoti, aliye wilayani atatetea kwa sababu analetewa ripoti lakini je, *are we sure* kwamba wale watu walioko huko chini wanatenda haki kwa hawa watu? Kwa nini wananchi wanalalamika kila wakati? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa watu wametutuma humu sisi kama sauti yao. Sasa sauti yetu sisi kama Wabunge tunapoongea leo *three years* niko humu ndani tunaongelea jambo hilo hilo la wananchi kunyanyaswa? Tunaongelea jambo la kuomba maeneo yapanuliwe ili wananchi waweze kupata maeneo ya kuchungia zaidi na kufanya shughuli zao za uchumi lakini tusisikilizwe; sasa anatakiwa asikilizwe nani? Yule mtu aliyeenda kusimamia pale au sisi tunaowawakilisha wale wananchi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tuombe Serikali chonde chonde tunaiomba Serikali kwenye hili itusikilize. Ilani ya CCM iliahidi watatenga maeneo kwa ajili ya wafugaji na kilimo, maeneo hawatayatenga kutoka kwangu mimi kwa sababu mimi sina eneo la kutengwa; yatatengwa kutoka kwenye maeneo ya Serikali yaliyohifadhiwa. Idadi ya watu inaongezeka, kama watu wanaendelea kuzaliana tunawaambia waongeze uzazi halafu maeneo ya kufanya shughuli zao za uchumi hatuwapi, hawa watu ni wa nini kuongezeka? Ni bora tukaanza sasa kufunga *speed governor* idadi ya watu isiongezeke kwa sababu hatuna maeneo ya kuwapa ijulikane, lakini watu wanaongezeka maeneo hayapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe Serikali ilichukue hili ili iweze kutusaidia hususani kwangu Biharamulo wananchi wangu wanateseka. Hili naomba wafugaji wa Biharamulo wanateseka, wananchi wa kawaida wanateseka. Mtu kama hana hata kuni akapikie nini? Kijijini tumezaliwa tunapikia kuni ndiyo nishati yetu ya kupikia. Siku gesi ikifika kule hata wao wataacha, hakuna mtu anayetaka kushinda kwenye moshi lakini *for the time being that's an alternative* tuwaache wananchi wafanye shughuli zao za uchumi. *(Makofi)*

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa kuna taarifa huku; upande gani? Ahaa, Mheshimiwa Pallangyo.

**TAARIFA**

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Naomba nimpe taarifa Mheshimiwa *Engineer* Chiwelesa kwamba siyo kule kwake tu hata kule Arumeru Mashariki Eneo la Momela wananchi wananyanyasika sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Engineer* Ezra unaipokea hiyo taarifa?

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa naipokea. Sasa nikiondoka hapo liko suala jingine ambalo limepigiwa sana kelele suala la wanyama hawa waliohifadhiwa (wanyamapori). Mimi kwangu Kata ya Nyakahura eneo moja linaitwa Nyabugombe kijiji kimeisha wananchi wote wamehama pale. Kwa sababu tembo wakihama usiku kila siku wanageuza kambi pale. Wanatoka porini wanaingia pale wanavuruga kila kitu siku wakiridhika wanaondoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa tunaambiwa hapa habari ya kupanda pilipili, hivi kweli mwananchi akaoteshe pili pili kwanza pili pili kwenye *buffer zone* anaiotesha wapi? Kwa sababu *buffer zone* ile ya mita 500 mwananchi akisogea tu pale amekamatwa

kaingia kwenye hifadhi. Sasa pili pili wananchi wazioteshe wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaomba kwa sababu wanyama hawa tumeona wanathamani sana na kweli wanatuingizia pesa za kigeni; kwa nini tusitengeneze *electric fence* tukazungusha yale maeneo ili wanyama wasitoke tuondoe na hii migogoro? Si wanaingiza hela? Tukatafute pesa tuwekeze ili tuweze kutengeneza pesa nyingine zaidi lakini tusitake kutengeneza pesa kwa *expense* ya wananchi kuendelea kuumia. Kwa sababu kuna mtu mwingine utamletea barabara lakini mazao yake yote yameharibika kwake haoni faida kwa sababu vitu vyote vimeharibika. Hawezi kusomesha watoto wake, hana chakula, hana nini kwake hata hiyo ukienda ukamwambia mambo gani ya maana ya kuhusu hifadhi hayaoni. Kwa hiyo, tunaomba Serikali itafute *alternative. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wameongea wenzangu habari ya magari lakini mimi ipo kesi nyingine. Unakuta kijiji A kiko hapa kimezungukwa siyo hifadhi hata kusema ni hifadhi ya *national park* kama hii, hifadhi tu ya *TFS*. Mwananchi anatakiwa aende kijiji cha pili ambapo labda ni kama kilometa moja au kilometa mbili lakini kwa sababu kuna hifadhi imemzunguka hamna hata njia haruhusiwi kupita. Matokeo yake mwananchi anasafiri kwa kutumia nauli *kilometers and kilometers* wakati pale; hivi mbona kwenye hifadhi leo watu wanaoenda Iringa, wanaoenda Mbeya mnapita kwenye Hifadhi ya Mikumi? Inakuwaje sisi mtu wa *TFS* mwananchi tu wa kawaida kupita mule na yenyewe wanaona ni kero? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimechunga ng'ombe nikiwa mdogo nyumbani tulikuwa tunafuga. Hivi ng'ombe anayeenda kula majani pale chini kwenye miti ile ukamuacha akala majani anaharibu hifadhi gani pale? Sawa hata mimi nimesoma ingawa sijasomea hayo madude lakini *sometimes we have to think.* Ng'ombe ameenda amekula majani pale karudi nyumbani hifadhi gani anaiharibu pale? Yaani kuna migogoro mingine tunaitengeneza tu kwa sababu tumeamini watu wengine zaidi *the so called* wataalamu bila kuweza kwenda na *logic. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuwaache wananchi wafanye shughuli zao maana mimi ukiniambia leo unatengeneza *ranch* ya Taifa sasa mbolea na maziwa hayo mnayohamasisha watu wanywe ng'ombe tukiwafugia sehemu moja hawa watu wa vijijini watakunywa maziwa lini au wenyewe hawana haki ya kunywa maziwa? Hiyo mbolea ya samadi wataipata lini ili waweze kulima? Kwa hiyo, kuna vitu vingine lazima tukubaliane, kama mtu anafuga ng'ombe wake wachache maeneo yale tangu zamani wametukuta tunafuga hebu wajaribu kuangalia jinsi ya kutengeneza mazingira mazuri na wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu aliongea hapa akasema twende kwenye *dialogue* tuelewane lakini tukimaliza kuelewana ndani ya Bunge, Wabunge tunaondoka tunasema Serikali imetamka kupitia viongozi wakubwa lakini yanayofanyika kule siyo yale yanayotamkwa hapa ndani ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tuombe Waziri yuko hapa ayachukue, hawa ni watu wake, sauti yetu ndiyo sauti ya wananchi. Yaani hamtaweza kutawala kama Serikali kama wananchi tunaowawakilisha hawasikilizwi mambo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo naunga mkono hoja ahsanteni sana kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa *Engineer* Ezra Chiwelesa. Nilimwita Mheshimiwa Mwita Getere baadaye Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Mheshimiwa Geophrey Pinda ajiandae.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nichangie Wizara hii ya Maliasili, Kamati ya Maliasili na Ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya tunayozungumza hapa wala hayahusu Mawaziri, yanahusu Serikali yetu ya CCM. Haya mambo ambayo tunayaangalia miaka nenda rudi, miaka nenda rudi wananchi wanafilisika. Wanafilisika kwa kunyang'anywa ng'ombe zao, wanafilisika kwa mazao yao kuliwa na tembo, wanafilisika

watoto wao hawasomi, wanafilisika hawana chakula miaka nenda rudi tunaongea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sidhani kama ni Mawaziri, mimi nadhani tatizo liko kwenye sisi Wabunge kabisa. Sisi Wabunge tunaotoka kwenye maeneo haya tuna matatizo. Kwa nini tunapitisha Bajeti ya Maliasili na Utalii na Ardhi wakati sisi wananchi wetu wanaenda kuumia? Sisi ndiyo wenye matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tukubaliane bajeti ijayo na bajeti zinazokuja kama Serikali haina mpango wa kuweka fensi kwenye maeneo yetu, haina mpango wa kuzuia wanyama kwa mkakati tuzungumze mambo haya. Kuna haja gani ya kuwa Mbunge wakati watu wanakufa kila siku? Kuna haja gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi mama mmoja ameuawa na tembo pale, watoto wake wanauawa pale. Kila siku ni kuua watu, kila siku ni nini? Maeneo yangu yote ya vijiji 15 watu hawana chakula, hawana hata sasa hivi hamna kitu. Jana wanyama wote walishindia pale, kuna haja gani? Leo mtu wa Maliasili akipigiwa simu kwamba ng'ombe wako hapa dakika moja amefika lakini akipigiwa simu tembo wako hapa haji kuona hao tembo. Kuna nini kinachoendelea? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani; sidhani kama kuna watu wanafanya vizrui. Pengine mimi nataka kuzungumzia mambo miwili; la kwanza pengne fedha zilizokuwa zinakwenda maana yake sasa hivi na huko nyuma kumekuwa tofauti. Baada ya *Corona* zile fedha za *TANAPA,* fedha za *TFS,* Ngorongoro na *TAWA* zilipoenda Serikalini hazirudi kwa wakati. Kwa hiyo, watu kila mkiwaambia hawana mafuta, hawana nini na kila kitu na hapa nimeona Kamati imesema vizuri, kweli kabisa tukubaliane kwamba fedha hizi zilizokuwa zinakusanywa kwenda Serikalini wawaachie wenyewe ili tuone udhibiti wao unaendaje kwenye mambo haya.

Mhehimiwa Mwenyekiti, lakini mimi siamini kama tunaweza tukazungumza miaka 300 watu wanakufa, watu wanafilisiwa tupo hapa Bungeni, siamini mambo kama hayo, siamini kama Serikali

hatuwezi kuamu jambo, siamini kama wanyama walioumbwa na Mungu akatupa sisi wanadamu akili tuwatunze leo wanatuzidi akili, haiwezekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nafikiria Wabunge tulioko humu ndani tukubaliane kwamba hatuwezi kuongoza watu wanakufa, wanafilisiwa, watoto hawana madawati na kila kitu hakipo kwenye maeneo yetu, na tupo Wabunge humu tukafanye hiyo kazi. Kwa hiyo nafikiri kwamba hiyo ndiyo *message* inatakiwa iende eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vinginevyo kuna suala la fidia; fidia ya Vijiji vya Nyatwali, Serengeti na Tamau jamani kuna mambo ya ajabu sana. Nilizungumza Bunge lililopita hapa, Ngorongoro watu wamehama wamepewa maeneo mazuri ya kuishi wamepewa na fidia wamepewa na umeme wamepewa na mashamba. *The same* leo wakati wa Nyantwali wale nao wanapisha wanyama. Ngorongoro wanapisha wanayama ni kweli tunataka wananya wapite kwenye maeneo mazuri, wanapisha wananyama. Nyatwali, Tamau na Serengeti ni vijiji ambavyo vina *registration* zake vinapisha wanayama unawapa shilingi milioni mbili. Unawahamisha unasema mwezi wa tatu utawalipa, mpaka leo hawajalipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawalimi na hawafanyi chochote. Haya mateso ni ya nini. Haya mateso watu wanakula kwenye nchi hii ni ya nini sasa? Kwa hiyo, nawaomba wanaohusika na mama anasikia haya maneno tunazungumza anasikia nendeni mkawalipe. Nimeongea na Waziri asubuhi hapa amesema wako tayari kulipa wakati wowote, basi nendeni mkalipe. Nendeni mkawalipe wale watu angalau wajue wanaenda wapi. Mpaka leo hawalimi na hawafanyi kazi yoyote. Kwa hiyo, nafikiri kwamba nalo hilo mlichukue muende mkalifanyie kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nimesikia Wabunge hapa wanasema kifuta machozi na kifuta jasho. Sasa wakasema kilomita tano kilomita ngapi. Kuna sheria za ajabu na zimetungwa 2004 sijui 2009. Maana yake ni kwamba ukienda zaidi ya kilomita tano ukikuta shamba la hekari 20 limelimwa huyu mtu analipwa

hekari tano tu. Hekari tano kwa kipimo cha kawaida analipwa shilingi laki tano; ndivyo sheria ndiyo inasema hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake kwa hekari moja ambayo anapata gunia 30 ukizidisha kwa shilingi laki moja kwa gunia anayoweza kupata shilingi laki tatu, anapata shilingi laki tano kwa heka tano. Heka 15 nyingine ni sadaka kwa tembo. Haya maneno gani haya? Kanuni hiyo inasema hivyo, sasa ni maneno gani haya? Kanuni ambayo unaweza kuleta hapa kesho tukaibadili, haiji. Mheshimiwa Waziri aende alete hiyo kanuni ili tuibadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kusema kweli mimi nasema, Wizara ya Maliasili na Utalii, hii bajeti inayokuja mjiandae mtusaidie, itusaidie kwenye haya mambo. Hatuwezi kuwa tunakaa hapa kila siku tunapiga kelele watu wanaumia, haiwezekani. Kama fidia imeleta shida kwa nini *South Africa,* Botswana, Kenya wameweka *fence* wamefaulu, kwa nini Serengeti wameweka *fence* sehemu nyingine wamefaulu? Kwa nini tusikubali fedha zote hizi za fidia ziende kwenye *fence*? Shida iko wapi? Watu wanahangaika kila mwaka tunaangalia. Kwa hiyo, hilo nalo tulizungumze tuone linaenda maeneo gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la migogoro ya ardhi, migogoro ya ardhi tunaisababisha sisi. Waliunda hapa Kamati ya Mawaziri sijui 10 wakazunguka wakawa sijui na *interest* zao. Yaani huku ndani unashindwa kuelewa hiki ni kitu gani? Hivi kweli kwa mfano watu wa Bunda, Eneo la Nyatwali, Eneo la Serengeti, Eneo la Tamau mmechukua kwa ajili kuwapa wanyama wetu. Watu wamehamia Kijiji cha Mekomariro ambako kulikuwa na eneo; kijiji hicho hicho mnaenda mnatengeneza eneo kwamba kuna mwekezaji atakaa hapa. Mwekezaji hajulikani, yuko mfukoni mwa mtu; watu wanateseka maeneo hayo kila siku. Kijiji cha Mekomariro wameteka eneo la wafugaji, kuna mtu ameenda amejenga mule ndani, hatoki, Mkuu wa Mkoa anajitahidi sana kumtoa, hatoki. Sasa nashindwa kuelewa ni nini hiki, mtu hana hati hana nini, hatoki. Sasa Serikali hii tunakuwaje? Haya ni mambo gani haya yanaonekana? Nimemuomba Waziri Mchengerwa na nimemuomba Waziri wa Ardhi waende pale basi watusaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninaamini kama leo Mawaziri wa Maliasili na utalii, TAMISEMI na Waziri wa Ardhi tukikaa pamoja na Wabunge wote wenye matatizo tunaweza kutatua matatizo. Hivi ardhi ni ya nini? Hivi kweli ardhi ni ya Nani, si ni ya kwetu sisi? Hivi ukisema wewe sita una kashamba, chukua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi watalii wanahitaji tembo wangapi ili tupate hela? Hivi ili tupate hela kwenye hii Wizara tunahitaji tembo wangapi? Sasa mbona ardhi ni kubwa na bado tunanyanyasika, watu tunanyanyasika ili hali ardhi ipo. Pale kwenye matatizo gawa ibaki. Tuna mapori sijui mapori sijui mapori ya akiba, yale mapori hifadhi za Taifa 22. Zinazofanya kazi ziko tano tu. Nyingine zipo tunatunza tu. Hivi maana ya akiba ni nini? Maana ya pori la akiba ni nini? Maana yake ni kwamba wanadamu wakizidiwa wasaidiwe. Sasa haya ni maneno gani? Naona mambo haya yananishinda sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana jamani wala hamna mgogoro na Waziri, watendaji wetu wanafanya kazi vizuri na hawa *TANAPA* wanfanya kazi vizuri, isipokuwa wanazidiwa. Maamuzi tufanye sisi Wabunge. Maana sisi ndio tunatunga sheria. Si kila mtu amegawana? Tukubaliane kwenye maeneo haya ambayo ni hatari Wabunge tujikusanye tuandike matatizo tuliyo nayo kwenye maeneo yetu tuje hapa tukae na Mawaziri wa Ardhi, Maliasili na Utalii pamoja na wa TAMISEMI, tukubaliane bwana haya yatoke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake imefikia wakati sasa sisi Serikali ya CCM tukiwajengea watu madarasa, Barabara na tukiwapa watu umeme lakini wamekaa na nyongo za maisha hivi wanatupigiaje kura? Kwa nini watupigie kura. Lazima CCM tukubaliane hii hali, tutaendelea kutawala, tutoe au tuwatolee watu nyongo kwenye roho zao. Tutoe nyongo, watu wanatapika nyongo. Leo mnaona Mwenezi anatembea mahali watu wanaenda na makaratasi wamejaa kila mahali. Wamejaa nyongo, tuondoe hizi nyongo. Nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwita Getere. nilimtaja Mheshimiwa Geophrey Pinda, Naibu Waziri wa Ardhi na

baadaye Mheshimiwa Angellah Kairuki na mwisho mtoa hoja ajiandae.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nitumie nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia afya na leo tuko hapa mbele yake tukisikiliza mambo mbalimbali. Nianze kwa kuipongeza Kamati kwa maazimio mbalimbali ambayo yamewasilishwa kwetu. Sisi kama Serikali maazimio haya tunayachukua kwa ajili ya kwenda kuyafanyia kazi na kuyachakata kwa namna yoyote ile ili kuleta ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mambo machache ambayo yamezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge na kwa kweli kwa upande wa Wizara yetu Wabunge wengi wamechangia na sehemu kubwa sana walijikita kwenye hii migogoro ya adhi, fidia lakini pia mpango wa maboresho ya matumizi bora ya ardhi kwenye vijiji. Mambo yote haya na ushauri wote walioutoa sisi kama Serikali tunayapokea na tunakwenda kuyachakata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kama Wizara kwenye suala la mabaraza ya ardhi, sasa hivi tunaendelea na mchakato ambao, ili kukamilisha ile idadi ya wilaya tulizonazo ya kuajiri wale wenye viti wa mabaraza. Muda mfupi ujao tunaweza kabisa wilaya zote zikawa zimepata watendaji ambao watakwenda kutusaidia kupunguza hasa umbali kutoka wilaya moja mpaka wilaya nyingine, kwa mfano mtu wa Dodoma hapa tumempa mpaka Kiteto kule unakuta wakati mwingine tunakuwa na limbikizo la kesi ambazo zingetakiwa zitatuliwe kwa muda mfupi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ni imani yangu kwamba wakati ujao tutakapokuwa tunatoa taarifa ya utekelezaji tutakuwa tunawafikisha kwenye kuondoa kiu hii hasa kwenye upande wa mabaraza. Ninaomba mtupe nafasi ili tuweze kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la kubuni na kutekeleza mipango mbalimbali ya kupunguza migogoro ya ardhi naomba niwape *comfort* Waheshimiwa Wabunge, kwamba

Wizara imejipanga na kama Wabunge walivyosema asubuhi, tuna timu mbalimbali zinazotafiti kwa nini kuna migogoro mingi hapa nchini na nini asili yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ufupi tu unaweza ukaona migogoro hii ina sura kama mpaka tatu hivi. Iko sura ile ambayo ni wananchi wenyewe kugombania maeneo yao kwa mipaka ile isiyotambuliwa. Tunayo mashamba makubwa makubwa ambayo wananchi wanaoonekana wamekaa katika maeneo yale uasili wao ni kwamba wana historia ambazo haziwezi zikabadili uwepo wao pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano mashamba makubwa watu walichukuliwa kutoka sehemu mbalimbali kwenda kuongeza nguvu za uzalishaji kwenye yale mashamba. Hili nalo tumelipokea na tunalifanyia kazi kwa haraka ili kuangalia. *Case study* moja ni Mkoa wa Manyara ambao wananchi wake wengi ambao wanagombana na wale wawekezaji sehemu kubwa sana wana asili ya uwepo wao pale kwa sababu wazazi wao ambao walichukuliwa kutoka maeneo mbalimbali waliletwa na hao wenye mashamba na sasa hivi inaonekana ni tatizo na ni kadhia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunafanya nao kazi na nimekutana na wawekezaji wa mashamba makubwa takriban Mkoa mzima wa Manyara. Tumekubaliana na wengi wameanza kukubaliana kwamba *okay* tatizo *the way* lilivyo iko haja sasa ya kuangalia upya namna ya kuachia maeneo mengine ambayo hawa Watanzania wanaweza wakaendelea kuyatumia kwa namna yoyote ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hili suala la mipango ya kutatua migogoro tunaendelea nalo. Tunatengeneza mifumo ambayo baada ya muda kama mlivyosikia kwenye taarifa ya Kamati, tuko zaidi ya asilimia 80 katika kuanza kufanya majaribio ya kutumia TEHAMA katika *process* nzima ya mtu anapotafuta kiwanja. Kwa sasa hivi bado tunabeba mafaili mkononi, na hiyo imesababisha matatizo mengi sana. Matatizo mengi ya katikati ya miji ambayo tayari imeshapimwa siyo kwamba inahitaji kupimwa upya. Kule ku-*move* kwa njia ya mkono bila kutumia mitandao hii

mara nyingi imesababisha vitu vingi kuwa na mambo ya *double allocation* bila sababu za msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa dawa inachemka; niwaombe tu Waheshimiwa nadhani mpaka kufikia Bunge linalokuja tutakuwa tunatoa taarifa ya utekelezaji. Wengine mtakuwa mnaona kwenye mitandao yenu kupitia simu zenu jinsi mnavyopewa ripoti ya maeneo ambayo mnayamiliki kihalali. Kwa hiyo, niwaombe tuwe na muda wa kutosha ambao tutakwenda kuleta matokeo zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nizungumzie kwa ufupi sana kuhusu susala la maboresho ya mipango ya matumizi bora ya ardhi ya vijiji. Waheshimiwa Wabunge niwaambie, mpaka kufikia 2024 hapo tutakuwa tayari tumeshapima vijiji 5,000 na vijiji 5,000 ni karibu nusu ya safari ya vijiji vyote vya Tanzania. Kwa hiyo, naomba tu kwa sababu fedha zile ambazo zimeombwa kutoka kwenye mifuko mbalimbli, tunazo fedha zinazotegemewa kutoka kwenye halmashauri kama mtakumbuka Bunge lililopita na tuna fedha ambazo tunazitenga kwenye bajeti yetu ya kila siku. Kwenye huu mfuko ambao unatokana na mfuko wa *World Bank* tayari kwa sababu bajeti ya kwanza ilikuwa inasema tutenge bajeti ya shilingi bilioni saba; lakini nataka niwakikishie mpaka sasa tumeshatenga shilingi bilioni 21 katika zoezi hili na tunakwenda kupima vijiji zaidi ya 1,600.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachotokea hapa katika tofauti ya utekelezaji; Tume hii iko chini ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Utendaji kazi wake ni wa pamoja wala siyo kwa kutenganisha. Mradi kama huu wa *World Bank* una masharti magumu sana katika kutoa fedha yake kuihamisha kuipeleka Tume. Kwa hiyo, hizi shilingi bilioni 21 zinasimamiwa na Wizara yetu chini ya fungu la Wizara lakini watendaji ni wale wanaotoka kwenye tume kwenda kutekeleza yale majukumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe Waheshimiwa Wabunge ni kweli mnaweza msizione fedha kwenye *account* za tume lakini tume tunai-*facilitate* kwa asilimia 100; na mpaka sasa hivi maafisa wengi kutoka kwenye ile tume wako uwandani na wanaendelea na kazi, hatujakwama mahali popote. Kwa hiyo,

niwaombe tu kwamba ni mambo ambayo yanatekelezeka kwa utaratibu wa kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ongezeko la fedha. Mkopo huu ulikuwa na mambo mengi, na moja ya eneo lake ilikuwa ni kufanya mamboresho kwenye maeneo ya utawala wa Wizara. Niwakikishie Waheshimiwa Wabunge, mikoa yote inaenda kupata majengo kwa ajili ya maafisa wetu. Najua mnajua wanavyohangaika kwenye halmashauri kule, wanavyojibana kwenye vyumba vidogo vidogo. Tunakwenda kujenga ofisi za mikoa yote. Mikataba tayari imeshasainiwa ya kubaini wale wakandarasi. Tunakwenda vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na eneo hili vile vile tunakwenda kuanzisha ofisi za ardhi za wilaya ambazo kwa miaka yote hazijawahi kutokea. Kwa hiyo, kumekuwa na *miss communication.* Kumekuwa na mtengano wa kimawasiliano kati ya maafisa wetu ambao tumewa-*attach* kwenye halmashauri ambao wako chini ya Wizara yetu na kamishna wa mkoa; unakuta *load* ya kamishna wa mkoa ni kubwa. Tunakwenda kuwa na makamishna wasaidizi wa wilaya ili waweze kusimamia zile halmashauri zilizoko chini ya Wizara zao. Hii itatusaidia sana kutusogeza karibu na huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengi wamezungumzia masuala ya mabadiliko ya sheria na sera. Wizara iko kwenye mchakato na sera ilishakwenda mpaka kwenye Baraza la Mawaziri. Sasa Waheshimiwa Wabunge tukae mkao wa kuipokea huku Bungeni kwa ajili ya kuipitia, lakini iko mwishoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tuliabaini kwamba sera ile ni ya muda mrefu na ina mapungufu. Kwa hiyo, yale mapungufu yote mliyoyaona ninyi na kushauri, ushauri wenu wote tumeuweka kwenye haya mapendekezo ya sera mpya ambayo inakuja. Niwaombe tu kwa ujumla wake. Kwanza napokea shukrani nzote napongezi zote mlizozipeleka kwa Mheshimiwa Waziri na Wizara yake, na mimi nitamfikishia; lakini pongezi zote zilizotolewa kwa Serikali nzima kwa maana ya Mheshimiwa Rais pamoja na watendaji wake wote tuliopo. Tunashukuru sana kwa hizo shukrani ambazo kweli mnatambua mchango ambao unatolewa Serikali

ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania. Niwaombe tujipe muda kuhusiana na mambo haya. *The way* tunavyokwenda tunakwenda katika michakato tofautitofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo moja ambalo ningependa niwambiwa Watanzania wote ardhi ya Tanzania kwa ukubwa wake haina nyongeza nyingine yoyote tulikuwa nayo Mwaka 1953, tukawa nayo Mwaka 1960, tunayo Mwaka 1970 na tunayo 2024, haitaongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kupitia hilo sisi Watanzania Mwaka 1950 tulikuwa chini milioni tisa, leo tunapozungumza tuko milioni 61. Hekima ituongoze katika kupitia haya mambo ambayo yanaihusu ardhi. Ongezeko letu ni sababu nyingine ya msingi kabisa ya ongezeko la kusukumana sukumana katika maeneo yetu. Nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge na nawashukuru kwa jinsi ambavyo mnatupa mawazo jinsi ya kukabili ongezeko la watu bila ongezeko la ardhi, ahsante sana Mungu awabariki sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu wa Wizara ya Ardhi Mheshimiwa Geophrey Pinda. Sasa namkaribisha Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Angellah Kairuki na Baadae mtoa hoja akae tayari, karibu.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi, na nianze kwa kuunga mkono taarifa hii ya Kamati yetu ya Kudumu ya Ardhi, Maliasili na Utalii. Naipongeza Kamati kwa taarifa nzuri na maazimio waliyoyatoa; na zaidi nishukuru kwa ushirikiano ambao wanatupatia mimi, Naibu Waziri pamoja na uongozi mzima wa Wizara pamoja na taasisi zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote ambao mmeweza kuchangia hoja hii. Utaweza kuona ni kwa namna gani hoja hii au Wizara hii inavyogusa wananchi wetu huko, na tunawashukuru ninyi kama wawakilishi wa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza kujibia au kutoa ufafanuzi katika maeneo machache napenda tu kusema kwamba tutaendelea kutekeleza majukumu ya Wizara, na napenda kusema kwamba Mheshimiwa Rais amekuwa akifuatilia kwa ukaribu  na kutuelekeza katika maeneo mbalimbali. Kubwa ikiwa ni suala zima la kulinda na kuimarisha uhifadhi wetu; lakini vingine kuendele kuhamasisha na kutunza utalii tulionao na tunawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote na wajumbe wa Kamati kwa namna ambavyo wameendelea kutupa uongozi, lakini vilevile, kwa namna ambavyo wameendelea kutushauri katika kusimamia maeneo hayo makuu kama mlivyowaeleza kama tulivyokasimiwa na Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo napenda sasa kutoa ufafanuzi katika maeneo kadhaa ambayo yameelekezwa na Kamati kupitia taarifa. Vilevile, maeneo mengine ambayo wamegusia Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza kuhusiana na zoezi zima la uhamishaji kwa hiari kwa wananchi wa eneo la Ngorogoro ambao wanahamia Msomera, kwa wale ambao wako tayari kuhamia Saunyi, lakini vilevile wengeine ambao watahamia Kitwai *D* kule Simanjiro na wengine pia watahamia katika maeneo ambayo watayachagua. Niishukuru Kamati ilitembelea Msomera na waliweza kutoa maoni mbalimbali walipofika huko. Maelekezo na ushauri ambao kweli tunaendelea kutekeleza na tunaamini yatatuletea tija kubwa pamoja na ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepokea maelekezo ya kuendelea kuunda timu ya Wizara za Kisekta. Niwahakikishie tu waheshimiwa wajumbe wa Kamati na Wabunge tumeunda timu ya Wizara za Kisekata na wataalamu wetu wamekuwa wakiendelea kufanya uratibu kupitia ofisi ya Waziri Mkuu, Sera Uratibu na Bunge. Namshukuru dada yangu Mheshimiwa Jenista na wengine wpte chini ya Ofisi ya Waziri mkuu ambao wamekuwa wakishirikiana nasi lakini na Wizara zile nyingine; kwa sababu bila wao kutekeleza matakwa mbalimbali ikiwemo ujenzi wa miundombinu, upelekaji wa huduma ya maji na barabara tusingeweza kufika hapa tulipofika na kuweza kukamilisha ujenzi huu wa nyumba. Kipekee nashukuru sana. Mimi na wenzangu

tunashukuru Wizara hizo za kisekta pia kwa namna ambavyo wametimiza wajibu wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa kuna hoja ya utekelezwaji wa bajeti kwenye miradi ya maendeleo, tunashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati na Wabunge wote ambao wameweza kutoa ushauri wa bajeti yetu kuweza kutoka kwa wakati na hasa ile ya maendeleo pamoja na Matumizi Mengineyo *(OC)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeendelea kufanya mashauriano na Wizara ya Fedha ili kuweza kuongeza kasi ya utoaji wa fedha za miradi ya maendeleo, na bahati nzuri Jumanne tutakutana na Mheshimiwa Waziri wa Fedha na timu yake na tunaamini tutaweza kupiga hatua kubwa lakini tunashukuru na tunapokea ushauri huu ambao mmeweza kuutoa na tunaamini tutakapokutana, lengo letu, na Waziri wa Fedha pamoja na Serikali kwa ujumla ni kuona ni kwa namna gani tunaendeleza zaidi miundombinu ndani ya hifadhi zetu, vilevile kuona ni kwa namna gani tunaunganisha barabara kati ya Wilaya moja na nyingine na kwenye hili tutaendelea kupata ushirikiano mkubwa wa *TARURA*. Pia zile ambazo zinavuka Mkoa na Mkoa ili tuhakikishe kwamba na hata zile hifadhi nilimsikia dada yangu Mheshimiwa Taska, za Katavi na kwingineko ambako unakuta labda huoni zikitangazwa sana au zikipata watalii wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utalii wa Kusini na maeneo mengine tunaamini tukiweza kupata miundombinu ya kuunganisha Wilaya zetu vizuri basi itakuwa rahisi hata tunavyofanya uhamasishaji na watalii waweze kufika katika maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa kuna hoja ya ile *account* ya *ESCROW* lakini vilevile kuona ni kwa namna gani taasisi zetu zitapata *retention*. Ni eneo ambalo vilevile tumeendelea kufanya mashauriano na Wizara ya Fedha, watakopokuwa wakiandaa ule Muswada wa Fedha ambao unakuja kila mwaka basi kuweza kuona ni kwa namna gani taasisi zetu zitawezeshwa kubaki na makusanyo yake moja kwa moja badala ya kuzipeleka Mfuko

Mkuu wa Hazina na kurudi ili tuweze kuzitumia katika kuendeleza taasisi zetu. Vilevile, pale itakapohitajika kuendeleza miundombinu na kufanya shughuli nyingine kwa ufanisi, tuweze kufanya hivyo huku tukitambua pia bado tuna jukumu la ulinzi pamoja na suala zima la uhifadhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo kubwa ambalo ukiliangalia kwa leo lilikuwa ni changamoto la wanyama wakali na waharibifu, limesemewa kwa kiasi kikubwa sana. Kwenye hili kwa kweli napenda kusema kwamba tunaendelea kutoa pole kwa wananchi wetu ambao wameathirika na wanyama hawa. Hatuwezi kusema kwamba tunajali wanyama kuliko binadamu. *Obviously* binadamu ni namba moja, ndiyo sisi tupo. Mheshimiwa Mbunge wa Biharamulo mpaka ameamua kutoa na maandiko kabisa ya Biblia, wakati huo huo na hifadhi zetu tunazihitaji kwa hiyo lengo letu kubwa ni kuona kunakuwa na hiyo *balance* kuhakikisha kwamba utajiri tuliopewa huo wa wanyamapori basi usije ukaathiri na wananchi wetu wakaona hakuna umuhimu kabisa wa kuweza kuwa na uhifadhi na uwepo wa wanyama hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea kuchukua hatua za dhati kabisa na bahati nzuri mtakumbuka hata Mheshimiwa Rais alipofanya ziara katika Mkoa wa Lindi alielekeza Kamati zetu za ulinzi na usalama lakini alituelekeza pia na sisi tuweze kutafuta muarobaini wa changamoto hii ya muingiliano kati ya wanyamaporti na binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusema kwamba tulishafanya tathmini hasa kwa Wilaya ambazo zimeathiriwa sana takriban Wilaya 44, tayari ukiangalia kwa Mkoa wa Simiyu, Mkoa wa Lindi na kwingineko tunaendelea kuchukua hatua kuhakikisha kwamba kwa wale ambao walitoka nje tunawarudisha ndani. Pia, kama kuna wengine wanafanya vitendo visivyo ndani na wenyewe kuweza kuwatoa nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ukiangallia chanzo kikubwa, tunahangaika na chanzo. Wanyamapori wengi wanatoka nje hasa wakati wa kiangazi wanapokuwa wanatafuta

maji, kwa hiyo kwenye eneo hili kama Serikali tunaendelea kufanya kazi kwa kuchukua hatua kuona ni kwa namna gani tunaongeza kasi ya uwekezaji zaidi, kuhakikisha tunachimba mabwawa mengi zaidi katika hifadhi zetu ili kuhakikisha kwamba wanyama hawa hawalazimiki kutoka nje ya hifadhi kuweza kutafuta maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshaanza katika hifadhi yetu ya Mkomazi na nyinginezo na tutaendelea kuongeza bajeti ili kuhakikisha tunatekeleza katika hifadhi zote kwa idadi inayojitosheleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ni matumizi ya teknolojia, mmeeleza vizuri sana Waheshimiwa Wabunge. Tumeshaanza kuangalia ni kwa namna gani tutatumia *drones* ili kuhakikisha kwamba zinatusaidia katika suala zima la doria, udhibiti na ulinzi. Tumeshaanza mafunzo kwa wanafunzi wetu, askari wetu ili waweze kuzitumia kwa suala zima la doria pamoja na kuhakikisha tunadhibiti Tembo wetu na wanyama wengine wakali na waharibifu wasiweze kutoka ndani ya hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la tatu, nimesikia kulikuwa kuna hoja ya kuweka fensi za umeme, watu wametoa mfano wa Botswana na Afrika Kusini. Ni kweli na sisi tumefanya kwa kiasi kidogo kwa upande wa Grumeti kwa Serengeti na tunaona mafanikio. Kwa changamoto tuliyonayo kama Tanzania ukilinganisha na nchi zingine, wenzetu wengi zaidi hifadhi zao wanamiliki watu binafsi. Wengine pia kwa nchi hizo maeneo hayo ni madogo kwa hiyo hata akiweka fensi ya umeme unajikuta pia inawezekana na wala hamiliki eneo kubwa sana. Kwa upande wetu tutafanya kwa maeneo kwa hali ya uwezo wetu wa kiuchumi utakavyoruhusu. Pia, tunatumia mfumo mwingine wa kielektroniki wa *geo-fencing* ili kuweka *parameters* ambazo ikitokea mnyama ametoka amevuka kiasi kadhaa kitakachokuwa kimekuwa *set* basi iweze kutoa *alert* na kuweza kujua mapema ameelekea wapi kabla ya hajafika mbali kutoka nje na kuleta madhara ili aweze kurudishwa ndani hifadhini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tunaendelea kuchukua hatua kuhakikisha kwamba tunaendela kuongeza vituo vyetu vya

askari. Tayari kwa miaka miwili tumejenga zaidi ya vituo vya askari 16 na mwaka huu pia tunajenga vingine 16 katika bajeti hii ya 2023/2024 na tutaendelea kufanya hivyo mwaka hadi mwaka ili kuhakikisha kwamba yale maeneo ambayo yanapakana na hifadhi zetu basi tunakuwa na vituo ambavyo vitakuwa na askari. Tayari kwa mwaka huu wa 2023/2024 tutakuwa na askari tutakaoajiri zaidi ya 350 na tumeendelea kupata vibali kutoka Ofisi ya Rais, Utumishi, kwa ajili ya kuweza kuajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa kuna hoja nyingine ilijitokeza ya kuwawezesha *TAWIRI* na *TAFORI*, tunapokea ushauri tukitambua kwamba taasisi zetu za utafiti hizi ni muhimu sana katika suala zima la maendeleo ya uhifadhi, menejimenti, uendelevu na usalama wa uhifadhi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla muda wangu haujaisha najitahidi kuongea kuhusu suala zima la masuala ya fidia na hasa eneo la kifuta jasho na kifuta machozi. Waheshimiwa Wabunge mmelieleza vizuri sana, na kwa kweli kama nilivyosema tunaumia tunapoona binadamu, tunapoona wanyama wengine wanaumizwa, tunapoona ndugu zetu mazao yao yanaathiriwa na wengine kumalizika kabisa na wengine kufilisika hata kupelekea kuingia katika njaa kubwa kutokana na mazao yao kuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge tumeendelea kufanya uhakiki, tunaendelea kufanya malipo na hata mwezi Januari mwaka huu tumeweza kufanya uhakiki kwa ajili ya kuweza kulipa katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa kanuni za kifuta jasho na kifuta machozi, tayari tulishafanya mapitio na tulishayakamilisha. Tumepeleka Wizara ya Fedha kwa wenzetu ili nao waweze kuangalia tathmini, waweze kuona ni athari kiasi gani za kiuchumi zitakazoweza kujitokeza na kuona uwezo wa nchi katika kulitekeleza suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Sheria ya Uendeshaji wa Mamlaka ya *TAWA* na *TFS,* yenyewe bado ni

maeneo ambayo tunayatekeleza, Nawahakikishia Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati na Wabunge wote waliochangia hoja hiyo, tunaendelea kulifanyia kazi ndani ya Serikali na pindi litakapokamilika basi litaweza kuwasilishwa Bungeni sambamba na kuhuisha sera mbalimbali na sheria nyingine zinazosimamia wanyamapori, misitu na sera nyingine chini ya Wizara yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa vivutio vya utalii tutaendelea kutangaza na tutaendelea kubuni mikakati mbalimbali kuhakikisha kwamba tunaongeza idadi ya watalii wanaokuja nchini sambamba na kuongeza uwekezaji katika ujenzi wa vyumba vya malazi ili watalii hao wanaokuja nchini waweze kupata maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru kwa pendekezo lile la kuunda mfuko wa maendeleo ya utalii ambalo Kamati mmelitoa. Napenda kusema kwamba tumeunda Kamati ya kimkakati ambayo nayo pia itaendelea kufanya uchambuzi wa eneo hilo ili kuona endapo linaanzishwa lianzishwe kwa namna gani lakini ni eneo ambalo kwa kweli tunaliunga mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja kabla muda haujaniishia ya *WMA*, nisipoeleza nitakuwa sijatenda haki. Tunazo *WMA* takribani 22 na tunaendelea kufanya nazo kazi vizuri sana. Tunawategemea sana katika suala zima la uhifadhi na maendeleo na lengo letu ni kuona ni kwa namna gani tunaendelea kushirikiana nao kwa karibu zaidi ili kuhakikisha kwamba wanatusaidia katika ulinzi. Vilevile, kuona ni kwa namna gani masuala ya utalii kupitia *WMAs* hizo zinaweza kutuletea ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa fedha ambazo zinadaiwa, tunaendelea kushauriana na Wizara ya Fedha zitoke haraka, lengo letu kubwa ni ikiwezekana kile kilicho chao wapewe mapema halafu zile zingine za taasisi za Serikali ikibidi kama itahitajika ndiyo ziende Serikalini badala ya kuchanganya na zile za *WMAs* pamoja na Halmashauri zetu za Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa kulikuwa kuna hoja kuhusiana na utekelezaji wa Azimio la Bunge la kuridhia

mapendekezo ya kurekebisha mpaka wa Hifadhi ya Taifa ya Ruaha. Napenda kuwashukuru Kamati hii ni hoja ambayo kwa kweli azimio wamekuwa wakilifuatilia sana kwa niaba ya Bunge. Tunaiona hoja ya Kamati kama Wizara na kama Serikali, kama Serikali tumeshafanyia kazi suala hili tulirekebisha mpaka, *GN* iliweza kutoka 754 lakini bado haijaweza kukidhi kama vile ambavyo Kamati au Bunge liliweza kuelekeza katika Azimio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusema kwamba tunaiona hoja ya Kamati na tunaiona hoja ya Bunge na ni Azimio halali la Bunge ambalo linapaswa kutekelezwa. Hata hivyo, wiki iliyopita tuliweza kuitishwa na Waziri wetu wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mawaziri Nane kuweza kufuatilia utekelezaji wa maagizo yote kuhusiana na migogoro ile ya vijiji 975 lakini tukabaini pia kuna shauri limefunguliwa, Shauri Namba 46 la mwaka 2023, lilifunguliwa mwezi Disemba katika Mahakama ya Haki za Binadamu ya Afrika Mashariki, takriban wananchi 855 wamefungua shauri hilo kuweza kupinga baadhi ya utekelezaji wa maeneo. Kwa hiyo bado tunaendelea kuhangaika lakini napenda kusema kwamba hiyo bado haituzuii kufanya hatua za kiutawala sisi ndani ya Serikali, kuweza kuendelea kuangalia Azimio lilitutaka nini, tufanyeje tathmini uwandani tutaendela nayo, lakini wakati huo huo kuweza kuona endapo tutatoa ardhi basi tutoe ardhi kwa kiasi gani bila kuathiri masuala mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi letu kwa namna Azimio lilivyowekwa sasa kama ikiwaridhia Wajumbe wa Kamati maana hili ni Azimio lao na hii nii taarifa yao, tulikuwa tunaomba marekebisho kidogo kwenye lile Azimio mwishoni pale kama ilivyowekwa ili kuweza kuona ni kwa namna gani sasa basi wakati tunaendelea na hatua zingine, itakapohitimishwa ile kesi, basi tutekeleza kwa mujibu wa hukumu itakavyokuwa imetoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, nawashukuru sana Wajumbe wote wa Kamati yetu pamoja na Wabunge wote waliochangia katika taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana naomba kuwasilisha, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Waziri wa Maliasili na Utalii Mheshimiwa Angellah Kairuki. Sasa namwita mtoa hoja, Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Timotheo Mnzava.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia tena kukushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuhitimisha hoja hii ya Kamati ambayo tuliianza mapema asubuhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natumia nafasi hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, kwanza, kwa kukubali kupokea hoja hii ya Kamati lakini kuijadili na kuiunga mkono. Tumepata bahati ya kuwa na wachangiaji wengi, hoja yetu imechangiwa na wachangiaji karibu 16, siwezi kuwataja wote kwa sababu ya muda lakini tunathamini na kutambua sana michango ambayo Waheshimiwa Wabunge wameitoa katika kuchangia hoja yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, pia, namshukuru Mheshimwa Waziri wa Maliasili na Utalii kwa michango yao ambayo imesaidia kwa sehemu kubwa kutoa ufafanuzi wa yale yote ambayo yamesemwa kwenye taarifa ya Kamati na ambayo yamesemwa na Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu hiyo wamenirahisishia kazi yangu ya kuhitimisha hoja itakuwa fupi. Naomba kutumia nafasi hii kuongeza ufafanuzi kwenye maeneo machache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye upande wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, katika eneo ambalo limechangiwa sana na Waheshimiwa Wabunge karibu wote ni migogoro ya ardhi na suala la kupanga, kupima na kumilikisha pamoja na jambo zima linalohusiana na mipango ya matumizi bora ya ardhi. Lazima tukubaliane, nchi hii ni ya kwetu sisi sote, nchi yetu ni ya amani yenye utulivu wa kutosha, tunaweza kuchukua mfano wa amani na utulivu wa nchi yetu kama shati zuri jeupe lakini migogoro ya ardhi inaweza kuwa sehemu au

naweza kuifananisha na kidoa kidogo chekundu kinachokuja kwa kasi kwenda kuchafua shati letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tusipochukua hatua za haraka kwenye eneo hili, huko tunapokwenda hatma yake siyo nzuri. Kama tulivyosema kwenye taarifa ya Kamati tunaiomba Serikali iendelee kuangalia namna ya kutatua migogoro mbalimbali ya ardhi tuliyonayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee tunaipongeza Wizara, kama tulivyosema asubuhi tunaamini sehemu kubwa ya utatuzi wa migogoro hii ya ardhi kwanza ni mfumo wa kidijitali wa kusimamia ardhi yetu. Mfumo ambao mtu anaweza kuingia, akakaa mahali alipo, akaangalia akajua kila kipande cha ardhi katika nchi hii kinasimamiwa na nani? kinamilikiwa na nani? na kipo kwa ajili ya kazi gani? Tukifanya hivyo tutakuwa tumefika pazuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, njia nyingine ya kutatua migogoro hii ya ardhi ni hili zoezi la kupanga, kupima na kumilikisha lakini hasa kutengeneza mipango ya matumizi bora ya ardhi. Ziko tafiti zimefanyika duniani kote na nyingine zimefanyika ndani ya nchi yetu. Mimi nimefanikiwa kuona tafiti mbili zimefanywa na Chuo chetu Kikuu cha Kilimo cha Sokoine kuhusu utatuzi wa migogoro ya ardhi. Walifanya moja kwa nchi nzima lakini moja walifanya kwenye Wilaya za Kilombero, Mvomero pamoja na Kilosa. Moja ya njia bora inayoshauriwa kama sehemu ya utatuzi wa migogogro ya ardhi ni kutengeneza mipango ya matumizi bora ya ardhi kwenye nchi yetu. Ndiyo maana kama Kamati tumeweka msisitizo kwamba Serikali iendellee kutafuta fedha zaidi kwa ajili ya jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ninalotaka kusema kidogo ni kuhusu suala la kodi ya ardhi *(land rent)*. Waheshimiwa Wabunge wamechangia vizuri, ni kweli sisi Bunge ndiyo tulipitisha Sheria ya Fedha na ilikuja na pendekezo la kuhamisha makusanyo ya *land rent* yakafanyike kwenye Halmashauri. Changamoto ya jambo hili, moja ni mifumo yote ya kiutumishi na mifumo yote ya kusimamia ardhi iko Wizara ya Ardhi. Mwenye *database* ya wamiliki wa ardhi wanaopaswa kulipa kodi ya ardhi iko Wizara ya

Ardhi. Zaidi ya yote changamoto nyingine kubwa sisi kwenye nchi yetu ardhi ni mali ya umma na iko chini ya usimamizi wa Mheshimiwa Rais. Kila mmoja anapopewa hati masharti makubwa mawili ya kuwa na hati ni kulipa kodi na kufanya maendelezo. Mtu asiyelipa kodi Sheria inaruhusu kufanya *revocation* ya hati yoyote ambayo hailipiwi kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa anayesimamia ardhi ni mwingine, anayeweza kufanya *revocation* ni mwingine lakini mapato au kodi anakwenda kukusanya mtu mwingine, jambo hili haliwezekani! Tunaomba Serikali ikubali kama siyo kubadilisha basi tunakokwenda kwenye Sheria ile ya Fedha tutoe jambo hili tuwaachie watu wa Wizara ya Ardhi kazi ya kuendelea na jukumu hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, limekuwepo hapa jambo kuhusu watumishi wa sekta ya ardhi. Jambo hili lina mjadala mpana, kwamba waendelee kubaki Wizara ya Ardhi au warudi Halmashauri. Waheshimiwa Wabunge tukumbuke, kabla ya mfumo huu wa sasa Watumishi wa Ardhi walikuwa chini ya Halmashauri zetu na tumeona ndiyo sehemu kubwa ya changamoto hizi za ardhi kwa sababu Wizara ilikuwa haina nguvu ya kuwasimamia moja kwa moja. Kamati tumeliona lakini tumeliacha kwa Serikali, Bunge tunaendelea kulitafakari zaidi, huu ni mjadala mpana namna gani ya kwenda na jambo hili, lakini kwa hili tunaona kama Kamati watumishi hawa wakiendelea kuwa chini ya Wizara ya Ardhi itasaidia kuwasimamia vizuri na kwa ukaribu zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko jambo moja Mheshimiwa Kunambi alilisema kwamba kwa Serikali kuwapeleka watumishi Wizara ya Ardhi imevunja Sheria ya Mipango Miji, naomba niliweke hili sawasawa. Sheria ya Mipango Miji kwa asilimia zaidi ya 70 mtekelezaji wake ni Wizara ya Ardhi. Sheria ya Mipango Miji ni kweli inatoa jukumu, *planning authority* kuwa ni Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kwa watumishi hawa kutokuwa kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa hakuathiri chochote kwenye sheria, kwa sababu hata wakati wakiwa kwenye Halmashauri, tunaposema Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwenye Halmashauri ni *Full Council*. Hawa watumishi kazi yao ni kuwa-*facilitate* Madiwani

ili waweze kufanya kazi vizuri, jukumu ambalo wanaweza kulifanya hata wakiwa chini ya Wizara ya Ardhi kwa sababu wanafanya kazi kule kwenye Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine kwenye upande wa ardhi ni kwenye eneo la fidia. Limesemwa sana na kwa kirefu na Waheshimiwa Wabunge naomba Serikali ilisikie. Changamoto kubwa kwenye fidia ni tatu, moja, kuna kuchelewa kwa kulipwa fidia hasa kama ardhi inatwaliwa. Changamoto ya pili kumekuwa na malalamiko ya fidia ambayo ni kidogo na ya tatu mara nyingi Serikali inafanya uthamini halafu baadaye inaahirisha kuchukua yale maeneo na kuwarudishia wananchi. Jambo hili linawakwaza wananchi linawarudisha nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumetoa ushauri mzuri na mapendekezo mazuri kwenye taarifa yetu ya Kamati namna ya kuhakikisha kwamba uhakika wa fedha unapatikana kabla Serikali haijafanya uthamini na kuchukua ardhi za wananchi. Naamini mapendekezo tuliyoyatoa yakifanyiwa kazi na Serikali yatatufikisha mahali pazuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho kwenye upande wa sekta ya ardhi ni Kamati ile ya Mawaziri Nane wa kisekta, jambo hili limesemwa muda mrefu, binafsi natambua na kukiri kazi kubwa na nzuri inayofanywa na Kamati ile ya Mawaziri Nane, tunachokiomba kwa Serikali ni jambo hili lifike mwisho. Tumelisema muda mrefu lakini hatma yake ni nini? Kwenye kila eneo tumeamua nini, tumetekeleza nini? Tunaomba Serikali ifikishe mwisho jambo hili ili matunda ambayo yalitarajiwa na Mheshimiwa Rais wakati wa kuunda Kamati hii yaweze kuonekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa hoja za Wizara ya Maliasili na Utalii, pia yamesemwa mengi na siwezi kuyasema yote na Mheshimiwa Waziri amenisaidia, amesema vizuri, ntasema machache tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, ni kuhusu utendaji kazi wa Taasisi zetu za Uhifadhi; kwanza natumia Bunge lako Tukufu kukiri na kuwapongeza watumishi wetu, askari wetu wa Jeshi la Uhifadhi

kwenye Taasisi zote, kwa kweli wanafanya kazi nzuri sana kwenye mazingira magumu. Kama Bunge na kama viongozi, lazima tuwatie moyo askari wetu hawa, wanafanya kazi nzuri kupambana na ujangili, wanafanya kazi nzuri kutunza maeneo yetu ya uhifadhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, tumesema vizuri kuna changamoto nyingi, tunampongeza Mheshimiwa Rais ametangaza utalii kwa mfano, watalii wameongezeka. Kutangaza utalii, utalii ni biashara, kwenye biashara kutangaza ni hatua ya kwanza kwa maana kuisema na kuizungumzia biashara yako, lakini matangazo ya pili ambayo ni ya msingi, ni huduma anayokuja kupata huyo mteja wako unayemkaribisha kwenye biashara. Bila kuweka mikakati mizuri ya kukarabati miundombinu kwenye maeneo ya uhifadhi, watalii wanaokuja hawatapata huduma nzuri watakasirika, wataondoka na wengi wao hawatarudi na hawatatusemea vizuri kule wanapokwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaendelea kuiomba Serikali tumeweka azimio lile, tuunge mkono tukalitekeleze, tuwape taasisi za uhifadhi fedha ili waende wakatekeleze majukumu yao vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri amekiri, eneo kubwa ambalo Waheshimiwa Wabunge wamelisema na kwa kweli kama kuna jambo ambalo pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Serikali ya Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, lakini kama kuna eneo ambalo linawakwaza wananchi kwa sasa ni athari za wanyama wakali na waharibifu, jambo hili ni kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada zinazofanywa na Serikali, tunaiomba ilione kwa ukubwa huo, ilione kwa upana wake, lakini kubwa pia na kile kifuta jasho na kifuta machozi kwa muda mrefu tumesema tumeweka azimio, tumeomba Serikali ikatekeleze kufanya marekebisho ili kiendane na maisha na hali halisi ya uchumi ya sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni eneo la *WMA;* namshukuru sana Mheshimiwa Olelekaita, amelisema vizuri na ametoa darasa zuri sana kuhusu Jumuiya za Hifadhi za Jamii. Tunaiomba Serikali, pendekezo letu lina nia njema sana na pendekezo hili hata wenyewe watu wa *TAWA* linawakwaza, *TAWA* anapotengenezewa *ceiling* kwenye bajeti, wana-*include* mpaka na hela za *WMA* wakati *TAWA* hana kazi nazo wala siyo sehemu ya mapato yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, inafanya *ceiling* inakuwa chini, wakipata fedha zinakwenda kwenye *WMA*, wanapunguza mapato kwa ajili ya kufanya wao kazi zao za uhifadhi. Tunawaomba pendekezo hilo mlichukue, tuweke utaratibu, inawezekana, kama mwekezaji anataka kulipa, kwa sababu kwenye kanuni inajulikana, alipe hela ya Serikali, alipe hela Halmashauri, alipe hela *WMA* tuachane, kusiwe na haja kubwa ya watu kusubiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni eneo hili la *TAWA* na *TFS;* kwa kweli kama kuna eneo ambalo tumesema sana kama Bunge, ni eneo hili. Tunaposema leo *TAWA* ina Bodi ya Ushauri, ilianzishwa kwa Amri ya Serikali ambayo ilitengenezwa chini ya kifungu cha 8 cha Sheria ya Wanyamapori. Jambo hili linapunguza ufanisi kwenye utendaji kazi wa *TAWA*. Tunaiomba Serikali ituelewe kwenye eneo hili, na kwa kuwa tumelipigia kelele muda mrefu, tunaomba itoke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri amesema kwamba wako katika hatua mbalimbali, lakini mara ya mwisho alivyokuja kwenye Kamati walisema kwamba wao kama Serikali kwa sasa hawaoni umuhimu. Bunge lako Tukufu liliona umuhimu na ndiyo maana tuliweka azimio. Tunaiomba Serikali ikatekeleze azimio hilo ili mambo yakae vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni azimio lile kuhusu hoteli na *lodge* ambazo zimetelekezwa. Mtu mwingine anaweza akasema kwa nini Kamati inazungumzia hoteli na *lodge* hii ni mara ya pili. Malazi ni eneo muhimu sana katika shughuli za utalii, leo tunapozungumza, kwa mujibu wa Taarifa ya Wizara yenyewe ya uthamini wa maeneo hali ya malazi nchini ya mwaka 2021,

kwenye nchi hii tuna maeneo ya malazi 10,432 ambayo yana vitanda 132,676. Katika hivyo vyote, maeneo ambayo yana hadhi ya juu ambayo watalii wanayapenda na yanawafaa ni maeneo ya malazi 1,437 ambayo ni sawa na asilimia 13 ya maeneo yote ya malazi. Katika haya maeneo ambayo yapo ndani ya hifadhi au yanamilikiwa na Serikali, ni maeneo 261.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini tunasema kuhusu hizi hoteli, ziko hoteli ambazo zilikuwa kwenye maeneo ambayo ni *potential* kabisa kwenye hifadhi zetu ambazo watalii walipenda kukaa kwenye hizo hoteli zilikuwa zinafanya kazi. Tunajua Serikali ilizibinafsisha, iliziuza. Tumeenda mbali kwenye Kamati, tumeona mpaka na sehemu ya ile mikataba, maeneo mengine pamoja na kwamba ziliuzwa, lakini ziliuzwa kwa masharti. Lazima kuwe na sharti la kuendeleza, kulikuwa na kiwango cha fedha cha kuwekeza, lakini lazima ulete na mpango wa masoko na mpango wa uwekezaji. Serikali ilipewa nafasi ya kuendelea kufuatilia utendaji kazi wa hizi hoteli. Tunaiomba Serikali ilifanyie kazi eneo hili ili mambo yaweze kwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni mahitaji ya ardhi kwa ajili ya matumizi mengine. Amesema vizuri Mheshimiwa Margaret Sitta na ni kweli alikuja kwenye Kamati, tulisema wakati ule na leo amesema tena. Hakuna anayepinga kuanzishwa kwa hifadhi; mwaka 2019 bahati nzuri ilikuwa ndani ya Bunge hili, tulianzisha Hifadhi za Taifa mbili; Hifadhi ya Taifa ya Kigosi na Hifadhi ya Taifa ya Mto Ugala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya maeneo sehemu kubwa yalikuwa ni maeneo ambayo kwenye misitu hiyo wananchi wengi walikuwa wanafanya shughuli za kufuga nyuki. Baada ya kuanzisha haya maeneo, wananchi wale wameshindwa kuendelea kufanya shughuli zao. Baada ya kelele nyingi Serikali mmeona na kwa moyo mzuri wa Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, mwaka jana tumeishusha hadhi Kigosi ili kuruhusu wananchi hawa wafanye kazi za kufuga nyuki. Tunaiomba Serikali, ilione na hili la Ugala tuwasaidie Watu wa Kaliua, watu wa Urambo na watu wa maeneo mengine ili mambo yaweze kwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la mwisho, ni hili eneo la Hifadhi ya Taifa ya Ruaha na urekebishaji wa mipaka. Jambo hili lina historia ndefu na nikiri kama kuna jambo mojawapo gumu tumewahi kukutana nalo kwenye Kamati yetu ni jambo hili. Hata baadhi ya Wajumbe wangu walipata kashkash kidogo, wengine wakiambiwa maneno haya na yale lakini katika kufanya kazi ya Kibunge vizuri na kuitendea haki nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wote tunaupenda uhifadhi, nchi hii ni ya kwetu, na asiwepo mtu wa kutudanganya kwamba tutaondoa maeneo yote ya hifadhi yakawa ni maeneo ya kutumiwa na watu eti kwa ajili ya kuchunga au kufanya shughuli nyingine, maeneo ya hifadhi lazima yawepo, lazima yaendelee kutunzwa na huo ndiyo uhai wa hii nchi yetu na lazima tuungane kwenye eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili pamoja na kuwa na historia ndefu, sitaieleza sana, lakini nasema tu kidogo, baada ya Serikali kumaliza kufanya ile kazi kwenye Kamati ya Waheshimiwa Mawaziri nane, walipokwenda kuchambua wakagundua migogoro 975; katika migogoro 975, migogoro 35 ilikuwa inaangukia kwenye Hifadhi ya Taifa ya Ruaha. Katika hii migogoro ya vijiji 35, Kamati ya Mawaziri ikafanya kazi, ikamaliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yakatoka maazimio matatu; eneo la kwanza wakasema Ranchi ya Usangu, lakini kuna shamba la madibira ile *phase one* na vijiji 14, Serikali ya Chama Cha Mapinduzi, ikakubali virudishwe kwa wananchi ili wafanye shughuli zao. Jambo hili ni kubwa sana la kupigiwa mfano, lazima tuipongeze Serikali kwa moyo huu na kwa uamuzi huu ambao umefanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo Serikali ilifanya, kuna vijiji vitano walisema kwa namna yeyote kwa maslahi ya nchi hii, vijiji hivi vitano haviwezi kuvumilika lazima wananchi wahame, na sisi tuliunga mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la tatu, kulikuwa kuna vijiji 16 kwenye baadhi ya vitongoji walikuwa wanataka kutoka nje na vingine vibaki hifadhini, kwa hiyo jumla ya vitongoji 47 vilitakiwa

kubaki hifadhini. Baada ya Kamati ya Mawaziri nane kumaliza kazi yake, wakaenda kuandaa azimio kwa ajili ya kuleta Bungeni. Wakati wa kupitisha maazimio, yakaibuka malalamiko kwamba haya maeneo wanayoondolewa wananchi, wako wawekezaji wanalima kama wanavyolima hao wananchi, wao wameachwa, lakini wananchi wanaondolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukasema kama Kamati lazima tujiridhishe, Mheshimiwa Spika akatupa kibali, tarehe 22 Juni, 2023 tulikwenda Mbarali. Tulifanya ziara angani, tulifanya ziara ardhini, tukajionea. Ukiachana na maeneo mengine yote ambayo tunajua Serikali inayashughulikia kwa namna ya tofauti, lipo eneo moja linaitwa Mpungamoja; hilo eneo, shamba la wananchi na shamba la wawekezaji vimefanana, viko sambamba, wanatenganishwa na barabara, lakini wanaambiwa wananchi wanarudi hifadhini, lakini wanaambiwa huyu mwekezaji yeye anakuwa ni nje ya hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukasema jambo hili ni gumu, inawezekanaje kwamba wananchi wanatoka nje ya hifadhi, lakini hawa wengine wawekezaji wanaambiwa wao siyo sehemu ya hifadhi. Tukakaa na Wizara, tukazungumza na Wizara, tukakubaliana vizuri na tarehe 27 Juni, 2023 tukawasilisha Bungeni hapa. Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, alitoa *commitment* ya Serikali kwamba wako tayari kufanyia kazi ushauri wa Serikali na kwa sababu ya muda, sitasema lakini ninayo *Hansard* ya tarehe hiyo, ukienda ukurasa wa 136 na ukurasa wa 137.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Kamati na kama Bunge, tukawa tunasubiri utekelezaji wa jambo hili. Tulikutana na Wizara mwezi wa Agosti, 2023, hatukuwa na majibu ya utekelezaji, tulikutana na Wizara mwezi wa Oktoba, 2023, hatukuwa na majibu ya utekelezaji, tumekutana na Wizara Januari, 2024 hatukuwa na majibu ya utekelezaji. Katika mazingira hayo lazima turipoti kwamba azimio hili halikutekelezwa ndiyo maana tulileta Bungeni na kuliomba Bunge lako Tukufu liazimie na kuitaka Serikali ikatekeleze jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa, ni jambo hili moja, siyo hayo mengine yote yanayohusiana na Mbarali tunajua Serikali ina

utaratibu wake inaendelea nao hatuna shida, liko eneo moja ambalo sisi wote Serikali na Bunge tulikubaliana, tulipoona halijatekelezwa ndiyo maana tumekuja kuliambia Bunge kwamba jambo hili halijatekelezwa. *We have nothing, nothing and nothing personal* kwenye jambo hili, ni shughuli za Kibunge, ni utendaji kazi wa Kibunge na tulichokifanya sisi, tumefanya sehemu yetu kama Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na yote hayo lakini busara inatuongooza, lazima tutafute namna ya kwenda mbele na kukubaliana kwenye mambo hayo. Pamoja na michakato yote hiyo na kukaa muda mrefu pasipo kukamilika kwa azimio hilo, tumetaarifiwa hapa, amesema Mheshimiwa Waziri kwamba ipo kesi imefunguliwa kwenye Mahakama ya *East Africa (East African Court of Justice)* kuhusu eneo hili la Mbarali. Bahati mbaya hatujapata nafasi kama Kamati kujua nini kesi inasema, nini maelekezo ya kesi hiyo, nini madai ya kesi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tungeijua pengine tusingekuwa tumeweka kwenye jahazi hilo kwa sababu tunajua sisi kama Wabunge na Bunge letu, tunao wajibu wa kulinda utawala wa sheria kwenye nchi yetu ikiwemo kuheshimu vyombo vyote vya kimahakama. Sasa kwa sababu hatukupata nafasi hiyo ya kujiridhisha na kwa sababu Mheshimiwa Waziri amelisema hapa na tunamwamini kama Waziri aliyepewa dhamana na Serikali na Mheshimiwa Rais, sisi kama Kamati, tunaomba Bunge lako Tukufu tukubaliane twende vizuri kwenye eneo hili, kwenye eneo la azimio hili ambalo ni Azimio Namba 3.2.8, naomba Wabunge turidhie, tuongeze maneno ili ku-*take consideration* ya hiki kilichosemwa ili kama kipo kweli na kina madhara kwenye jambo hili, tusifanye Bunge kama tulivyokuwa tunataka kufanya mwanzoni ikaonekana kwamba Bunge tumedharau kile kinachoendelea kwenye Mahakama au Bunge hatujasikiliza kilichokuwa kinaendelea kule mahakamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kwa sababu hiyo, tunaomba tuongeze maneno machache tu kwenye lile azimio, baada ya maneno; "Bunge linaazimia kwamba, tuseme; "kwa kuzingatia hatma ya shauri lililoko mahakamani."

Kwa hiyo, azimio hili naomba lisomeke hivi; "Azimio la Bunge kuridhia mapendekezo ya kurekebisha mpaka wa Hifadhi ya Taifa ya Ruaha:-

Kwa kuwa, Taifa linahitaji uhifadhi wenye tija ambao ni endelevu usiokuwa na migogoro ya mipaka kati ya maeneo ya hifadhi na ardhi za vijiji;

Na kwa kuwa, utekelezaji wa Azimio hili la Bunge ulilenga kusaidia kulinda mifumo ya ikolojia katika Bonde la Usangu ili kurejesha uoto wa asili kwenye Hifadhi ya Taifa ya Ruaha na kuimarisha mtiririko endelevu wa maji katika Mto Ruaha Mkuu ambao unategemewa katika uzalishaji wa umeme wa maji katika Vituo vya Mtera, Kidatu na Mwalimu Nyerere;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba kwa kuzingatia hatma ya shauri lililoko mahakamani, Serikali itekeleze Azimio la Bunge na masharti yake kama ilivyowasilishwa na Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii na Taarifa ya utekelezaji huo italetwa Bungeni kazi hiyo ikikamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni imani yangu kwamba tukiliweka hivi jambo hili, itatusaidia kuwa tumejiweka vizuri na wenzetu wa Mahakama, lakini pia isionekane kwamba tumedharau hicho kinachoendelea kwenye upande huo wa mihimili mingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, narudia tena kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha lakini pia na kuhitimisha hoja hii. Nawashukuru sana Wabunge, sisi kama Kamati tuko tayari kuendelea kufanya kazi hii ya kuishauri na kuisimamia Serikali kwa maslahi mapana ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia haya marekebisho kwenye lile azimio moja ambayo nimeyasema, naomba sasa kutoa hoja kwamba Bunge lako lipokee Taarifa ya Kamati na likubali Maoni na Mapendekezo yote kama yalivyowasilishwa ikijumuisha na marekebisho yale ambayo tumeyasema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa Iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii kwa hitimisho hilo, kwa umakini wa hali ya juu na hoja imeungwa mkono takribani na Waheshimiwa Wabunge wote. *(Makofi)*

Sasa nitalihoji Bunge kuhusu Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii ya mwaka 2023 pamoja na Maoni na Mapendekezo yake sasa yawe Maazimio ya Bunge.

*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**MWENYEKITI:** Ahsanteni sana, natumia fursa hii kutangaza rasmi kwamba Taarifa ya Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii ya mwaka 2023 pamoja na Maoni na Mapendekezo yake, sasa yamepitishwa kuwa Maazimio ya Bunge.

Kwa hiyo, natumia fursa hii kwanza kabisa kuishukuru Kamati ikiongozwa kwa umakini kabisa na Mwenyekiti wake Mheshimiwa Timotheo Mnzava pamoja na Wanakamati wake wote kwa kazi nzuri ambayo wamekuwa wakiifanya muda wote wa mwaka 2023 hadi kufikia kuleta taarifa hii hapa. Pia nipongeza upande wa Serikali wakiwakilishwa na Naibu Waziri wa Ardhi Mheshimiwa Geophrey Pinda pamoja na Waziri wa Maliasili na Utalii Mheshimiwa Angellah Kairuki kwa niaba ya Serikali, mmepokea kwa unyenyekevu, nimewasikia hapa na Bunge limewasikia, kwa hiyo naamini kwamba unyenyekevu huu ambao mmeutumia leo kwa kupokea maoni haya, Mwenyezi Mungu atawajalia muweze kutekeleza na baadaye kuondokane migongano ama migogoro baina ya Waheshimiwa Wabunge au Kamati pamoja na Serikali pamoja na wananchi kwa ujumla. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo, nawatakia kila la kheri kwa kazi zote ambazo tunaenda kuzifanya. Naamini kwamba bila ushirikiano wa sekta zinazohusika kwa Wizara hizi mbili, hatutaweza kufika pazuri. Kwa hiyo, nawaomba sana mwende mkashirikiane kwa ukaribu kabisa kwa sekta zote ambazo

zinahusisha Wizara hizi mbili na hata nyingine ambazo hazihusishi, lakini zina uwiano fulani wa kuweza kufanya kazi pamoja, basi kwa Serikali mkafanye pamoja. Naamini mwisho wa siku mtafika pazuri. Mwenyezi Mungu awasaidie sana.

Baada ya kusema hayo, naahirisha Shughuli za Bunge hadi kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 12.52 Jioni Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Ijumaa, Tarehe 9 Februari, 2024 Saa Tatu Asubuhi)*